# Mazungumzo

## Katika Dini, Utamaduni na Jamii

أحاديث في الدين والثقافة والإجتماع

**Kimeandikwa na:**
**Sheikh Hasan Musa as-Saffar**

**Kimetarujumiwa na:**
**Abdul Karim Juma Nkusui**

ترجمة

# أحاديث في الدين والثقافة والإجتماع

تأ ليف

الشيخ حسن بن موسى الصفار

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 – 9987 – 17 – 001 –2

Kimeandikwa na:
Sheikh Hasan Musa as-Saffar

Kimetarujumiwa na:
Ustadh Abdul-Karim Juma Nkusui

Kimehaririwa na:
Ustadh Hemedi Lubumba

Kimesomwa Prufu na:
Al-Haji Ramadhani S. K. Shemahimbo

Kimepitiwa na:
Al Haji Mujahid Rashid

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Tole la kwanza: Machi, 2018
Nakala: 2,000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
**Al-Itrah Foundation**
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.alitrah.info
Vitabu mtandaoni: www.alitrah.info/ebooks/

ILI KUSOMA QUR'ANI MUBASHARA
KWA NJIA YA MTANDAO,
TEMBELEA www.somaquran.com

# YALIYOMO


Dibaji ………………………………………………………. 9
Neno la Mchapishaji……………………………………... 10
Utangulizi……………………………………………….. 12
Sehemu ya Kwanza……………………………………… 17
Mazungumzo ya Kwanza…………………………………... 17

Katika maisha ya Familia yenye Mafanikio 22

Kisimamo katika Hadithi ya Kisai:………………………….. 25
Kuchunga haki ndani ya familia:……………………………. 27
Mafanikio katika mahusiano ya kijamii:…………………….. 31
Mwanadamu baina ya mbinyo wa kimada na utukufu wa kiroho:…………………………………………………….. 38
Kwanza: Baina ya matamanio na akili: …………………….. 39
Pili: Baina ya ubinafsi na utukufu:………………………….. 40
Tatu: Baina ya ufinyu na maadili:…………………………… 40

Muamala wa Kibinadamu katika Sira ya Imamu Ali عليه السلام: 41

Maji ni haki ya wote:……………………………………... 42
Hata mhaini ana haki yake:………………………………….. 45
Kuzuia kutoa adhabu:……………………………………….. 47
Kumfanyia Wema Mkosaji:…………………………………. 47
Kusamehe kosa:……………………………………………... 49

Kukataza maovu ni Huruma na kufanya Marekebisho 49

Kwanza: Kujali Maslahi ya Mwanadamu na Faida Zake:….. 52
Pili: Kuanza na Upendo wa Kweli kwa Mwanadamu:……… 54
Tatu: Kuchunga Hali ya Jumla ya Mwanadamu:……………. 55
Anawalingania waasi:……………………………………….. 58

Ujumbe Wa Manabii Imani Na Utekelezaji 60

Kwanza: Haja ya Kupata Maarifa:………………………….. 61
Pili: Haja ya Kijamii:……………………………………... 64
Tatu: Haja ya Kitabia:…………………………………….. 65
Watu wa Mada na Utekelezaji wa Sharia:…………………... 66

Upande wa Kijamii katika Maisha ya Imamu Husein عليه السلام 70

Upande wa Kijamii Katika Maisha ya Imamu: ……………. 70
Uhudhuriaji wa Kijamii:………………………………….. 71
Mfano wa Kitabia: ……………………………………….. 75
Kuzingatia sehemu za madhaifu katika jamii:………………. 76

Uchaguzi wa Mume baina ya Binti na Watu Wake 79

Mwanamke thayibu (mtu mzima):………………………….. 81
Binti bikra:………………………………………………... 81
Hekima ya idhini ya walii:…………………………………... 82
Kutumia haki vibaya:……………………………………….. 84

Mwanachuoni wa Kidini na kuitakasa Nafsi 87

Maana ya utakaso: ………………………………………….. 89
Mwanachuoni wa kidini:……………………………………. 90
Kigezo chema:………………………………………………. 92
Kutoka katika umateka wa tamaa: …………………………. 93
Usafi wa kuamiliana na watu:………………………………. 95

Upole wa Imamu Hasan عليه السلام ni Njia ya Ukunjufu wa Kijamii 96

Maana ya Upole: ……………………………………………. 98
Madhara ya ghadhabu na kukasirika: ………………………. 100
Upole ni manhaji ya kijamii: ………………………………... 101
Namna gani tutaamiliana na hasira za makundi: …………… 101
Mfumo wa Imamu Hasan: …………………………………. 102

Ugomvi wa Kidini, Je una Kisingizio? 105

Ni Iddi ya Upendo na Usafi, na si Iddi ya Kugombana:……. 105
Mazingira ya Ugomvi: ……………………………………… 105
Ugomvi Katika Dini: ……………………………………... 106
Katika Duara la Uislamu: …………………………………… 110
Mtazamo wa Kifikihi: ………………………………………. 111
Iddi ya Upendo na Usafi: …………………………………… 113

Uswalihina na Kutafakari 115

Kulazimiana baina ya uswalihina na akili: …………………. 116
Uswalihina na kutafakari: …………………………………... 117
Kutafakari na kufuata uongozi wa kidini: …………………. 119
Rejea ya akili: ………………………………………………. 123

Wenye Rai na Jukumu la Mjadala 124

1. Udhaifu wa kujali mambo ya jamii: ……………………… 127
2. Hisia za kutawala na kutisha: …………………………….. 128
3. Utengenezaji na hukumu zilizotangulia: …………………. 129
4. Kibano cha uchochezi kwa watu: ………………………... 132
5. Sehemu zenye nguvu: ……………………………………. 133

Pengo la Kiroho: Huzuni na Mkanganyiko 134

Mahitaji ya roho: ……………………………………………. 136
Je, maendeleo ya kimaada yanatosha? ……………………… 139
Albert Einstein ni mfano: …………………………………… 139
Kuhusu hali ya jamii ya Kimarekani: ………………………. 140
Somo na zingatio: …………………………………………... 142

Maendeleo ya Mtu Binafsi na Maendeleo ya Jamii 143

Kuandaa fursa za maendeleo: ………………………………. 144
Athari ya mazingira: ………………………………………... 145
Matokeo na mwongezeko: ………………………………….. 146
Nafasi ya jamii: ……………………………………………... 147

Nafasi ya mtu binafsi katika maendeleo ya jamii: ………… 148
Namna gani mtu binafsi anachangia katika maendeleo ya jamii yake? ……………………………………………….. 148
Mazingatio ya kijamii: ……………………………………… 152

Jamii yenye Uelewa 153

Uelewa katika mantiki ya Qur'ani: …………………………. 154
Uelewa wa kijamii: …………………………………………. 156
1. Uelewa na maarifa: ……………………………………… 158
2. Muamala mzuri: …………………………………………. 160
3. Kunufaika kutokana na uwezo…………………………… 162

Mwanzo wa Kutengeneza Upya 163

Mabadiliko ni sifa ya mwanadamu: ………………………… 165
4. Ulimwengu ni uboreshaji wenye kuendelea: ……………. 166
Malengo ya kutafakari na kudadisi katika ulimwengu:……... 169
5. Ushindani wa mabadiliko: ………………………………. 169
6. Kukabiliana na changamoto: ……………………………. 170
7. Uislamu: Ni Daawa ya Kujadidisha: ……………………. 170

Roho ya Kujadidisha 172

Alama na sifa za uvumbuzi: ………………………………… 175
1. Uelewa na matarajio: …………………………………….. 175
2. Kujiamini: …………………………………………….... 177
3. Mwanzo wa akili: ………………………………………… 180
4. Ushujaa na ujasiri: ……………………………………….. 180

Kanisa: Historia ya Dhuluma kwa Jina la Dini 182

Msamaha wa Papa: …………………………………………. 184
Ubabe wa ugomvi wa kimadhehebu:………………………... 185
Ugaidi wa kifikra: …………………………………………... 186
Ukandamizaji na ukoloni: …………………………………... 187
Somo na Mazingatio: ……………………………………….. 189

Ashura: Uelewa Na Upeo 189

Utajiri wa kimaanawi: ………………………………………. 191
Msimu wa Muharam: ……………………………………….. 195
1. Kuimarisha Uchamungu: ………………………………… 196
2. Ustawishaji wa kijamii: …………………………………... 197
3. Mafunzo ya Ashura: ……………………………………… 198
4. Kujenga umoja wa kitaifa na Kiislamu:…………………... 199

Shi'ah Na Ulimwengu 200

Mbinyo wa kuiga: …………………………………………... 217
Kiwango cha khatibu na lengo lake: ……………………….. 217
Na jambo la mwisho: ……………………………………….. 217

بسم الله الرحمن الرحيم

# DIBAJI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenye kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam

**Al Itrah Foundation**
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
SMS: +255 778 300 140

بسم الله الرحمن الرحيم

## NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la, Ahadith fi‘d-Din wa ‘th-Thiqafah wa ‘l-Ijtima’, kilichoandikwa na Sheikh Hasan Musa as-Saffar. Sisi tumekiita kwa Kiswahili, Mazungumzo katika Dini, Utamaduni na Jamii. Kitabu hiki kimekusanya khutba na mihadhara iliyokuwa ikitolewa na Sheikh wetu huyu katika nyakati na sehemu mbalimbali

Katika mfululizo wa vitabu vya mwandishi huyu, anahimiza waumini kuishi kwa kufuata mafundisho ya Uislamu ambayo yanagusa kila nyanja ya maisha na kiroho. Katika kitabu hiki anazungumzia juu ya mahusiano kuanzia katika familia, ndugu, jirani, jamii na utamaduni.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumini yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Abdul Karim Juma Nkusui kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kitabu hiki kwa lugha ya

Kiswahili; pia na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

بسم الله الرحمن الرحيم

## UTANGULIZI

Allammah, Dr. Sheikh Abdil Fadhil al-Haadiy al-Fadhiliy[1] Kitabu hiki kimekusanya mihadhara mbalimbali ya utamaduni wa jumla aliyoitoa Allammah, Mhutubu, Sheikh Hasan Saffar katika siku za Ijumaa, katika msikiti ulioko al-Qatif, ambao yeye ndiye Imam wa swala ya jamaa humo. Na kabla ya kuzungumzia kitabu na mtunzi wake napenda kuashiria katika yale yanayozungumziwa na ambayo ndio anwani ya kitabu, nayo ni MAZUNGUMZO YA IJUMAA,[2] huu ni mwonekano wa utamaduni wa Kiarabu uliokuwepo tangu mwanzo wa utunzi na uandishi wa Kiarabu, uliendelea kuchukua sura mbalimbali na kubadilika kadiri sababu na mazingira yalivyohitajia mabadiliko hayo. Kwa kweli hali yake ni sawa na hali za aina zingine za utunzi katika mazingira yetu ya utamaduni wa Kiarabu.

Hali hii ndio iliyokuwa inajulikana kwetu kwa jina la IMLA huko mwanzoni mwa ustawi, na jina hili lilitokana na uhalisia wake wa kivitendo ndani ya utamaduni, ambapo mwalimu alikuwa – aghlabu – anaandika mada za imla zake katika kara-tasi, kisha anaziwasilisha kwa wanafunzi wake ambao wamemzunguka pembezoni mwake kandokando ya mimbari

[1] Faqihi na mwanafikra wa Kiislamu kati ya wanachuoni wenye kuchomoza katika sehemu ya Mashariki katika mamlaka ya Saudi Arabia, kati ya waasisi wa harakati za Kiislamu Iraki amesoma katika kitivo cha fiqihi Najaf na chuo kikuu cha Maliki Abdul-Aziz, Jiddah na Chuo Kikuu cha Kiislamu London, na utunzi mwingi katika fiqihi na utamaduni wa Kiislamu baadhi ya vitabu vyake vimechaguliwa kuwa ni mataala wa masomo katika vyuo vingi vya kidini.

[2] Anwani ya kitabu iliyopendekezwa kabla ya kutegemea anwani ya sasa.

yake, na wanafunzi nao wanaandika anayowasomea. Na wakati mwingine mwalimu alikuwa anawasomea kutoka katika maalumati yake, yaani bila ya kutumia karatasi.

Na mada ya imla – mwanzoni – ilikuwa inaishia katika hadithi Tukufu, kisha wanachuoni wakaipanua ikawa inajumuisha elimu ya lugha ya Kiarabu, na fasihi yake, elimu ya sharia ya Kiislamu na hukumu zake, mawaidha na hekima, na aina mbalimbali zingine katika historia ya Kiislamu na mengineyo. Na zilizo mashuhuri zaidi katika imla, ni zile zilizopo katika maktaba zetu za Kiarabu:

- Imla za Abu Ali al-Qaaliy
- Imla za Sharifu al-Murtadhwa
- Imla za Ibnu al-Haajib na Nah'wiyah
- Imla za Abi Saadati Ibnu Shajariy.

Na wakati huo huo, na kwa upande mwingine, hali hii ilikuwa inaitwa Majlisi (kikao), kwa sababu mwanachuoni anawasomea au anahutubia katika kikao cha wakati maalumu, kilichopangwa kwa muda maalumu na sehemu maalumu, na miongoni mwa Majalisi mashuhuri ni:

- *Majalisul-Abrari wa Masalikul-Akhiyaar*, cha Sheikh Ahmad Rumiy, nazo ni Majlisi mia moja katika kusherehesha hadithi mia moja.
- *Majalisu Thaalab an Nah'wiy al- Baswariy*
- *Majalisu Abi Sahli Naubakhatiy*.

Na mada inayotolewa inaweza kupewa majina mawili pamoja, huitwa: Imla na huitwa: Majlisi. kama ilivyo katika yale aliyo-kuwa anayawasilisha Sheikh Suduqu, ambapo yamekuwa yakijulikana kwa jina la Aamaliy Suduqu (Imla za Sheikh Suduqu), na wakati huo huo yakijulikana kwa jina la Majalisu

Suduqu (Vikao vya Sheikh Suduqu), ambapo ni majlisi mia moja. Na imla aghlabu hutolewa misikitini.

Radio zilipoingia katika nchi za Kiarabu na kuanzishwa idhaa za Kiarabu, kulipatikana sambamba na majilisi hizo za misikitini ambazo bado zingalipo hadi leo, vipindi vya idhaa chini ya anwani MAZUNGUMZO. Nayo ni aina ya kuendeleza mwonekano huu wa kiutamaduni. Na walishiriki humo zaidi ya mmoja kati ya Maulamaa wa wakati huo, miongoni mwao ni:

- Dr. Twaha Husein, alikuwa anazungumza kila siku ya Jumatano kwa njia ya Idhaa ya Cairo katika fasihi ya Kiarabu, kisha yakakusanywa mazungumzo yake chini ya anwani MAZUNGUMZO YA JUMATANO, na yakasambazwa katika juzuu tatu, na zikawa ni katika rejea za fasihi ya Kiarabu.

- Dr. Mahmud Mahdiy al-Baswiir, ambaye alikuwa anazungumza katika idhaa mara moja kwa wiki katika fasihi ya Iraki, katika karne ya kumi na tisa, kwa njia ya idhaa ya Baghdad, kisha mazungumzo yake yakakusanywa na yakaitwa *Nahdwatul-Iraq al-Abadiyati Fil-Qarni Tasii Ashara*, na yakasambazwa, na leo ni kati ya rejea muhimu ya fasihi ya Iraki katika karne ya kumi na tisa.

- Na hivi sasa Sheikh Saffar anaongeza katika kazi yake nguvu katika kunyanyua kiwango cha watu wa jamii yake kiutamdani:

- Majlisi zake za Siku ya Jumamosi katika nyumba yake huko Qatif, nayo ni mkusanyiko wa utamaduni.

- Mazungumzo yake ya Siku ya Ijumaa, nayo ndiyo haya yaliyoko mbele ya msomaji mpendwa.

Na lengo la kuwasilisha mazungumzo haya ya kila wiki ni

kuelimisha na kufikisha ujumbe. Kwa sababu ni jukumu la kila mwenye kubeba fikra kunyanyua kiwango cha jamii kiuta-maduni.

Na hitimisho ni kwamba hotuba za Ijumaa na mazungumzo ya kila wiki - sawa yawe yale yanayotolewa Ijumaa au katika siku nyingine kati ya siku za wiki – yana nafasi kubwa katika kuinua kiwango cha uelewa kiutamaduni kwa wanajamii, na kuchangia katika kujenga utu wa mtu kiutamaduni na kuongeza hazina ya maarifa yake kiutamaduni.

Ama tablighi – na nakusudia tablighi ya dini – ni wajibu muhimu sana kati ya wajibu wa mwanachuoni wa kidini na khatibu wa kidini, kwani kwa njia yake anashawishika Mwislamu kihisia juu ya dini yake, na kunyanyuka katika kiwango cha ujumbe wake katika maisha haya.

Na umeshathibitisha uzoefu wa kuelimisha na kutangaza, kwamba mafanikio ya mwenye kufanya hayo yanategemea uwezo wake katika kufungamanisha fikra na uhalisia, na kiwango cha maarifa yake na nafsi za wasikilizaji wake na daraja za uelewa wao kiutamduni. Na haya ndio tunaweza kuyapata - kwa uwazi katika mazungumzo ya kitabu hiki ambacho kipo mbele yetu.

Hakika Sheikh Saffar ni kati ya hao wachache ambao wame-kusanya baina ya ujumbe wa msikitini na mimbari, kwani amehitimu katika Hawza ya elimu baada ya kukamilisha masomo yake ya elimu ya Kiislamu, na akashughulika na nafasi ya mwanachuoni wa dini katika mji wake wa Qatif.

Naye ni kati ya wanaharakati watendaji katika nyanja hii, na hususan wale wachache ambao wanakusanya baina ya asili na

usasa, na amethibitisha hilo katika uwasilishaji wake mbalimbali. Hakika utayaona wazi haya katika utunzi wake na mihadhara yake. Na anahesabiwa kati ya wenye vipaji kwa hotuba zake, kwani yeye anamiliki ala za kuathiri za mimbari, na ana ala za kupenya kwenye akili za wasikilizaji kwa njia ya kuhutubia hisia zao.

Hakika katika mazungumzo yake haya anaisukuma fikra kwa kasi ili kugusa uhalisia wa watu, na kufanya kazi ya kuwa-badilisha kwenda kwenye yaliyo bora zaidi. Inafaa nisirefushe katika maelezo, niache mambo kwa msomaji mpendwa, ili aburudike na mazungumzo haya kwa kusoma, kufahamu na kisha kuelewa ili anufaike kwayo na kuwanufaisha wengine.

Mwenyezi Mungu azibariki juhudi za ndugu yetu Saffar na ampe elimu zaidi katika huduma hii ya kheri. Hakika Yeye ni Mwenye kutoa taufiki na ndiye Mwenye kukusudiwa.

**Abdul-Haadiy al-Fadhwily**.

# SEHEMU YA KWANZA

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu**
**Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu**

ادعُ إِلىٰ سَبيلِ رَبِّكَ بِالحِكمَةِ وَالمَوعِظَةِ الحَسَنَةِ وَجٰدِلهُم بِالَّتى هِىَ أَحسَنُ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبيلِهِ وَهُوَ أَعلَمُ بِالمُهتَدينَ

**"Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola Wako ndiye anayemjua zaidi aliyepotea njia yake na Yeye ndiye anayewajua zaidi walioongoka." (Sura An-Nahl; 16:125).**

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu. Ewe Mwenyezi Mungu mteremshie rehema Muhammad hitimisho la Manabii na ukamilisho wa idadi ya Mitume, na Ahali zake wema watwaharifu na Masahaba wake wema.

بسم الله الرحمن الرحيم

# MAZUNGUMZO YA KWANZA

Mazungumzo ya kidini yanabeba jukumu kubwa mbele ya mazingira ambayo jamii ya Kiislamu inaishi. Hiyo ni kwa sababu yana fursa kubwa katika kuathiri na kupenyeza, na yana nafasi kubwa na kiwango cha juu katika kukubalika na kuitikiwa. Ambapo watu wenye kushikamana na dini wanayasikiliza kwa usikivu na unyenyekevu, kama sehemu ya faradhi za ibada na

shughuli za kidini, kama hali ilivyo katika Swala ya Ijumaa ambayo inatanguliwa na hotuba mbili, na Swala ya Idd ambayo inafuatiwa na hotuba mbili. Ukiongezea na minasaba mingine ya kidini ambayo inakusanya humo waumini wenye kusikiliza kwa masikio yao na wenye kuhamasika kwa nyoyo zao na hisia zao, kwa yale yanayotolewa kwao miongoni mwa mawaidha na miongozo.

Lakini angalizo ni kwamba harakati za kuathiri kwa mazungumzo ya kidini katika hali ya jamii ni ndogo kuliko inavyotarajiwa, ukilinganisha na nguvu ya kimaanawi inayomiliki na uwezekano uliopo wa kupenya katika nafsi, na kwa kuangalia hali ya hatari na mazingira nyeti unayoishi nayo umma.

Umma unakabiliana na changamoto kubwa katika hali yake ya ndani, na katika upande wa nje, na inatakiwa mazungumzo ya kidini yaamshe nguvu za umma na kusheheni nguvu zake na uwezo wake ili kukabiliana na changamoto hizo za kimaisha.

Wakati ambapo sehemu ya kubwa ya hotuba na mazungumzo haina uelewa wa changamoto hizi, na wala haioni kuwa inalengwa katika kukabiliana nazo, na badala ya kuwa ni mhamasishaji wa kuzinduka, aghlabu unafanya kazi ya kuimarisha hali ya kurejea nyuma, kwa kuweka mkazo katika mas’ala binafsi ya kiibada, na kukuza vipengele na ufafanuzi katika nyanja za kiitikadi kwa kueneza ikhitilafu, na kushughulika na uchochezi na hamasa za kimadhehebu na makundi. Wakati ambapo mhutubu anasahau mazungumzo kuhusu jukumu la mwanadamu katika kujenga ulimwengu, na yanayomlazimu kati ya juhudi na harakati katika kujua mbinu za maisha na kanuni za mazingira, na anaghafilika kukumbuka nafasi ya umma katika kumshuhudia mwanachuoni, na kutoa mfano wa kisasa

ulio bora, na kusahau maadili ya msingi katika dini kama vile umoja, uhuru, uadilifu na haki za binadamu. Hii ni kwa upande wa malengo.

Ama kuhusu kiwango cha muundo na mbinu za kueleza, aghlabu mazungumzo haya yanatumia njia ya mawaidha ya kuiga, na kutosheka na kusoma nususi za kurithi na ushahidi wa kihistoria bila ya kunufaika na ustawi wa elimu ya binadamu kama vile elimu ya nafsi na elimu ya jamii, na bila ya kutegemea lugha ya takwimu na taarifa za kitafiti, njia ya udadisi, ubainifu na utafiti wa kimedani jambo ambalo linaifanya lugha ya mazungumzo kuwa ni insha ya kukariri katika hali ya kaida na mifano.

Na tunapoangalia kwa jicho la mazingatio yale mazungumzo yaliyo katika ushindani wenye nguvu na mkali, katika upande wa mazungumzo mengine ambayo yanamiliki nguvu zaidi, uwezo na uzoefu wa kielimu, teknolojia na fani, hakika hilo linaweka wazi kwetu sababu ya udhaifu na ufinyu wa kuathiri.

Kwa hakika wasifu huu unalingana na sehemu kubwa ya mazungumzo ya kidini, lakini sasa hivi kuna mifano yenye kuchanua katika medani ya Kiislamu. Inatoa mazumgumzo yenye uelewa na yaliyofunguka, ambayo athari zake zinaonekana bayana na matokeo yake mazuri yanadhihiri katika kuanzisha harakati za kubadilisha medani ya Kiislamu tukufu, na katika uwepo wa kundi la ujumbe la kiimani kwa ajili ya kuhuisha maadili ya kimsingi na kulinda hali ya umma katika msingi wake.

Hakika mabadiliko ya mazungumzo ya kidini ili yawe katika kiwango cha maadili ya kidini yenye kutukuka na ili yatatue changamoto za kileo zinazobana, na ili yaweze kuamsha umma, kuna haja ya kushirikiana na kuongeza juhudi kutoka kwa Marajii na viongozi wa kidini, na sehemu zenye uelewa wenye

kujali mustakabali wa dini na umma kwa ajili ya kuweka mbinu za miundo ya jumla.

Na kila jamii inaweza kuhitaji mahitaji yake binafsi kutokana na baadhi ya hali zake na mazingira yake, na hivyo kuwataka wahusika wenye kujitolea humo kwa ajili ya mambo ya kidini kuboresha fikra zaidi, na kufikia mikakati iliyofanyiwa utafiti, ili kuelekeza mazungumzo katika mazingira yao, kwa kutoa kipaumbele chake na mbinu zake.

Na ili yatimie matarajio haya hakika ni juu ya mwenye jukumu katika medani ya maelekezo ya kidini ajitahidi katika kuboresha kiwango cha utekelezaji wake, na aanzie katika sehemu ya kuhisi majukumu katika dini na jamii, na ajue kwa kina changamoto za kileo ili yainuke mazungumzo yake na yapande daraja hadi kwenye upeo unaotakiwa na unaofaa.

Na mazungumzo haya ambayo yako mbele ya msomaji, hakika ni tajriba ndogo katika njia hii. Nilikuwa nazingatia kugusa matatizo ya jamii na mambo yake, na kujitahidi katika kutoa yale ambayo yanaweza kuchangia katika kutatua na kutibu, nikienda mbio kuboresha malengo ya mazungumzo na njia zake, kulingana na uwezo wangu na nguvu zangu ndogo.

Niliyatoa mazungumzo haya kupitia mimbari ya Ijumaa katika msikiti wa al-Fatih Qatif, mwaka 1420 hijiria, na nilikuwa naandika kila mazungumzo baada ya kuyatoa ili wayapate ndugu zangu waumini, na huenda baadhi ya ndugu watukufu wamenisaidia kuandika baadhi yake kutoka kwenye kanda zilizorekodiwa.

Na leo ninapotoa mkusanyiko huu katika kitabu hiki natarajia yapatikane humo ambayo yanamnufaisha msomaji na kuchangia katika kuboresha uzoefu baina ya wenye kuzingatia jambo la mazungumzo ya kidini.

Kama ambavyo hainipiti kuwashukuru ndugu zangu watukufu ambao walishiriki pamoja nami katika kuzitoa juhudi hizi, na hususan ustadhi Dhakir Habil, Ustadhi Mirza al-Khuwailidiy, ambao mara nyingi nimesaidiana nao katika kuandaa mazungumzo na kuhakiki maalumati. Na vilevile Sheikh Husein Suwaileh ambaye amesimamia uchapishaji mazungumzo haya na kuyasambaza, na pia ndugu wengine, Mwenyezi Mungu awalipe wote malipo mema.

Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu aikubali juhudi hii ndogo na ajaalie humo manufaa na faida na atupe taufiq sote ya kuitumikia dini na umma. Hakika Yeye ndiye mwenye kutoa taufiki, na sifa zote njema anastahiki Mola Mlezi wa walimwengu.

**Hasan Saffar**
**10/3/1422 Hijiria - 2/6/2001.**

بسم الله الرحمن الرحيم

## KATIKA MAISHA YA FAMILIA YENYE MAFANIKIO

Riwaya za kihistoria zinatofautiana kuhusu mwaka wa kuzaliwa Bibi Fatimah Zahra عليها السلام, ilikuwa ni kabla ya utume wa Nabii kwa miaka mitano kama wanavyopokea wengi wa Maulamaa wa Kisunni? Au ni baada ya utume kwa miaka mitano kama wanavyoona Maulamaa wa Kishia? Lakini takriban zinaafikiana katika siku na mwezi, ambapo riwaya nyingi zinasema kwamba kuzaliwa kwake ilikuwa ni tarehe 20 ya mwezi wa Jumadul-Akhir.

Na sisi tunaweza kufikiria kiwango cha furaha ambayo ilijaa moyo wa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم kwa uzao wa binti yake Zahra عليها السلام.

**Kwanza:** Kwa ukamilifu wa ubinadamu wake na kina cha hisia zake, ni lazima afurahie kwa kuzaliwa mtu mpya katika familia yake.

**Pili:** Kwa yale ambayo Mwenyezi Mungu amemweleza kupitia wahyi miongoni mwa fadhila za mtoto huyu na nafasi yake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kwamba mwendelezo wa ukoo na kizazi chake kitukufu utapatikana kupitia kwake.

**Tatu:** Kwa kuakisi ukarimu wake katika uhai wake na ujio wake mtukufu.

Anasema Dr. Muhammad Abduh Yamaniy:

Na Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alifurahia kuzaliwa kwake na akamwambia mke wake Khadija: "Ewe Khadija hakika ni mtoto twahara aliyebarikiwa, na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu atajaalia kizazi changu kwake." Na kwa sababu hii alikuwa ni mahala pa

mazingatio ya baba yake na husasan kwamba alikuwa anafanana naye. Amepokea al-Hakim katika *Mustadrak* kwa sanadi yake kutoka kwa Anas bin Maliki رضي الله عنه kwamba alisema:

"Alikuwa ni mtu anayefanana sana na Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم, mweupe anaelemea kwenye wekundu na ana nywele nyeusi."

Na kutoka kwa Ummul-Muuminin Ummu Salama رضي الله عنها amesema: "Fatimah binti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم alikuwa ni mtu anayefanana sana kwa uso na Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم."

Kutoka kwa Aisha Ummul-Muuminina رضي الله عنها hakika amesema: "Sijaona yeyote katika viumbe vya Mwenyezi Mungu anaye-fanana sana kwa mazungumzo na maneno na Mtume wa Mwenyezi Mungu kama Fatimah."

Mwenyezi Mungu amridhie na amridhishe. Ilikuwa ni mbegu twahara, na mtoto mkarimu mwema. Bibi mtukufu anayefanana sana na Bwana wa viumbe, na alirithi utukufu kutoka kila pande na akapata utukufu.[3]

Katika kukumbuka uzao wake mtukufu tunataka kudondoa katika uongofu wa sira yake tukufu yale ambayo yanatuangazia njia ya maisha. Hiyo ni kwa sababu tutajaribu kudondoa sura yenye kuchanua katika upande wa maisha yake ya kifamilia ili tupate kutoka kwake somo na mazingatio, na ili tuendeshe maisha yetu ya kifamilia katika uongofu wake.

Hakika familia ndio bembea la kwanza katika malezi ya binadamu, na inabakia kuwa ni ngao yake na kinga yake ambayo inamhami na ambayo anarejea kwayo anapokabiliwa na chamgamoto yoyote au tatizo lolote katika maisha yake. Na kila

[3] Yaani: ni Muhammad Abduh, *Innahaa Fatwimah Zaharaa*, uk: 15 chapa ya kwanza 1996 Darul al- Manaar-Muasasatu ululm- Qur'ani Dimishiq.

yanapokuwa mafungamano ya mwanadamu na familia yake ni yenye nguvu na imara ndivyo anavyoweza kuathari katika mazingira yake, na maadili yake yanakuwa ni yenye nguvu zaidi vile vile. Katika familia hii mtoto anajifunza lugha, anajifunza tabia na mwendo, nayo ndio inatengeneza njia ya ulinzi wa kwanza katika shakhsiya ya mwanadamu na matatizo yake, na Qur'ani tukufu inatia mkazo mazingatio makubwa katika familia wakati muumini anapoomba kwa Mola Wake kumpa familia itakayokuwa ni kitulizo chake.

**"..... رَبَّنا هَب لَنا مِن أَزوٰجِنا وَذُرِّيّٰتِنا قُرَّةَ أَعيُنٍ وَاجعَلنا لِلمُتَّقينَ إِمامًا"**

**".....Mola Wetu! Tupe katika wake zetu na wanetu yaburudishayo macho, na utujaalie tuwe waongozi kwa wenye takua." (Sura al-Furqan; 25:74.)**

Na kuomba kitu kunaakisi raghaba katika kupatikana kwake, na kwenda mbio kwa ajili ya kukipata pamoja na kuomba taufiki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya hilo, na msaada Wake katika hilo katika kuondoa vizuizi na vikwazo.

(Kiburudisho cha jicho) ama imechukuliwa kwenye neno: (*qara*) kwa maana ya baridi kwa sababu jicho katika hali ya sururi na furaha linatoka machozi ya baridi, na maana inakuwa: Tujaalie ni wenye sururi wenye kufurahia katika familia zetu hadi tupate humo machozi ya furaha ya baridi kutoka katika macho yetu. Hakika ni kinaya nzuri.

Na ama imechukuliwa katika (*qara*) kwa maana amethibiti na ametulia. Hiyo ni kwa sababu mwanadamu anapotafuta mtu au kitu anageuka kulia na kushoto, na anapopata anachotaka linatulia jicho lake, yaani anaacha kugeuka na kutafuta kwa macho yake, na maana inakuwa: Jaalia nafsi zetu ziwe na utulivu zenye furaha katika hali yetu ya kifamilia ili tusitafute raha wala utulivu katika sehemu nyingine.

Lakini ni mambo yapi yanayosaidia familia kuwa ni kitulizo cha jicho kwa mume na mke? Tukiangalia maisha ya kifamilia ya Bibi Fatimah Zahra tutakuta ni tajriba nzuri, njema kwa ajili ya kuiga na mfano. Yeye ni mfano kamili ambao Uislamu umeutoa kwetu ili tumfuate ili tufikie lengo hili tukufu.

Namna gani yalikuwa maisha ya kifamilia ya Bibi Fatimah عليها السلام na mume wake Imamu Amirul-Muuminina عليه السلام?

**Kisimamo katika Hadithi ya Kisai:**

Inafaa sana tukitaka kupata sura ya familia hiyo tukufu tupate funzo katika tukio mashuhuri lililotokea katika nyumba ya Zahra na nyumba ya Amirul-Muuminina na limepokewa na vitabu vyote vya Waislamu, nalo ni kisa cha Hadithi ya Kisai, ambayo imepokewa katika rejea nyingi, isipokuwa ni kwamba rejea za Ahlulbayti عليهم السلام zimelipokea kwa kirefu kwa shauku yenye manufaa.

Na Alhamdulilahi hivi karibuni imetoka fasili nzuri kwa kirefu ya Hadithi ya Kisai na imenyambua hukumu na adabu na makusudio ya ibara zake kwa utunzi wa Marjaa wa dini Imamu Sayyid Muhammad Shiraziy. Fasili hiyo ina kurasa 320 kwa anwani ya *Min Fiqhi Zahra*.

Ukiachilia mbali kwamba hadithi hii inabainisha nafasi ya kizazi kitukufu, pia inawezekana ikawa moja ya sababu iliyopelekea Ahlulbayt عليهم السلام kuwahimiza wafuasi wao kusoma hadithi hiyo ya Kisai na kuisambaza ni kwa sababu hadithi hiyo inanukuu sura ya uhusiano na muamala ndani ya familia tukufu ya Nabii, ambapo tunasoma humo kwamba kila mwanafamilia anapoingia nyumbani anaanza kwa kuwasalimia watu wake. Mtukufu Mtume صلى الله عليه وآله وسلم anaingia kwa binti yake Zahra, anaanza kwa salamu, na Imam Hasan, naye ni mtoto mdogo anaingia nyumbani anamsalimia mama yake Zahra, na vilevile alifanya hivyo ndugu yake Imamu Husein mdogo kuliko wote alipoingia baada yake,

na vilevile baba yao alipoingia nyumbani anaanza kumsalimia mke wake Zahra عليها السلام.

Kama ambavyo tunasoma katika Hadithi ya Kisai heshima baina ya wanafamilia ambapo Hasan anaomba ruhusa kwa baba yake Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم ili aingie pamoja naye katika shuka, na vivyo hivyo alifanya ndugu yake Husein na baba yao Ali na mama yao Zahra عليها السلام.

Katika Hadithi ya Kisai tunasoma kila mmoja katika wanafamilia kutangaza kwake upendo wake na shukrani zake kwa mwanafamilia mwingine, na kuthibitisha umahususi wake ambapo Bibi Fatimah عليها السلام anawasemesha watoto wake wote kwa kauli yake: "Ewe mwanangu mpendwa na kiburudisho cha jicho langu na tunda la moyo wangu." Na Husein عليه السلام anamsemesha babu yake kwa kusema: "Amani iwe juu yako ewe babu yangu, ewe Mteule wa Mwenyezi Mungu." Na Imamu Ali anamsalimia mke wake Zahra عليها السلام kwa kusema: "Amani iwe juu yako ewe binti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu." Naye anamjibu: "Amani iwe juu yako ewe baba Hasan na ewe Amirul-Muuminina." na maneno mengine mengi yaliyopokewa katika Hadithi ya Kisai yanayoelezea upendo wa kila mmoja kwa mwingine na kuheshimu kwake shakhsiya yake.

Na katika Hadithi ya Kisai tunaona thamani ya kukutana na vikao vya familia vya upendo, ambavyo vinajaza nyoyo za wanafamilia mahaba, upole, heshima na kutoa fursa kwao ya kubadilishana hisia na fikra na kuzidisha ushirikiano na mshikamano wa familia. Na imepokewa katika hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم kwamba alisema: "Mtu kukaa na familia yake kunapendeza kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kuliko kukaa itikafu katika misikiti hii miwili."[4]

[4] Raishahary: al-Mahdiy, *Mizanil-Hikimah*, Juz. 4, uk: 287

Wakati ambapo familia nyingi katika baadhi ya jamii zetu zinakosa mazingira ya huruma na upole, ambapo mwanaume yuko katika ulimwengu wake maalumu na mambo yake maalumu, na mke vilevile. Mwanamke na watoto wanamaliza wakati wao mwingi kwenye runinga na kompyuta au pamoja na marafiki zao nje ya familia.

Hakika hali ya kutangamana na upendo katika familia inakuza katika nafsi ya mwanadamu kujiamini, utulivu, uadilifu na muamala mzuri pamoja na wengine, wakati ambapo mazingira ya familia yenye mkanganyiko yanazalisha mtikisiko katika shakhsiya ya mwanadamu na kupanda katika nafsi yake chuki mbalimbali.

**Kuchunga haki ndani ya familia:**

Na sura hii inayowasilishwa na Hadithi ya Kisai na inayonukuliwa na historia katika sira ya Ahlulbayt عليهم السلام, hakika ni utekelezaji wa kivitendo wa mafunzo ya Uislamu na adabu zake katika mazingira ya familia. Mwanadamu ndani ya familia yake mume au mke, au mtoto au mzazi, wote wana haki na adabu za kupokezana, hapati ridhaa ya Mola wake wala maisha yake hayawi mazuri ya kifamilia isipokuwa kwa kuzichunga na kushikamana nazo.

Na cha ajabu ni kwamba baadhi ya watu wanaona nafsi zao zina haki kutoka kwa wengine kutoka nje ya familia yake, lakini yeye anadharau na anapuuza katika kuamiliana pamoja na familia yake na watu wake walio karibu naye. Haheshimu haki zao, bali anaruhusu katika nafsi yake kuwafanyia uadui, pamoja na kwamba Qur'ani tukufu inatia mkazo katika kujilazimisha sana katika kufanya uhusiano mzuri na familia, na inazingatia kuwa ni usadikishaji wa sharia ya Mwenyezi Mungu. Hilo limedokezwa katika sehemu kumi na tatu katika Qur'ani tukufu. Kumi kati yake katika nyanja ya mahusiano ya kifamilia, kama ilivyo katika

Suratul-Baqarah, aya ya 230, na katika Surat Nisaa aya ya 13, na katika Surat al-Mujadala aya ya 4, na Surat Twalaqa aya ya 1.

Na tunasoma katika hadithi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ nususi nyingi ambazo zinatilia mkazo suala la kuheshimu na kuchunga haki za ndoa. Imepokewa kutoka kwake ﷺ: "Mke mwenye kumuudhi mume wake, Mwenyezi Mungu hatokubali swala zake wala jema katika amali yake hadi amsaidie na amridhishe hata kama atafunga maisha. Na mwanamume naye ana mfano wa dhambi na adhabu hiyo, ikiwa atamuudhi na kumdhulumu mkewe."[5]

Kana kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anataka kuwaambia watu kwamba hakika swala na saumu ni kuamiliana pamoja na muumba, lakini Mwenyezi Mungu hakubali muamala huu pamoja naye, maadamu muamala wako pamoja na viumbe hauko ndani ya mpaka na kanuni za kisharia zilizowekwa. Na miongoni mwa watu wa karibu zaidi kwa mke ni mume wake na vilevile kinyume chake.

Na katika riwaya nyingine kutoka kwa Imamu al-Baqir عليه السلام nayo ni muhimu katika nyanja hii, anasema Imamu عليه السلام: "Hakuna uombezi kwa mwanamke mwenye kufaulu kwa Mola Wake kuliko ridhaa ya mume wake." Na alipofariki Fatimah عليها السلام alisimama kwake Amirul-Muuminina عليه السلام akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi niko radhi na binti wa Nabii Wako."[6]

Na tunanufaika na riwaya hii kwamba ikiwa Zahra عليها السلام anahitajia ridhaa ya mume wake juu yake naye ni binti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na Bibi wa wanawake wa watu wapeponi, hakika mwanamke mwingine yeyote anahijia zaidi hayo. Hakika

[5] Al-Huru al-Amiliy: Muhammad bin al-Hasan, *Wasailus-Shi'ah* Juz. 20, uk: 165 hadithi namba 25315
[6] Al-Majiisiy: Muhammad Baaqir, katika *Biharul- Anuwar*, Juz. 100, uk: 256

sisi tuna haja ya kutilia mkazo juu ya haki za mke zaidi kuliko haki za mume, hiyo ni kwa sababu mume kwa tabia yake anahisi nguvu na kwamba yuko juu na ni mtawala kwa mke wake, ambapo ana haki za usimamizi… ama mke hayuko hivyo, hivyo Mtume ﷺ anasema: “Jibril hakuacha kuniusia juu ya mwanamke hadi nikadhani kwamba haipasi kumwacha.”[7]

Baadhi ya wanaume wanayapuuza maelekezo yote haya, na mtu anavunja haki za mke wake na anamkalifisha zaidi ya wajibu wake. Na anaamiliana pamoja naye kama mwajiriwa katika nyumba yake, na anaona kwamba yeye ni mwenye jukumu hata la kumhudumia yeye binafsi katika chakula chake, mavazi yake na makazi yake, na uhakika ni kwamba mke kumhudumia mume wake sio wajibu, bali ni jambo la mazoea tu na ni mustahabu kisharia na sio zaidi ya hapo.

Na mwanamke akimhudumia mume wake hakika hilo ni jambo jema (hapana njia ya kuwalaumu wanaofanya wema), hivyo haijuzu kumkemea au kumpiga au kumdhalilisha anapoacha kufanya hivyo, kwa sababu sio wajibu juu yake aslani. Hakika mafunzo ya Kiislamu yanashajiisha mume kumhudumia mke wake, hivyo kuhudumiana iwe ni kwa kubadilishana kama hali ilivyo katika kusaidiana. Katika riwaya kutoka kwa Nabii ﷺ amesema: “Mume akimnywesha mke wake maji anapata malipo.”[8] Na katika hadithi nyingine: “Hakika mwanaume analipwa anapomlisha mke wake tonge.”[9] Na kuna riwaya nyingi na hadithi ambazo zinashajiisha mume kumhudumia mke wake hususan, na familia yake kwa ujumla.

Na kwa hiyo anasema Mtukufu Mtume ﷺ: “Mbora wenu ni

[7] Al-Majilisiy: Muhammad Baaqir katika *Biharul- Anuwar*, Juz. 100, uk: 253

[8] Al-Hindiy: Ali al- Mutaqiy, katika *Kanzul-Umaal*, Juz. 6, uk: 275, hadithi namba 444435

[9] Al-Kaashaaniy: al- Maula Muhsin, katika *al-Mahajatul-baidhaa*, Juz. 3, uk: 70

yule aliye mwema zaidi kwa ahali yake, na mimi ni mwema kwa ahali zangu.” Na alipoulizwa Ummul-Muuminina Aisha mke wa Mtume ﷺ kuhusu tabia ya muamala wa Mtume ﷺ pamoja ahali yake, alisema: “Alikuwa anashona kiatu chake, anashona nguo yake na anafanya kazi katika nyumba anayoifanya mmoja wenu katika nyumba yake. Alikuwa anawatumikia ahali zake, unapowadia wakati wa swala anasimama kwenda kuswali.”[10]

Anasema Amirul-Muuminina عليه السلام: “Mke wako asiwe ni kiumbe muovu zaidi kwako.”[11] Baadhi ya watu wanajitolea kuwatumikia wengine katika hafla za watu wengine, lakini hayuko tayari kumtumikia mke wake, anawatumikia wageni katika nyumba yake lakini anakataa kuihudumia familia yake.

Maisha ya Ali na Zahra عليهما السلام ni kielelezo dhahiri na kinachoonekana katika mafunzo, na ni maelekezo hayo ambayo yanafanya maisha ya kifamilia kuwa ni maisha yenye mafanikio bila ya kikomo. Naye kiongozi wa waumini عليه السلام anafafanua heshima yake na uchungaji wake katika haki za mke wake Zahra عليها السلام katika maneno yake yafuatayo: “Wallahi sijamkasirisha wala sijamchukiza katika jambo hadi Mwenyezi Mungu Mtukufu alipochukua roho yake. Wala hajanikasirisha wala hajaniasi kwa jambo. Nilikuwa ninapomwangalia zinaondoka taabu na huzuni.”[12] Imamu Ali عليه السلام hakuvuka mpaka wala Bibi Fatimah عليها السلام hakuzembea.

Na kwa upande mwingine Bibi Fatimah عليها السلام yeye pia amesisitiza hayo katika wasia wake maarufu kabla ya kufariki kwake ambapo amesema: “Ewe mtoto wa Ami yangu, hujanikuta ni

---

[10] Tirimidhiy katika *Auswafu Nabiyi*, chapa ya Daru al-Jiiyl Beirut, na taaliq na Samihu Abbasi uk: 276

[11] Al-Musawiy: Saharifu Ridhaa katika *Nahjul-Balaghah*, barua ya 31

[12] Al-Qazuwiniy: Muhammad Kaadhim, katika *Fatimatuz-Zaharaa minal-Mahdiy ilaa al-Laha* chapa ya kwanza 1991 Musasatu Nur lilimatubuat – Beirut uk: 142.

muongo wala mwenye hiyana wala sijakukhalifu tangu umeishi na mimi." Na Ali عليه السلام anamjibu papo hapo "Najilinda kwa Mwenyezi Mungu, wewe unamjua mno Mwenyezi Mungu, wewe ni mwema na mchamungu, ni mkarimu na unamuogopa sana Mwenyezi Mungu, huwezi kunikhalifu."[13]

Na katika mnasaba huu mtukufu nao ni kukumbuka uzao wa Zahra عليها السلام inapasa kwetu kusoma maisha ya familia hiyo ambayo iliishi katika nyumba ya Bibi Fatimah عليها السلام na kuzitaka nafsi zetu kubeba majukumu yake kikamilifu katika hayo, na kila upande usitupie majukumu kwa mwingine, na uiepushe nafsi yake na uzembe.

Ni wajibu wetu tufanye kwa maelekezo ya Uislamu katika uhusiano wetu wa kifamilia na kuwaiga Ahlulbayt ili Mwenyezi Mungu atujibu dua zetu tunaposema: "Mola Wetu, tupe katika wake zetu na wenetu kiburudisho cha jicho."

**Mafanikio katika mahusiano ya kijamii:**

Mwanadamu katika mahusiano yake na muamala wake pamoja na watu anakabiliwa na mtihani wa daima. Yeye kwa upande mmoja anakabiliwa na mawimbi mbalimbali na hali tofauti tofauti, na katika upande mwingine anahitajia muamala wa kubadilishana na kupeana pamoja nao, na ili awe ni mtu mwenye kufaulu katika muamala huu inapasa amiliki kifua kipana na nafsi yenye usamehevu.

Kanuni za kuamiliana na mwanadamu zinatofautina na zile za kuamiliana na mazingira, ambapo kanuni za mazingira ni thabiti, wakati ambapo binadamu wana hali mbalimbali, na akili zenye kutofautiana, na maslahi mbalimbali. Na zaidi ya haya hakika tabia ya mtu mmoja sio thabiti daima bali inabadilika kwa kubadilika hali na mazingira ambayo yanamzunguka, jambo

[13] Rejea iliyotangulia uk: 425

ambalo linaongeza ugumu mwingine juu ya ugumu uliopo. Unaweza kukutana na mtu siku moja na humo anakuwa ni mwenye furaha, sururi na bashasha, kisha unakutana naye siku nyingine, unakuta yuko kinyume kabisa.

Na sio sahihi mwanadamu kutupia lawama katika matatizo ya kuamiliana na wengine, na kuizingatia kuwa nafsi yake haina hatia katika kila kasoro, au kuona kasoro na aibu za wengine tu. Sio sahihi kusema hakika watu hawamwelewi wala hawamheshimu, na kwamba wao hawafai kuheshimiwa na kutukuzwa. Na hakika wao kama wangekuwa hivyo muamala wake pamoja nao ungekuwa bora zaidi, na kama wangekuwa kama fulani na fulani, ningefaulu pamoja nao.

Na ukweli ni kwamba watu hawawezi kuwa kama anavyotamani na anavyotaka kila mtu. Je, anadhani kwamba Mwenyezi Mungu anaumba kiumbe kulingana na matakwa yake na raghaba yake yeye? Je, watu ni vazi unalikunjua kulingana na utashi wako ili ulivae, au ni chombo unataka kukitumia na kutoa kipimo chake kwa fundi anapokutengenezea? Hakika watu hao ni watu, katika kila sehemu utakapowaendea watabakia hivyo.

Mwenyezi Mungu hajamuumba yeyote katika viumbe Vyake hata Manabii Wake na Mitume Wake, kumuumbia watu wenye sifa maalumu ili afaulu katika muamala wake pamoja nao. Namna gani mwanadamu atafaulu katika muamala wake pamoja na watu pamoja na kutofautiana nafsi zao? Haya ndiyo ambayo aya ya 63 katika Suratu Furaqan imeyajibu ambapo anasema (swt):

وَعِبَادُ الرَّحْمَٰنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا

**"Waja wa Mwingi wa rehema ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu. Na wajinga**

**wakiwasemesha, husema: 'Salama.'" (Surat Al-Furqan; 25:63).**

Ambapo aya inatia mkazo kwamba (waja wa Mwenyezi Mungu) ni wale ambao wananyenyekea katika amri Zake na makatazo Yake. Wanasifika kwa sifa muhimu zinazosaidia katika kufanikisha uhusiano pamoja na wengine na kuwaathiri juu yake. Na sifa hii ni kwamba wao (wanatembea katika ardhi kwa unyenyekevu) na wala hawatembei kwa kiburi na ubabe, na kwamba wao hawaangalii nafsi zao kwa kujitofautisha na wengine, wala hawahisi kwamba wao ni wa daraja la juu kuliko watu wengine.

Na nafsi hii yenye kiburi haiwezi ikafaulu katika muamala pamoja na mtu mwingine, kwa sababu msingi muhimu wa kufaulu ni mwanadamu awe anaweza kunyanyuka katika daraja la kivitendo, na mwenye kuweza kudhibiti nafsi mbele ya athari za mchemko. Na atawezaje mwenye kiburi kufikia katika kiwango hiki? Hapana, hawezi. Kisha aya tukufu inasema: "Na wajinga wakiwasemesha, husema Salama." Na wajinga sio lazima wawe katika tabaka la wasiosoma au wasioelimika, bali wanaweza kuwa ni watu waliosoma na wanachuoni waliobobea, isipokuwa wao ni wajinga katika namna ya kuamiliana pamoja na wengine, na wao sio lazima wawe wadogo kwa umri bali wanaweza kuwa ni wakubwa kwa umri ila miamala yao ni ya kitoto.

Wale ambao ni katika waja wa Mwenyezi Mungu wenye uelewa hawakubali uchochezi wa wajinga bali majibu yao yanakuwa kama inavyotia mkazo aya (amani). Na amani hapa inamaanisha heri, yaani huu ni wakati wa kuagana baina yetu, yaani hakika sisi hatutowakubalia kusimama katika kila kitendo cha kijahili mnachokifanya, bali tunaendelea nayo na kupita kwa amani, kama inavyoashiria aya nyingine ambapo anasema (swt):

**"وَإِذا مَرّوا بِاللَّغوِ مَرّوا كِرامًا ....."**

**"…..Na wanapopita kwenye upuuzi hupita kwa heshima zao" (Surat Al-Furqan; 25:72)**

Na katika aya nyingine:

وَإِذا سَمِعُوا اللَّغوَ أَعرَضوا عَنهُ وَقالوا لَنا أَعمٰلُنا وَلَكُم أَعمٰلُكُم سَلٰمٌ عَلَيكُم لا نَبتَغِى الجٰهِلينَ .

**"Na wanaposikia upuuzi hujitenga nao na husema: Sisi tuna vitendo vyetu na nyinyi mna vitendo vyenu: Salaamun alaykum! Hatuwataki wajinga." (Surat Al-Qasas; 28:55.)**

Haifai kwao kujibu kila jambo la kijahili, bali wao wako juu na wametukuka, na wao wanaondoka kwenda kwenye majukumu yao na kazi zao nzuri za msingi. Hawashughulishwi na uongo na ugomvi wa pembezoni.

Na hizi ndio sifa ambazo zinasifika nazo shakhsiya zilizofaulu katika muamala pamoja na wengine. Na Imamu Ali bin Husein عليه السلام anatupa mfano wa shakhsiya hizo: Ilitokea kwamba mwovu alimfanyia uovu akamtukana lakini yeye عليه السلام hakukunja uso wake mbele yake. Muovu akakasirika na akawa anasema: "Nakukusudia wewe." Imamu akasema haraka: "Nami naku-puuza." Imamu akamwacha na akaondoka.[14]

Na siku moja alitoka msikitini na mara mtu akamtukana. Watu wakafanya haraka kutaka kumpiga, lakini yeye akawakataza hayo, na akamwelekea kwa kusema: "Aliyoyasitiri Mwenyezi Mungu kwako ni mengi je, una shida tukusaidie?" Mtu yule akaona aibu na akatamani ardhi immeze. Imamu alipomwangalia akamhurumia akamtupia nguo iliyokuwa juu yake na akaamuru apewe dirhamu elfu moja.[15]

[14] Al-Qarashiy: Baaqir, katika al-Imamu Zainul-Abidin juzuu 1 uk: 77, chapa ya kwanza 1988 Darul- Adhuwaai Beirut
[15] Rejea iliyotangulia

Haya ndio matendo ya shakhsiya tukufu. Wakati unakuta baadhi ya watu wanakasirika hata kwa maneno ambayo yananukuliwa kwao kutoka kwa watu wengine pamoja na kwamba kunukuu kunaweza kusiwe sahihi.

Inanukuliwa kutoka kwa Sheikh Akhundiy Muhammad Kadhim al-Khurasaniy ﵀ kwamba alikuwa ni kilele katika muamala wake na maadui zake na alikuwa anazingatia hususan kurejesha ubaya kwa wema.

Siku moja aliingia kwake mmoja wa makhatibu maarufu kati ya waliokuwa wanampinga Sheikh Akhundiy kwa kuongoza kwake harakati yenye masharti, ambayo ilimtaka Mfalme al-Qajaariy wa Iran kutunga katiba ya nchi na kuanzisha bunge, na khatibu huyo alikuwa amejiunga na kundi lingine lililokuwa linaitwa *al-Mustabiddah*, linataka hali ibaki kama ilivyo, kwa kuogopa kuingia kanuni zisizokuwa za Kiislamu katika katiba, au kupenya watu kutoka nje ya mazingira ya kidini katika bunge. Na kwa kuwepo hali hii ya ikhitilafu, mara nyingi khatibu huyo alimzungumza Sheikh al-Akhundiy juu ya mimbari kwa kumkosoa na kushutumu msimamo wake. Na kudra ya Mwenyezi Mungu ikataka khatibu huyu auze nyumba yake ili alipe deni lake, mnunuzi akamwambia: "Kama al-Akhundiy atatia saini katika mkataba wa nyumba yako nitainunua, vinginevyo hapana."

Akaja Najaf akakutana na Sheikh al-Akhundiy, na Sheikh akamheshimu sana na akamkalisha mbele ya majilisi na akaelezea furaha yake kwa kukutana naye. Khatibu akamwambia: "Naomba usaini mkataba huu ili niweze kuuza nyumba yangu." Sheikh akachukua mkataba kisha baada ya muda Sheikh akatoa katika hazina yake mifuko kadhaa ya pesa na akampa Khatibu na akasema: "Wewe ni katika watu wenye elimu na mimi siridhii kamwe watu wenye elimu kukabiliwa na shida. Chukua kiasi hiki, lipa deni lako, na usiuze nyumba yako na kuitaabisha

familia yako." Khatibu akaona aibu kwa kitendo cha Sheikh, na baada ya hapo akawa ni kati ya wafuasi wa Sheikh na wapenzi wake.[16]

**Jamaa wa karibu wa kwanza:**

Vyovyote itakavyokuwa, kuna haja ya kutumia tabia hii, wakati wa kuamiliana na watu ni muhimu sana, ila hakika kuamilina nayo pamoja na mazingira ya watu wa karibu kati ya watu ni muhimu zaidi na kubwa zaidi. Msamaha na huruma una thamani kubwa unapofanywa na mtu wa mbali, lakini thamani yake inaongezeka zaidi unapofanywa ndani ya familia kwa kuwafanyia jamaa na watu wa karibu na mtu, wazazi wawili wazee, mke na watoto, mafakiri na wanyonge na wasiokuwa na uwezo kabisa.

Hiyo ni kwa sababu mwanadamu mwenye nguvu, nguvu yake inaweza kumsukuma kumsamehe kwa msukumo wa hofu, haiba na kujiepusha na matatizo. Ama mnyonge ambaye hamiliki uwezo wala nguvu, hakika kusamehe kwake hakusukumwi na hofu bali ni kutaka thawabu na malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kutokana na uzuri wa moyo na utu.

Ama baadhi ya watu, na sisi mara nyingi tunasikia visa hivi, wanapokosea katika haki yao baadhi ya ndugu zao, hakika wao wanakunjua makucha yao na wanalipiza kisasi kwa ubaya na kwa ukali zaidi. Na watu wengine wanapowakosea watu wageni kwao au wenye nguvu katika vituo vyao hakika wao wananyenyekea na wanarukuu na wanainamisha vichwa vyao chini, kisha hawakawii watakariri kwako neno la subira na kuvumilia (usijali dogo hilo, sio vibaya kuvumilia, shida na litaondoka), na kwa hiyo wanakuwa ni wasadikishaji wa kauli ya mshairi:

---

[16] Mukhutaariy: Sheikh Ridhaa katika *Simaai Swalihina*, tarjama ya Sheikh Husein al-Kuraaniy - Darul- Balagha – Beirut 1992 uk: 278

"Ni simba kwangu na katika vita ni mbuni, muoga anaogopa kwa unyayo, Je usingejitokeza kuwinda asubuhi, bali kabla yako alikuwa katika mabawa ya ndege."

Natamani, yalikuwa wapi maneno haya alipokosea katika haki yako ndugu yako katika nasaba au imani? Na kwa nini umezingatia ghadhabu yako? Huko ni kurejesha utukufu wako na heshima yao ambayo ulidhani kwamba imevunjwa na imedharauliwa, ama hapa unageuka mwenye kusubiri anayengojea malipo? Ulikuwa wapi wewe na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**"..... أَشِدّاءُ عَلَى الكُفّارِ رُحَماءُ بَينَهُم ....."**

**"…wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao…" (Surat Al-Fath; 48:29)**

Hakika njia ya mtu ya kufikia mafanikio katika kuvuka changamoto za uhusiano wake pamoja na wengine, bila shaka inapita katika utangulizi huu, na maadamu mwanadamu si mwenye uwezo katika kudhibiti hasira za vitendo vyake mbele ya vitendo vya mwingine, hakika hatokuwa ni mwenye kufaulu katika muamala wake. Na tunayo katika sira ya Nabii ﷺ na Ahlul-Bayt wake kigezo na mfano bora, na hebu tufaidike na sira ya watukufu ambao walifikia vyeo vya juu lakini wao walishinda hisia za kulipiza kisasi. Huyu ni Yusuf mkweli عليه السلام anawaambia ndugu zake walipoingia kwake Misri, naye akiwa ni mfalme, baada ya ndugu zake kumfanyia ubaya katika haki yake. Walimuonea husuda wakamtupia kwenye kisima kisha akauzwa kama mtumwa Misri. Akafungwa na akatuhumiwa, lakini alikuwa ni mtukufu na mkubwa kuliko kulipiza kisasi na chuki, bali aliwaambia:

**قالَ لا تَثرِيبَ عَلَيكُمُ اليَومَ يَغفِرُ اللَّهُ لَكُم وَهُوَ أَرحَمُ الرّحِمينَ**

**"Akasema hakuna lawama kwenu leo Mwenyezi Mungu atawasamehe Naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote" (Surat Yusuf; 12:92).**

Hakika usamehevu ni sifa ya lazima katika kufaulu katika maisha ya kijamii, na kuvuka matatizo, kushirikiana na kuamiliana pamoja na wengine katika jamaa wa karibu na wa mbali, nayo inafanya nafsi ya mwanadamu ipumzike na kukasirikia mabaya ya wengine, kama ambavyo inaipatia mishipa ya mwanadamu na hisia zake hali ya mkanganyiko na shinikizo linalotokana na kulipiza kisasi katika vitendo vya uadui.

**Mwanadamu baina ya mbinyo wa kimada na utukufu wa kiroho:**

Mwenyezi Mungu amemuumba mwanadamu akiwa ni mchanganyiko wa vitu viwili, kimoja wapo ni cha kimada na kingine ni cha kiroho. Tapo linalotokana na udongo na nuru inayotokana na roho, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

إِذ قالَ رَبُّكَ لِلمَلٰئِكَةِ إِنّى خٰلِقٌ بَشَرًا مِن طينٍ ﴿٧١﴾ فَإِذا سَوَّيتُهُ
وَنَفَختُ فيهِ مِن روحى فَقَعوا لَهُ سٰجِدينَ ﴿٧٢﴾

**"Mola wako alipowaambia Malaika: Hakika Mimi nitaumba mtu kutokana na udongo. Na nitakapomkamilisha na nikampulizia roho Yangu, mwangukieni kwa kusujudu." (Surat Swad; 38:71-72).**

Mchanganyiko huu katika kuumbwa mwanadamu baina ya vitu viwili vya kimada na kiroho, ndio sababu ya hali ya mvutano ndani ya mwanadamu baina ya pande mbili za uwiano huu, udongo na roho. Sehemu ya udongo inavutia kwenye ardhi na kumteremsha kwenye mazingatio ya kimada, wakati ambapo sehemu ya roho inamsukuma kwenda juu na inapaa naye katika

anga la maadili mema. Na katika mvutano huu unatokea mtihani kwa mwanadamu, inakuwa ni changamoto kubwa, na katika matokeo ya mvutano huu inapangwa hatima ya mwanadamu na kinapevuka kiwango chake; ama katika unyoofu ambapo ataishi katika hali ya uwiano na anafanya mazingatio yake ya kimada katika kivuli cha maadili na chini ya dari la misingi, na ama anakuwa chini kuliko walio chini, ambapo atakapoyafanya matamanio yake kuwa ndio mungu wake, na akatawaliwa na matamanio yake na raghaba zake.

Na tunaweza kupanga mikakati ya vitendo vyetu na nukta za mgongano baina ya mielekeo miwili katika maisha ya mwanadamu katika nyanja tatu zifuatazo:

**Kwanza: Baina ya matamanio na akili:**

Kutokana na sehemu ya udongo umepatikana kwa mwanadamu utashi na matamanio, nayo yanambana ili ayashibishe na kuyatimizia mahitaji yake ya kimwili na raghaba zake za chakula, vinywaji, mambo ya kijinsia na raha. Na yanayofungamana nayo miongoni mwa mali, cheo na jaha. Lakini kukubali moja kwa moja mwelekeo huu kunambadilisha mwanadamu kwenda kwenye kiwango cha wanyama, mifugo ambayo haina lengo isipokuwa raghaba zake tu, na haina mazingatio isipokuwa hayo tu. Wao wanakula kila sehemu; kwenye jalala au kwenye malisho, na wanakunywa maji yoyote safi au machafu, na wanafanya jimai katika hali yoyote kwa sababu wanaendeshwa na matamanio tu.

Lakini hali ya akili kwa mwanadamu ambayo inatokana na sehemu ya roho, ndio inayomwekea mpaka na masharti katika kufanya vitendo vya matamanio yake na raghaba zake, anakula, kunywa, anaoa, anamiliki na anatawala, lakini yote hayo ndani ya maelekezo ya akili na uongofu wake.

Na kuyakubalia kwa wingi matamanio, inamaanisha kuporomoka

zaidi kwenda kwenye kina cha hali ya udongo ya kimaada, wakati ambapo kutumia akili na udhibiti mzuri wa raghaba na matamanio, inamaanisha kutukuka zaidi katika upeo wa maarifa ya kiroho na kimaanawiya.

**Pili: Baina ya ubinafsi na utukufu:**

Upande wa udongo unaimarisha kwa mwanadamu hali ya ubinafsi, na inamaanisha kujali dhati yake tu, na maslahi binafsi kushinda kila kitu, ambapo mada kama mada yenyewe haina nguvu katika mwelekeo wa nje, kwani inaishi kwa ajili ya dhati yake tu. Wakati ambapo upande wa kiroho unamwelekeza mwanadamu kwenye upeo mpana zaidi, nje ya dhati yake. Anajua ridhaa ya Mola Wake na Muumba Wake, na kuzingatia hali za wengine pembezoni mwake. Na anafikiria katika maslahi ya jamii. Hakika ubinafsi unaotokana na udongo ndio ambao unamsukuma mwanadamu katika kuzifanyia uadui haki za wengine kwa ajili ya kupata yeye, nao unamzuia kutoa na kujitolea ili alimbikize kiasi kikubwa cha uwezo kwa ajili ya nafsi yake.

Lakini dhamira ya mwanadamu na uwepo wake unaotokana na upulizo wa roho ya Mwenyezi Mungu, ndio ambao unamkanya juu ya dhulma na uadui na unamshajiisha kunufaisha wengine na kuwasaidia wao bali na kuwapendelea kabla ya dhati ya nafsi yake.

Mwanadamu kuzingatia dhati yake zaidi ni mporomoko wa kimaada, na kuelekea kwake kwa wengine na kujali maslahi ya jamii ni utukufu wa kiroho.

**Tatu: Baina ya ufinyu na maadili:**

Udongo ni mada inayochukua sehemu ndogo ya muda na sehemu, nayo inamdhibiti mwanadamu kwa mpaka wa ufinyu wake mdogo na kumshughulisha na matakwa yake na mahitaji

yake ya muda na ya haraka. Wakati ambapo roho inafungamana na nguvu kuu isiyo na mpaka wala kikomo. Hakika ni upulizo kutoka kwa Mwenyezi Mungu "na nikapuliza humo roho Yangu" na nyongeza hapa ni ya utukufu, vinginevyo Mwenyezi Mungu hana mwili wala roho kwa maana iliyoenea kwetu.

Na roho inamfungulia mwanadamu ulimwengu wa maadili na ubora, nao ni ulimwengu mpana uliotanuka na mpana, mwanadamu anapoujua anakuwa juu ya mada finyu na anaiandaa nafsi yake kutumikia maadili ya Mwenyezi Mungu ya milele. Anakuwa ni mlinganiaji wa kheri, na kiongozi wa uadilifu na mtendaji kwa ajili ya haki.

Hapa hakika mwenye kuimarisha maisha yake kwa ajili ya mada anakuwa ni mwenye kuelemea kwenye udongo katika kuumbwa kwake, wakati ambapo mwenye kuiwekea nafsi yake nadhiri kwa ajili ya maadili na misingi anakuwa anaelea katika ulimwengu wa roho, mwenye kudumu katika neema za ridhaa ya Mwenyezi Mungu.

## MUAMALA WA KIBINADAMU KATIKA SIRA YA IMAMU ALI عليه السلام:

Imejitofautisha sira ya Amirul-Muuminina Ali عليه السلام, kwa mambo mengi, na lililokuwa wazi zaidi ni muamala wake wa kibinadamu wakati wa kuamiliana na wengine, uliojengeka katika msingi wa kumheshimu binadamu kama binadamu, kwa kufumbia macho kitu kingine chochote, na kuhifadhi haki zake na shakhsiya yake kimaada na kimaanawi katika nafasi yoyote na sehemu yoyote, na vyovyote litakavyokuwa umbo lake na kiwango chake.

Na umuhimu wa mwelekeo huu katika nyanja hii katika sira ya Amirul-Muuminina عليه السلام unatokana na nafasi yake katika kuathiri maisha ya mwanadamu. Ni shakhsiya ya kijamii na ni njia ya

kuelekea katika ridhaa ya Mola Mtukufu.

Mimi na wewe tunaamiliana na binadamu, sawa wawe wanaafikiana na sisi katika dini na mwelekeo au hawaafikiani nasi. Na jambo muhimu hapa ni kujua namna gani tutaamiliana pamoja nao kwa muamala mzuri wa kinadamu, ambao utaakisi usafi wa Uislamu, na kumheshimu mwanadamu kama mwanadamu kabla ya kupata sifa yeyote nyingine itakayoongeza kwake mazingatio mengine.

Na sira ya Amirul-Muuminina عليه السلام imejaa mifano mingi katika muamala wa kibinadamu wakati wa kuamiliana na wengine, katika hali na mazingira mbali mbali. Naye kwa haki – baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم – ni mfano bora wa kuigwa, hususan katika wakati huu ambao tunajiandaa kukumbuka uzao wake mtukufu.

Hakika kuwepo upeo huu katika maisha yake, ndiko kulikofanya shakhsiya yake iwe ni shakhsiya ya kibinadamu yenye kudumu katika kiwango chote cha ubinadamu, na sio katika historia ya Waislamu peke yao. Na kabla ya siku kadhaa zilizopita imetoka diwani mpya ya ushairi huko Beirut, ya Mkristo Maruniy naye ni Joseph al-Hashim, kuhusu Imamu Ali, chini ya anwani *'Matukufu ya Ali.'* Ama kitabu *Sauti Ya Uadilifu Wa Ubinadamu* cha mwanafasihi wa Kikristo Geoge Jordak ni Enklopedia nzuri mno, imechukua nafasi yake katika maktaba ya utamaduni na fasihi ya Kiarabu. Na vilevile rejea kubwa ya *Idul-Ghadir*, kitabu cha Paulo Salamah ambaye naye ni Mkristo, na visivyokuwa hivyo katika kazi ya fasihi na historia na fikra, ambavyo vinaelezea nafasi ya Imamu katika kiwango cha ubinadamu.

**Maji ni haki ya wote:**

Miongoni mwa ushahidi wa muamala wa kibinadamu wa Imam Ali عليه السلام, ni yaliyotokea katika vita vya Sifiin. Jeshi la Muawiya

lilipolitangulia jeshi la Imamu kufika katika sehemu ya mapigano na kudhibiti ufukwe wa Mto Furati, na wakazuia jeshi la Imamu kwenda kuchota maji. Wafuasi wa Imamu wakapiga kelele kwa hilo, akasimama kwao akiwahutubia na akasema neno lake mashuhuri: "Wamekuandalieni vita basi kubalini udhalili na kuchelewa kuyafikia maji. Au zinywesheni panga damu ndipo mtakunywa maji. Mauti yapo katika maisha yenu mkishindwa, na uhai upo katika mauti yenu mkishinda."[17]
Kwa maneno hayo Imamu alihamasisha jeshi lake kwenda kwenye ufukwe na haya ndio yaliyotokea kwa hakika, ambapo waliweza kuliondoa jeshi ufukweni na wao kuchukua udhibiti wake. Ilipotokea hali hiyo askari wake walipiga kelele kwa kumwambia: "Tuwazuie maji kama walivyotuzuia, na tuwapige vita kwa upanga wa kiu." Lakini yeye alikataa hilo na akasema: "Chukueni mahitaji yenu na rejeeni kwenye kambi yenu na acheni njia baina yenu na maji. Hakika mimi sifanyi waliyoyafanya wajinga."[18]

Na hivi ndivyo anatupigia mfano wa kuigwa katika kupinga kutumia vikwazo na kibano kuzuia mahitaji ya lazima ya maisha kwa adui. Ambaye anapigana naye katika vita kali hata kama adui atakimbilia kwenye njia hii. Kwa kweli hii ni tabia ya Kiislamu katika upeo wake mkubwa wa kibinadamu.

Na unapotafuta mtazamo huu katika hali ya kiulimwengu wa kimadola, utakuta haupo katika kamusi ya siasa ya kimadola leo. Wewe utaona dola kubwa na yenye utawala, inatumia vikwazo dhidi ya wananchi dhaifu kwa hoja ya kusawazisha ikhitilafu zake na baadhi ya mifumo na watawala, pamoja na kwamba wao wanajua kwamba muhanga wa vikwazo hivi ni wananchi wenyewe.

---

[17] Al-Musawiy: Sharifu Ridhaa katika *Nahjul- Balaghah*, khutuba ya 51

[18] Al-Qazuwiniy: Sayid Kaadhim katika *Aliyu minal – mahadi ilaa llahad*, uk: 334 chapa ya al-Adabu Najaf al-Ashraf, 1967.

Wakati Marekani na nchi za Magharibi zinapoweka vikwazo kwa wananchi wa Iraki, wao wanajua kwa yakini kwamba vikwazo havitabadilisha chochote katika hali ya ubabe wa serikali ya Iraki, na hivyo havitaleta mabadiliko ya kisiasa humo, bali kinyume chake vitazidisha udhaifu katika msimamo wa wananchi dhidi ya utawala, kwa sababu watu mazingatio yao makubwa yatakuwa ni tonge la kuishi na kujilinda. Ama utawala utafaidika kutokana na hali hii katika kuweka kanuni ya udhibiti wa mamlaka yake kwa maslahi yake, kwa sababu serikali hii inapata katika vikwazo vilivyowekwa propaganda katika kutengeneza adui wa nje, na katika kubakisha hali ya hatari isiyotangazwa na kisha kukandamiza kila upinzani.

Je, atadhurika kiongozi wa Iraki kwa vikwazo? Na je, watoto ambao wanakufa kwa sababu ya upungufu wa dawa na chakula ni katika watoto wa Raisi au Mawaziri au wanajeshi wa ngazi za juu?

Hakika wamagharibi wanajua kwamba watoto ambao wanakufa kwa matokeo ya vikwazo wao ni watoto wa watu mafakiri na wasio na kitu, ama watoto wa wakubwa wao hawazaliwi isipokuwa na vinywani mwao kuna kijiko cha dhahabu kama inavyosemwa.

Na wamagharibi wamelazimisha vikwazo Libya miaka mingi kwa ugomvi wao na serikali, na tumeona wakifanya zaidi ya hayo na Sudani, hadi mambo yakafikia kupiga mabomu na kuangamiza viwanda vya dawa katika nchi fakiri inayokabiliwa na upungufu mkubwa katika nyanja hii, na baadhi ya wanachi wake wanakufa kwa sababu ya upungufu mkubwa wa dawa na utapia mlo.

Uko wapi ubinadamu katika haya yote… je, hiyo sio dalili ya kutoweka upeo wa ubinadamu katika fikra ya ustaarabu wa kimagharibi na mtazamo wake katika maisha? Na kinyume cha hayo tunaona ustaarabu wa Kiislamu na viongozi wake.

**Hata mhaini ana haki yake:**

Na miongoni mwa ushahidi katika sira Ali عليه السلام katika nyanja hii ni kisa muhimu:

Mwanaume katika wafuasi wa Imamu Ali عليه السلام jina lake ni Ubaidullahi bin al-Hur al-Ja'afi, alimfanyia Imamu hiyana na akajiunga na jeshi la Muawiya wakati wa usiku, na hiyo ni wakati vita vya Sufini vikiwa vimepamba moto. Na katika kanuni za vita huadhibiwa huyu mhaini kwa kuuliwa. Ubaidullahi aliweza kutoa msaada mkubwa kwa Muawiya. Ama mke wake alikuwa Kufah na akasikia habari za kufariki Ubaidullahi katika vita, akakaa eda ya kufiwa na baada ya hapo akaolewa na mwanaume kati ya watu wa Kufah. Wakati ambapo Ubaidullahi alikuwa hai huko Shamu, na alipopewa habari ya kuolewa mke wake, akatoka Sham usiku na akakata masafa marefu na akawasili Kufah na akaingia usiku. Akaelekea haraka kwenye nyumba ya mke wake, na mke wake akatoka kwenda kwake akiwa amevaa gubigubi, na baada ya majadiliano mafupi akampa habari ya kuolewa kwake na mwanaume mwingine.

Ubaidullahi akaona milango ya kurejea kwa mke wake imefungwa mbele yake, na akaona njia bora ya kutatua ni kwenda kumuona Maulana Amirul-Muuminina عليه السلام na kumweleza kisa chake, na Amirul-Muuminina ni mtu mwadilifu na mshika haki, na haachi haki hata kama mwenye haki ni mhaini.

Ubaidullahi alikutana na Amirul-Muuminina عليه السلام hali yakuwa amevunjika moyo mwenye aibu, kwa kujua kwake kwamba yeye ni mhaini. Akamsalimia Imamu عليه السلام, Imamu akaitikia na akamuuliza kwa kumkanusha: "Je, wewe ni Ubaidullahi? Eee wewe mnafiki ambaye ulimfanyia hiyana Imamu wako na dini yako na ukajiunga na safu ya ukafiri na unafiki na hiyo ni katika hali ya vita. Je, wewe ni huyu mwanaume?"

Ubaidullahi anajua kwamba Ali ni mtu wa haki na uadilifu, akatumia fursa na akasema:

"Je, hiyana yangu inakuzuia kufanya uadilifu ewe Amirul-Muuminina?"

Imamu akamjibu: "Vipi?" Akaomba kwake asimulie kisa chake na akamtaka Imamu amsaidie katika jambo lake. Na Imamu akaamuru aletwe mke na mume wake wa pili na akasema: "Ni wajibu mke ajitenge na mume wake wa pili na aanze eda kuanzia sasa, na baada ya kumalizika eda yake arejee kwa mume wake wa kwanza kama si mjamzito, na ikiwa ni mjamzito harejei kwa mume wa kwanza hadi ajifungue, na mtoto ni halali ni twahara na anamfuata baba yake, mume wa pili. Na baada ya hapo mwanamke atarejea kwa mume wake wa kwanza."

Na inafaa kutaja hapa kwamba mke ambaye mume wake ametoweka kama akienda katika mahakama ya Kiislamu ya kisharia na hakimu wa kisharia akampa talaka, kisha mume wa kwanza akarejea, hawezi kurejea kwake, wala haivunjiki ndoa ya pili, nayo ni sahihi. Ama mke wa Ubaidullahi hakuenda kwenye mahakama ya Kiislamu, bali yeye mwenyewe alikaa eda na kuolewa, na kwa hiyo imevunjika ndoa ya pili baada ya kurejea mume wa kwanza moja kwa moja na bila ya talaka.[19]

Hakika uadilifu ni sharia madhubuti haivunjiki hata katika kuamiliana na adui. Anasema Mwenyezi Mungu:

"....وَلا يَجرِمَنَّكُم شَنَأٰنُ قَومٍ عَلىٰ أَلّا تَعدِلُوا اعدِلوا هُوَ أَقرَبُ لِلتَّقوىٰ... "

**"Na wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni**

[19] Shiraziy: Sayid Muhammad Shiraziy katika *al-Hukumatu al-Islamiyatu fiy ahdi Amirul-Muuminin*, uk: 69 Muasasatu al-Fikri al-Islamiy lilithaqati wal-Ilaami – chapa ya kwanza.

**kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu ndiko kunakokurubisha kwenye takua…..” (Surat Al-Maida; 5:8).**

**Kuzuia kutoa adhabu:**

Sira ya Imamu Ali imejaa ushahidi wa visa ambavyo vinatia mkazo kuheshimu kwake ubinadamu wa mwanadamu na kuhifadhi kwake utukufu wake, Imamu عليه السلام alijiwa na mwanamke akasema: “Hakika mume wangu amemwingilia kijakazi wangu bila ya ruhusa yangu (yaani amembaka).” Akamwambia mwanamume: “Unasemaje?” Akasema: “Sikumwingilia ila kwa ruhusa yake.” Akasema kwa kumwelekea mwanamke: “Kama wewe ni mkweli basi nitampiga mawe na kama wewe ni muongo tutakupiga viboko.” Swala ikakimiwa na Imamu Ali عليه السلام akasimama ili kuswalisha. Mwanamke akafikiria katika nafsi yake hakuona njia ya kutokea katika kupigwa mawe mume wake wala yeye kupigwa viboko, akatoka na hakurejea, na Imamu Ali عليه السلام hakumuulizia tena.

Wakati ambapo Imamu عليه السلام alikuwa anaweza kuamuru akamatwe na kuletwa mume wake na kuadhibiwa mmoja wao, lakini yeye عليه السلام alikuwa hapendi kuadhibu. Alihifadhi haki na nidhamu na hakuwa anabeba katika maamuzi ya nafsi yake chuki ya kuadhibu watu, na alikuwa anasamehe kadri anavyoweza.[20]

**Kumfanyia Wema Mkosaji:**

Ama hali nzuri zaidi ya kibinadamu katika maisha ya Imam Ali عليه السلام ilionekana wazi katika wakati wa mwisho wa maisha yake

[20] Shiraziy: Sayyid Muhammad Shiraziy katika *al-Hukumatu al-Islamiyatu fiy ahdi Amirul-Muuminin*, uk, 23 Muasasatu al-Fikri al-Islamiy lilithaqati wal-Ilaami – chapa ya kwanza.

matukufu, wakati wa kuamiliana na mtu ambaye alimpiga upanga naye yuko kwenye mihirabu ya swala yake.

Abdurahmani bin Muljim alikimbia kutoka msikitini akitaka kutoroka ila makelele ambayo yalienea katika anga la Kufah yaliwatoa wengi katika nyumba zao kwa kumtafuta muuwaji wa Amirul-Muumina katika vichochoro vya Kufah, na njia za Kufah zikaziba mbele ya Ibnu Muljim, hadi akakamatwa na baadhi ya wafuasi wa Ali عليه السلام na wakamleta kwake. Wakati huo Imam alikuwa bado ameathirika na pigo la upanga wenye sumu na damu zinatiririka kutoka katika utosi wa kichwa chake, na wafuasi wake wanapiga kelele huyu hapa adui wa Mwenyezi Mungu tumeshakuletea ewe Amirul-Muuminina. Imamu akamwangalia kwa mtazamo wa huruma na sio mtazamo wa kulipiza kisasi na kuadhibu na akamwambia: “Ewe Ibnu Muljim je, nilikuwa ni Imamu mbaya kwako?” Ibnu Muljim akawa analia na anasema: “Hapana, lakini je, wewe utamuokoa ambaye yuko motoni?”

Na ukaendelea muamala wake mzuri wa kibinadamu pamoja naye hadi pumzi ya mwisho ya maisha yake. Matabibu walieleza kwamba maziwa ndio dawa na chakula cha Imamu عليه السلام, watu wakajitolea hadi mafakiri na wasio na kitu katika mji wa Kufah, kuleta wanayoweza katika maziwa kwenye nyumba ya Imamu. Imamu Hasan alibeba moja ya gilasi za maziwa kupeleka kwa Ali, alipokunywa kidogo alimpa mtoto wake kiasi kilichobakia na akasema: “Mpelekee mfungwa wenu, mlisheni katika mnavyokula na mnywesheni katika mnavyokunywa muangalieni mfungwa wenu.”

Na sio ajabu – matokeo ya hayo – wanayoyaitakidi baadhi ya watu kwamba Imamu kama angeishi angemsamehe Ibnu Muljim. Na haya yanaafikiana na msamaha wa daima wa Imamu.

**Kusamehe kosa:**

Hakika kiwango hiki cha juu cha mwanadamu ambacho kilizunguka shakhsiya ya Ali, ndio ambacho kimemnyanyua Ali katika daraja za juu za utukufu na kudumu, ni mara chache kukuta mfano huu isipokuwa katika shakhsiya ya ustadhi wake na mwalimu wake, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Imepokewa kwamba yeye عليه السلام alikuwa amekaa na wafuasi wake, akapita kwao mwanamke. Mara watu wakamkodolea macho, akasema عليه السلام: "Hakika macho haya ya mafahali yanatamaa na hakika hiyo ni sababu ya kuangamia kwake. Atakapoangalia mmoja wenu mwanamke anayemvuatia basi na amwendee mke wake, hakika yeye ni mwanamke kama alivyo mke wake." Akasema mwanamume katika Makhhawariji: "Mwenyezi Mungu amlaani, ni kafiri anajua nini?" Watu wakamrukia ili wamuuwe. Akasema عليه السلام: "Taratibu tulieni – hakika ni tusi kwa tusi au kusamehe kosa." [21]

Na katika kumbukumbu ya Ali tunaweza kujifunza mengi na kushikamana na mengi katika mitazamo mitukufu na kudumu katika shakhsiya yake, isipokuwa uelewa wa upeo wa kibinadamu katika maisha yake yenye kudumu unabakia kuwa ndio upeo wenye mazingatio na umuhimu zaidi, ambapo mwanadamu anapata humo maendeleo ya kushangaza katika nyanja nyingi za maisha yake na anaweza kughafilika kwamba mafanikio yake hayatokamilika kama ukikosekana uwepo wa nyanja hii.

## KUKATAZA MAOVU NI HURUMA NA KUFANYA MAREKEBISHO

Uislamu unaheshimu uhuru wa mwanadamu na kuupa umuhimu

[21] Al-Musawiy: Sharifu Ridhaa katika *Nahjul- Balaghah*, Qisqaaru al-hikam namba 420.

mkubwa katika sharia zake na mafunzo yake. Uhuru katika mtazamo wa Uislamu ni jambo tukufu haijuzu kuligusa wala haijuzu kwa mwanadamu mwenyewe kuvuka katika uhuru wake na kugeuka kuwa ni mtumwa wa mwingine: "Usiwe mtumwa wa mwingine wakati Mwenyezi Mungu ameshakufanya huru."[22]

Na haijuzu kwa wengine kufanya uadui uhuru wa watu "Tangu lini mmewafanya watu watumwa wakati mama zao wamewazaa wakiwa huru."

Na hakuna kugawanya katika uhuru wa mwanadamu bali umeenea nyanja zote za maisha yake, nazo zinalindwa katika kufuata kwake dini, itikadi na mwelekeo, nao unaagaliwa katika juhudi yake ya kiuchumi, kiasi kwamba mafakihi wamenufaika katika jumla ya hukumu za miamala, na kupata kanuni ya jumla, jina lake ni kanuni ya umiliki "watu ni wamiliki wa mali zao."

Vivyo hivyo katika kila jambo ambalo maamuzi yake yanahitajia matakwa ya mwanadamu mwenyewe. Pamoja na Uislamu kutambua uhuru huo kwa namna ambayo haijafika katika kiwango chake dini wala ustaarabu mwingine wowote, isipokuwa ni kwamba kuna baadhi ya wajibu wa kisharia ambao mwanadamu anaweza kudhani kwa mara ya kwanza kuwa unapingana na uhuru wa mwanadamu. Baadhi wanaweza kuuliza uko wapi wajibu wa kuamrisha mema na kukataza maovu sambamba na Uislamu kudhamini uhuru wa mwanadamu? Kuamrisha mema na kukataza maovu dhahiri ni kuingilia uhuru wa wengine kwa sababu unaamuru kitu walichokiacha wengine kwa uhuru wao na matakwa yao, na unawakataza kitu walichokifanya kwa matakwa yao na maamuzi yao, vinginevyo kama wangekuwa wamelazimishwa basi kusingekuwepo na haja ya kuamrisha mema na kukataza maovu.

Hata daraja za chini kabisa za kuamrisha na kukataza zinadha-

[22] Al-Musawiy: Sharifu Ridhaa katika *Nahjul-Balaghah*, barua ya 31

mini katika uhalisia wake kupinga kitendo cha mwingine katika uhuru wake, hatua ya kwanza ya ulazima wa kuamrisha mema na kukataza maovu ni kupinga kwa moyo, ama hatua ya pili ni kubadilisha kwa ulimi na tatu ni kubadilisha kwa mkono, na hiyo ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: “Mwenye kuona miongoni mwenu uovu basi na auondoe kwamkono wake, asipoweza basi kwa ulimi wake, na kama hatoweza basi achukie kwa moyo wake, na hiyo ni imani dhaifu kabisa.”[23]

Hatua hizi tatu ni kuingilia katika uhuru wa wengine na matakwa yao kwa dhahiri?

Namna gani tunafahamu kuamrisha mema na kukataza maovu katika duara la ufahamu wetu juu ya uhuru wa mwanadamu? Na ulazima wa ufahamu huu ni kwa ajili ya kuondoa mkanganyiko na kutokuelewa ambako kumetokea kwa baadhi ya watu ambao wameacha wajibu huu kwa sababu ya kufahamu vibaya, kwamba hakika kunapingana na uhuru wa wengine.

Unapowauliza baadhi ya watu: Kwa nini humuamrishi mema au hukatazi maovu? Jibu linakuwa: Tutafanyaje watu wanatumia uhuru wao. Hata wanaofanya maasi na maovu unapowaamuru au kuwakataza juu ya jambo jibu lao linakuwa: Wewe inakuhusu nini? Mimi niko huru nafanya nitakayo! Na baadhi yao wanakuambia kwa maneno makali: Hakika wewe hutaungua kwa moto wangu hivyo niache na mambo yangu.

Na haya kwa pande zote mbili ni mkanganyiko na ni kosa kubwa … kwa nini?

Kwa sababu uhuru wa mwanadamu hauna maana nje ya duara la hukumu na wajibu wa kisharia kwa wengine, kama unavyoamuru Uislamu kuheshimu uhuru wa mwanadamu, hakika vile vile

[23] Al-Qashiiriy, Muslimu bin al-Hajaji katika *Sahihi Muslimi* hadithi ya 78.

unawaamrisha wenye kukalifishwa kutekeleza faradhi ya kuamrisha mema na kukataza maovu, kwani ni moja ya faradhi ambazo zina umuhimu na huenda unazidi faradhi zingine kama vile swala, saumu, hija na zaka.

Na katika haya anasema Imamu Ali عليه السلام katika neno muhimu na lenye mazingatio: "Na matendo yote mema na jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu mbele ya kuamrisha mema na kukataza maovu ni kama vile tone katika bahari kubwa."[24]

Na katika hadithi yake nyingine عليه السلام: "Kuamrisha mema ni bora kuliko amali za viumbe."[25] Na katika hadithi nyingine kutoka kwa Imamu al-Baaqir عليه السلام: "Kuamrisha mema na kukataza maovu ni njia ya Manabii, na manhaji ya wema, ni faradhi kubwa, kwayo husimamishwa faradhi, yanasalimika madhehebu na huhalalishwa chumo, yanarejeshwa yaliyodhulumiwa, inastawishwa ardhi, wanafanyiwa uadilifu maadui na mambo yanayooka."[26]

Je, kuamrisha mema na kukataza maovu kunapingana na uhuru wa mwanadamu au laa?

Jawabu: Hakika hakuna mgongano wala kupingana. Hiyo ni kwa sababu Uislamu umeweka faradhi hiyo ndani ya mpaka na upeo, haupingi uhuru wa mwanadamu, bali ni kinyume cha hayo, kwani unaulinda na unadhamini mafanikio ya mwandamu, na mpaka huu na upeo huu ambao Uislamu unautarajia katika faradhi hii ni:

**Kwanza: Kujali Maslahi ya Mwanadamu na Faida Zake:**

Kuamrisha mema na kukataza maovu hakika kunalenga kwa

---

[24] Al-Musawiy: Sharifu Ridhaa katika *Nahajul-Balaghah* – Qiswaaru l-hikami 374

[25] Al-Amadiy al Tamimiy: Abdul-Wahid katika *Ghurarul-hikam* namba 1198

[26] Al-Huru al-Amiliy: Muhammad bin al-Hasan katika *Wasailush-Shi'ah*, Juz. 16 uk: 119 hadithi ya 21132.

uhakika kumwepusha mwanadamu na makosa na hatari zenye kuangamiza ambazo anaweza kutumbukia humo, kama hakuzinduka juu yake. Unapomwamrisha mwanadamu anayepita katika barabara ili atanabahi na shimo katika njia yake ili asitumbukie humo, jambo hilo ni kwa ajili ya maslahi yake yeye mwenyewe, ili asitumbukie na kuumia. Hivyo haingii akilini wakati huo kukujibu kwamba wewe huhusiki katika hilo. Na vivyo hivyo unapompa nasaha mtu kuepuka kula chakula chenye sumu, sio sahihi kukuambia kwamba mimi niko huru na kwamba wewe hupaswi kuingilia mambo yangu, kwa sababu wewe katika hilo unatarajia maslahi yake, lakini ni haki yake apate tumaini la usahihi wa kuamrisha kwako au kukataza kwako, na sio kupinga kuamrisha na kukataza kwako.

Kwa sababu Uislamu unataka watu kuishi katika hali ya kushirikiana na kujali maslahi ya wengine, na kuenea katika nyoyo za wanajamii upendo wao baina yao wao kwa wao, hivyo umeamuru mmoja wao kumwamuru mwingine yale ambayo humo kuna maslahi yake, au kumkataza mwenzake yale ambayo humo kuna madhara yake "Mpendelee ndugu yako unayoipendelea nafsi yako na chukia kwake unayoyachukia kwayo."

Na hiyo ndio njia ya kuwalingania wengine ambayo Mwenyezi Mungu ameuamuru umma wa Nabii Wake Muhammad ﷺ waipite

وَلـتَكُن مِنكُم أُمَّةٌ يَدعونَ إِلَى الخَيرِوَيَأمُرونَ بِالمَعروفِ وَيَنهَونَ عَنِ
المُنكَرِ وَأُولـٰئِكَ هُمُ المُفلِحونَ

**"Na lipatekane miongoni mwenu kundi linalolingania katika kheri na linalokataza maovu na hao ndio wenye kufaulu." (Surat Aali-Imran; 3:104)**

**Pili: Kuanza na Upendo wa Kweli kwa Mwanadamu:**

Vipi unapasa kuwa mtazamo wetu kwa wenye madhambi na maasi ambao ni wajibu waamrishwe mema au wakatazwe maovu?

Baadhi ya watu wanaangalia maasi na wenye maasi bila ya mazingatio wala kujali na wanaburudika na hali wanayoiona! Na kufanya hivyo hakika ni:

**Kwanza:** Hakika ni aina ya ubinafsi kwa kutozingatia maslahi ya wengine.

**Pili:** Ni msimamo asiouridhia Mwenyezi Mungu, kwani wenyewe kwa dhati yake ni maasi, kukubali maasi na kuyanyamazia ni maasi kwa Mwenyezi Mungu. Kisha hakika maasi yote hayo ni madhara kwa maslahi ya jumla ya jamii, kwa sababu kubakia maasi bila ya kuyabadilisha inamaanisha hatari kwa wanajamii ya kupatwa na hali hiyo.

Na wengine wanaweza kuchukua msimamo wa kinyume kwa wenye maasi, nao ni msimamo wa kisasi na kumalizana nao. Na msimamo huu ni kosa kubwa, hiyo ni kwa sababu Uislamu unataka kwetu tuwaangalie waasi kwa mtazamo wa huruma na upole. Huyu mwanadamu mwenye kutenda maasi si kingine ila ni mtu mgonjwa katika roho yake na nafsi yake, na sio katika mwili wake na kiwiliwili chake. Je inajuzu kwa yeyote anapomuona mgonjwa amchukie na ammalize? Je, Daktari anayetibu alipize kisasi au ni wajibu wake amhurumie kwa hali yake na kufikiria matibabu yake?

Ilitokea wakati wa Nabii ﷺ kwamba alipelekewa mnywa pombe. Nabii akawaamuru Masahaba wake wamwadhibu, kisha wakasema: "Je, huoni haya kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kufanya haya?" Kisha akaachiwa. Alipoondoka watu waka-

wa wanamuombea laana na wanamtukana. Anasema msemaji: Ewe Mwenyezi Mungu mfedheheshe! Ewe Mwenyezi Mungu mlaani? Nabii ﷺ akasema: “Msiseme hivyo, msimlaani, msimsaidie shetani kwa ndugu yenu, lakini semeni: Ewe Mwenyezi Mungu msamehe. Ewe Mwenyezi Mungu muongoze.”[27]

Na makusudio ya nasaha, kuamrisha mema na kukataza maovu ni kutibu maradhi ya mwenye dhambi na mwenye kuasi. Ni lazima aanze matibabu kwa njia yenye madhara machache na muhimu kwa shakhsiya yake, na uadui shutuma, chuki na laana hazitotatua tatizo, bali inaweza kuongeza king’ang’anzi katika maasi. Ama kumuombea uongofu na mafanikio, na kufuata hekima na mawaidha mazuri katika mazungumzo pamoja naye yatakuwa na athari kubwa kwake katika kumili moyo wake na kubadilisha nyendo zake, na kwa hiyo inapasa kwa warekebishaji na watoa nasaha wafikirie katika mbinu na namna inayofaa kwa hilo, kama vile kuanza kwa mazungumzo pamoja naye kwa njia inayovutia, na kwa nukta iliyo mbali na maudhui ya maasi na dhambi yenyewe, ambapo mrekebishaji anaweza kupata upendo kwanza kisha anaelekeza kwake baada ya hayo angalizo au tanbihi inayohusiana na kosa na dhambi ambayo ameifanya, na hii ndio njia ya warekebishaji.

**Tatu: Kuchunga Hali ya Jumla ya Mwanadamu:**

Kiasi kwamba mrekebishaji anahifadhi kutomfedhehesha mwenye dhambi na kutangaza dhambi yake. Kuamrisha na kukataza ni wajibu na ni faradhi, isipokuwa kuvunja heshima ni haramu na mtendaji wake anaingia katika wale ambao Mwenyezi Mungu amewahesabu katika

---

[27] Al-Kaandhalawiy: Muhammad Yusufu katika *Hayatu Swahabati*, Juz. 3 uk: 512, chapa ya Darul-fikri Beirut - Lenanon chapa ya kwanza 1974.

"إِنَّ الَّذِينَ يُحِبّونَ أَن تَشيعَ الفٰحِشَةُ فِى الَّذينَ ءامَنوا....."

**"Hakika wale ambao wanapenda kueneza uchafu kwa walioamini….." (Surat An-Nur; 24:19)**

Na maadamu mvunjaji hajatoa ushahidi wa kisharia juu ya usahihi wa madai yake na tuhuma yake kwa mwenye dhambi katika kutokea kwake, hakika inajuzu kwa mwenye kutuhumiwa kupeleka mashitaka ya kisharia kwa mtawala wa kisharia na kumwadhibu kwa kumzulia uongo na wala haijuzu kwa mtawala wa kisharia mwenyewe kumtuhumu mtu kwa dhambi maadamu hana ushahidi.

Ilitokea katika zama za khalifa Umar bin Khattab kwamba yeye alikuwa anatembea usiku mmoja, akamuona mwanaume na mwanamke wanafanya uchafu. Kulipokucha akawaambia watu: Je, mnaonaje kama kiongozi akiona mwanaume na mwanamke wanafanya uchafu na akawaadhibu mtafanyaje? Wakasema: Hakika wewe ni kiongozi. Akasema Ali bin Abi Twalib عليه السلام hilo sio lako, hivyo utaadhibiwa, hakika Mwenyezi Mungu hakuamini jambo hili chini ya mashahidi wanne, kisha akawaachia aliyowaachia Mwenyezi Mungu, kisha akasema waulize watu. Wakasema mfano wa maneno yao ya kwanza na Ali akasema mfano wa maneno yake ya kwanza, na Umar akachukua kauli yake.[28]

Haya ni ikiwa mwenye dhambi na muasi anafanya maasi mbali na macho ya watu au bila ya kutaka kudhihirisha ufuska na maasi. Ama anayefanya maasi hadharani mbele ya watu basi amesha fedhehesha nafsi yake na wakati huo hakuna uharamu kwake kwa sababu hajavunja yeyote heshima yake bali yeye ndio ambaye amevunja heshima ya nafsi yake. Na tofauti ni kubwa

[28] Al-Amin: Abdul-Husein, Juz. 6, uk: 53, Muasasatu al-Alammiy lilimatubuaati Beirut '- Lebanon chapa ya kwanza 1994.

baina ya mwenye kufanya dhambi kwa kuathirika pande kati ya pande za udhaifu wake, na baina ya anayeng'ang'ania maasi hata mbele ya watu. Huyu wa pili inajuzu kwake kuvunja heshima yake kwa sababu hajasitiri nafsi yake.

Ama wa kwanza inapasa kumsaidia kuvuka hali ya udhaifu, na kusitiri dhambi yake ni kati ya hatua muhimu katika nyanja hii, ambapo kubakia utajo mzuri mbele ya watu itakuwa ni sababu yenye athari katika kumtoa kwake kwenye dhambi. Kana kwamba sisi tunampa fursa ya kuishi kwa utukufu baada ya utajo wake kukaribia kuharibika, amesema ﷺ: "Mwenye kumstiri muumini katika ovu basi kana kwamba amempa uhai mtoto mchanga aliyeuliwa."[29]

Na amesema Imamu Hasan عليه السلام katika haki ya rafiki: "Hakika akiona kwako pengo analiziba au akiona kwako jema analihesabu." Na katika upande mwingine hutokuta mtu yeyote aliyeepukana na kasoro au dhambi, mwenye kuona aibu za yeyote katika ndugu zake haijuzu kwake kufurahia, kwa sababu hajui nini kitatokea kwake miongoni mwa madhambi katika mustakbali wake. Anasema Imamu Ali عليه السلام: "Usifurahie kosa la mwingine, hakika wewe humiliki kupatia kamwe."[30]

Na maadamu mwanadamu hamiliki kinga ya kutofanya maasi, hakika ni wajibu wake asimfedheheshe mwingine, vinginevyo Mwenyezi Mungu atamfedhehesha. Je mwanadamu anataka fedheha katika nafsi yake? Anasema Nabii ﷺ: Usifuatilie aibu za waumini, hakika mwenye kufuatilia aibu za waumini Mwenyezi Mungu atafuatilia aibu zake, atamfedhehesha hata ndani ya nyumba yake."[31]

---

[29] Al-Hindiy: Ali al-Mutaqiy katika *Kanuzl-Umaal*, Juz. 2, uk: 249, hadithi namba 6388

[30] Al-Amadiy Tamimiy: Abdul-Wahid katika *Ghurarul-Hikam*, fasil 85 hadithi namba 144

[31] Al-Majlisiy: Muhammad Baaqir katika *Biharul-Anuwar*, Juz. 7, uk: 214

Na imetokea kwa mtu mmoja kwamba alikuwa ni mwingi wa kufichua aibu za watu, na nasaha hazikumfaa kuacha hayo, hadi ikaja siku moja ambayo Mwenyezi Mungu alimfedhehesha mbele ya watu katika aibu zake na dhambi zake ambazo alikuwa anazifanya ndani ya nyumba yake. Na hiyo ni kwa ulimi wa mke wake ambaye alihitalifiana naye akawaambia watu aibu zake na maovu yake yote.

Mtu mmoja alimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema: Napenda Mwenyezi Mungu asitiri aibu zangu, nifanye nini? Akasema ﷺ: "Sitiri aibu za ndugu zako Mwenyezi Mungu atasitiri aibu zako."[32]

Bali hata katika Akhera Mwenyezi Mungu atasitiri aibu za wenye dhambi kwa fadhila za kusitiri kwao aibu za ndugu zao katika dunia, amesema ﷺ: "Mwenye kumsitiri ndugu yake katika ovu aliloliona kwake Mwenyezi Mungu atamsitiri katika dunia na akhera."[33]

Hakika kuamrisha mema na kukataza maovu sio tu ni chukio linalochemka analolitoa mwanadamu kwa mwenye madhambi, na sio tu ni wasila kati ya wasila wa kudhihirisha aibu bali ni raghaba ya kweli ndani ya mrekebishaji kwa ajili ya kubadilisha hali ya mwenye kuwa nayo kwenda kwenye hali nzuri zaidi. Hivyo na uwe wasila wake ni neno jema, njia inayopendeza na dua njema, maadamu ni wasila wenye kuathiri kwa watu na ni wenye kuhitajika kisheria.

**Anawalingania waasi:**

Na katika mazuri yanayonukuliwa katika kisa cha mwanachuoni mchamungu aliyejulikana kwa jina la Maarufu al-Karikhiy,

[32] Al-Raishahariy: Muhammadi katika *Mizanul-Hikimah*, Juz. 7, uk: 145.
[33] Rejea iliyotangulia uk: 145

ambaye ni kati ya wafuasi na wanafunzi wa Imamu Ridhaa عليه السلام, ametajwa na Ibnu al-Jauziy katika kitabu chake *Swafuwatus-Swafuwah* ni kwamba: Maarufu alikuwa amekaa katika ufukwe wa mto Dijilah, wakapita vijana na mtumbwi, wanapiga makasia na wanakunywa. Ibrahim al-Atwirashi akamwambia na alikuwa pamoja naye: "Je, huoni hawa wanamwasi Mwenyezi Mungu, waombee." Akanyanyua mikono yake mbinguni na akasema: "Ewe Mungu Wangu na Bwana Wangu! Nakuomba uwafurahishe peponi kama ulivyowafurahisha katika dunia." Wakastaajabu wafuasi wa Maarufu kwa dua hii, Maarufu akasema kwa kufafanua: "Kama Mwenyezi Mungu atawafurahisha katika akhera atawasamehe duniani, na wala hawatowadhuru ninyi kwa chochote."[34]

Hivi ndivyo inavyopaswa uwe mtazamo wa muumini kwa wenye madhambi. Na hivi ndivyo alivyokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم hata pamoja na washirikina. Kila washirikina wanapozidi uasi na ukaidi hilo halikumzidishia ila subira na uvumilivu na kumnyenyekea Mwenyezi Mungu na kuwaombea awaongoze kwani wao hawafahamu! Na historia haijatutajia kwamba Nabii صلى الله عليه وآله وسلم aliwaombea maangamizi washirikina hata mara moja. Amesema swahaba Abdillahi bin Masuudi: "Kana kwamba mimi namtazama Nabii صلى الله عليه وآله وسلم anamzungumzia Nabii kati ya manabii, ambaye alipigwa na kaumu yake wakamtoa damu naye anapangusa damu usoni mwake na akasema: Mola Wangu wasamehe kaumu yangu hakika wao hawajui."

Na amesema Kadhi Ayaadh katika *Shifaa*: Hakika alipovunjwa meno yake ya mbele na akachanwa uso wake siku ya Uhudi, hilo likawa zito sana kwa masahaba wake wakasema: Walaani? Akasema: "Hakika mimi sijatumwa kuwa ni mwenye kulaani

[34] Al-Answaariy Shaaraniy: Abdul-Wahaab bin Ahmad, katika *Mukhitaswar Kitabu Swawafuti as Swafuwah*, uk: 232 chapa ya nahadhwatu al-Hadioithah – Makkah 1967

lakini mimi nimetumwa kuwa ni mlinganiaji na rehema. Ewe Mwenyezi Mungu waongoze kaumu yangu hakika wao hawajui."[35]

Ama Imamu Husein عليه السلام imenukuliwa kutoka kwake kwamba yeye alionekana analia Karbalaa, mmoja wa wafuasi wake akamuuliza. Ewe Mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu unalia kwa yaliyokufika? Akasema عليه السلام: "Hapana, nalia kwa ajili ya hawa watu hakika wao wananiua na wataingia motoni kwa sababu yangu." Ama wale ambao upeo wao ni mfinyu hakika wao wanaishi kwa uadui hata na watu waliokaribu sana nao, hawahisi kosa kwao ila wanawashambulia, wala hawagundui kwao dhambi ila wanaitangaza miongoni mwa watu.

Hakika faradhi ya kuamrisha mema na kukataza maovu kama itatekelezwa katika mipaka yake na udhibiti wake haitapingana na uhuru wa mwanadamu. Bali hakika itanyanyua kiwango cha uelewa wa mwanadamu kwa uhuru wake, na itakuwa ni sababu ya kurekebisha mianya ya hali ya kijamii na kumnyanyua kwenda katika kiwango bora kinacholeta maslahi ya jumla, na kinachodhamini mafanikio ya wote.

## UJUMBE WA MANABII IMANI NA UTEKELEZAJI

Mwanadamu anahitaji mwongozo wa Mwenyezi Mungu unaomwelekeza katika mambo mbalimbali ya maisha yake. Na mwanadamu alishapata uongofu huo katika mikono ya watu aliowachagua Mwenyezi Mungu ili kufikisha ujumbe Wake kwa watu, nao ni Manabii. Na baadhi wanaweza kudhani kwamba mwanadamu maadamu anamiliki akili basi hahitajii Manabii, kwa sababu akili inampa mwanadamu uwezo wa kupambanua

[35] Al-Qazuwiniy: Hasan Murtadhwa, katika *Rasulul-Akram Madrasatul Akhilaaq*, uk: 187 – 187, Darul bayaan al-arabiy chapa ya kwanza 1991.

kheri na shari, na kujua manufaa na madhara, jema na ovu. Na swali hili linaweza kuzunguka katika akili ya mwanadamu wa kileo, kama lilivyokuwa linaulizwa wakati uliopita, isipokuwa uelezaji wake leo unatimia kwa njia ya kina zaidi na yenye nguvu zaidi kuliko ilivyokuwa inaulizwa mwanzo. Hiyo ni kwa sababu mwanadamu ameweza kufikia kwa akili yake mafanikio makubwa, amezidi kuiamini akili yake kiasi anadhani kwamba amefikia kwenye kilele cha kujitegemea, na kwamba hahitaji upande mwingine wa nje.

Na jawabu la swali hili na shaka hii, ni lile lile ambalo watu wa Mungu na wapwekeshaji waliwauliza wakanushaji, watu wa maada na wapinga utume. Swali halikubadilika bali limezidi kuulizwa, na jawabu pia halijabadilika bali limezidi kuwa wazi. Mwanadamu anahitaji kuwa na mawasiliano na mbinguni na mwongozo wa Mwenyezi Mungu katika nyanja tatu:

**Kwanza: Haja ya Kupata Maarifa:**

Akili pamoja na nguvu na uwezo inayoumiliki ila hakika haiwezi kujua kila jambo, na kupenya vizingiti vyote na vizuizi vyote, ambavyo vinasimama mbele ya njia ya kupata ziada ya majibu na maarifa anayoyatafuta. Na jambo muhimu ni kwamba mambo ambayo akili inashindwa kutoa majibu yenye kutosheleza ni mas'ala muhimu na makubwa na nyeti sana, yanahusiana na msingi wa mwanadamu, kukua kwake na lengo la kuumbwa kwake na kutengenezwa kwake, samabamba na mpangilio huu wa kiulimwengu ambao unamzunguka, na mustakabali ambao unamsubiri hapo baadaye.

Ni ipi hiyo nguvu ambayo imetuumba na ni ya namna gani? Na ni yapi mazingira ya mafungamano yetu Nayo na mafungamano Yake kwetu? Na mas'ala haya akili haiwezi kuyajibu.

Ndio, inaweza kuamua kwamba hakuna muumba na kwamba

yeye hakuumbwa kutoka katika hali ya kutokuwepo, na kwamba hakuumba nafsi yake yeye mwenyewe

أَم خُلِقوا مِن غَيرِ شَىءٍ أَم هُمُ الخٰلِقونَ

**“Au wao wameumbwa pasipo kutokana na chochote; au wao ndio waumbaji” (Surat At--Tur; 52:35)**

Isipokuwa hawezi kujibu zaidi ya haya, sio kwa sababu ya kasoro iliyopo katika dhati ya akili, bali ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu hakumpa zaidi ya uwezo huu. Na wahyi wa Mwenyezi Mungu ndio unaoweza kujibu mas’ala haya, na bila ya hayo mwanadamu ataishi bila ya kujua sababu ya kuwepo kwake na lengo la kubakia kwake, na hilo litaathiri katika kufikia mafanikio yake, kwa sababu atabakia mwenye kukanganyikiwa, mwenye huzuni na mwenye mashaka. Na hata kama akifikia utatuzi wa matatizo yote ya kielimu na maarifa mengine na yakabakia mas’ala haya ya msingi bila ya maarifa yanayokata kiu yake humo, hiyo itakuwa ni huzuni na sababu kati ya sababu ya uovu wake na ubaya wake.

Na namna gani akili hii itafikia yenyewe ukweli huo? Kwani bado haijajua maalumaati yote ya kimaada yanayohusika ambayo anayahitajia, na wanakiri hilo wataalamu ambao walikuwa ni viongozi wa uvumbuzi wa kielimu. Huyu hapa Albert Einstein, anasema: “Hakika kiasi cha maalumati yangu katika nisiyoyajua ni kama kiwango cha ngazi hii ndogo katika maktaba yangu mbele ya maktaba pana na kubwa.” Yaani hakika asiyoyajua ni mengi zaidi na zaidi kuliko anayoyajua.

Na siashirii katika ukweli huu kumteremsha mwanadamu upande wa kuongezeka elimu yake na maendeleo ya maalumati yake na fikra zake. Mwanadamu kila siku anavumbua elimu au kanuni ya elimu mpya, ambapo inamaanisha kwamba kuna vitu vingine atavivumbua katika mustakabali, na hivi sasa havijui. Na ukweli

ni kwamba mwanadamu aghlabu anafikia kwenye hatua ya juu katika elimu kwenye maalumati muhimu zaidi kuliko maalumati ya zamani.

Na ikiwa hajui ukweli wote wa kimaada, namna gani atajua ukweli wa ghaibu kuhusu mwanzo wake na mwisho wa hatima yake? Nayo ni maarifa ya lazima ambayo anayahitajia kabla ya maarifa yoyote mengine, namna gani atamjua ambaye amemuumba, na kwa nini amemuumba na nini hatima yake?

- Hivyo ima mwanadamu abakie kuwa ni mwenye kupotea kuhusu mas'ala haya ya lazima na muhimu juu yake daima.
- Na ima iingilie huruma ya Mwenyezi Mungu Mjuzi ili kuwaonyesha waja juu yake na kwa mitume Wake, kwa sababu (swt) ametakasika na kuwanyima waja Wake maarifa ya lazima kwao, na ametakasika vilevile kuwapa waja Wake hoja dhidi Yake wakawa na udhuru Kwake Siku ya Kiyama, kwamba wao hawakutii kwa sababu wao hawakuwa wanamjua, wala hawakuwa wanajua mas'ala ya lazima kwa ajili ya uongofu wao katika ibada Yake na utii Kwake, akatuma (swt) Mitume ili iwe ni hoja ya wazi katika kuumbwa kwake. "Sema Mwenyezi Mungu ana hoja ya wazi." (Suratul- An' am: 149), na amesema (swt):

"رُسُلًا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعدَ الرُّسُلِ ....."

**"Mitume wabashiri na waonyaji ili isije ikawa watu wana hoja dhidi ya Mwenyezi Mungu baada ya Mitume." (Surat An-Nisaa'; 4:165).**

Hakika utume unaiongezea akili ukweli thabiti wa ulimwengu huu wa ghaibu, unaelekeza hisia za mwanadamu na unaijuza na kuielimisha juu ya ukweli na kuipatia njia ya kuwasiliana nayo.

**Pili: Haja ya Kijamii:**

Watu wanaishi kwa kujumuika baadhi yao na baadhi, hivyo ni lazima kuwepo na utaratibu wa kuendesha mambo yao na kuweka kanuni za uhusiano baina yao. Na kuweka nidhamu ya kijamii ya jumla, inalazimu kumjua kwa kina mwanadamu katika tabia zake, utashi wake na raghaba zake, kama ambavyo inalazimu kujua kwa umakini ulimwengu ambao unamzunguka mwanadamu, na maisha ambayo anaishi. Na namna gani yatapatikana haya maarifa na kuyajua kama si kutoka kwa Mola wa mwanadamu na ulimwengu?

> وَلَقَد خَلَقنَا الإِنسٰنَ وَنَعلَمُ ما تُوَسوِسُ بِهِ نَفسُهُ وَنَحنُ أَقرَبُ إِلَيهِ مِن حَبلِ الوَريدِ
>
> **"Na hakika tumemuumba mtu, na tunayajua yana-yoitia wasiwasi nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingo." (Surat Qaf; 50:16)**

Katika upande mwingine hakika kuweka sharia ya utaratibu wa kijamii wa jumla inahitajia usafi wa kimaudhui, kiasi kwamba mwenye kuweka sharia asifungamane na pande zote au asinyenyekee kwenye maslahi au asiathirike na raghaba au matamanio. Na mwanadamu anapotegemea nafsi yake katika kuweka utaratibu kama huu, hakika ataingia katika tajiriba yenye kufeli moja baada ya nyingine. Na historia ya leo inatuonyesha namna gani nusu ya jamii ya binadamu takriban imekabiliwa na tajiriba ya ujamaa wa kikomonisti hadi ikaporomoka, na nini kinamkabili mwanadamu hivi sasa katika utawala wa kibepari wa kimagharibi, ambao wanadai baadhi watazamaji wake kwamba ni mwisho wa historia kulingana na maneno ya Yoshihiro Francis Fukuyama.

Kwa sababu hiyo wenye kuamini Mungu wanaitakidi kwamba

binadamu anahitaji mwongozo wa Mwenyezi Mungu, ambao unampa uratibu wa kijamii unaotengeneza mambo yao na kuelekeza nyendo zao kuelekea kwenye mafanikio na ukamilifu.

**Tatu: Haja ya Kitabia:**

Mtazamo wa mwanadamu kwenye kanuni inayomhukumu hutofautiana kwa kuzingatia inatoka kwa nani. Inatoka kwa wanadamu wenyewe au inatoka kwa Muumba wa binadamu. Inapokuwa ni kanuni ya kibinadamu wakati huo hakika mwanadamu huwa hahisi kulazimika kwa kina katika kushikamana nayo, na kujizuia kuikhalifu kwake, na kwa hiyo anaweza kufanya hila juu yake na kuiacha huku akidai kwamba anaitekeleza. Ama inapokuwa kanuni husika ni ya mbinguni na kwamba aliyeamrisha ni Muumba wa watu, hakika kanuni hii itamiliki, wakati huo – nguvu ya ndani katika nafsi ya kila mtu, inayomsukuma katika kuitekeleza, kwa kuitakidi kwamba, ambaye amemuumba anamwangalia katika vitendo vyake na shughuli zake zote na kwamba Yeye atamhisabu kwa kukhalifu kwake.

Na huenda baadhi wakapinga na kusema kwamba, tabia hii wakati huo itakuwa ni mwenendo uliolazimishwa kwa mwanadamu, kwa kitendo cha nguvu kuu, naye ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, wakati inapasa kitendo cha kitabia kiepukane na mbinyo na kulazimishwa. Isipokuwa ni kwamba upinzani huu sio madhubuti, kwa sababu kitendo kitatokana na matakwa ya mwanadamu huru. Ama kuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu, yeye analipa mema na anaadhibu katika uovu, hili ndio lengo la uadilifu na mwanadamu kuwa ni mwenye hiyari.

Na inacholenga kanuni na sharia za mbinguni ni kumfanya mwanadamu katika nafsi yake awe ni mwenye kupewa tabia safi ya kimaumbile ambayo inaafikiana pamoja na imani na itikadi, na itikadi iwe ndio yenye kusukuma na kuendesha vitendo vya

kheri, na uwe ni mwenendo mwema kwa kuakisi wema wa itikadi na usafi wa imani.

**Watu wa Mada na Utekelezaji wa Sharia:**

Mwanadamu kujiuliza juu ya haja ya kuwepo Manabii hilo ni swali la kawaida, ambalo linapelekea kuamini Manabii, kama atatumia akili yake na fikra yake kwa namna ya kimaudhui na ya kimantiki. Ama Mwislamu na mwenye kumwamini Mtume na mwenye kukubali ujumbe wake, kuuliza juu ya haja ya kutekeleza sharia ambayo amekuja nayo Mtume kutoka kwa Mola Wake, swali hilo ni geni na la ajabu sana!! Kwa sababu maana ya kukubali na kumwamini Mtume, Mwislamu anaposema: "Nashuhudia kwamba Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu" ni kunyenyekea sharia yake na kutekeleza ujumbe wake:

"..... وَما ءاتىٰكُمُ الرَّسولُ فَخُذوهُ وَما نَهىٰكُم عَنهُ فَانتَهوا ....."

**"…Na anachowapa Mtume kichukueni na anachowakataza jiepusheni nacho." (Surat Al-Hashr 59:7)**

Maadamu unaamini kwamba yeye ni Mtume, na kwamba aliyokuja nayo ni ujumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuja kwako, namna gani inajuzu kwako kuuliza au kushuku au kusitasita katika utekelezaji wake? Hakika inasikitisha sana kusikia baina ya wakati mmoja na mwingine kwamba, baadhi ya Waislamu katika nchi ya Kiislamu wanasita kutekeleza sharia. Kama ambavyo inasikitisha kwamba kudai tu kutekeleza sharia katika baadhi ya nchi za Kiislamu ni kosa ambalo dola inaadhibu juu yake. Na baadhi ya nchi za Kiislamu kuzuia baadhi ya mambo ya kidini kama vile hijabu na kusimamisha mambo ya Kiislamu. Na baadhi kuhesabu baadhi ya mambo haya au mengineyo ni kosa analotuhumiwa mwanadamu kwa sababu yake. Kama hali ilivyo Uturuki kwa mfano, nayo ni dola ya

Kiislamu, bali ilikuwa kabla ya muda mfupi ni makao makuu ya ukhalifa wa Kiislamu, na wengi wa wananchi wake ni Waislamu, lakini kulingania kutekeleza Uislamu humo inazingatiwa kuwa ni kosa, na kuvaa hijabu katika taasisi rasmi ni kosa ambalo mtu anaadhibiwa kwalo kama ilivyotokea kwa mbuge Merve KAVAKÇI.

Hakika baadhi ya watu kukataa kutekeleza sharia kunatokana na sababu kadhaa, miongoni mwazo ni:

**Sababu ya Kwanza:** Sharia kutokuwa wazi na utaratibu wake kwa namna ya kutosha, na ni upi utaratibu wa Kiislamu tunaoutaka kuutekeleza? Na ni yapi mafunzo yake na vigezo vyake? Na ni ipi mipaka yake na miko yake? Waislamu wengi leo – kwa masikitiko – hawajui kwa ufafanuzi utaratibu wa kisiasa, kijamii, kiuchumi na wala hawaelewi ila baadhi ya hukumu na sharia za ibada, wakati ambapo upande huu hauwakilishi isipokuwa sehemu tu ya utaratibu kamili unaokidhi mahitaji yote ya binadamu, nao ni upande wa ibada. Na mara nyingine katika akili za watu fikra ya kutekeleza sharia hujifunga upande wa kutoa adhabu katika yale yaliyoharamishwa tu, na hilo ni jambo la kimakosa kwani adhabu ni sehemu ya utaratibu kamilifu.

Na kama tukiweza kuuelezea na kuubainishia ulimwengu utaratibu wa Kiislamu kwa ukamilifu wake kwa njia inayofaa, yasingeulizwa maswali haya na sharia ingechukua nafsi yake katika jamii ya Kiislamu na ya kibinadamu.

**Sababu ya pili:** Utekelezaji wa kupaka matope Uislamu katika zama za kihistoria zilizotangulia, ambapo Uislamu ulitumiwa kama pazia la vitendo vinavyopingana na haki za binadamu, na uadilifu wa kijamii. Bali baadhi ya utekelezaji wa kileo ambao unafanywa kwa jina la Uislamu kwa sura yake umeleta adha na uovu mkubwa, kama inavyotokea Afghanistan. Pamoja na kwamba kuna mifano yenye kuchanua na mizuri ya utekelezaji

wa Uislamu katika wakati uliopita na hivi sasa, ila macho yanaelekezwa kwenye dhana mbaya zaidi na mifano inayo-jitokeza zaidi na iliyo mingi zaidi. Hivyo wengi wanaogopa utekelezaji wa Uislamu kuwa ni aina ya kurejea nyuma na kurejesha tajiriba mbaya katika historia au kuelekea hali mbaya katika wakati wa sasa.

**Sababu ya tatu:** Kushindwa mbele ya fikra ya kimada ya kimagharibi**:**

Fikra hiyo imesheheni elimu na teknolojia na maendeleo ya kijamii. Ama Waislamu wanaishi katika hali mbalimbali, wakati baadhi ya watu wanafikiri katika hali ya kutoendelea ambako wanaishi nayo Waislamu, wanafikiri kwa kudhani kwamba utatuzi ni kuacha dini na sharia!!

Na matangazo ya kigeni, na utamaduni wa kimagharibi yana nafasi kubwa katika kueneza picha hii na kuiimarisha katika akili, hususani kalamu kutoka miongoni mwa Waislamu zina-sambaza mahubiri ya fikra ya kimagharibi, sasa utatuzi uko wapi?

**Kwanza:** Ni lazima kufungua mlango wa ijitihadi, kwa ajili ya kufichua na kuvumbua mifumo ya Kiislamu na ratiba zake, na kuvuka rundo hili katika picha iliyopakwa matope yenye makosa, na kuweka wazi mafuhumu ya Kislamu, na kubainisha mifumo na manhaji ya Kiislamu katika nyanja za maisha.

**Pili:** Inapasa tusimamie tajiriba zetu za kihistoria na za sasa kwa kila ujasiri, ushujaa na upekee na tuweke wazi kwa ulimwengu na vizazi, pande zenye mwanga miongoni mwazo ambazo zinawakilisha Uislamu, na tutambue sehemu zenye giza humo ambazo ni kukhalifu Uislamu na hauziridhii. Na wala tusikubali kiukamilifu tajriba mbaya zilizotangulia na zinazonasibishwa na Uislamu.

**Tatu:** Tujipambe na maanawiya yetu ya juu na wala tusishindwe mbele ya upakaji matope wake, na wala tusiache misingi yetu kwa mapambano na changamoto ndogo tu. Hakika ni wajibu wetu kuandaa nguvu zetu kubwa za kimaanawi na kufahamu kwamba sababu ya kurudi kwetu nyuma sio utekelezaji wa Uislamu, bali ni kinyume cha hayo. Hakika sababu ya kurudi kwetu nyuma ni kuacha kuufanyia kazi Uislamu!! Vinginevyo hakika dini yetu ni dini ya haki nayo ni njia ya kumkomboa mwanadamu na kumuokoa kutokana na adhabu na mateso kama alivyosema mshairi:

> "Wanasema katika Uislamu kuna dhulma
> kwa sababu,
> unazuia watu wake njia ya maendeleo, ikiwa
> ni kweli vipi waliendelea,
> watangulizi wake katika zama yake ya mwanzo,
> ikiwa dhambi ya Mwislamu leo ni ujahili wake,
> Uislamu unahusikaje na ujahili wa Mwislamu?"

Kisha hakika sisi katika mnasaba wa kumbukumbu ya utume wa Nabii ni lazima kila mmoja wetu afikiri yaliyo wajibu kwake kufanya katika kushikamana na ujumbe wa Nabii ﷺ) na sharia yake tukufu ambayo alikuja nayo. Vinginevyo sisi wakati huo tutakuwa kati ya wale wanaodai Uislamu nao hawautekelezi, na hivyo kuwa walengwa – Mwenyezi Mungu asijaalie hivyo – wa kemeo la aya:

يٰأَيُّهَا الَّذينَ ءامَنوا لِمَ تَقولونَ ما لا تَفعَلونَ ﴿٢﴾ كَبُرَ مَقتًا عِندَ اللَّهِ أَن تَقولوا ما لا تَفعَلونَ ﴿٣﴾

**"Enyi mlioamini! Kwa nini mnasema msiyo-yatenda. Ni chukizo kubwa kwa Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda." (Surat As-Saf 61:2-3)**

## UPANDE WA KIJAMII KATIKA MAISHA YA IMAMU HUSEIN عليه السلام

Hakika tunasherehekea kwa kuwakumbuka Maimamu watwaharifu عليهم السلام na tunaadhimisha minasaba ya Kiislamu ili tuungane na historia kongwe, na tuchukue kutoka humo mafunzo na mazingatio katika yale yatakayotunufaisha kwa wakati wetu na kujenga mustakabala wetu. Na inapopita kwetu kumbukumbu ya uzao au kufa shahadi kwa Imamu kati ya Maimamu, hakika sisi tunazingatia ili tuangaziwe na sira ya Imamu huyo na tuongoke kwa maelekezo yake na mwongozo wake.

Na kwa sababu sisi leo tupo katika kumbukumbu ya kuzaliwa bwana wa mashahidi Imamu Husein bin Ali عليه السلام, hakika sisi tutajaribu kuchukua dondoo katika maisha yake matukufu.

Na ikiwa riwaya za kihistoria zimehitalifiana katika kuainisha tarehe ya kuzaliwa kwake je, ilikuwa ni katika mwaka wa tatu au wa nne hijiria? Je ilikuwa ni mwezi wa Shabani au ni mwisho wa mwezi wa Rabiul-Awwal, na je ni katika siku ya kwanza au ya tano ya mwezi wa Shabani, hakika ikhitilafu hii tunakabiliana nayo katika mengi ya matukio na historia, na maelezo ya watu wake, na hakuna tatizo katika kutegemea riwaya tunayoona ina nguvu zaidi katika kusherehekea mnasaba wowote muhimu, maadamu lengo ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kuadhimisha alama Zake na kufaidika na uongofu wa mnasaba na utoaji wake.

### Upande wa Kijamii Katika Maisha ya Imamu:

Na tutazungumzia – katika mnasaba huu – upande kati ya pande za maisha, upande tajiri wenye manufaa, nao ni upande wa kijamii katika sira yake tukufu. Na kwa kudokezea tu kwa haraka upande huu tunaufupisha kwa nukta tatu:

1. Uhudhuriaji wa kijamii
2. Mfano wa kitabia
3. Kuzingatia sehemu za udhaifu katika jamii.

**Uhudhuriaji wa Kijamii:**

Mwanadamu kubeba malengo makubwa au kumiliki kiwango cha juu cha elimu hakuathiri kitu katika harakati za uhalisia wa maisha, kama hakujaambatana na uhudhuriaji wa kijamii, unaoonyesha njia mbele ya malengo hayo makubwa, na kufasiri elimu kwa kitendo kinachoonekana. Na kwa hiyo Manabii na Maimamu walikuwa wanaishi ndani ya mazingira ya watu, na wanaamiliana pamoja nao na hawakuwa wanajitenga katika vilele vya milima au katika mapango na mabonde wala hawakuwa wanajinyanyua na kujikweza kwa watu katika maghorofa marefu. Na vyovyote kitakavyokuwa kiwango cha jamii katika kutoendelea na ujahili, au katika uovu wa mazingira ya ufisadi na upotovu, hakika hayo hayaleti kisingizio cha kukimbia na kujitenga na watu kwa warekeibishaji wa kimungu.

Ni sahihi kwamba kuamiliana na watu ambao wanaishi katika hali ya ujahili na kutoendelea, au wanaonyenyekea katika mazingira ya ufisadi na upotovu, kunaweza kusababisha mengi miongoni mwa adha na taabu kwa watu wa Mungu, lakini hiyo ndio njia ya mabadiliko na marekebisho, kama ambavyo ni wasila wa kupata thawabu za Mwenyezi Mungu na radhi Zake. Imepokewa katika hadithi iliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwamba amesema: "Muumini ambaye anatengamana na watu na anasubiri katika adha zao ni bora kuliko muumini ambaye hatangamani na watu wala hasubiri juu ya adha zao."[36] Na katika hadithi nyingine ni kwamba ﷺ alimkosa mwanaume mmoja na akamuulizia akaja akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika mimi nilitaka kwenda kwenye mlima huu ili nijitenge humo na kufanya ibada. Mtume

[36] Al-Hindiy: Ali al-Mutaqiy katika *Kanzul-Umaali,* hadithi namba 686

wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema: "Mmoja wenu kusubiria saa katika anayoyachukia katika baadhi ya nchi za Kiislamu, ni bora kuliko ibada ya kujitenga miaka arobaini." Na katika ibara nyingine: "Miaka sitini."[37]

Na Imamu Husein عليه السلام amekuwa tangu mwanzo wa maisha yake ndani ya makuzi ya kijamii na ndani ya matukio, babu yake Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa ndio kitovu cha jamii na kiongozi wa juu, na baba yake عليه السلام alikuwa ni waziri wa Mtume na msaidizi wake mkuu, bali alikuwa ni nafsi yake kama inavyosema Aya ya mubahala.

Uwepo wake katika medani ni jambo la jumla na ni jambo la kawaida, kwa kuambatana kwake na babu yake Mtume ﷺ ambaye alikuwa anambeba mjukuu wake hata akiwa katika Swala, na anamchukua pamoja naye juu ya mimbari. Imepokewa kutoka kwa Abdillahi bin Buraidah kutoka kwa baba yake amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa anatuhutubia, mara akaja Hasan na Husein عليهما السلام huku wakiwa wamevaa kanzu mbili nyekundu wanaanguka na kusimama. Akateremka na akawachukua na akapanda nao kwenye mimbari."[38]

Na katika msimamo ule nyeti baina ya Waislamu na manaswara Mtume ﷺ alipowaita katika mubahala, Husein alikuwa amebebwa katika mabega ya babu yake. Yeye na ndugu yake ndio watoto waliotajwa katika kauli yake (swt):

**"…..فَقُل تَعالَوا نَدعُ أَبناءَنا وَأَبناءَكُم وَنِساءَنا وَنِساءَكُم وَأَنفُسَنا وَأَنفُسَكُم …..“**

**"…..Waambie: Njooni tuwaite watoto wetu na**

[37] Rejea iliyotangulia hadithi namba 11354

[38] Al-Sajastaniy: Abu Daud bin Suleiman bin al-Ash'athi katika *Sunan Abi Daudi*, Juz. 1, uk: 358 hadithi namba 1109

**watoto wenu, wanawake zetu na wanawake zenu, na nafsi zeti na nafsi zenu…..” (Surat Aali-Imran; 3:61)**

Na baada ya kufariki Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ Husein aliikuta nafsi yake ndani ya machungu ya familia yake na mateso ya mama yake Zahraa عليها السلام, alikuwa anaandamana naye katika mizunguko yake katika nyumba za Muhajirina na Answari akitafuta haki yake.[39]

Na historia inanukuu msimamo wa Imamu Husein عليه السلام katika mwanzo wa zama ya khalifa wa pili Umar bin Khattab, na Husein wakati huo alikuwa ndio kwanza anamaliza muongo wa kwanza katika umri wake:

Anapokea Ibnu Hajar al-Asqalaaniy katika kitabu chake *al-Iswabatu* kutoka kwa Yahya bin Said al-Answariy kutoka kwa Ubaidullahi bin Hunain: “Amenisimulia Husein bin Ali akasema: Nilimwendea Umar naye anahutubia juu ya mimbari nikapanda kwake nikamwambia: ‘Shuka kwenye mimbari ya baba yangu, na nenda kwenye mimbari ya baba yako.’ Umar akasema: “Baba yangu hakuwa na mimbari.” Na akanichukua akanikalisha pamoja naye nageuzageuza changarawe katika mikono yangu, alipoteremka akaenda nami katika nyumba yake akaniambia: Nani amekufundisha haya: Nikamwambia: Wallahi hakunifundisha yeyote. Akasema: Naapa kwa baba yangu natamani ungejaaliwa uwe unatutembelea mara kwa mara. Akasema: Siku moja nikamwendea, naye alikuwa amekaa faragha na Muawiya, na Ibnu Umar yuko mlangoni. Ibnu Umar akasimama bila kuingia ndani nami nikarejea. Baadaye akakutana nami akaniambia: Sijakuona. Nikasema: Ewe kiongozi mimi nilikuja, ulikuwa umekaa na Muawiya, basi nikarejea pamoja na Ibnu Umar. Akasema: Wewe una haki ya kuruhusiwa kuliko Ibnu

[39] Al-Qazuwiniy: Muhammad Kaadhim katika *Fatimahtu Zahraa minal mahadi ilaa llahad* uk: 407 chapa ya kwanza 1991 Muasasatu Nuur lilimatubuaati - Beirut.

Umar, hakika ameotesha unayoyaona katika vichwa vyetu Mwenyezi Mungu kisha nyinyi. Sanadi sahihi.[40]

Na katika kisa hiki kuna dalili za wazi zenye kuathiri, naye yuko katika umri mdogo anakwenda msikitini na anasema yaliyopo katika nafsi yake kwa khalifa, na anakiri kwamba kitendo hicho kimetokana na maamuzi yake mwenyewe, na hajaambiwa na yeyote, kisha anakwenda kumtembelea khalifa kwenye nyumba yake.

Na tunamuona Imamu Husein katika zama za khalifa Uthman ameshajiunga na jeshi la Kiislamu kwa ajili ya ufunguzi wa Afrika, na jeshi lilikuwa chini ya uongozi wa Uqubatu bin Naafi'i Abdi Shamsi, Abdillahi bin Nafii bin al-Harith, na humo kuna kundi la masahaba kama vile Abdillahi bin Abbasi, Ibnu Umar, Ibnu Ja'far, Hasan na Husein. Kama ambavyo Husein alishiriki katika vita vya Waislamu pamoja na Waajemi huko Twabristaan na pande zake, na jeshi lilikuwa chini ya uongozi wa Said bin al-Asi.[41]

Katika mkazo wa uwepo wake kijamii, majilisi yake ilikuwa katika msikiti wa Nabii, ambapo watu walikuwa wanamzunguka miongoni mwa wanaotafuta maarifa na watafuta elimu, na wenye shida, mtu alimuuliza Muawiya kwamba Husein anapatikana wapi? Akasema: Utakapoingia msikiti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ukiona mkusanyiko humo kuna watu wametulia kana kwamba juu ya vichwa vyao kuna ndege basi mkusanyiko huo ni wa Abu Abdillahi.[42] Na ushahidi katika nyanja hii katika maisha

[40] Al-Asqalaaniy: Ibnu Hajar katika *Iswabatu fiy tamyiizi swahabati* Juz. 2, uk. 77 chapa ya kwanza 1992 Daru al-Jili - Beirut.

[41] Al-Husniy: Hashim maarufu katika *Siratu al-Aimati al-Ithnaashara*, Juz. 2, uk. 16 daaru taaruf lilimatubuaati – Beirut 1990.

[42] Al-Qarashiy: Baaqir Saharif katika Maisha ya al-Imamu al-Husein, Juz. 1, uk: 137 chapa ya 1993 chapa ya Darul- Balagha – Beirut.

ya Imamu ni mwingi hakuna nafasi ya kuelezea.

**Mfano wa Kitabia:**

Katika kuamiliana pamoja na jamii, anakuta mbele yake sehemu zinazotofautiana kiwango na tabia, na baadhi yao wanakabiliwa na chuki ya kinafsi, au upotovu wa kimwenendo, unaosukuma kwenye ubaya na uadui kati ya yanayosababisha mwanadamu kulipiza kisasi, na kujitetea dhati yake mbele ya sehemu hizi, na kukasirika kutokana na vitendo vyake. Lakini watu wa Mungu kwa mioyo yao mikubwa na nafsi zao za juu wanaelewa hali hizo na wanakabiliana nazo kwa upole, utulivu na wema.

Na Imamu Husein عليه السلام alikuwa ni kilele katika nyanja hii, alikuwa – katika ambayo wapokezi wamekusanya – haamiliani na muovu kwa ubaya wala na mwenye dhambi kwa dhambi yake, bali alikuwa anawahurumia kwa wema wake na ihsani yake. Jambo lake katika hilo ni jambo la babu yake Mtume صلى الله عليه وآله وسلم ambaye aliwaenea watu wote kwa tabia yake njema na fadhila zake na alijulikana kwa hali hii na ikaenea kwake, na baadhi ya watumwa wake walitumia fursa hii. Walikuwa wanakusudia kufanya ubaya kwake, ili waneemeke kwa uhusiano wake na wema wake. Wanasema wanahistoria: Hakika mmoja wa watumwa wake alifanya kosa kwake, kosa linalopelekea kutiwa adabu, akaamuru aadhibiwe, mtumwa akasema: Ewe kiongozi wangu, hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Na wenye kuzuia hasira."

Imamu akaamiliana naye kwa tabasamu la ukunjufu na akasema: "mwacheni, nimeshazuia hasira yangu…"
Na mtumwa anafanya haraka "na wenye kuwasamehe watu."
Akasema: Nimeshakusamehe.
Mtumwa akataka ziada ya wema kwa kusema: "Na Mwenyezi Mungu anawapenda wanaofanya wema."
Akasema: "Wewe uko huru kwa ajili ya Mwenyezi Mungu." Kisha akaamuru apewe zawadi nzuri inayomtosheleza kuomba na

kuuliza watu.[43]

Na Marwan aliomba msaada wa uombezi kwake na kwa ndugu yake, naye ni kati ya maadui zao wakubwa baada ya kushindwa vita vya jamali na akaomba kwao uombezi kwa baba yao waka-kaa faragha naye na wakamzungumzia kuhusu jambo lake na wakasema: "Atakupa baiya ewe Amirul-Muuminina."

Akasema: "Je hakunipa baiya baada ya kuuliwa Uthman, sina haja ya baiya yake, hakika ni mkono wa kiyahudi, kama atanipa baiya kwa mkono wake basi atafanya hiyana kwa kidole chake cha shahada." Hawakuacha kumbembeleza hadi akamsamehe.[44]

**Kuzingatia sehemu za madhaifu katika jamii:**

Unadhihirika ubinadamu wa mwanadamu na kusadikisha imani yake kwa kuwajali kwake wenye haja na mafakiri katika jamii vyovyote atakavyofikia mwanadamu katika elimu, au akijitahidi katika ibada. Hakika hautotimia ubinadamu wake wala hautasihi uswalihina wake atakapopuuza sehemu za udhaifu katika jamii. Je hajasema Mola Wetu:

أَرَءَيتَ الَّذى يُكَذِّبُ بِالدّينِ ﴿١﴾ فَذٰلِكَ الَّذى يَدُعُّ اليَتيمَ ﴿٢﴾ وَلا يَحُضُّ عَلىٰ طَعامِ المِسكينِ ﴿٣﴾

**"Je, umemuona ambaye anakadhibisha dini? Huyo ni ambaye humsukuma yatima. Wala hahimizi kumlisha masikini." (Surat Al-Ma'un; 107:1-3)**

Mwenye kuwapuuza mayatima na asiyejali njaa ya mafakiri ni

[43] Rejea iliyotangulia uk: 124
[44] Rejea iliyotangulia uk: 126

mwenye kukadhibisha dini, na si mkweli katika madai yake ya uswalihina, hata kama akijitahidi sana katika swala yake na ibada yake, bali anastahili maangamio na adhabu:

فَوَيلٌ لِلمُصَلّينَ ﴿٤﴾ الَّذينَ هُم عَن صَلاتِهِم ساهونَ ﴿٥﴾ الَّذينَ هُم يُراءونَ ﴿٦﴾ وَيَمنَعونَ الماعونَ ﴿٧﴾

**"Basi ole wao wanaoswali. Ambao wanasahau swala zao. Ambao wanafanya ria. Na wanazuia msaada." (Surat Al-Ma'un; 107:4 -7)**

Imamu Husein عليه السلام ni kama Ahlul-Bayt عليهم السلام, walikuwa wanaishi kwa ajili ya watu zaidi kuliko wanavyoishi kwa ajili yao:

"..... وَيُؤثِرونَ عَلىٰ أَنفُسِهِم وَلَو كانَ بِهِم خَصاصَةٌ....."

**"…Na wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji." (Surat Al-Hashr; 59:9)**

Na tangu mwanzo wa maisha yake, naye ni mtoto mdogo alishiriki na familia yake kufunga siku tatu na hawakuwa wanafuturu humo ila kwa maji tu, kwa sababu wakati wakufuturu walikuwa wanawaendea wenye kuhitaji na wanamwaachia chakula chao. Na kwao imeshuka kauli yake (swt):

وَيُطعِمونَ الطَّعامَ عَلىٰ حُبِّهِ مِسكينًا وَيَتيمًا وَأَسيرًا ﴿٨﴾ إِنَّما نُطعِمُكُم لِوَجهِ اللَّهِ لا نُريدُ مِنكُم جَزاءً وَلا شُكورًا ﴿٩﴾

**"Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima na mateka. Hakika tunawalisha kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu tu. Hatutaki kwenu malipo wala shukurani." (Surat Al-Insan; 76:8–9)**

Na katika maisha yake yote alikuwa ni kimbilio la mafakiri na wasio nacho, na kimbilio la wenye shida, na alikuwa ni wazo la wageni wanaokwenda kwake kwa zawadi zake na utoaji wake.
Anasema Kamalu Diyn bin Twalaha: "Ilikwishaenea kunukuliwa kwake kwamba alikuwa anamkirimu mgeni na anampa mwenye kuomba, anaunga udugu, anamsaidia mwenye kuomba, na anamvisha asiye na nguo, anamshibisha mwenye njaa, anampa mwenye kudaiwa, anamtia nguvu mnyonge, anamhurumia yatima na anamtosheleza mwenye haja na haikumfikia mali ila anaigawa."[45]

Na wanasema wanahistoria kwamba hakika alikuwa anabeba katika giza la usiku mifuko iliyojaa chakula na fedha kwenda kwenye nyumba za wajane, mayatima na maskini, hadi hilo liliathiri mgongo wake, na alikuwa anapelekewa vitu vingi na hasimami hadi avigawe vyote."[46]

Usama bin Zaid aliugua maradhi yake ambayo humo alifariki. Imamu aliingia kwake kwa ajili ya kumtembelea. Alipokaa na akatulia, Usama akasema: Eee huzuni yangu!

- Ni ipi huzuni yako ?
- Deni langu nalo ni elfu sitini
- Basi ni juu yangu
- Naogopa nitakufa kabla ya kulipwa?
- Hutokufa hadi nikulipie.

Imamu akajitolea kulilipa kabla ya kufariki kwake, na alimsamehe Usamah kwani hakumpa baba yake baiya, na hakumlipa kwa ubaya bali alimfanyia wema.

Na siku moja alipitia kwa masikini wa Swaffah, aliwakuta

[45] Al-Qarashiy: Baaqir Saharif: Katika *Hayatul-Imamu al-Hasan*, uk: 127 chapa ya kwanza 1993 Darul al- Balaagha – Beirut
[46] Rejea iliyotangulia uk: 128

wanakula. Wakamkaribisha chakula, akashuka kwenye kipando chake na akala pamoja nao, kisha akawaambia: Nimewaitikia basi nanyi niitikieni. Wakakubali maneno yake na wakaenda naye kwenye nyumba yake akasema عليه السلام kumwambia mke wake Rubab: Toa ulichokiweka. Akatoa aliyokuwa nayo katika fedha na akawapatia.[47]

Haya ni kidogo kati ya rundo na machache kati ya mengi na tone kati ya bahari katika maisha ya Imamu Husein عليه السلام, na tunaposherehekea uzao wake mtukufu hakika sisi tunalinganiwa kuiga uongofu wake na kufuata mwenendo wake, kwa kuzingatia hali za jamii yetu, na kukithirishe uhudhuriaji wetu katika medani ya jamii na tuvuke hali ya ubinafsi na kujitenga na kukaa kando, ili tuchangie katika kujenga nchi zetu na kuhudumia mambo ya umma wetu na kushirikiana katika wema na uchamungu.

## UCHAGUZI WA MUME BAINA YA BINTI NA WATU WAKE

Kila yanapokuwa maamuzi ambayo mwanadamu anataka kuyachukua yana athari kubwa zaidi katika maisha yake anahitajia utafiti zaidi na utulivu kabla ya kuchukua maamuzi, ili aepuke kuakisi hatari wa kosa katika maamuzi hayo. Ama ikiwa maamuzi yanahusiana na jambo jepesi, basi asiikalifishe nafsi yake taabu ya ziada katika kutafakari humo. Na huenda katika maamuzi muhimu zaidi ambayo mwanadamu anayachukua ni maamuzi ya kuchagua mshirika wa maisha, ili kuanzisha maisha yake ya kifamilia ya kijamii, kwa kuwa hayo yana athari pana yenye kuendelea katika mustakabali wake, na kwa kuwa maisha ya ndoa yana umuhimu na unyeti, yanagusa pande zote za shakhsiya ya mwanadamu.

Ikiwa ameafikiwa kuchagua na Mwenyezi Mungu akamruzuku

[47] Rejea iliyotangulia, uk. 125.

mke mwema, anaishi maisha mema. Ama akipata balaa ya kupata mke mbaya basi atakabiliwa na maisha mabaya na maisha machungu, na kwa sababu hiyo muumini anamwelekea Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa dua “Mola wetu tupe katika wake zetu na wanetu yaburudishayo macho.” (Suratul-Furqan: 74). Na wakati wa kufikiria katika uchaguzi wa mshirika mwanadamu anahitaji usalama na uwazi wa vipimo vya kuchagua, ni kwa msingi gani anachagua? Na ni sifa zipi zina-pasa kutimia katika upande mwingine?

Na mafunzo ya Uislamu yanamwelekeza mwanadamu kwenye vipimo sahihi ambavyo ni wajibu aviweke mbele ya macho yake wakati wa kuchagua, na tunahitajia utafiti maalumu ili kuelezea na kuzungumzia juu yake. Na ambayo tunataka kuyatilia mkazo katika maudhui haya ni uamuzi wa binti katika kuchagua mshirika wa maisha yake. Mambo kwake ni muhimu sana kuliko mwanaume, hiyo ni kwa sababu fursa ya mwanaume katika kutatua kosa katika uamuzi huu ni kubwa zaidi kuliko fursa ya mwanamke, hamiliki haki hii ya kisharia ila katika hali finyu.

Hapa binti anahitajia zaidi kutafakari wakati wa kuchagua, na tatizo wengi wa wasichana hakika wao wanatumbukia katika athari kwa sababu za matamanio ya kihisia kwa daraja kubwa zaidi, ambapo binti anaathirika aghlabu kwa anayoyasikia miongoni mwa maneno ya kutongoza na mapenzi na anahadaika na baadhi ya muonekano wa harakati za ujana, ambapo anaona nafsi yake inaishi duara la pembeni katika nyumba ya familia yake anavutika kwa fursa ya karibu zaidi ili kujenga maisha yake ya kijamii ya baadaye.

Kwa kawaida haiwezekani kujumuisha. Kuna mabinti ambao wanamiliki upevu na uelewa na wanavuka athari hizi. Na ulinzi wa mustakabali wa binti, na kuongoza maamuzi ya uchaguzi wake, Uislamu umempa walii wa jambo lake nafasi ya maamuzi haya kwa mujibu wa rai ya jopo la mafakihi. Na hilo litabainika

zaidi kupitia nukta zifuatazo:

**Mwanamke thayibu (mtu mzima):**

Ikiwa mwanamke alikwishaolewa na akaishi maisha ya ndoa, yaani alishaingiliwa na mume wake kisha akaachana naye, hakika wakati huo maadamu ni baleghe na mwelewa na ameshapitia tajiriba ya ndoa, maamuzi ya kuchagua mume mpya yanakuwa katika mamlaka yake na wala hamiliki yeyote haki ya kumpinga na kumzuia. Hii ni katika rai ya mafakihi wa Kishia na kihanafi. Yeye sio mgeni katika maisha ya ndoa, na inategemewa kwamba amenufaika na tajiriba iliyotangulia na maamuzi yake yanatokana na ukomavu na ujuzi na sio msukumo wa kihisia na matamanio. Hakika haya hayamhusu ambaye amejitenga na mume wake au aliyefiwa na mume wake kabla ya kuingiliwa, kwa sababu ndoa tu haimfanyi awe thayibu (mtu mzima).

Na ikiwa Uislamu umeafiki rai hii – haujampa yeyote katika familia yake haki ya kumzuia kuchukua maamuzi, hii haimaanishi kutohitajia ushauri wao, na kunufaika na rai yao, na hivyo mafakihi wamesema hakika inapasa kwa mwanamke ambaye anamiliki maamuzi yake, atake ruhusa kwa baba yake au babu yake, na kama hawapo basi kaka yake na kama wako wengi anachagua mkubwa zaidi.[48]

**Binti bikra**:

Ama binti bikra ambaye hajawahi kuingia katika tajiriba ya maisha ya ndoa kuna rai mbili zilizo dhahiri:

**Rai ya kwanza:** Kwamba yeye ana maamuzi kamili ya kuchagua, na wala hahitaji idhini ya kutoka kwa baba yake, babu yake au yeyote, na kwa rai hii limesema jopo la mafakihi wa Kishia

[48] Al-Yazidi: Sayid Muhammad Kaadhim Twabatwabaiy katika *al-Uruwatu al-wuthiqah auliyaul Aqid* – mas'ala namba 14

waliotangulia, kama vile Sayidi al-Murtadhwa al-Iskaafiy, al-Hiliy, al-Mufidiy, al-Dailamiy, al-Muhaqiq, al-Fadhil na Mashahidi wawili.[49] Na katika Mafakihi wa zama hizi ni Sayid Sabzawariy, Sheikh Muhammad Amin Zainul-Abidini, Sheikh Muhammad Jawad Mughuniya. Na wenye rai hii katika maimamu wa Kisunni ni Abu Hanifa na Abu Yusufu.

**Rai ya pili:** Ni sharti kuwe na idhini ya walii wa binti nayo ni rai ya mafakihi wengi wa Kishia wa zama hii kwa fat'wa au tahadhari ya wajibu. Na vilevile ni rai ya jamhuri ya Ahlul-Sunna. Walii wa binti ambaye inachukuliwa rai yake katika fikihi ya Shia ni baba au babu wa upande wa baba tu, ambapo inatosha kuafiki mmoja wao na hakuna uwalii kwa wasiokuwa wao kwa binti aliyefikia umri wa uelewa. Wakati ambapo duara la uwalii katika nyanja hii kwa Ahlus-Sunna linawaenea pia jamaa wa mwanamke: baba kisha watoto kisha ndugu kisha baba wadogo katika ikhitilafu baina yao katika mpangilio wa mawalii.

**Hekima ya idhini ya walii:**

Imetangulia kuashiria kwamba sharia ya kuweka sharti la idhini ya walii katika kupitisha ndoa ya binti bikra, ni kwa ajili ya kuongoza maamuzi yake, ili uchaguzi usiwe unatokana na hali ya kihisia bila ya kuhakiki kufaa anayetaka kuwa mwenza wake. Na hususan katika jamii inayojilinda, hakika binti hayuko wazi katika jamii ya wanaume, ili kujua mwenendo wa anayemchumbia, kiwango chake na kiasi cha kufaa kwake, na baba yake au babu yake anatakiwa kuchunga maslahi yake na kupendelea kwao mafanikio yake, kwa hiyo rai yao inaingilia katika kupitisha ndoa yake.

Ama wasiokuwa wao hawana haki ya kumzuia, kulingana na fikihi ya Shia. Ndio ni mustahabu kwa binti kumuomba ushauri anayemwamini katika jamaa zake lakini si haki kwa yeyote

[49] Shiraziy: Sayid al-Huseiniy katika *al-Fiqihi*, Juz. 64, uk. 20

kumzuia. Na wanayoyafanya baadhi ya jamaa wa karibu katika kuingilia jambo la ndoa ya dada yake, binti wa kaka yake au binti wa dada yake au binti wa Ami yake au mfano wa hayo katika kuzuia na kukwaza, ni uingiliaji wa kitoto sharia haikubali. Anasema al-Faqihi Sayid Muhammad Said al-Hakim:

"Hana yeyote katika jamaa pamoja na kutokuwepo baba au babu wa upande wa baba, haki ya usimamizi wa aliyebaleghe ambaye ni bikra ukiachilia wengine, bali anakuwa huru mwenyewe, na wanayoyafanya baadhi kwa mazoea ya jamaa kuingilia na kumzuia mwanamke anayoyataka au anayoyataka walii wake pamoja na kuwepo kwake ni dhulma iliyo wazi, na ni kutoka katika vipimo vya kisharia na kuvunja mipaka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na ni kupuuza hukumu Zake katika waja Wake. Nayo ni kati ya sababu za ufisadi mkubwa, ambao unaweza kusababisha kulipiza kisasi ambako hakuna mwisho mwema. Unabeba ufisadi na aibu yake duniani na akhera, na athari yake na majukumu yake katika akhera. 'Siku ambayo rafiki hatomfaa rafiki yake kwa chochote wala wao hawatonusuriwa.'"[50]

Hakika baadhi ya wasichana – kama nilivyoona – wanakasirika kwa vitendo vya walii wao kuchukua nafasi hii, na wanapatwa na hasira kali dhidi yao wakati walii anasimama dhidi ya raghaba zao katika kuchagua mume. Lakini kinachotakiwa kwa binti ni kufahamu hukumu hii ya kisharia, na kufahamu nafasi ya baba yake ambaye amemlea na amebeba jukumu la uangalizi wake, naye ni mwenye kujali mafanikio yake na mustakabali wake, naye ni mwingi wa tajiriba na ujuzi kuliko yeye na kujua hali ya jamii na watu wake, na anapomkataa mwenye kuchumbia anayekuja kumposa hakika ni kutokana na kutokuwa ni laiki yake na kutofaa kwake.

---

[50] Al-Hakim: Sayyid Muhammad Twabatwabaiy katika *al-Ahkaami al-Fiqihiya aqidu Nikaahi wa auliyaai al-aqd*i, uk: 356, mas'ala namba 9 chapa ya tatu 1997 Darul-Swafuwatu - Beirut.

Na inatokea katika baadhi ya hali kwamba binti anang'ang'ania katika raghaba yake katika kuolewa na mposaji maalum, pamoja na kukataa baba yake, na hapo baba analazimika kuacha rai yake, na kukubali matakwa yake, pamoja na kumbebesha jukumu la mustakabali wake, hutokea nini baada ya hapo?

Mara nyingi inatokea binti mwenyewe anajikuta katika matatizo pamoja na mtu ambaye hana muamala mzuri pamoja naye, na wala hana sifa inayotakiwa na tabia inayofaa. Anatambua baada ya kupitwa na muda kwamba alikuwa ana makosa katika kuchagua, na analipa thamani kubwa.

**Kutumia haki vibaya:**

Lakini baadhi ya baba wanaweza kutumia vibaya haki hii. Anapinga uchaguzi wa binti yake bila ya sababu, na anamzuia kuolewa pamoja na kwamba aliyekuja kwake ni laiki yake na anafaa, jambo ambalo linasababisha kuchelewa kwa muda mrefu na anaweza kuwa katika orodha ya wasiolewa. Na inaweza kuwa sababu ya msimamo huo wa baba ni baadhi ya vipimo vya kimaada na maslahi, ambayo anataka yatimie katika kuposwa binti yake, kama vile kuwa tajiri au kuwa katika kiwango cha kazi maalumu. Au kwa sababu baba anataka kumuozesha binti yake kwa mtu maalumu, katika jamaa zake au marafiki zake, au kwa sababu baina ya baba na mama wa binti kuna tatizo, kama vile kuwa ni mtalaka wake, au amemlea tu. Hivyo anamaliza tofauti yake pamoja naye kwa hisabu ya binti yake. Na imeonekana kwamba mmoja wa wazazi alikuwa na tamaa ya pato la binti yake anayefanya kazi na kwa hivyo anaweka vikwazo na kucheleweshа ndoa yake, kwa kutunga sababu na visingizio mbele ya waposaji.

Hakika mfano wa hali hizi unaweza kutokea, lakini haipasi kuziangalia. Hakika Uislamu unapokonya haki ya walii ambaye anaitumia vibaya, hakika ni haki kwake kuzuia na kupinga ikiwa mposaji sio laiki yake na hafai. Ama akiwa ni laiki yake na

anafaa, na pamoja na hivyo baba akapinga, hakika haki yake katika kupinga na uwalii wake kwa binti hapa unaporomoka. Wanasema mafakihi: "Walii akimzuia kuolewa na anayefaa ilihali ndiye raghaba yake, basi idhini yake inaporomoka."[51]

"Maulamaa wameafikiana kwamba si ruhusa kwa walii kumzuia anayemsimamia, na kumdhulumu kwa kumzuia kuolewa, akitaka kuolewa na anayefaa kwa mahari ya mfano wake. Akimzuia katika hali hii ni haki kupeleka suala lake kwa kadhi ili amuozeshe. Na wala uwalii hauhami katika hali hii kwenda kwa walii mwingine atayechukua nafasi ya walii huyu dhalimu, bali unahamia kwa kadhi moja kwa moja, kwa sababu kizuizi ni dhulma, na mamlaka ya kuondoa dhulma ipo kwa kadhi."[52]

Na Qur'ani tukufu inakataza kumzuia mwanamke, yaani kuzuia kuolewa kwake, anasema (swt):

وَإِذا طَلَّقتُمُ النِّساءَ فَبَلَغنَ أَجَلَهُنَّ فَلا تَعضُلوهُنَّ أَن يَنكِحنَ أَزوٰجَهُنَّ إِذا تَرٰضَوا بَينَهُم بِالمَعروفِ ذٰلِكَ يوعَظُ بِهِ مَن كانَ مِنكُم يُؤمِنُ بِاللَّهِ وَاليَومِ الآخِرِ ذٰلِكُم أَزكىٰ لَكُم وَأَطهَرُ وَاللَّهُ يَعلَمُ وَأَنتُم لا تَعلَمونَ

**"Na mtakapowapa wanawake talaka na wakafikia muda wao, msiwazuie kuolewa na waume zao, ikiwa wamepatana kwa wema. Hayo anaonywa nayo yule miongoni mwenu, anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hayo ni mazuri mno kwenu na safi kabisa. Mwenyezi Mungu anajua, na ninyi hamjui" (Surat Al-Baqara; 2:232)**

---

[51] Al-Yazidiy: Sayyid Muhammad al-Kaadhim Twabatwabaiy *katika al-Uruwatu al-Wuthiqah, auliyaul- aqid* - mas'ala namba 1

[52] Sabiq: Sayid katika *Fiqihi Sunna*, Juz. 2, uk: 136 chapa ya tatu 1977 Darul-Kitabu al-Arabiiy - Beirut

Hakika Mwislamu yeyote anayeamini kwamba Mwenyezi Mungu ndio Muweka sharia na Msimamizi na Siku ya Kiyama ni ahadi ya hisabu na malipo, ni juu yake kuwaidhika kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na wala hasababishi kuzuia ndoa ya binti yake bila ya sababu ya kisharia, kwa sababu hiyo ni dhulma kwake, na ni sababu ya kutumbukia katika ufisadi na matatizo katika jamii, na kwa sababu hiyo mwisho wa aya unasema: “Hayo ni mazuri mno kwenu na safi kabisa.”

Na zimepokewa riwaya na hadithi nyingi zinazohadharisha kuzuia kuwaozesha mabinti na kuwachelewasha kwake, kwa sababu hiyo inampotezea fursa inayofaa, kama inavyosababisha madhara ya kinafsi na kitabia katika jamii. Ali bin Asbaati alikuwa ni kati ya wafuasi wa Imamu Muhammad al-Jawad عليه السلام, na alikuwa na mabinti anaotaka kuwaozesha kwa maulamaa watukufu mfano wake, hiyo ikawa ni sababu ya kuchelewa kuwaoza, akaandika barua kwa Imamu al-Jawadi عليه السلام, Imamu akamjibu: “Nimefahamu uliyoyataja katika jambo la mabinti zako na kwamba wewe humpati yeyote aliye mfano wako, hivyo usisubiri katika hilo Mwenyezi Mungu akuhurumie, hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم amesema: ‘Anapokujieni mnayeridhia tabia yake na dini yake basi muozesheni, kama msipofanya hivyo kutatokea fitina katika ardhi na ufisadi mkubwa.’”[53]

Na katika hadithi nyingine: “Mwenye kuposa kwenu na mkaridhia dini yake na uaminifu wake basi muozesheni, msipofanya itatokea fitina katika ardhi na ufisadi mkubwa.”[54] Na kutoka kwa Ali عليه السلام amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم: “Anapokujieni mnayeridhia tabia yake na dini yake basi

[53] Al-Huru al-Amiliy: Muhammad bin al-Hasan katika *Tafswil Wasailu Shi’ah*, Juz. 20, uk: 76 chapa ya kwanza 1993 Muasasatu Aali al-Bait liihiyai turathi – Beirut.
[54] Rejea iliyotangulia uk: 77

muozesheni." Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hata kama ni duni katika nasaba yake? Akasema: "Atakapokujieni mnayeridhia dini yake na tabia yake, basi muozesheni msipofanya hivyo itakuwa fitina katika ardhi na ufisadi mkubwa."[55]

Na siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu alipanda mimbari akamshukuru Mwenyezi Mungu na akamhimidi kisha akasema: "Enyi watu hakika Jibril amenijia kutoka kwa Mpole na Mjuzi amesema: Hakika mabikira ni sawa na matunda juu ya mti, na litakapoiva tunda lake na lisichumwe linaharibiwa na jua na litapeperushwa na upepo." Akasimama mwanaume akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu: Nani tutamuoza? Akasema: "Wanaofaa." Akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu na wanaofaa ni akina nani? Akasema: "Waumini baadhi yao ni laiki ya baadhi yao, waumini baadhi yao ni laiki ya baadhi yao."[56]

Vipimo vya saizi na kufaa: ni dini na tabia njema, na zitakapotimia kwa mwenye kumposa binti hakuna sababu kwa walii wake kuchelewesha au kuzuia. Na inaonekana kukariri sana na tahadhari katika hadithi kwamba kuzuia ndoa kunasababisha fitina na ufisadi mkubwa katika jamii.

## MWANACHUONI WA KIDINI NA KUITAKASA NAFSI

(SHEIKH MANSUR AL-BAYAATI NI MFANO)

Jukumu kubwa na lengo la msingi la dini ni kuitakasa nafsi, na katika hadithi katika wadhifa wa Mtume ﷺ, Qur'ani tukufu inataja kutakasa kama kazi ya kwanza, anasema (swt):

"هُوَ الَّذى بَعَثَ فِى الأُمِّيّنَ رَسولًا مِنهُم يَتلوا عَلَيهِم ءايٰتِهِ وَيُزَكّيهِم
وَيُعَلِّمُهُمُ الكِتٰبَ وَالحِكمَةَ ....."

[55] Rejea iliyotangulia uk: 78
[56] Rejea iliyotangulia uk: 61

> **"Yeye ndiye aliyempeleka Mtume kwenye watu wasiojua kusoma, aliyetokana na wao awasomee aya Zake, na awatakase. Na awafunze Kitabu na hekima….." (Surat Al-Jumu'a; 62:2)**

Na yanakaririwa mfano wa hayo katika sehemu tatu zingine.

Na utakaso ni hekima ya vipengele vingi vya sharia ya Uislamu. Kuchukua zaka, sadaka ni kwa ajili ya kuleta utakaso katika nafsi za wenye kupewa mawaidha. Anasema (swt):

"خُذ مِن أَموٰلِهِم صَدَقَةً تُطَهِّرُهُم وَتُزَكّيهِم بِها ….."

**"Chukua katika mali zao sadaka uwasafishe na uwatakase kwayo." (Surat At-Tawba; 9:103).** Na kuinamisha macho dhidi ya yale yaliyoharamishwa, na kudhibiti matamanio ya kijinsia ni njia ya kutakasa vilevile, anasema (swt):

"قُل لِلمُؤمِنينَ يَغُضّوا مِن أَبصٰرِهِم وَيَحفَظوا فُروجَهُم ذٰلِكَ أَزكىٰ لَهُم ….."

> **"Na waambie waumini wanaume wainamishe katika macho yao na wazilinde tupu zao. Hayo ni usafi zaidi kwao….." (Surat An-Nur; 24:30)**

Na utakaso ni njia ya kufaulu na kushinda: **"Hakika amefaulu aliyeitakasa" (Surat Shamsi; 91:9)**, pamoja na angalizo kwamba aya hizi zimekuja zikiwa ni jawabu la viapo alivyoapa Mwenyezi Mungu katika mwanzo wa Surat Shamsi, anasema (swt):

وَالشَّمسِ وَضُحىٰها وَالقَمَرِ إِذا تَلىٰها وَالنَّهارِ إِذا جَلّىٰها وَاللَّيلِ إِذا يَغشىٰها وَالسَّماءِ وَما بَنىٰها وَالأَرضِ وَما طَحىٰها وَنَفسٍ وَما سَوّىٰها فَأَلهَمَها فُجورَها وَتَقوىٰها

> **"Naapa kwa Jua na mwangaza wake. Na kwa**

**mwezi unapolifuatia. Na kwa mchana unapolidhihirisha. Na kwa usiku unapolifunika. Na kwa mbingu na kuzijenga kwake. Na kwa ardhi na kuitandaza kwake. Na kwa nafsi na kuilinganisha kwake. Akaifahamisha uovu wake na takua yake." (Surat Ash-Shams 91:1-8)**

Baada ya viapo hivi vingi kwa vitu muhimu katika ulimwengu linakuja jawabu la kiapo **"Hakika amefaulu mwenye kuitakasa."** Jambo ambalo linaonyesha juu ya umuhimu wa ukweli huu na unyeti wake. Na katika aya nyingine anasema (swt): "Amefaulu aliyejitakasa" (Suratul-Alaaa: 14).

Na Malaika alipombashiria Bibi Mariyam binti Imran kwa kumzaa Nabii Isa عليه السلام alitosheka na kumwelezea kwamba ni mtoto mwema.

قالَ إِنَّما أَناْ رَسولُ رَبِّكِ لِأَهَبَ لَكِ غُلٰمًا زَكِيًّا

**"Akasema: Hakika mimi ni mjumbe wa Mola Wako ili nikupe mwana mtakatifu." (Surat Maryam 19:19)**

**Maana ya utakaso:**

Utakaso ni lengo la ujumbe na ni jukumu la Manabii, na ni hekima ya sharia, ni njia ya kufaulu na kushinda. Una maana gani na nini makusudio yake?

Tazikiya (utakaso) linatokana na *zakau* na *zakaatu*. Amesema katika *Lisanul- Arab*: Ni kwa maana ya kustawi. Imekuja katika maneno ya Imamu Ali عليه السلام: "Mali inapungua kwa kuitoa na elimu inaongezeka kwa kuitoa." Na kila kitu kinachoongezeka na kumea basi kinastawi na kunawiri.

Na *Zakaatu* pia inamaanisha: Utwahara. Na kauli yake (swt): *Tuzakiihim Bihaa* wamesema: unawatakasa kwayo. Kama am-

bavyo linamaanisha: wema. Amesema al-Farau: *Zakatu* ni wema, na vilevile kauli yake (swt): "Na tukampa huruma itokayo kwetu na utakaso." Amesema wema. Lakini Mwenyezi Mungu anamtakasa amtakaye yaani anamfanya kuwa mwema. Na katika hadithi ya Imamu al-Baaqir عليه السلام amesema: "Utakaso wa ardhi ni kukauka kwake" anakusudia utwahara wake kutokana na najisi kama vile haja ndogo na mfano wake kwa kukauka na kuondoka athari yake.[57]

Na imekuja katika *Majimaul-Bahrain*: *Tazikiya*: Ni kutakasika na tabia mbaya. Na katika *al-Gharib*: "Amefaulu mwenye kuitakasa" yaani amefaulu aliyetwaharisha nafsi yake kwa amali njema. Kauli yake (swt): "Je, umeuwa nafsi isiyo na hatia" yaani twahara. Na kauli yake (swt): "Kijana mwema" yaani ni mwenye kutwaharika kutokana na madhambi. Na umekaririwa utajo wa *zaka* katika Kitabu na Sunnah, nao ima unatokana na ustawi kwa sababu italeta baraka katika mali na kuongezeka kwake. Na ima unatokana na utwahara kwa sababu mali inatwaharika kutokana na uchafu, na nafsi bakhili inatwaharika kutokana na ubakhili.[58] Na kutokana na maana yake ya kilugha yanabainika makusudio yake, na kwamba ni kuitakasa nafsi na kuirekebisha na kustawi utashi na mielekeo ya kheri kwayo.

**Mwanachuoni wa kidini:**

Na ikiwa dini inalenga kuleta hali ya utakaso katika nafsi ya mwanadama, hakika mafanikio yake na utekelezaji wake hakika unatimia kwa kujua uongofu wa kidini na maelekezo yake, na kwa kuwa karibu na vyanzo vyake na mazingira yake. Na mwanachuoni wa kidini kwa kujua kwake juu ya mafunzo, na kwa kuwasiliana daima na mafuhumu na nususi za kidini, hakika ni mbora zaidi na anafaa zaidi kumiliki hali hii ya utakaso wa

[57] Ibnu Mundhir katika *Lisanu al-Arab al-Muhit*, Juz. 3, uk: 36- Daru Lisanu al-Arab – Beirut 1988
[58] Twariyhy: Fakhar Diyn katika *Majiumaul-Baharain*, Juz. 1, uk: 203 - 205

nafsi. Na vilevile kwa kuwa yeye yuko katika nafsi ya kigezo kwa wengine, na mlinganiaji na mwelekezaji wao, ni lazima yeye asifike na ajipambe na yale anayowalingania wengine.

Na hapa nususi za kidini zinatia mkazo dharura ya kupatikana kwa mwanachuoni wa kidini utwahara wa nafsi na usafi wake, na asiwe amening'inia katika matamanio na shahawati, au amejifungia kwenye hasira, anasema (swt): **"Hakika wanaomuogopa Mwenyezi Mungu katika waja Wake ni wanachuoni." (Suratu Fatwir: 28).**

Na imepokewa kutoka kwa Amirul-Muuminina عليه السلام kwamba amesema: "Mwanachuoni hawi ni mwanachuoni hasa mpaka asimhusudu aliye juu yake, wala asimdharau aliye chini yake, wala asichukue chochote katika elimu yake miongoni mwa manufaa ya kidunia."[59]

Na kutoka kwake vilevile عليه السلام:

"Mwenye kuifanya nafsi yake ni kiongozi wa watu basi na aanze kuifunza nafsi yake kabla ya kumfundisha mwingine. Na awaadabishe kwa sira yake kabla ya kuwaadabisha kwa ulimi wake. Na awe mwalimu wa nafsi yake mwenyewe na mwadabishaji wake kabla ya kuwa mwalimu wa watu na mwenye kuwaadabisha wao."[60]

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم kwamba amesema: Katika usiku niliopelekwa Israi nilipita kwa watu wanaokatwa midomo yao kwa mikasi ya moto. Nikasema: Ni nani hawa ewe Jibrail? Akasema: "Hawa ni makhatibu wa umma wako ambao wanasema wasiyoyatenda."[61]

---

[59] Al-AmadiyTamiymiy: Abdul-Wahdi katika *Ghurararul-Kalimi*, Juz. 2, uk. 270, Muasasatu al-Ilimiy lilimatubuati - Beirut

[60] Al-Musawiy: Sharifu Ridhaa katika *Nahjul-Balaghah Qiswaril-hikam* namba 73

[61] Raishahariy: Muhammady katika *Mizanul-Hikima*, Juz. 6, uk. 514

Na katika hadithi kutoka kwa Imamu Ja'far Sadiq عليه السلام: "Atasamehewa jahili dhambi sabini kabla ya kusamehewa mwanachuoni dhambi moja."[62]

**Kigezo chema:**

Katika siku hizi tumepata msiba mkubwa, msiba wa kumpoteza mwanachuoni mchamungu mwenye kujinyima, kilele cha kigezo chema na utakasifu wa nafsi, naye ni Allammah Sheikh Mansuri al-Bayaan (Mwenyezi Mungu amrehemu).

Hakika kufariki kwake kumeambatana na mazingatio ya wananchi, ambapo mazishi yake alasiri ya siku ya Jumanne iliyopita 29 Shaaban, yalionesha mshikamano mzuri wa kidini na wa kiraia katika Qatif, kama ambavyo mkusanyiko mkubwa ambao unaadhimisha majilisi ya maombolezo uliokusanyika kwa ajili ya marehemu, na rambirambi ambazo zimekuja kutoka kwa viongozi wakuu na kutoka kwa Marajii wa kidini na watu mbalimbali, yote hayo yanatia mkazo athari ya sira njema katika nafsi za watu.

Na hatutaki kuzungumzia kuhusu fadhila yake ya kielimu, kwani ushahidi wa wanachuoni na Marajii juu yake unabainisha nafasi yake tukufu, kama ambavyo hatutaki kuzungumzia kuhusu utunzi wake na vitabu vyake ambavyo vinafikia vitabu 35, pamoja na kwamba alikuwa ni mlemavu wa macho, mzee, anakabiliwa na maumivu, magonjwa na maradhi.

Hakika nitaelekeza mazungumzo yangu kuhusiana na aliyokuwanayo katika usafi wa nafsi na utwahara wa moyo, ambapo aliakisi uhalisia katika jamii yetu wa sira ya mwanachuoni mchamungu, ambaye alitakasa nafsi yake. Basi mwendo wake ukawa mzuri na sira yake ikawa nzuri. Na tunaashiria mafunzo

[62] Al-Majilisiy: Muhammad Baaqir katika *Biharul-Anuwar*, Juz. 2, uk. 27.

mawili yanayoonekana katika sira yake nzuri, ili yawe ni mahala pa kuigwa na kigezo.

**Kutoka katika umateka wa tamaa:**

Wengi wanastaajabu katika maisha ya uchamungu ambayo alikuwa anaishi Sheikh, naye anatokana na familia tajiri, na chini ya harakati zake kulikuwa na uwezo mkubwa, lakini yeye tangu mwanzo wa maisha yake alichagua njia ya elimu, na dini ikachanganyika na nafsi yake na hivyo maisha ya kujinyima na kujizuia yakadhahiri. Yeye anakaa nyumba ndogo ya zamani na samani chache sana, na anajiepusha na aina mbalimbali za vyakula na vinywaji, isipokuwa kinachomuwezesha kuishi, na kumbakisha katika uhai.

Kama ambavyo alikuwa ni mzalendo, mnyenyekevu katika muamala wake pamoja na watu na mambo, haihusishi nafsi yake na kiburi chochote, na baada ya kukata masafa katika masomo yake katika mji wake wa Qatif, alikuwa na nafasi, heshima na kuaminika, lakini aliamua kuacha mji wake na kuhamia Najaf tukufu mwaka 1380 hijiria. Wakati huo alikuwa ana miaka 55 katika umri wake Alikwenda huko ili kuendelea na masomo, nao ni uamuzi wenye ushujaa mkubwa kwa mtu mwenye umri kama wake na hali yake, kama vile kukosa macho, na hana mtoto anayemsaidia, ambapo alikuwa ameshapoteza mtoto wake wa pekee (Ahmad) ambaye alikuwa katika umri wa ujana wake, kama ambavyo katika uamuzi huo ni kuachana na hali ya jamii inayomzunguka.

Hivi ndivyo alivyochukua uamuzi wake na akasafiri akiwa tayari kwa matatizo na ugeni bila ya kumzuia katika hayo tamaa au kuelemea kwenye raha. Na akarejea katika nchi yake baada ya miaka 25, hali na mambo yalipoharibika Iraki. Alikuwa ameshapata kiwango cha juu cha elimu, lakini yeye hakuwa anataka cheo chochote au nafasi yoyote, na haikubadilika hali yake ya kuamiliana na watu, bali alizidi unyenyekevu na uchamungu, na

kujiweka kando na tamaa.

Na mwanachuoni wa kidini hawezi kutekeleza jukumu lake kwa ukamilifu ila atakaposifika kwa uchamungu, na asili ya uchamungu ni kutonyenyekea tamaa na matamanio, ili awe ni mwenye kuwalingania watu kwa sira yake na tabia yake, na kuwa ni mfano na usadikishaji wa kushikamana na maadili na misingi. Na kisha mawaidha yake yanachukua nafasi yake katika nyoyo. Ama ikiwa mwanachuoni wa kidini anapupia tamaa na vyeo na matamanio, hakika atatengeneza hatari kubwa katika dini ya Mwenyezi Mungu.

Imepokewa katika hadithi kutoka kwa Imamu Ja'far Swadiq عليه السلام: "Mwenye kuzidi kumjua Mwenyezi Mungu, na akazidi kuipenda dunia, basi anazidi kuwa mbali zaidi na Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu anazidi kuwa na ghadhabu juu yake."[63] Na kutoka kwake عليه السلام: "Mtakapoona mwanachuoni anaipenda dunia basi mtuhumuni katika dini yenu, hakika kila mwenye kupenda anajongea kwa anayoyapenda."[64]

Hakika muonekano wa kujinyima uwazi wake unatofautiana kati ya mwanadamu na mwingine, na kinachotakiwa sio kuiga neno kwa neno maisha ya mwanakujinyima kati ya wanakujinyima, lakini cha muhimu ni kupata uhalisia wa kujinyima na asili yake, nayo ni kujikomboa kutokana na tamaa na matamanio, kama inavyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم kwamba amesema: "Kujinyima sio kuharamisha halali lakini ni kuyatumaini zaidi yaliyoko katika mamlaka ya Mwenyezi Mungu kuliko yaliyopo mikononi mwake mtu."[65] Na inapokewa kutoka kwa Imamu Ali عليه السلام: "Kujinyima sio kutomiliki kitu lakini kujinyima ni kutomilikiwa na kitu."

[63] Rejea iliyotangulia, Juz. 70, uk: 124
[64] Rejea iliyotangulia, Juz. 2 uk: 107
[65] Rejea iliyotangulia, Juz. 74, uk: 172

**Usafi wa kuamiliana na watu:**

Sheikh aliyeondoka alikuwa amefunguka kwa watu, kwa makundi yao mbalimbali, na mirengo yao mbalimbali. Na hakuwa anabeba katika moyo wake husuda kwa yeyote, wala chuki kwa yeyote. Pamoja na kwamba alikuwa na fikra zake na rai zake maalum, lakini hakumfanyia uadui yeyote kwa kuhitalifiana kwake naye katika rai, na wala hajaingia katika vita wala mzozo kuhusu kadhia kati ya kadhia. Ameishi pamoja na ikhitilafu za Marajii, baina ya nyumba ya Marjaa huyu na Marjaa yule, na baina ya kundi la Marjaa huyu na la Marjaa yule, lakini hakuchukua msimamo dhidi ya yeyote katika msingi huu, wala hajalitenga mbali kundi kati ya makundi, au kupiga vita mrengo kati ya mirengo, bali alikuwa amejiepusha na mambo haya na kuchukua msimamo wa ubaba na upendo katika jamii. Na kwa sababu hiyo wote walimheshimu na waliwasiliana naye na wamehisi hasara kwa kumkosa kwake.

Hakuwa anamtaja mwanachuoni yeyote katika wanachuoni ila kwa kheri, na hakuwa anaridhia kusengenywa yeyote au kudharauliwa katika majilisi yake, bali aliwalea waliokuwa pembezoni mwake kuwaheshimu watu wote. Na hivi ndivyo inapasa kuwa mwanachuoni wa kidini. Aepukane na chuki, awe mbali na uadui na mizozo, anaeneza upendo wake na anazatiti hali ya umoja na uelewano katika jamii. Jamii yetu imeteseka sana na ikhitilafu na mizozo ndani ya mazingira ya kidini, ambapo kila upande unatia mkazo misimamo yake na kuushadidia upande mwingine, na mtu anaifanya nafsi yake ndio mwamrishaji na ndio mwenye kuwahisabu wengine, katika rai zao na misimamo yao na maelekezo yao. Dini na haki ni ambayo anaiona yeye tu, ama wengine anawahukumu kwa kupotea, ufasiki na upotovu.

Hivi ndivyo imeparaganyika jamii, na ukapungua usadikishaji na uaminifu wa wanachuoni wa kidini katika nafsi za watu. Hakika sisi tuna haja sana ya kuvuka hali hizi, na kujikita katika changamoto hatari ambazo dini yetu na jamii yetu inakabiliana

nazo, na kusaidiana katika mambo ya pamoja, nayo ni mengi zaidi na muhimu zaidi kuliko mas'ala ya ikhitilafu ndogo ndogo na za pembezoni.

Na tuikuze hazina hii ya kimaanawiya ya kijamii, ambayo ameianzisha Sheikh aliyeondoka. Na mkusanyiko huu mkubwa ambao wote wameshiriki humo, ni kwa ajili ya kuimarisha hali ya umoja na uelewano katika jamii. Na iwe tabia yake njema na sira yake nzuri ni kigezo kwa waumini, na hususani kwa wanajamii wa aina yake kati ya wanachuoni na wanaotafuta elimu ya dini.

## UPOLE WA IMAMU HASAN عليه السلام NI NJIA YA UKUNJUFU WA KIJAMII

Miongoni mwa sifa zinazoonekana sana za Imamu Hasan عليه السلام ambazo amejulikana kwazo ni safu ya upole. Ambapo amekuwa ni mashuhuri kuwa ni mpole wa Ahlul-Bayt. Amepokea al-Madainiy kutoka kwa Juwairiya bin Asmai, amesema: Alipofariki Hasan, walitoa jeneza lake. Mar'wan bin al-Hakam akabeba jeneza lake, Husein akamwambia: "Leo unabeba jeneza lake na jana ulikuwa unammezea hasaira?" Mar'wan akasema: "Ndio, nilikuwa nafanya hayo kwa ambaye upole wake ni sawa na uzani wa milima."[66]

Na sifa hii kwa hakika ni manhaji ya muamala wa kijamii. Imamu amefanya kazi ya kuimarisha katika maisha yake na ni juu ya wafuasi wake na wapenzi wake kumwiga katika manhaji hii.

Hakika sisi ni wajibu kusoma upole wa Imamu Hasan عليه السلام kama manhaji katika usamehevu wa kijamii na tufanye kazi ya

[66] Ibnu Abi al-Hadid: Abdul-Hamid katika Sharh ya *Nahjul-Balaghah*, Juz. 16 uk: 13 Darul-Jiyl – Beirut chapa ya kwanza 1978.

kuiwezesha jamii sifa hii. Na ni lazima sisi tuashirie kwamba Ahlul-Bayt عليهم السلام wote wanasifika kwa upole ila mazingira ambayo aliishi Imamu Hasan عليه السلام yalipelekea na yamesaidia kudhihirisha sifa hii katika shakhsiya yake kwa namna iliyo wazi zaidi. Imamu alikuwa anakabiliwa na uasi na maudhi ya pande mbili:

**Upande wa kwanza:** Wa nje, na unawakilishwa na Muawiya bin Abi Sufian, na kambi ya Sham, ambapo aliwekeza jitihada na nguvu yake na uwezo wa utawala wake na serikali yake katika kupaka matope sifa nzuri za Imamu Hasan, ili kumtenga na raia. Akafanya kazi ya kusambaza propaganda na uzushi wa uongo na wa chuki dhidi ya Imamu Hasan عليه السلام, na baba yake Amirul-Muuminina, na akaweza kutokana na hayo kutengeneza kundi huko Sham linalowachukia Ahlul-Bayt عليهم السلام, hadi baadhi walisadiki kwamba Ali bin Abi Twalib alikuwa haswali!!

Na Muawiya alikuwa anafanya makusudi sana kumsikilizisha Hasan mbele yake baadhi ya maudhi. Na baadhi ya wafuasi wake na watu wake wa karibu, kama Mar’wan bin al- Hakam na Amru bin al-A’si na Mughira bin Shubah wanafanya mfano wa jukumu hili.

**Upande wa pili:** Wa ndani, ambapo uamuzi wa Imamu wa kufanya suluhu pamoja na Muawiya, ambao ulilazimishwa kwake na mazingira, na kwa kuchunga maslahi ya Umma, ulichochea hisia kwa baadhi ya wanaomzunguka Imamu, na wakaiangalia suluhu kwamba ni msimamo wa udhalili na unyonge na kujisalimisha. Wakawa wanamuelekezea lawama zao za ubabe na shutuma zao kali kwa maneno mabaya na yasiyofaa.

Huyu hapa Hujur bin Adiy, Swahaba Mtukufu anamsemesha kwa kusema: “Ama wallahi siku hiyo nilitaka ufe natufe pamoja na wewe.” Na Adiy bin Hatim anasema: “Umetutoa katika uadilifu na kutupeleka kwenye dhulma.” Na Bashir al-Hamdaniy na Suleiman bin Swarid al-Khuza’iy anaingia kila mmoja wao

kwake wakisema: "Amani iwe juu yako ewe mwenye kuwadhalilisha waumini." Na baadhi ya wafuasi wake walimsemesha kwa kusema: "Ewe mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu umedhalilisha shingo zetu kwa kusalimisha kwako jambo kwa huyu muovu."[67]

Na imekuja katika *al-Iswabah*: "Wafuasi wa Hasan walikuwa wanamwambia: "Ewe fedheha ya kiongozi wa waumni." Na anasema: "Fedheha ni bora kuliko moto."[68] Na mfano wa maneno haya hakuna shaka kwamba yanamuudhi mwanadamu na kuamsha hasira yake, lakini Imamu Hasan alikabiliana nayo kwa upole na utulivu mkubwa, na akaweza kwa hayo kufyonza athari na matokeo mabaya, ambayo yanaweza kumkasirisha. Kambi ya Imamu Hasan ilikuwa inahitaji mshikamano na ushirikiano. kulikuwa na masharti kwa Muawiya ya kuyatekeleza, lakini yeye atakapoona kambi ya Imamu Hasan imesambaratika na imehitalifiana na nafasi ya Imamu imetetereka ndani ya jamaa zake, hakika hilo litamhamasisha zaidi kupuuza maafikiano hayo naye kimsingi hakuwa ameazimia kuyatekeleza.

**Maana ya Upole:**

Ni kudhibiti nafsi na kutulia wakati wa kuchemka ghadhabu, kama anavyosema Raghib.[69]

Imamu Hasan عليه السلام aliambiwa upole ni nini? Akasema: "Ni kudhibiti hasira na kuimiliki nafsi,"[70] yaani mwanadamu

[67] Al-Qarashiy: Baqir Sahri katika *Hayatul-Imamu Hasan*, Juz. 2, uk: 273 - 182 Darul-kutubi al-Ilimiya Qum
[68] Al-Asqalaaniy: Ibnu Hajar katika *al-Iswabah*, Juz. 2, uk: 72 chapa ya kwanza 1992 Darul-Jiyl - Beirut
[69] *Majumuatu minal-Mukhtaswina*: Mausuatu Nadhwaartu naim fiy makaarim akhilaq Rasul al-karim uk: 1735, juzuu ya tano chapa ya kwanza 1998 Darul Wasilati Jiddah
[70] Al-Majilisiy: Muhammad Baqir katika *Biharul-Anuwar*, Juz. 75, uk: 102

kudhibiti nafsi yake wakati anapokabiliwa na mtu mwingine kwa kitendo kinachoudhi. Hiyo ni kwa sababu utashi wa ghadhabu unataharuki kwake na kumpelekea mchemko ili kukabiliana na maudhi yanayoelekezwa kwake. Lakini mpole ni ambaye anajidhibiti katika kuelekeza utashi huu, na wala hautumii isipokuwa katika wakati wake unaofaa, kwa sababu kutoa fursa kwa utashi huu ulipuke katika utendaji wa mwenye hasira unaweza kumdhuru mwanadamu badala ya kumnufaisha. Ni mara ngapi aliyedhulumiwa alitumia hasira na akageuka kwa sababu ya kitendo hicho kuwa ni dhalimu mwenye kutuhumiwa, akatoa fursa kwa adui yake. Anasema Imamu Ali عليه السلام: "Ghadhabu ni shari ukiiachia inabomoa."[71]

Ghadhabu kwa hakika ni matokeo ya uchochezi wa nje anaopokea mwanadamu, na kumfanya alipize kisasi kwa hasira. Na katika kudhibiti utashi huu, na katika kuuelekeza mwelekeo unaofaa, maelekezo ya Kiislamu yanasihi kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu. Katika Hadithi al-Qudusiy: "Ewe mwanadamu nikumbuke unapokasirika."[72] Na amesema صلى الله عليه وآله وسلم: "Ewe Ali usikasirike, na unapokasirika basi kaa na utafakari kudra ya Mola kwa waja, na upole Wake juu yao. Na unapoambiwa Muogope Mwenyezi Mungu, basi puuza ghadhabu yako na rejea kwenye upole wako."[73]

Na hakuna kilicho kizuri zaidi kuliko mwanadamu kutibu mchemko wa ghadhabu yake kwa kurejea kwenye ibada, kuswali rakaa mbili kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ikhilasi na unyenyekevu, hakuna shaka kwamba itamhamisha mwanadamu na kuwasiliana na ulimwengu wa ukamilifu na wa kiroho, ambapo anapata kutoka kwa Muumba wake neema za huruma Yake na upole wa ukarimu Wake.

[71] Al-Amaadiy Tamiymiy: Abdul-Wahid katika *Ghurarul-Hikami wa durarilkalimi*
[72] Al-Kulainiy: Muhammad bin Yaaqub katika *al-Kaafiy*, Juz. 2, uk: 304
[73] Ibnu Shubatu al-Haraniy: al-Hasan bin Ali katika *Tuhful-Uqul*, uk: 18

Kama zinavyonasihi baadhi ya riwaya kutoka katika hali moja kwenda kwenye hali nyingine wakati wa ghadhabu: Kutoka kwa Abu Dhari رضي الله عنه, hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema: "Anapokasirika mmoja wenu naye amesimama basi akae, kama itaondoka hasira yake basi, vinginevyo alale."[74]

Na lengo la hilo ni kuondoa athari za ghadhabu katika harakati na hakuna madhara humo. Na katika hadithi kutoka kwa Mtume ﷺ hakika yeye anasihi kutawadha, amesema ﷺ: "Hakika ghadhabu inatokana na shetani na shetani ameumbwa kwa moto, na hakika moto unazimwa kwa maji. Anapokasirika mmoja wenu basi na atawadhe."[75]

**Madhara ya ghadhabu na kukasirika:**

Baadhi ya watu wanatawaliwa na hali ya ghadhabu na kukasirika haraka kwa sababu za kipuuzi sana, kama ambavyo hutoa fursa kwa wepesi wa ghadhabu yake kuchukua mwelekeo wake wa ubabe, na hali hii ni mbaya na ni yenye kudhuru. Na matokeo yake makubwa ni mambo mawili:

**Kwanza:** Madhara ya kiafya, ambapo ripoti za kitabibu zinaashiria kwamba ghadhabu na kukasirika kunazingatiwa kuwa ni sababu ya maradhi ya kisukari, shinikizo la damu na maradhi ya moyo, na kwa hiyo hakika mambo ya muhimu wanayousia matabibu kwa wagonjwa hawa ni kuidhibiti nafsi na kutokasirika.

**Pili:** Kuongeza hali ya mshikamano wa kijamii, ambapo watu wa jamii wanashughulika na matatizo madogo madogo na ya pembezoni, ambayo yanachochewa na hali ya hasira. Na katika zogo hilo yanatoweka malengo na matarajio makubwa ambayo

[74] As Sajastaniy: Abu Daud Suleiman bin al-Ashi'ath katika *Sunnan Abi Daud*, Juz. 2, uk: 664 hadithi namba 4782

[75] Rejea iliyotangulia hadithi namba 4784

yalikuwa yanapasa kila mtu kushugulika nayo, na jamii inachelewa kufikia malengo na maslahi makuu kwa sababu ya kushughulika na ikhitilafu za pembezoni.

**Upole ni manhaji ya kijamii:**

Wakati mwingine mazungumzo juu ya upole hufanyika kwa kuzingatia kuwa ni sifa nzuri ya pekee, na wakati mwingine upole unatafitiwa kama harakati ya kijamii kwa ujumla, baina ya mtu mmoja mmoja kati ya wanajamii, na baina ya makundi na mikusanyiko. Ambapo ni wazi kwamba kila jamii ina migawanyiko mbalimbali ya kijamii, kisehemu na kimakazi au kiukoo na kikabila, au kifikra na kimadhehebu au ufuasi wa kisiasa na mfano wa hayo.

**Swali:** Namna gani inapasa uwe uhusiano baina ya kila kundi na lingine?

Hakika kuenea hali ya hasira na ghadhabu inaathiri katika uhusiano huu wa ufuasi na kila kundi kutengana na kundi lingine. Ama upole ukitawala na ukunjufu ukaenea baina ya mikusanyiko na mirengo, upole wakati huo unageuka na kuwa ni mfumo wa jumla wa kijami na kuleta matunda yake katika kuleta umoja wa jamii na mshikamano wake, na kuelekeza juhudi zake na nguvu zake kwenye malengo makuu na changamoto hatari.

Na angalizo ni kwamba ikhitilafu na mizozo baina ya makundi, mara nyingi inatokea kwa sababu ya vitendo vya kibinafsi vya hasira, kwa upande huu au ule, na kuamiliana na upande mwingine kwa mtazamo wa jumla na kuchukua hasira kwa msingi huo.

**Namna gani tutaamiliana na hasira za makundi:**

**Kwanza**: Kutojumuisha ubaya, na kuadhibu kundi lote kwayo.

**Pili**: Kueneza roho ya ukunjufu na kufumbia macho mabaya, ambayo yanaweza kutokea kwa huyu dhidi ya yule na kinyume chake, ambapo inapasa watu binafsi na vingozi wa makundi wajipambe kwa upole, kwa sababu ubaya huo unaweza kuwa ni matokeo ya ufahamu au mkanganyiko, au kwa sababu upande fulani unataka kutengeneza tatizo baina ya pande mbili.

**Tatu**: Kutokuza hali ya ikhitilafu ya kifikra na kiutamaduni hadi kwenye kiwango cha ikhitilafu na mzozo. Na kueneza utamaduni wa wingi na kukubali rai ya mwingine.

Hakika kukuza ikhitilafu kuhusu baadhi ya mambo ya pembezoni, kama vile kuthibiti mwandamo wa mwezi wa Ramadhani au Iddi au kuchagua marjii taqlid au kufuata fikra hii au ile. Na kuzingatia mfano wa mambo haya ya pembezoni ni mpaka wa utenganisho baina ya imani na ukafiri, uadilifu na ufuska, ni jambo la kimakosa linalotokana na ujahili ua tabia mbaya.

**Mfumo wa Imamu Hasan:**

Upole ulikuwa ni mfumo wa mwenendo, na mafunzo yenye kujitokeza katika maisha ya Imamu Hasan عليه السلام, na alikuwa anaamiliana nayo mukabala wa maudhi binafsi ya uadui, pamoja na wenye mielekeo yenye kumkhalifu, na inayotofautiana naye, na ushahidi wa aina ya kwanza. Inapokewa kwamba alikuwa عليه السلام na kondoo, siku moja akakuta amevunjwa mguu wake. Akamuuliza kijana wake: Nani amemfanyia haya? Kijana akasema: Mimi. Imamu akasema: Kwa nini umefanya hivyo? Kijana akasema: Ili nikuudhi na nikutie huzuni. Akatabasamu عليه السلام na akamwambia: Basi nitakufurahisha. Akamwacha huru, na akampa zawadi nzuri.[76]

Na kwa aina ya pili, wanahistoria wananukuu: kwamba alipenya

[76] Al-Qarashiy: Baaqir katika *Hayatu al-Imamu al-Hasan*, Juz. 1, uk: 214

kwa Imam mtu kutoka kwa watu wa Shamu kati ya ambao Muawiya amewajaza chuki na ubaya dhidi ya Ahlul- Bayt, akawa anammiminia Imamu matusi na shutuma, na Imamu yuko kimya hakumjibu kwa chochote katika maneno yake, na baada ya kumaliza, Imamu akamgeukia akamsemesha kwa kauli ya upole na akakabiliana naye kwa hali ya ukarimu na bashasha kwa kusema:

"Ewe mzee: Nadhani wewe ni mgeni? Kama ungetuomba tungekupa. Na kama ukitutaka muongozo tungekuongoza. Na kama utatulaumu tutakulaumu. Na kama una njaa tutakulisha. Na kama unahitajia basi tutakutosheleza. Na ikiwa umefukuzwa tutakupa makazi." Na hakuacha عليه السلام kumfanyia upole mtu wa Shamu kwa haya na mfano wake ili aondoe roho ya uadui na shari kutoka katika nafsi yake, hadi akashangaa na hakuweza kujibu maneno na akabakia ametahayari kwa aibu namna gani ataomba msamaha kwa Imamu, na namna gani atafuta dhambi kwake! Akatikisa kichwa kwa kusema: "Mwenyezi Mungu anajua ni mahala gani anaweka ujumbe wake."[77]

Hakika kati ya yanayosaidia katika kuchukua msimamo wa upole ni kufahamu upande mwingine na kujua mazingira ya kinafsi na kifikra ambayo yanamzunguka. Ukijua kwamba yeye ni mpotoshaji au mchochezi, na kwamba yeye pia ni muhanga wa adui mmoja, utakuwa ni mwenye kuweza kudhibiti msimamo, na kuubadilisha kwa maslahi yake na sio kwa maslahi ya adui yake.

Na kwa hiyo mwenye akili ndio ambaye anamiliki upole, anasema Imamu Ali عليه السلام: Kwa utimilifu wa akili unapatikana upole."[78] Na anasema: "Shikamana na upole hakika ni tunda la elimu."[79] Na anasema Mtukufu Mtume صلى الله عليه وآله وسلم: "Naapa kwa ambaye nafsi

[77] Rejea iliyotangulia uk: 314 - 315
[78] Al-Amadiy Tamiymiy: Abdul-Wahid katika *Ghurari-Hikami wa Duraril-Kalimi*
[79] Rejea iliyotangulia

yangu iko mikononi Mwake, hakijajumuishwa kitu kwenye kitu kilicho bora kuliko upole kujumuishwa na elimu."[80] Mwanachuoni ndio ambaye anapaswa kujipamba na upole, kwa sababu anafahamu mabaya ya majahili na sababu za makosa yao.

Na wakati mwingine inatokea wanakuja katika jamii watu kutoka katika jamii zingine wanabeba maalumati na fikra zenye kupotosha kuhusu jamii, fikra zake na itikadi zake. Ikiwa mtu anayekabiliana nao ni mwelewa, anajua kwamba wao ni wapuuzi na ni wenye kupotosha. Hakika anajua kwanza mgongano ambao utaletwa na maneno yao, kisha anaanza kubadilisha hali hiyo mbaya na kuwapa wageni kwa tabia yake na mwenendo wake mfano hai dhidi ya kosa la mawazo yake ya awali.

Ama ikiwa anayekabiliana naye ni shakhsiya yenye hasira, basi yatamuudhi maneno hayo na kumjibu kwa maneno makali zaidi na kwa tuhuma na kwa sifa za kinyume. Na njia hii aghlabu inapelekea kuimarisha hali ya makosa katika jamii. Na katika yanayoleta mshangao na majivuno wakati mwingine, ni kuzingatia hawa watu vitendo vyao hivyo vya hasira ni ushujaa na mafanikio yanayostahiki kutajwa na kupongezwa. Utaona baadhi yao wanakuhadithia juu yake kana kwamba amenusurika dhidi ya adui, naye anajua kwamba kwa hilo amethibitisha kushindwa kwake.

Katika hadithi kutoka kwa Mtume ﷺ: "Mshindi sio yule mwenye kwenda mbio zaidi, bali mshindi ni ambaye anamiliki nafsi yake wakati wa ghadhabu."[81]

Katika kumbukumbu ya kumkumbuka Imamu Hasan عليه السلام ni haja ilioje sisi kusoma sira yake nzuri na kushikamana na njia yake ya kiujumbe na kuchukua mfumo wake katika ukunjufu wa kijamii, ili mazingira yetu yatawaliwe na upendo, uelewano na tuelekee

---

[80] Al-Majilisiy: Muhammad Baaqir katika Biharul-Nauwar juzuu 2 uk: 46
[81] Raishahariy: Muhammadiy katika *Mizanul-Hikima*, Juz. 7, uk: 234

kukabiliana na maadui na hatari kwa kushikamana kama jengo madhubuti.

## UGOMVI WA KIDINI, JE UNA KISINGIZIO?

### Ni Iddi ya Upendo na Usafi, na si Iddi ya Kugombana:

Ugomvi unakwaza maisha mazuri kwa watu, na unahadaa mazingatio ya jamii, na unapotosha mwelekeo wake. Ambapo ugomvi unateketeza sehemu kubwa katika mazingatio ya mwana-damu. Na katika ugomvi na mzozo mwanadamu anatumia nguvu zake nyingi, fikra na mawazo, na anatumia juhudi na muda wake wa thamani kwa ajili ya kupata ushindi, nguvu ambazo ilipaswa kuzielekeza katika kujenga na kukuza na kuendelea kuelekea kwenye kheri. Na kila jamii inapojiepusha na ugomvi na matatizo ya mizozo inaweza kukita juhudi zake kwa ajili ya kupata maslahi mazuri ya kijamii na lengo kubwa na zuri.

### Mazingira ya Ugomvi:

Ugomvi unaweza kuwa ndio sababu ya kuzifanyia haki uadui au dhana ya kutaka kufanya uadui. Ikiwa upande wowote utafanya uadui katika haki za wengine, hakika hilo linachochea kwao utashi wa kutetea nafsi kulipiza uadui, na Uislamu unatia mkazo kuheshimu haki za wengine za kimada na za kimaanawi, na unaharamisha sana uadui au dhuluma yoyote. Na ikiwa utatokea ubaya au uadui baina ya wanajamii hakika unashajiisha kusamehe na usamehevu:

**"..... فَمَن عَفا وَأَصلَحَ فَأَجرُهُ عَلَى اللَّهِ ....."**

> **"Na mwenye kusamehe na kusuuluhisha basi huyo malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mun-gu." (Surat Ash-Shura; 42:40)**.

"...وَالكَاظِمينَ الغَيظَ وَالعافينَ عَنِ النّاسِ وَاللَّهُ يُحِبُّ المُحسِنينَ"

**".....Na wazuiao ghadhabu na wenye kusamehe watu na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao ihisani." (Surat Aali-Imran; 3:134)**.

Na kutoka kwake ﷺ: "Sameheaneni mtaondosha chuki baina yenu."[82]

Na wakati mwingine sababu ya ugomvi inakuwa ni dhana tu, kwamba upande mwingine umefanya uadui au kwamba pengine utafanya uadui katika siku zijazo, jambo ambalo linaingia chini ya anwani ya dhana mbaya kwa wengine, au kuhisi husuda katika nafasi yao, na kuwa na ghera katika dhati kati yao. Anasema Imam Ali عليه السلام: "Dhana mbaya inaharibu mambo na inaleta shari." "Mwenye kushindwa na dhana mbaya hatoacha baina yake na rafiki suluhu."

Na inawezekana kuugawa ugomvi na uadui katika aina nyingi:
- Ugomvi wa kidini.
- Ugomvi wa kimaslahi katika kugombania mali au cheo au ladha.

Na nukuu za historia zimekusanya matukio ya umwagaji damu yaliyotokea kwa sababu ya ikhitilafu za kidini na kiitikadi, ingawa wakati mwingine inafichikana chini yake ikhitilafu za kimaslahi za kimaada, na dini itakuwa ni mwelekeo tu au anwani au silaha katika vita.

**Ugomvi Katika Dini:**

Je, katika dini kuna yanayopelekea na kutoa kisingizio cha ugomvi? Na kwa maneno mengine je, inajuzu kukhitalifiana kwa

[82] *Mizanul-Hikma*, Juz. 6, uk. 367.

sababu za kidini na kiitikadi na kutatua ikhitilafu zao hizo kwa vita na mapigano?

Kwa kweli, hakika sisi tunapofuatilia hukumu za kisharia tunakuta kwamba hakuna kisingizio cha ugomvi katika dini kabisa na hiyo ni kwamba:

**Kwanza:** Hakika dini ni jambo la moyoni na wala hakuna uwezekano wa kuwalazimisha watu itikadi fulani maadamu hawajakinaika nayo. Na Mwenyezi Mungu ameshawaumba watu wakiwa huru na wala hakuwalazimisha wamwamini, na wala hakuruhusu hata kwa Manabii Wake kuwalazimisha watu kuamini.

**"لا إِكراهَ فِي الدّينِ قَد تَبَيَّنَ الرُّشدُ مِنَ الغَيِّ ....."**

**"Hakuna kulazimisha katika dini; uongofu ume-kwisha pambanuka na upotovu." (Surat Al-Baqara 2:256)**

**فَذَكِّر إِنَّما أَنتَ مُذَكِّرٌ ﴿٢١﴾ لَستَ عَلَيهِم بِمُصَيطِرٍ ﴿٢٢﴾**

**"Kumbusha hakika wewe ni mkumbushaji tu. Wewe si mwenye kuwatawalia." (Surat Al-Ghashiya; 88:21–22)**.

**"وَقُلِ الحَقُّ مِن رَبِّكُم فَمَن شاءَ فَليُؤمِن وَمَن شاءَ فَليَكفُر ....."**

**"Sema hii ni haki itokayo kwa Mola Wenu, basi atakaye aamini na atakaye akufuru." (Surat Al-Kahf; 18:29)**.

**Pili:** Hakika njia pekee inayomruhusu mwanadamu kumkinaisha mwingine kwa yale anayoyaamini na kuona ndio sahihi ni majadiliano na mdahalo, ama uadui na ugomvi hakika sio tu

unashindwa kukinaisha upande mwingine, bali unamfanya kuwa adui mkubwa na uwiano unapobadilika basi matokeo pia yanabadilika:

وَلا تَستَوِى الحَسَنَةُ وَلَا السَّيِّئَةُ ادفَع بِالَّتى هِىَ أَحسَنُ فَإِذَا الَّذى بَينَكَ وَبَينَهُ عَدٰوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِىٌّ حَميمٌ

**"Mema na maovu hayawi sawa. Zuia uovu kwa lililo jema zaidi. Mara yule ambaye baina yako na yake pana uadui atakuwa kama rafiki mkubwa." (Surat Fussilat; 41:34)**

Na Qur’ani tukufu inatia mkazo kwamba mjadala na mdahalo pamoja na Ahlulkitabu ima uwe kwa njia iliyo bora au usifanyike kabisa:

وَلا تُجٰدِلوا أَهلَ الكِتٰبِ إِلّا بِالَّتى هِىَ أَحسَنُ إِلَّا الَّذينَ ظَلَموا مِنهُم وَقولوا ءامَنّا بِالَّذى أُنزِلَ إِلَينا وَأُنزِلَ إِلَيكُم وَإِلٰهُنا وَإِلٰهُكُم وٰحِدٌ وَنَحنُ لَهُ مُسلِمونَ

**"Wala usijadiliane na watu wa Kitabu isipo-kuwa kwa njia iliyo nzuri kabisa; isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: Tumeamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu. Na Mungu Wetu na Mungu Wenu ni Mmoja na sisi ni wenye kusilimu Kwake." (Surat Al-‘Ankabut; 29:46)**.

Na anasema (swt):

ادعُ إِلىٰ سَبيلِ رَبِّكَ بِالحِكمَةِ وَالمَوعِظَةِ الحَسَنَةِ وَجٰدِلهُم بِالَّتى هِىَ أَحسَنُ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبيلِهِ وَهُوَ أَعلَمُ بِالمُهتَدينَ

**"Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola Wako ndiye anayemjua zaidi aliyepotea njia yake na Yeye ndiye anayewajua zaidi walioongoka." (Surat An-Nahl; 16:125)**.

**Tatu:** Ikiwa inajuzu kwako kuwafanyia watu uadui na kugombana nao kwa sababu wameshikamana na kukinai kwao kinyume na kukinai kwako, hakika hilo linamaanisha kwamba wao pia wana haki kuamiliana pamoja nawe kwa njia hiyo hiyo, na ilihali wewe hukubali hilo. Na unapenda watu wangeheshimu itikadi yako na kukinaika kwako, maadamu uko hivyo basi amiliana na watu kwa yale unayopenda waamiliane na wewe.

Anasema Imam Ali عليه السلام: "Ifanye nafsi yako ndio kipimo kwa yaliyo baina yako na wengine, mpendelee mwingine unayoyapenda kwa ajili ya nafsi yako na chukia kwake unayoyachukia kwa ajili ya nafsi yako."[83]

Na kutokana na ukweli huu, hakika Uislamu haujaruhusu jihadi na vita pamoja na makafiri isipokuwa katika hali ya kujitetea, kama watawafanyia Waislamu uadui au katika hali ya kuwazuia na kuwakwaza kueneza Uislamu na kulingania imani yao. Na katika yasiyokuwa hayo hakika Uislamu unalingania kwenye muamala mwema pamoja na mwingine, anasema (swt):

لا يَنهىٰكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذينَ لَم يُقٰتِلوكُم فِى الدّينِ وَلَم يُخرِجوكُم مِن
دِيٰرِكُم أَن تَبَرّوهُم وَتُقسِطوا إِلَيهِم إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ المُقسِطينَ

**"Mwenyezi Mungu hawakatazi kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakuwapiga**

[83] *Nahjul-Balaghah*, barua ya 31, uk. 397.

**vita, wala hawakuwatoa makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu. " (Surat Al-Mumtahana; 60:8).**

**Katika Duara la Uislamu:**

Na ikiwa kugombana na watu wa dini zingine inakatazwa, basi suala hilo la kugombana na watu wa madhehebu mengine katika dini moja inafaa lipingwe kabisa, ambapo anwani ya Uislamu inawaenea wote na "Kila Mwislamu kwa Mwislamu mwingine ni haramu mali yake, damu yake na heshima yake."[84]

Bali kinachotakiwa kwa watu wa madhehebu zote wafunguke na kuwa wawazi kwa madhehebu mengine, na Maimamu wa Ahlul-Bayt wamewafundisha adabu wanafunzi wao juu ya hilo.

Kutoka kwa Muawiya bin Wahab amesema: Nilimwambia Imam Ja’far as-Sadiq عليه السلام: Namna gani inatupasa tufanye kati yetu, na watu wengine miongoni mwa watu kati ya wale ambao hawako katika jambo letu? Akasema: “Mtawatazama Maimamu wenu ambao mnawafuata na mtafanya wanayoyafanya. Wallahi hakika wao wanawatembelea wagonjwa wao na wanasindikiza jeneza zao na wanatoa ushahidi kwao na kwao wanatekeleza amana."[85]

Na duara finyu sana ndani ya duara la Uislamu ni duara la madhehebu, ambapo inaweza kukawa na makundi na mirengo mingi ndani ya madhehebu moja. Katika madhehebu ya Ja’fari kwa mfano, kuna tofauti baina ya *Akhbariyina* na *Usuuliyina* katika mfumo wa kung’amua hukumu za kisharia na kuna ikhitilafu baina ya *Shaikhiya* na wengineo katika baadhi ya rai

---

[84] Muslimu bin al-Hajaj al-Qarashiy Anisaburiy katika *Sahihi Muslim*, Chapa ya kwanza 1998, Riyaadh (Darul-Mughuniy) Hadithi namba: 2564.

[85] Muhammad bin Yaaqub al-Kulainiy katika *al-Kaafiy*, Juz. 2, 1405 A.H (Beirut Darul Adhuwaai) uk. 136.

zinazofungamana na nafasi ya Ahlul-Bayt (a.s), kisha kuna mafungamano ya kisiasa na kijamii na kuwepo Marjaa wengi wa kukalidiwa. Lakini ikhitilafu hii na tofauti hii haisihi abadani iwe ni kisingizio cha ugomvi na uadui baina ya watu wa madhehebu moja na dini moja.

Hakika jamii inapokuwa inashikamana na adabu za Uislamu na inajua madhara ya ugomvi juu yake, na inapokuwa imepevuka katika muamala wake pamoja na taklifu zake za kisharia, hakika itabadilisha kila mas'ala yenye ikhitilafu ya kielimu juu yake na kuwa ni nukta yenye nguvu inayoongezwa katika hazina yake, na sio kiungo cha kulipua na matatizo.

Na mbele yetu kuna mifano ya ikhitilafu katika kuthibiti mwezi, nayo ni mas'ala siku hizi yamekuwa ni mazingatio ya wananchi wote wa nchi za Kiislam, ambapo inawezekana sana baadhi ya dola za Kiislamu kutangaza Iddi katika siku hii na dola nyingine katika siku nyingine.

Na hata ndani ya madhehebu moja inawezekana kutofautiana rai katika kuthibiti mwezi au kutothibiti kwake. Je, inasihi mfano wa ikhitilafu hii kuwa ni sababu ya ugomvi au mzozo ndani ya jamii?

**Mtazamo wa Kifikihi:**

Ili kutatua maudhui haya ni lazima tutaje utangulizi. Nayo ni kwamba mbele ya mukalafu kuna kauli dhahiri ya kufunga katika hali ya kutothibiti mwandamo wa mwezi wa Shawwali, na kufungua inapothibiti kuandama kwake. Na maadamu hayajapatikana matumaini ya kuthibiti mwezi mwandamo haijuzu kwake kufungua bali ni juu yake kukamilisha idadi ya siku thelathini.

Na ama matumaini ya kuandama mwezi yanapatikana kwa moja ya njia za kisharia zilizotajwa katika vitabu vya kifiqihi, nazo ni

mtu mwenyewe kuona mwezi au waadilifu wawili kushuhudia, au kuenea habari (ya kuandama mwezi) kwa tawatur.

Na kwa kuwa hukumu inategemea kupatikana kwa matumaini kupitia moja ya njia zilizotajwa, hivyo kama yatapatikana kwa njia yoyote kati ya hizi inathibiti kwa mukalafu hali ya kuwajibika kwa kufuata athari yake.

Na kwa kuwa mukalafu wengi aghlabu hawaoni mwezi, kama ambavyo sio rahisi kila mmoja kusikia ushahidi wa mashahidi wawili waadilifu wa kuonekana kwake, na inawezekana zisienee kwa walio wengi, kwa hiyo watu wamezoea kutegemea rai ya maulamaa wanaoshughulikia jambo hili, ambao wao ndio sehemu ya matumaini yao na uaminifu wao, na anapothibitisha mwanachuoni ambaye anatumainiwa, hakika watu wanaomwamini wanafuata kauli yake.

Na hapa ni wajibu kutia mkazo juu ya mambo mawili muhimu sana:

**Kwanza:** Kila mukalafu anapofuata athari ya kisharia inayotokana na matumaini yake au kutopata matumaini haijuzu katika hali ya kukhitalifiana kumfanyia uadui huyu na yule au kinyume chake, kwa sababu pande zote mbili zimefanya kulingana na taklifu yake ya kisharia. Na kulazimiana na hukumu ya kisharia katika mas'ala, hivyo haijuzu kuwa ni sababu ya ugomvi. Kama mtu atamkaribisha msafiri katika nyumba yake na akaswali kwa kupunguza swala haijuzu kwa mwenye nyumba kumfanyia uadui kwa hilo. Na hata kama jamaa watakhitalifiana kuainisha upande wa kibla na kila mmoja miongoni mwao akaswali kwa kuelekea upande anaoitakidi au anaodhani ndio kibla haijuzu hilo kuwa ni sababu ya ugomvi. Ndio, inawezekana kila mmoja wao kubainisha sababu ya kushikamana kwake na rai hii bila ya ile, pamoja na kuchunga adabu ya mjadala kulingana na ikhitilafu.

**Pili:** Hakika watu kutegemea rai ya maulamaa katika kuthibiti

mwezi au kutothibiti kwake ni kwa sababu wao wanaweza kutekeleza vipimo vya kisharia, isipokuwa ni kwamba hilo halisihi kuwa ni sababu ya kugeuza kitendo cha kuthibiti mwezi mwandamo au kupinga kwake kuleta hali ya mgawanyiko. Kila kundi litachukua rai ya mwanachuoni ambaye wanaelemea kwake, pamoja na kufumbia macho mtazamo wa wanachuoni waliobaki. Na hii haiwezi kutimia isipokuwa ikiwa huyu mwanachuoni ndio pekee katika mtazamo wao ambaye rai yake inaweza kuleta matumaini, ama mwinginewe kati ya maulamaa hana thamani katika maneno yao.

Hakika haisihi kugeuza mas'ala haya ya kisharia kuwa ni kadhia ya mgawanyiko, yanapopatikana matumaini kwa mukalafu ya mwandamo wa mwezi wa Shawwali kwa uthubitisho wa mwana-chuoni yeyote mwaminifu kwake, ni wajibu juu yake kumfuata katika hilo. Na ikiwa hajapata matumaini ya kuthibiti kwake basi hatofuata na hata kama aliyemthibitishia ni Marjaa anaye-kalidiwa, hakuna mafungamano baina ya Marjaa anayekalidiwa na mukalafu katika kadhia hii ya kimaudhui. Mukalafu anaweza kupata matumaini kwa moja ya njia za kisharia na kufungua wakati ambapo Marjaa wake amefunga, na anaweza kuwa kinyume cha hivyo. Na hata katika kujengea juu ya nguvu ya utawala wa kisharia kwa mwandamo wa mwezi, hakika hiyo inashurutishwa kwamba asijue mukalafu kosa la mtawala wa kisharia wala kosa la tegemeo lake katika hukumu yake ya mwandamo wa mwezi.[86]

**Iddi ya Upendo na Usafi:**

Hakika inatakikana sote tufanye juhudi ili Iddi iwe ni mnasaba wa kusambaza hali ya upendo na usafi, na kuzatiti upendo na udugu baina ya waumini na Waislamu. Hivyo ni muhimu kujon-

---

[86] Imamu Ruhullah al-Musawiy al-Khumainiy katika *Taharir al-Wasilah*, Juz. 1, 1424 A.H (Beirut Daru Taarifu Lilimatubuati), Uk. 265.

gea katika mambo yafuatayo:

1. Kuzingatia na kufuatilia mwandamo wa mwezi kwani ni Sunna kufanya hivyo, na inapasa kudumu katika hilo kwani kila inapozidi idadi ya wanaotazama mwezi basi fursa ya kuona mwezi mwandamo inakuwa kubwa zaidi katika usiku wa kuandama mwezi.
2. Mwenye kuona mwezi mwandamo kutoa ushahidi wake mbele ya wanachuoni wanaohusika katika nchi yake wala wasizembee na kwenda kwa baadhi yao bila ya kuwashirikisha wengine, ili wanachuoni wote wanaohusika wawe katika mazingira yanayokaribiana yanayosaidia katika msimamo mmoja.
3. Tuwasukume na tuwashajiishe kukutana maulamaa wanaoshughulika na kuthibitisha mwezi mwandamo pamoja na baadhi yao na washauriane baina yao ili kuchukua msimamo mmoja utakaowapa raha watu kutokana na taabu ya ikhitilafu.
4. Kila upande uheshimu rai ya upande mwingine wakati wa kuhitalifiana katika kuthibiti mwezi. Atakayefungua au kufunga hiyo ni taklifu yake ya kisharia baina yake na Mola Wake, na wala haisihi kutuhumu nia, wala kuwa na dhana mbaya, wala kufanya uadui juu ya haki za wengine na kupaka matope shakhsiya zao au uchochezi dhidi yao.
5. Kueneza utamaduni wa kusameheana, na mafunzo ya Uislamu katika maingiliano mazuri na kuamiliana pamoja na watu hata kama wametofautina katika dini zao na madhehebu yao na rai zao na mielekeo yao. Kuna hadithi nyingi zilizopokewa kutoka kwa Maimamu watoharifu عليهم السلام zinazokataza ugomvi katika dini, wala sijui ni kwa nini tunasahau hadithi hizi na wala hatuelezani pamoja na kuzihitajia sana.

Imepokewa kutoka kwa Imam Ja'far as-Sadiq عليه السلام: "Msigombane na watu kwa ajili ya dini yenu, hakika ugomvi unatia ugonjwa katika moyo."[87]

[87] *Biharul-An'war*, Juz. 2, uk. 133.

Na kutoka kwake عليه السلام: "Jihadharini na ugomvi katika dini, hakika unashughulisha moyo na kuzuia utajo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na unarithisha unafiki na unaleta chuki."[88]

Na kutoka kwa Ali bin al-Yaqitwin amesema: Amesema Abu Hasan Imam Musa bin Ja'far عليه السلام: "Waamuru wafuasi wako wazuie ndimi zao na waache ugomvi katika dini na wajitahidi katika kumwabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu."[89]

Na katika riwaya hizi kuna ishara ya madhara ya ugomvi katika dini nayo ni:

a. Unamuudhi mwanadamu kinafsi (unaleta maradhi katika moyo)
b. Unasababisha chuki na uadui katika jamii (unaleta chuki).
c. Unamzuia mwanadamu na mazingatio halisi (unashughulisha moyo na kuzuia utajo wa Mwenyzi Mungu).

## USWALIHINA NA KUTAFAKARI

Zinazunguka katika mazingira ya baadhi ya waswalihina, fikra zinazokhalifu akili na mantiki, nazo zinafanana na uongo na ukhorafi na baadhi miongoni mwao wanatazama maisha ya vitu na matukio mtazamo wa kipuuzi na usioendelea, kama ambavyo inatokea kwa baadhi ya pande za kidini vitendo na misimamo mibaya na miovu. Na kinachosikitisha sana katika jambo ni kwamba kuna fikra, mitazamo na misimamo inanasibishwa na dini, jambo ambalo limeleta mushkeli na maswali juu upeo wa kuafikiana na uhusiano baina ya dini na akili, je, inamaanisha uswalihina ni kuondoa akili? Na je, dini ni badala ya akili?

Hakika baadhi ya hao waswalihina unapojadiliana nao kuhusu rai

[88] Rejea iliyotangulia, Uk. 128.

[89] As Suduq Muhammad bin Ali bin Babawayhi al-Qummiy, katika *Tauhid* (Beirut Darul-Maarifah) uk. 460.

zao, fikra zao na vitendo vyao, katika mwangaza wa akili na mantiki, wanafunga mlango wa majadiliano na mjadala, kwa msingi kwamba mambo ya kidini ni ya ibada na kwamba dini ya Mwenyezi Mungu haifahamiki kwa akili. Sasa ni upi uhakika wa uhusiano baina ya dini na akili? Je, uswalihina unamaanisha kudumaza dauru ya akili na kuifuta?

**Kulazimiana baina ya uswalihina na akili:**

Akili ni neema kubwa Mwenyezi Mungu Mtukufu amemtofautisha kwayo mwanadamu na viumbe vingine, na dini ni ujumbe na uongofu wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu amemneemesha kwayo mwanadamu. Chanzo cha akili na dini ni kimoja naye ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, navyo vinalazimiana na hakitengani kimoja wapo na kingine. Na tunapoona mparaganyiko na utengano baina ya dini na akili, ni wajibu tudadisi, ili tufichue nukta za kutofahamika na mkanganyiko katika ambayo tumeyazingatia kuwa ni dini au akili, kwani dini sahihi haigongani na akili salama. Na uhusiano baina ya dini na akili ni uhusiano wa kukamilishana na kusaidiana kwa kubadilishana, ambapo akili inaongoza dini na dini inaielekeza akili.

Kwa sababu imekaririwa katika Qur'ani tukufu kauli yake (swt): **"Ni ishara kwa watu wenye akili." (Suratul-Baqarah; 2:164).** Na wahyi wa Mwenyezi Mungu hakika unawahutubia wenye akili, na kuamsha akili zao**: "Hakika tumeifanya Qur'ani kwa lugha ya Kiarabu ili mfahamu" (Suratu Zukhuruf; 43:2)** na anasema (swt):

وَلَقَد ءاتَينا موسَى الهُدىٰ وَأَورَثنا بَنى إِسرٰءيلَ الكِتٰبَ ﴿٥٣﴾ هُدًى
وَذِكرىٰ لِأُولِى الأَلبٰبِ ﴿٥٤﴾

> **"Na kwa hakika tulimpa Musa uongofu, na tukawarithisha wana wa Israil Kitabu. Ni uongofu na ukumbusho kwa wenye akili." (Surat Al-Mu'min (Al-Ghafir) 40:53-54).**

Na kama tungesoma nususi za Sunnah za Nabii na Hadithi za Maimamu wa Ahlul-Bayt عليهم السلام tungezikuta zinatia mkazo mshikamano mkubwa baina ya dini na akili. Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم: "Dini ya mtu ni akili yake na asiye na akili hakuna dini kwake."[90]

Na kutoka kwake صلى الله عليه وآله وسلم: "Hakika inafikiwa kheri yote kwa akili na hakuna dini kwa ambaye hana akili."[91]

Kutoka kwa Imamu Ali عليه السلام: "Akili ni mtume wa haki." [92] "Asili ya mwanadamu ni akili yake na akili yake ndio dini yake."[93]

Kutoka kwa Imamu Musa al-Kadhim عليه السلام: "Hakika Mwenyezi Mungu ana hoja mbili kwa watu: Hoja ya dhahiri na hoja ya ndani. Ama hoja ya dhahiri ni Mitume, Manabii na Maimamu عليهم السلام, na ama hoja ya ndani ni akili."[94]

**Uswalihina na kutafakari:**

Ikiwa uhusiano baina ya dini na akili ni uhusiano wa kulazimiana, hakuna kutengana humo wala kuachana, namna gani tunafasiri hali hizo mbaya katika maisha ya wenye dini? Kwa hakika baadhi ya wenye dini wanafahamu dini vibaya, na

[90] Al-Hindiy: Ali al-Mutaqiy katika *Kanzul-Ummal*, Juz. 3, uk. 379, namba 7033 chapa ya tano 1985 Muasastu Risalat – Beirut.
[91] Al-Majilisiy: Muhammad Baaqir katika *Biharul-Anuwar*, Juz. 74, uk. 143 chapa ya tatu 1983 Daru Ihiyai Turathi al-Arabiy – Beirut
[92] Al-Amadiy Tamimiy: Abdul-Wahdi katika *Ghuraril-Hikami*.
[93] Al-Majilisiy: Muhammadi Baaqir katika *Biharul-Anuwar*, Juz. 1, uk: 82
[94] Rejea iliyotangulia uk. 137.

wanadumaza akili zao kwa ujahili wao na kwa ubaya wa fahamu zao. Kisha wanazifunga nafsi zao na harakati zao dhidi ya dini, na kwa hiyo wanadhuru nafsi zao, na wanaichafua dini. Na haya ndio ambayo hadithi na nususi za kidini zimehadharisha, ambazo zinatia mkazo umuhimu wa kutafakari katika maisha ya mwanadamu mswalihina. Vinginevyo mwenye kunasibiana na dini, anabeba nembo yake na anwani yake na kufanya ibada zake na amali zake, lakini yeye ikawa hatumii akili yake, wala hafaidiki na fikira yake hakika uswalihina wake utakuwa ni wenye kukatika na una upungufu, bali umepakwa matope na una giza.

Kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه amesema: Kaumu ilimsifu mtu mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: Akasema ﷺ: Vipi akili yake? Wakasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu tunakueleza kuhusu juhudi yake katika ibada na mambo ya kheri, na unatuuliza kuhsu akili yake? Akasema ﷺ: Hakika mpumbavu anafanya kwa upumbavu wake makubwa zaidi kuliko uovu wa muovu. Hakika watanyanyuka waja kesho katika daraja na wanapata ukaribu kwa Mola Wao kwa kadiri ya akili zao."[95]

Na hadithi tukufu inaeleza wazi vitendo vya baadhi ya waswalihina wapumbavu, ambao umekosekana kwao uelewa, na ikatoweka akili, vikawa vitendo vyao ni vibaya kuliko uovu wa muovu, kwa sababu unapaka matope sura ya dini na sifa ya waswalihina. Na yanayotokea hivi sasa Aljeria na Afghanistani na Pakstani kati ya mauji na uovu na mapigano yanayofanywa kwa jina la dini ni ushahidi juu ya hilo.

Na katika hadithi nyingine anatuhadharisha Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuhadaika na muonekano wa uswalihina kwa mtu yeyote ikiwa hatujawa na uhakika na fikira yake kwa sababu fikra ndio kipimo cha uswalihina wake, na ni kipimo cha

[95] Rejea iliyotangulia uk. 84

unyoofu, anasema ﷺ: "Inapowafikia kuhusu mtu uzuri wa hali yake tazameni katika uzuri wa akili yake, hakika mtu analipwa kutokana na akili yake."[96]

Na kwa utekelezaji wa maelekezo haya ya Nabii ﷺ amesema Salman رضي الله عنه: Nilimwambia Abu Abdillahi Ja'far Swadiq عليه السلام: Kwamba fulani katika ibada yake, dini yake na fadhila yake ni kadha na kadha. Akasema: Namna gani akili yake? Nikasema: Sijui. Akasema: Hakika thawabu ni kwa kadiri ya akili.[97]

Hakika tatizo la baadhi ya waswalihina hakika wao wanaiweka dini katika mpaka wa fahamu zao dhaifu, na uelewa wao duni, kisha wanazingatia yasiyokuwa hayo ni ukafiri na ufasiki, kama inavyonukuliwa kutoka kwa mmoja wa masheikh ambaye alikuwa anasherehesha kwa wanafunzi wake ibara ya fikihi, anasema: Akitumbukia panya katika samli na akatoka hai basi samli inabakia twahara na halali. Na maana ya ibara ni kwamba panya hajafia katika samli, bali *kharajati hayan* – yaani ametoka akiwa hai – lakini Sheikh akafasiri: *al-Faaratu tukhriju hayatan*, yaani panya atatoa nyoka. Mmoja wa wanafunzi wake akambishia: Namna gani panya atatumbukia katika samli kisha anatoka akiwa ni nyoka? Na badala ya Sheikh kuzinduka katika kosa lake, akang'ang'ania katika maneno yake na akamfukuza mwanafunzi katika somo, kwa kumtuhumu kwa ukafiri na kuwa na shaka katika uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Je, Mwenyezi Mungu si anaweza kumbadilisha panya na kuwa nyoka?

## Kutafakari na kufuata uongozi wa kidini:

Baadhi ya uongozi wa kidini unafanya jukumu lake la kimsingi katika kuondoa hali ya kufikiri katika medani ya Kiislamu, na

[96] Rejea iliyotangulia, Juz. 1, uk. 106
[97] Rejea iliyotangulia uk. 84

kuimarisha hali ya kijuu juu na kutokuwa na maendeleo katika kiwango cha dini. Na hiyo ni ama kwa ufinyu wa uelewa wake na fikra yake au kwa sababu ananufaika na hali ya kutoendelea, na kuiacha, na kuistawisha kwa msukumo wa maslahi.

Na hapa uswalihina unahitaji kutafakari katika mas'ala ya kufuata uongozi. Uongozi wa kidini na kijamii. Mwislamu hasamehewi katika kusalimisha uongozi wake na hatamu za mambo ya dini yake kwa yeyote maadamu hajajua uadilifu wake, na hata mwanachuoni mwadilifu haisihi kumfuata kwa kufumba macho na upofu, maadamu sio maasumu na anakabiliwa na kupotoka na kukosea.

Ni lazima kufikiri na kutafakari katika kuchagua upande wa kidini ambao unaufuata. Ibnu Sakiti al-Kufiy رحمه الله alimuuliza Imamu Ali bin Musa Ridhaa عليه السلام: Nini hoja ya viumbe leo? Imamu عليه السلام akajibu: Akili, anamjua kwayo mkweli kwa Mwenyezi Mungu na hivyo kumsadikisha, na muongo kwa Mwenyezi Mungu na kumkadhibisha. Ibnu Sakiiti akasema: Wallahi hili ndio jawabu.[98]

Na mwanachuoni wa kidini anahukumiwa kwa misingi ya kidini, na vidhibiti vya akili. Inapasa kupima rai zetu na misimamo yetu katika mwanga huo, na wala haisihi kumfuata na kumtii katika ambayo yanakhalifu dini, na yanapingana na akili.

Imekuja katika *Sahih al-Bukhariy* kutoka kwa Abi Abdurahaman kutoka kwa Ali bin Abi Twalib عليه السلام amesema: Nabii صلى الله عليه وآله وسلم alituma kikosi – kikundi kidogo cha jeshi - akampa uongozi mwanaume katika Answar na akawaamuru wamtii. Akakasirika akasema: Je, amewaamuru Nabii mnitii? Wakasema: Ni kweli. Akasema nikusanyieni kuni. Wakakusanya akasema: washeni moto,

[98] Rejea iliyotangulia, Juz. 1, uk. 105

wakauwasha. Akasema: Ingieni. Wakaogopa ikawa baadhi yao wanawashika baadhi na wanasema: Tumekimbilia kwa Nabii kutokana na moto. Hawakuacha kuwa hivyo hadi moto ukazimika, basi hasira yake ikatulia, ikamfikia Nabii ﷺ akasema: Kama wangeingia wasingetoka humo hadi Siku ya Kiyama, utii ni katika mema.[99]

Hakika Qur'ani tukufu inawalaumu manaswara kwa sababu wao wamewapa viongozi wao hatamu zao za dini kufuata kwa upofu, na wamewafuata wao kufuata kwa jumla, bila ya vidhibiti vyovyote kutoka katika dini au akili, kana kwamba wao kwa hayo wanawafanya ni waungu na wanawaabudu wao kinyume cha Mwenyezi Mungu. Anasema (swt):

"اتَّخَذوا أَحبارَهُم وَرُهبٰنَهُم أَربابًا مِن دونِ اللَّهِ ....."

> **"Wamewafanya makuhani wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu..." (Surat At-Tawba; 9:31).**

Amesema Udai bin Hatim: Nilimwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: Hakika sisi hatuwaabudu wao, akasema ﷺ: Je, si wanaharamisha aliyoyahalilisha Mwenyezi Mungu na mnayaharamisha, na wanahalalisha ambayo ameyaharamisha Mwenyezi Mungu na mnayahalalisha? Akasema: Nikasema: Ndio. Akasema: Hiyo ndio kuwaabudu kwao.[100]

Na kutoka kwa Maimamu wawili, al-Baqir na as-Swadiq عليهما السلام hakika wao wamesema: Wallahi hawajafunga kwa ajili yao wala hawajaswali kwa ajili yao lakini waliwahalalishia haramu na wakawaharamishia halali. Wakawafuata na wakawaabudu bila ya kujua.[101]

---

[99] Al-Bukhariy: Muhammad bin Ismail, katika *Sahih Bukhari*, Juz. 5, uk. 322 kitabul-Maghaaziy namba 340 al-Maktabat Thaqafiyati - Beirut

[100] Twabarisiy: al-Fadhil bin al-Hasan katika *Majmaul-Bayaan*, Jz. 5, uk. 43, chapa ya kwanza, 1995, Muasasatu al-Ilimiy lilimatubuaati – Beirut.

[101] Rejea iliyotangulia

Twalha na Zuberi walipoamua, na wao ni masahaba wawili maarufu kwa Waislamu, wakiwa pamoja na Ummul-Muuminina Aisha, mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kupambana na ukhalifa wa kisharia, ambao unawakilishwa na Amirul-Muuminina Ali عليه السلام, wakakanganyikiwa baadhi ya Waislamu. Harithi bin Hutwi akaja kwa Imamu Ali عليه السلام akisema: Je, unadhani watu wa jamali wako katika upotovu? Imamu akamjibu: Ewe Harithi hakika wewe umeangalia chini yako na wala haujaangalia juu yako ukatahayari. Hakika wewe hukujua haki na hivyo kumjua aliyeileta, na hukujua batili na kujua nani aliyeileta.[102]

Hakika baadhi ya wenye dini wanashangazwa na shakhsiya ya mwanachuoni fulani, na wanapita mpaka katika kumtukuza na kuichukulia kauli yake ni katika mambo ya kawaida, bila ya uelewa au kutafakari. Na hii ni kinyume cha maelekezo ya kidini.

Imepokewa kutoka kwa Ali عليه السلام: Chukua hekima kwa aliyekuletea, na tazama aliyosema na wala usiangalie aliyeisema.[103]

Na katika riwaya nzuri kutoka kwa Imamu Ja'afar Swadiq عليه السلام: "Chukua haki kutoka kwa watu wa batili wala usichukue batili kwa watu wa haki. Kuwa mchambuzi wa maneno, ni mara ngapi upotovu umepambwa kwa aya za Kitabu cha Mwenyezi Mungu, kama dirihamu ya shaba ilivyopambwa kwa fedha ya udanyanyifu? Kuangalia katika hilo ni sawa sawa, na watazamaji wake ni wajuzi."[104]

Ni maelekezo mazuri yalioje yanayoamsha akili kwa ajili ya

[102] Al-Musawiy: Sharifu Ridhaa katika *Nahjul-Balaghah* - Qiswaar al-Hikami 262

[103] Al-Amadiy Tamiymy: Abdul-Wahdi katika *Ghurarul-Hikami*, Juz.1, uk. 355 chapa ya kwanza 1987 Muasasatu al-A'alamiy - Beirut

[104] Al-Majilisiy: Muhammad Baaqir katika *Biharul-Anwaar*, Juz. 2, uk. 96 namba 39; Al-Answaariy: Sheikh Murtadha katika *Faraaid al-Usuul*, Juz. 1, uk: 382, chapa ya kwanza 1991 – Muasastu al- A'alamiy llilimatubuaati – Beirut.

kutekeleza dauru ya kukosoa na kunyoosha, katika rai na fikra (kuweni wachambuzi wa maneno). Na inahadharisha kwa mwanadamu kuingia kwake upotoshaji na udanganyifu (na mara ngapi upotovu unapambwa kwa aya) na ni juu ya mwanadamu kujipamba na uoni na uelewa, ili awe mjuzi mtambuzi baina ya sahihi na kosa katika mwanga wa misingi ya dini na akili.

**Rejea ya akili:**

1. Katika itikadi za msingi katika dini, akili inakuwa ndio rejea. Na kupitia kuangalia na kufikiri mwanadamu anafikia katika kuamini misingi ya dini. Na wengi wa maulamaa watafiti wanaona ni wajibu wa kulazimiana itikadi na njia ya akili na sio na nukuu na kufuata, bali Allammah al-Hiliy amedai kongamano juu ya hilo: "Maulamaa wamekongamana juu ya wajibu wa kumjua Mwenyezi Mungu na sifa Zake za thubutiya na yanayosihi kwayo, na yanayo kataliwa kwayo, utume, Uimamu na miadi kwa dalili na sio kwa kufuata."[105]

2. Katika Sharia ya Kiislamu akili inajitegemea katika rejea sehemu ya matawi na hukumu, anasema Sayyid Muhammad Taqiy al-Hakim: "Hakika akili ni chanzo cha hoja na kwayo inamalizikia, nayo ndio rejea pekee katika misingi ya dini, na katika baadhi ya matawi ambayo haiwezekani sharia tukufu kutoa hukumu yake humo, kama vile amri za kutii. Na vilevile migawanyiko inayofuatia taklifu, mfano elimu na kutokujua kwayo, au kuzingatia kujikurubisha kwayo inapotakiwa kuzingatiwa kwa kujaalia moja ya masharti ya taklifu, kwa ulazima wa dauru au mfuatano humo. Kwa kawaida hakika kutii amri za kutii kwa mfano, ama urejee kwenye akili au mfuatano usiokuwa na mwisho, ambapo ingekuwa ni ya kisharia swali lingeelekezwa juu ya ulazima wa utii wake, ikiwa ni ya kisharia swali linaelekezwa juu ya ulazima

[105] Al-Answaariy: Sheikh Murtadhwa katika Faraid al-Usuul, Juz. 1, uk. 382 chapa ya kwanza 1991 Muasasatu al-A'alamiy lilimatubauaati – Beirut.

wa kutii kwake, hivyo ni lazima ijaaliwe humo kuwa ni ya kiakili, na ambayo yamepokewa katika amri za kisharia kwa kutii, hakika ni muongozo na mkazo wa hukumu ya akili na sio kwamba ni amri za kuasisi."[106]

3. Na kwa akili mwanadamu anafahamu amri zingine za kidini, na anazichambua katika nususi zake na rejea zake za kisharia. Nayo haijitegemei humo na sharia, kwa sababu Mweka sharia ni Mwenyezi Mungu Mtukufu na wahyi ndio rejea ya kuweka sharia, lakini kufahamu maneno ya wahyi na kujua maana yake na sehemu za utekelezaji wake na kuainisha sehemu zake, rejea humo inakuwa ni akili. Na hapa vidhibiti wamevichambua na kuvihakiki maulamaa katika manhaji ya uchambuzi wa hukumu za kisharia, zinaratibu kazi ya ijitihadi ili kupata hukumu ya kisharia.

Na Ustadh al-Mudarisiy anafupisha dauru ya rejea ya akili, na upeo kukamilika kwake pamoja na wahyi, katika utafiti wake mzuri juu ya sharia ya Kiislamu anasema: "Kazi ya akili ni kujua wahyi, kuufahamu kwake na kujua wabebaji wake na kujua namna ya utekelezaji wake katika uhalisia wa matawi.[107]

## WENYE RAI NA JUKUMU LA MJADALA

Ili wananchi wetu wavuke hali ya kukwepana iliyoenea katika uhusiano wa makundi yake na mkusanyiko wake pamoja na baadhi yake kwa baadhi, na kufikia kiwango cha kufunguka, kuwasiliana na kushirikiana, ni lazima kuanze na kazi ya majadiliano mazuri ya wazi, yanayolenga kujuana moja kwa moja kila upande kwa mwingine, badala ya kutegemea

[106] Al-Hakim: Muhammad Taqiy katika *Usulul-Amati lilifiqihi al-Muqaarana*, uk. 299 – 300 chapa ya pili 1979 Daru al-Andalusi - Beirut

[107] Al-Mudarisy: katika *Tashiriul-Islamiy Manahijuhu wa Maqaaswiduhu*, Juz. 1, uk. 10 chapa ya kwanza 1991 Daru Raid al-Arabiy – Beirut.

maalumati yasio makini, na mazoea na misimamo iliyopita. Na itarajiwe kuvumbua mambo ya ushirikiano, na kutia mkazo katika maslahi makuu, maslahi ya Umma, na kukabiliana na changamoto hatari katika jamii na nchi.

Wakati utandawazi unalazimisha uwepo wake katika maisha, na ulimwengu kugeuka na kuwa kijiji kimoja kidogo, athari za mipaka ya kijiografia na kisiasa humo zinakuwa finyu, haisihi kwetu kuhifadhi vizuizi hivi na kuta zenye kuimarisha utengano, ili tutenganishe baina ya watu wa umma huu, chini ya anwani za utaifa au madhehebu au vyama au ukabila.

Na angalizo ni kwamba njia za mawasiliano baina ya kila kundi miongoni mwetu na ulimwengu ziwe ni nyingi zaidi pamoja na watu wa mazingira yake na washirika wake katika dini na nchi.

Na majadiliano baada ya hapo ni faradhi inayotulazimisha kwayo dini yetu, ambayo inatuamrisha kuthibiti katika hukumu zetu na rai zetu, na misimamo yetu mbele ya wingine. Haisihi kwetu kutengeneza picha kwa wengine kwa njia ya dhana na mazoea:

وَلا تَقفُ ما لَيسَ لَكَ بِهِ عِلمٌ إِنَّ السَّمعَ وَالبَصَرَ وَالفُؤادَ كُلُّ أُولـٰئِكَ كانَ عَنهُ مَسـٔولًا

**"Wala usifuatilie ambalo huna ujuzi nalo. Hakika masikio, macho na moyo, hivyo vyote vitasailiwa." (Surat Bani Israil; 17:36).**

Na wala tusichukue maalumati yetu kuhusu baadhi yetu kwa baadhi kutoka katika pande zisizoaminika, na kupanda baina yetu chuki na uadui.

يـٰأَيُّهَا الَّذينَ ءامَنوا إِن جاءَكُم فاسِقٌ بِنَبَإٍ فَتَبَيَّنوا أَن تُصيبوا قَومًا بِجَهـٰلَةٍ فَتُصبِحوا عَلىٰ ما فَعَلتُم نـٰدِمينَ

> **"Enyi ambao mmeamini! Akiwajieni fasiki na habari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kutojua, na mkawa wenye kujuta kwa mliyoyatenda." (Surat al-Hujurat; 49:6).**

Mwislamu mwenye kuzingatia ni ambaye anataka kujua rai mbalimbali na anajitahidi kujua rai kwa kutafuta ukweli:

> "...فَبَشِّر عِبادِ الَّذينَ يَستَمِعونَ القَولَ فَيَتَّبِعونَ أَحسَنَهُ أُولٰئِكَ الَّذينَ هَدىٰهُمُ اللَّهُ وَأُولٰئِكَ هُم أُولُوا الأَلبٰبِ"

> **"…..Basi wabashirie waja Wangu. Ambao husikiliza maneno, wakafuata mazuri yake zaidi. Hao ndio aliowaongoza Mwenyezi Mungu, na hao ndio wenye akili." (Surat Az-Zumar; 39:17–18)**

Ni wazi kwamba kutumia tamko (wanasikiliza) katika aya tukufu badala ya wanasikia, linaashiria kwenye aina ya umakini na kukusudia.

Lakini, nani ataanza kazi ya majadiliano? Na kwa nani linaangukia jukumu la kujitolea na kulifanyia kazi? Inanibainikia kwamba wenye kutafakari na wenye rai kati ya raia ndio kundi ambalo linapasa kubeba jukumu hili, kwa sababu wao ndio watu wenye rai na fikra, inatakiwa wawe wenye ufahamu wa kina zaidi, changamoto ambayo Umma unaishi nayo. Na wanaweza zaidi kuendesha mjadala kimaudhui na kwa ikhilasi. Kama ambavyo nafasi yao inawapa uwezekano wa kuathiri ndani ya makundi ambayo wanahusiana nayo na kuongoza rai kuu.

Kama baadhi ya wenye rai watajitolea kutoka kila upande kufunguka kwa watu wa mfano wao katika upande mwingine, na kujadili maudhui ya uhusiano wa ndani baina ya pande na makundi, na namna ya kuyaweka katika hali ya Uislamu na nchi,

jamii yetu ingekata masafa makubwa katika njia ya umoja, mshikamano na ushirikiano, na tungeutosheleza umma wetu hasara ya kutengana, mizozo na kupigana vita.

Na tunaowakusudia ni wale watu wenye uwezo wa kielimu na kifikra, miongoni mwa wanaotumia nafasi kuelekeza na kuathiri katika jamii, kama vile maulamaa wa dini, wanafikra wenye mafanikio, na viongozi wa kijamii. Hakika kuzembea wenye rai wenye ghera na maslahi ya dini na nchi kuhusu kujitolea kuzuri, na kunyanyua sauti juu kwa kulingania kwenye kufunguka na majadiliano, ndio ambako kunatoa nafasi na kuacha medani kuwa wazi, kwa sauti za wenye kulingania chuki na wenye kuchupa mipaka, kutoka katika pande mbalimbali.

Na tunaulizana hapa: Kwa nini inakosekana katika medani – au inapungua – kujitolea wenye rai katika kufunguka kwa baadhi yao kwa baadhi, na kujadiliana kwa ajili ya kuondoa mpasuko, na kuzingatia maslahi makuu, na kuvuka misimamo yao ya kifikra na kijamii?

Na katika kujibu swali hili tunaweza kusema: Hakika kuna sababu nyingi zinazodhoofisha mwelekeo wa wenye rai, na kupunguza kujitolea kwao katika majadiliano na zinazoonekana zaidi ni hizi zifuatazo:

1. **Udhaifu wa kujali mambo ya jamii:**

Mwenyezi Mungu akimpa mwanadamu taufiki ya kuwa na fungu la elimu na maarifa na uwezo wa uelewa na ujuzi, hakika hiyo peke yake ni daraja. Anakuwa ni mwenye jukumu la kutumia hayo katika kutumikia jamii na maslahi ya jumla, lakini baadhi ya wenye rai wanaishi na mambo yao maalumu, na wanajitahidi kulinda maslahi ya kibinafsi.

Na ikiwa majadiliano na kufunguka kwa wengine hakuleti manufaa binafsi, basi haiwi katika duara la mazingatio yao wala

haiwi ndani ya ngazi ya vipaumbele vyao. Nilipendekeza kwa mmoja wa maulamaa wa kidini maudhui ya uhusiano wake na mwanachuoni mwingine anayehitalifiana naye katika mtazamo na anafanya kazi katika medani ya kijamii, akanijibu kwa kusema: Sioni nafsi yangu kama ina haja ya uhusiano pamoja naye. Mambo yangu yametulizana na hali yangu imeratibika vizuri! Na haya ni maneno ya wengi wa maulamaa wa kidini na wanafikra katika jamii yetu. Hakika hahisi haja binafsi na wala hatarajii manufaa binafsi katika kufunguka kwa mwingine na majadiliano pamoja naye. Lakini vipi kuhusu maslahi ya jumla?

Hakika wewe unaweza kuwa humhitajii mwingine katika kiwango chako binafsi na yeye anaweza kuwa hakuhitajii vilevile, lakini nchi na jamii inahitajia kuafikiana rai na kuunganisha juhudi na kuziba mianya ya fitina na mizozo, na kuimarisha umoja wa nchi na kijamii.

**2. Hisia za kutawala na kutisha:**

Mwenye rai anapokuwa katika nafasi ya juu katika nguvu au vyeo au uwezo wa kimali na kijamii, hakika anaweza kutawaliwa na hisia za kujikweza na kuwa juu kwa walio mfano wake, miongoni mwa wenye rai ambao hawafikii kwenye kiwango cha uwezo wake na kudra yake, na hivyo anajitenga na kuacha kuwa wazi kwao, na anajiengua na majadiliano pamoja nao, kwa sababu hawaoni kuwa ni hadhi yake, na anaona kwamba ni juu yao kumnyenyekea, na kukiri juu ya haki yake na ubora wake. Na mwenye rai anaweza asiwe katika nafasi yenye nguvu, lakini uwepo wake katika kundi unakuwa katika nafasi ya nguvu, linatosha hilo kumpa hisia ya kujikweza.

Na kinyume cha hivyo, inaweza kuwa hisia ya udhaifu na woga kutoka upande mwingine ni sababu ya kujitenga na uwazi na majadiliano. Ambaye hajiamini katika nafsi yake au katika elimu

yake na rai yake, hakika anapata kigugumizi kuwasiliana na wengine kwa kuogopa kudhihirika udhaifu wake, au hofu yake kutekwa nao au kufungua mwanya wa kuathiriwa watu wake na ngome yake.

### 3. Utengenezaji na hukumu zilizotangulia:

Katika mazingira ya kutukanana na ugomvi, yanapokuwa mas'a-la ya ikhitilafu, yanagawa watu baadhi yao kwa baadhi mfarakano mkali, na baadhi yao wanatoa hukumu kali kwa baadhi hali ya kutokuwepo, huyu ni kafiri, na huyu ni fasiki na huyu ni mwanabidaa, na huyu ni fasiki na huyu ni Rafidhi, na huyu ni mughalii na huyu ni kibaraka! Hata taklid ya Marjaa imegeuka kuwa ni sababu ya mfarakano, watu wanatazamwa kupitia hilo. Mfarakano huu mbaya na yanayotokana nao ni katika hukumu mbaya. Kufanya haraka kuwaweka watu ndani ya makundi na mirengo finyu, yote hayo yanawakilisha hali ya kutoendelea inayovunja uaminifu baina ya watu wa umma, kama ambavyo haiafikiani na ukunjufu wa Uislamu, na wigo mpana wa tabia njema. Wako wapi hawa wanaofanya haraka kuwakufurisha watu, na kuwatuhumu katika dini yao, na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

"يٰأَيُّهَا الَّذينَ ءامَنوا إِذا ضَرَبتُم فى سَبيلِ اللَّهِ فَتَبَيَّنوا وَلا تَقولوا لِمَن أَلقىٰ إِلَيكُمُ السَّلٰمَ لَستَ مُؤمِنًا تَبتَغونَ عَرَضَ الحَيوٰةِ الدُّنيا ..."

**"Enyi mlioamini mtakaposafiri katika njia ya Mwenyezi Mungu, basi hakikisheni wala msim-wambie mwenye kuwapa salamu: Wewe sio muumini. Mnataka mafao ya duniani….." (Surat An-Nisaa'; 4:94).**

Anasema Sheikh Muhammad Twahir bin Ashur katika Tafsiri yake katika Aya hii:

"Na aya imeshaonyesha juu ya hekima kubwa katika kulinda mkusanyiko, nayo ni kueneza uaminifu na amana baina ya watu wa umma, na kutoa ambayo kazi yake ni kuingiza shaka, kwa sababu unapofunguliwa mlango huu ni vigumu kuufunga kwake. Na kama ambavyo anamtuhumu mwingine na mwingine pia anamtuhumu aliyemtuhumu, na kwa hiyo unaondoka uaminifu, na inakuwa rahisi wadhaifu wa imani na waovu, ambapo tuhuma imeshakuwa inamfunika mkweli na mnafiki. Angalia muamala wa Nabii ﷺ kwa wanafiki, aliamiliana nao kwa muamala wa Waislamu. Kwa kuwa dini hii ni nyepesi kusambaa katika nyoyo inatosha watu wake kuingia wenyewe bila mjadala, ambapo hawakawii kuwazoea, kutangamana furaha yake na nyoyo zao. Wao wanavamia kwa shaka na kusitasita na inakuwa ni imani madhubuti, na kati ya yanayosaidia katika hayo ni uaminifu wa waliotangulia humo kwa wanaojiunga nao."[108]

Na ananukuu Ibu Abi Shaibah katika kitabu chake kwamba: Ali aliulizwa kuhusu watu wa Jamal – ambao walimuasi na akawapiga vita – Akasema: Ikasemwa: Je, wao ni washirikina? Akasema: Walikwishakimbia ushirikina. Ikasemwa: Je, wao ni wanafiki? Akasema: Hakika wanafiki hawamtaji Mwenyezi Mungu ila kwa uchache. Ikasemwa: Sasa wao ni nani? Akasema: Ni ndugu zetu wametufanyia uovu."[109]

Imepokewa riwaya kutoka kwa Imamu Ja'far Swadiq عليه السلام ambayo inatia mkazo maana ya riwaya hii ambapo inapokewa kutoka kwa baba yake عليه السلام: Hakika Ali عليه السلام hakuwa anamna-sibisha yeyote kati ya watu vita vyake kwenye shiriki wala kwenye unafiki, lakini yeye alikuwa anasema: Wao ni ndugu zetu

[108] Ibnu Asour: Muhammad Twahiri katika *Tafsiri Tahariri wa Taniwir*, Juz. 4, uk. 226

[109] Ibnu Shaibah: al-Hafidh Abu Bakar katika kitabu al-Musnaf fiy al-Ahadiithi wal Athar, Juz. 15, uk. 256 khabar namba 19709 chapa ya kwanza 1983 Darul salafiyah, India

wametufanyia uovu.[110] Na mtu anapomnasibishia mwingine uadui na kuwatuhumu tangu awali, hakika hatopata msukumo wa kufunguka kwao na kujadiliana pamoja nao.

Lakini hata tukifumbia macho juu ya kosa la ubaguzi na hukumu iliyotangulia, hakika haisihi kupuuza kwamba mabadiliko yako wazi katika kiwango cha uelewa, na kujiamini, na uhuru wa kutoa rai. Imeshatokea katika medani ya kijamii, kwa matokeo ya mabadiliko ya kielimu na kijamii, na hii ina maanisha kwamba fikra ya kimadhehebu, na mirengo ya kififikra, haidhibiti tena mamlaka yake katika rai zote na misimamo kwa wafuasi wanaojinasibisha nayo, hivyo haisihi kumhukumu mtu au uchamungu wake kupitia anayoyafanya katika misimamo kuhusu mwelekeo au upande ambao ananasibiana nao, hivyo hukumu ya jumla na kujumuisha kwa ujumla sio makini na wala haipatii.

Kisha hakika mwingine kunasibiana na mrengo huu au ule na vyovyote litakavyokuwa kundi lako, hakika haisihi kukuzuia kujenga daraja la uhusiano wa kibinadamu na kijamii pamoja naye, na hususan pamoja na kuwepo maslahi ya pamoja. Na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alifanya mkataba na Mayahudi wa Madina na Manaswara wa Najrani, na makhalifa baada yake wameamiliana na wafuasi mbalimbali wa dini zingine. Na imefanyika mikutano na majadiliano baina ya wakuu wao na viongozi wa Kiislamu. Na inatutosheleza kauli yake (swt):

لا يَنهىٰكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذينَ لَم يُقـٰتِلوكُم فِى الدّينِ وَلَم يُخرِجوكُم مِن دِيـٰرِكُم أَن تَبَرّوهُم وَتُقسِطوا إِلَيهِم إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ المُقسِطينَ

**"Mwenyezi Mungu hawakatazi kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakuwapiga vita**

[110] Al-Huru al-A'Miliy: Muhammad bin Hasan katika *Tafswil Wasaili Shi'ah*, Juz. 15, uk. chapa ya kwanza 1993 Muasasatu Aal al-Bait liihiyai turathi - Beirut.

**katika dini, wala hawakuwatoa makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu." (Surat al-Mumtahana; 60:8).**

**4. Kibano cha uchochezi kwa watu:**

Baadhi ya viongozi wa kidini au wakifikira wakati mwingine wanapita mpaka katika kuwachochea watu wake dhidi ya rai nyingine na upande mwingine, na kuwatupia tuhuma mbalimbali na dosari humo, na kutia shaka katika nia zao, asili yake na tawi lake. Na kutokana na hilo anahukumu uharamu na hatia ya aina yoyote ya kuwasiliana pamoja naye, au kushirikiana hata katika mpaka wa ubinadamu wa chini kabisa.

Na inapatikana hata ndani ya madhehebu moja kwamba wafuasi wa Marjaa fulani kuchochea watu wao dhidi ya Marjaa mwingine, kiasi kwamba hawawasiliani wala baadhi yao hawaswali nyuma ya jamaa wala hawashirikiani katika shughuli za pamoja. Hakika mfano wa uchochezi huu unakuwa ni kikwazo na kizingiti katika harakati za uzalishaji na kutia ugumu wa sehemu ya kujasiri kufunguka kwa upande mwingine, au kujadiliana pamoja nao, kwa sababu watu wake wameleleka katika mwelekeo wa upinzani.

Na sijui nini kisingizio cha kisharia cha hawa katika kuwalea watu wao juu ya chuki na husuda, na tabia mbaya? Pamoja na kwamba Qur'ani tukufu inawaamuru Waislamu kuamiliana na makafiri wa kishirikina muamala ulio bora zaidi ili kudhihirisha mtazamo wa Kiislamu wa kimaendeleo wa kibinadamu, anasema (swt):

وَلا تَستَوِى الحَسَنَةُ وَلَا السَّيِّئَةُ ادفَع بِالَّتى هِىَ أَحسَنُ فَإِذَا الَّذى
بَينَكَ وَبَينَهُ عَدٰوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِىٌّ حَميمٌ

**"Mema na maovu hayawi sawa. Zuia uovu kwa**

**lililo jema zaidi. Mara yule ambaye baina yako na baina yake pana uadui atakuwa kama rafiki mkubwa." (Surat Fussilat; 41:34).**

Hakika muamala mzuri pamoja na wengine unakusaidia kuwavutia wao na kuwaathiri wakati ambapo muamala mbaya na tabia mbaya vinawakimbiza wengine katika haki ambayo nafsi yako inazingatia kwamba inailingania!!

Kama ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu anaamuru waja Wake waumini wawapokee watu – wote – kwa muamala mzuri na maneno mazuri anasema (swt):

**"..... وَقولوا لِلنّاسِ حُسنًا ....."**

**"Na semeni na watu kwa uzuri." (Surat Al-Baqara; 2:83)**

Na katika tafsiri ya Aya tukufu, anasema mwanachuoni wa Najid Abdurahmani As-Saadiy: "Kisha akaamuru kufanya wema kwa watu wote, akasema: "Na semeni na watu kwa uzuri." Na katika kauli njema ni kuwaamrisha mema na kuwakataza maovu, kuwafundisha wao elimu, kutoa salamu, bashasha na mengineyo katika maneno mazuri. Na ilipokuwa mwanadamu hawezi kuwaamrisha watu kwa amali yake akaamrishwa kwa amri anayoiweza kumfanyia wema kila kiumbe, nayo ni wema katika kauli na ikawa miongoni mwa hilo ni kukataza maneno mabaya kwa watu hata kwa makafiri.'"[111]

**5. Sehemu zenye nguvu:**

Kuna sehemu zenye nguvu za nje na za ndani, hazifurahishwi na kutawala mazingira ya uelewano na mshikamano kwa wananchi na umma, wala hawajitolei katika umoja wa nchi katika nchi za

[111] As-Saadiy: Sheikh Abdurahaman bin Naasir katika *Tafsir al-Karim Rahman fiy tafsiri kalaami al- Manaani*, uk. 66 Daru Dhakhair – Musasatu Rayaan – Beirut 1997.

Kiislamu, na kwa hiyo zinatumia kila njia na mbinu kubakisha hali ya mfarakano na mizozo, na kuzuia ukuruba wowote baina ya pande na mirengo mbalimbali. Hizo ndio sababu za dhahiri – kwa nionavyo mimi – ambazo zinazuia kuanza kujitolea kufunguka na majadiliano baina ya wenye rai katika maulamaa na wanafikra katika jamii hizi, lakini wenye kuelewa wenye ikhilasi wanaweza kuvuka vizingiti hivi kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

Imekwishawadia kubeba jukumu wenye rai katika jamii zetu na hususan maulamaa wa kidini, majukumu yao katika kuvuka hali ya utengano baadhi yao kwa baadhi, na wajipambe na ujasiri na ushujaa katika kufunguka na majadiliano na kuokoa jamii kutokana na matatizo, mizozo na ugomvi, kwani changamoto na harakati ambazo zinazikabili mara nyingi ni za kisasa, ni kubwa kuliko mambo ya pembezoni ambayo yanatimia katika msingi wake kubagua na mfarakano.

## PENGO LA KIROHO: HUZUNI NA MKANGANYIKO

Mwanadamu katika maisha haya ana haja na mahitaji, na wala hayatulii maisha yake ila anapopata mbele yake fursa ya kuyapata mahitaji hayo. Na tunaweza kugawa mahitaji yake katika mafungu matatu, kila fungu linafungamana na fungu lingine kwa pande kati ya pande za shakhsiya yake.

**Fungu la kwanza:** Mahitaji ya kimaada, na tunafungamana na upande wa kimwili wa kimaada katika maisha ya mwanadamu, kama vile haja ya chakula, kuvaa, kuishi, matibabu na jinsi. Nayo ni mahitaji ya dharura, ambapo yasipopatikana yanaparaganyika maisha ya mtu na jamii. Na inajulikana kwamba mateso ya ufakiri na ukosefu walau katika sehemu ya jamii yanapokonya amani na utulivu katika jamii yote, kwa sababu unatengeneza mazingira ya uasi na uovu, na kwa sababu hiyo imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwamba amesema:

"Ufakiri unakaribia kuwa ni ukafiri."[112] Na inanukuliwa kutoka kwa Swahaba mtukufu Abu Dharr al-Ghifariy ﷺ kauli yake: "Nimeshangaa kwa asiyepata chakula katika nyumba yake namna gani hatoki kwa watu hali ya kuwa mwenye kuchomoa upanga wake."[113]

**Fungu la pili:** Mahitaji ya kiakili. Akili ambayo Mwenyezi Mungu amempa mwanadamu inahitajia elimu na maarifa, na inahitajia mazingira ambayo yanaipa uhuru wa kufikiri na wasila na vifaa vinavyosaidia kustawisha elimu na fikra. Na katika sekunde ya mwanzo ambayo Mwenyezi Mungu alimuumba humo mwanadamu, alimpa fursa ya elimu na kujifunza, anasema (swt):

"وَعَلَّمَ ءادَمَ الأَسماءَ كُلَّها ....."

**"Na akamfundisha Adamu majina ya vitu vyote…" (Surat Al-Baqara; 2:31).**

خَلَقَ الإِنسٰنَ ﴿٣﴾ عَلَّمَهُ البَيانَ ﴿٤﴾

**"Amemuumba mtu. Akamfundisha ubainifu." (Surat Ar-Rahman; 55:3-4).**

Na unapozuiliwa kwa mwanadamu uhuru wake wa kifikra na uhuru wake wa kielimu, na akapokonywa haki ya kujua, hakika anakosa sehemu muhimu katika ubinadamu wake na kisha hatohisi utukufu na raha.

Na kwa hiyo Uislamu umewajibisha kutoa elimu na kutoa fursa ya maarifa na kujifunza. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa

[112] Al-Hindiy: Ali al-Mutaqiy katika *Kanzul-Umaal*, Juz. 6, uk. 492 namba 16682 chapa ya tano 1985 Muasasatu Risala – Beirut.
[113] Khalid: Khalid Muhammad katika *Rijaalu Haula Rasul*, uk. 100 Darul kutubi al-hadiythati – Qahira 1968.

Mwenyezi Mungu ﷺ kwamba amesema: "Mwenye kuficha elimu yenye manufaa Mwenyezi Mungu atampiga kwa kijinga cha moto Siku ya Kiyama."[114]

Na katika tafsiri ya kauli yake (swt):

"وَمِمَّا رَزَقْنَٰهُمْ يُنفِقُونَ ....."

**"Na wanatoa katika yale tuliyowapa." (Surat Al-Baqara; 2:3).**

Anasema Imamu Ja'far Swadiq عليه السلام: "Katika tuliyowafundisha wanayafundisha."[115]

**Fungu la tatu:**

Maarifa ya kiroho ya kimaanawi. Mwanadamu ni roho na mwili, na kama ambavyo mwili una haja zake na mahitaji yake, vilevile roho ina mahitaji yake nayo ni yenye athari kamilifu katika mwendeo wa upande wa kimaada katika maisha ya mwanadamu, kama atapata mahitaji yote ya kimaada lakini akawa anaishi katika upweke na njaa ya kiroho hakika maisha yake hayawezi kutulia au kuwa na raha.

**Mahitaji ya roho:**

Na roho inahitaji utulivu na uaminifu, ridhaa, raha ya dhamiri na uwepo, na maada kwa ufinyu wake, na harati zake, upungufu wake na dhiki yake haimpatii mwanadamu mafanikio, utulivu na utulivu wa kiroho. Hivyo ni lazima roho ya mwanadamu iwasiliane na ambayo yako juu ya maada kwa nguvu kuu ambayo haina mpaka na ambayo kwayo ndio marejeo ya mambo.

[114] Al-Majilisiy; Muhammad Baqir katika *Biharul-Anuwar*, Juz. 2, uk. 78
[115] Al-Majilisiy: Muhammad Baqir katika *Biharul-Anuwar*, Juz. 70, uk. 267

Ni sahihi kwamba mwanadamu anamiliki kiasi cha nguvu na kudra, hususan katika zama hizi, ambapo kuna maendeleo ya uwezo wa mwanadamu, na uwezo wao wa kielimu umeendelea na teknolojia. Lakini mwanadamu anajua hakika uhai wake na uwezo wake na nguvu zake sio za dhati. Yeye amekuja katika maisha bila ya maamuzi yake, na atatoka kwayo bila ya hiyari yake na wakati wowote ambapo hawezi kudhibiti wakati wake.

Na mwanadamu anajua kwa fadhila za maendeleo yake ya kielimu hivi sasa, upeo wa ufinyu wake na uchache wake ukilinganisha na ulimwengu huu mpana ambao anaishi ndani yake, umbo la ardhi ambayo anaishi juu yake. Umri wake ni kuanzia kabla ya miaka bilioni na nusu, nayo pamoja na ukubwa wake ni sayari tu inazunguka pembezoni mwa jua, pamoja na sayari zingine tisa, zinazotengeneza mkusanyiko wa jua. Na jua hili ukubwa wake ni mara 1,300,000 kwa ukubwa wa ardhi, nalo ni nyota moja tu baina ya bilioni ya nyota zinazotengeneza mkusanyiko unaoitwa *Milky Way* (mkusanyiko wa nyota), na unakadiriwa umri wake unakaribia kati ya miaka 10 na 15, na mkusanyiko huu ni mmoja kati ya mikusanyiko ambayo inaogelea katika anga la ulimwengu.[116]

Na kama anavyosema mmoja wa wataalamu: Kama tukitaka kufananisha ulimwengu tungesema: Hakika ni bahari kubwa na kila mkusanyiko kati ya mikusanyiko ni kisiwa katika bahari hiyo kubwa, na kila mkusanyiko wa jua katika kila mkusanyiko ni kipande cha ardhi katika kisiwa hicho, na kila mkusanyiko wa jua katika kila mkusanyiko unafanana na kipande cha ardhi katika kisiwa hicho, na ardhi yetu ambayo tunaishi juu yake ni kwa kiwango cha sisimizi katika kipande cha ardhi, ndani ya kisiwa kati ya mabilioni ya visiwa katika bahari hiyo kubwa!! Sasa nini ukubwa wa mwanadamu ukilinganisha na ulimwengu huu mkubwa?

---

[116] *Al-Mausuatu al-Arabiyati*, Juz. 14, uk. 246 chapa ya pili Riyaadhi.

Hakika anahisi udhaifu wake na kushindwa kwake, pamoja na yote aliyoyafanikisha na kuyapata katika maendeleo ya kielimu, na mafanikio ya teknolojia. Na yanadhihirika hayo wazi wakati majanga ya kimazingira yanapotokea kama vile tetemeko, volcano, mafuriko na upepo… naye anakosa udhibiti hata wa mwili wake na hisia za nafsi yake. Wakati yeye yuko katika kilele cha afya njema na uchangamfu, anashambuliwa na magonjwa na maradhi, na anapatwa na uzee na ukongwe. Na anapokuwa katika kilele cha furaha na burhani anaweza kupatwa na balaa na huzuni, na vivyo hivyo anageuka geuka katika hali mbalimbali, hawezi kuilinda nafsi yake kwa hali fulani, wala hawezi kujilinda nayo pia.

Hisia hii ya kina kwa ufinyu na udhaifu, na hisia kubwa katika udogo na kushindwa inamsukuma mwanadamu kutafuta chanzo cha nguvu na uwezo na kuhusu upande unaotawala katika ulimwengu na maisha, ili nafsi yake ipate matumaini na mafungamano nayo, na ili moyo wake utulie na zitulizane hisia zake kwa kujikurubisha kwayo. Hiyo ndio dini ambayo inampa mwanadamu jibu kuhusu maswali yake yenye kutatiza kuhusu uwepo wake na hatima yake, na kumfungulia njia ya mawasiliano na kuamiliana na Muumba wa ulimwengu na uhai.

Uswalihina ni hali ya kimaumbile kwa mwanadamu, kwa muundo wake wenye upambanuzi, roho, akili na mwili, William James Durant anasema katika *Qiswatul-Hadhwarah*: "Hakika Kuhani hakutengeneza dini, lakini ameitumia kwa ajili ya maslahi yake tu, kama mwanasiasa yeyote anavyomtumia mwanadamu kutokana na msukumo wa kimaumbile na ada. Haikumea itikadi ya kidini kutokana na ujanja ujanja au michezo ya kidini, hakika imemea kutokana na maumbile ya mwanadamu kwa ambayo humo kuna maswali yasiyoisha, hofu, huzuni, matarajio na kuhisi kujitenga."[117]

[117] Deoranet: Wool katika *Qiswatual-Hadhwarah*, Juz. 1, uk. 117 Darul-Fikiri 1988.

Lakini mwanadamu anaweza kupotea njia ya dini sahihi, asipopata taufiki ya uongofu wa Mwenyezi Mungu na ujumbe wa mbinguni.

**Je, maendeleo ya kimaada yanatosha?**

Baadhi wanaweza kufikiri kwamba jamii zetu zinahitaji maendeleo ya kielimu, na maendeleo ya teknolojia, mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi, ili kuungana na msafara wa ustaarabu na maendeleo. Ama pande za kiroho na za kidini, ni jambo la pembezoni la kukamilisha tu, halina dauru katika kutengeneza hali ya mabadiliko na maendeleo. Lakini pamoja na kukiri jamii zetu kuhitajia maendeleo ya kielimu kiteknolojia, kisiasa na kiuchumi, isipokuwa kushibisha upande wa kiroho kuna umuhimu wa kimsingi, haiwezekani kupuuza upande wake.

Hakika jamii za kimagharibi zilizoendelea ambazo tunataka kukaribia kiwango cha maendeleo yake unaishi katika matatizo hatari ya kijamii. Yanakwaza utamu wa maendeleo kwa sababu ya yale wanayokabiliwa nayo miongoni mwa mwanya na pengo la kiroho. Ustawi wa kimaada na maendeleo ya kielimu, peke yake haumpi mwanadamu mafanikio na matumaini, na ikiwa hajajaza pengo la kiroho hakika maisha ya mwanadamu yatakuwa yanakabiliwa na adhabu na mkanganyiko.

**Albert Einstein ni mfano:**

Mtu ambaye ameweka nadharia ya nisibiya alikuwa ni mwenye kufeli katika maisha yake binafsi, bali Albert Einstein alikuwa ni mpenda wanawake, mkali, mwenye muamala mgumu pamoja na watoto wake, baba wa binti asiyekuwa wa kisharia. Hakumuona wala hakumkubali anayeitwa Lieserl, na nyaraka zinafichua kumbukumbu baina yake kuna barua binafsi – ndani ya familia – kwamba ndoa ya Einstein ya kwanza kwa Malaga Marek ilipelekea talaka kwa sababu ya uhusiano wa siri uliomfungamanisha na jamaa yake wa karibu, Elissa.

Na barua zinaonyesha uovu wa Einstein wa kumfanyia hila mke wake Malaga wakati wa kufarakana kwao, jambo ambalo lilipelekea kupatwa na mdororo wa mishipa na hakupona kwawo hadi kufariki kwake. Na unaendelea uovu huo katika muamala wake na watoto wake Hans Albert Einstein mkubwa na alikuwa na miaka kumi na tano wakati mzazi wake alipohama nyumba ya familia, na Eduard Albert Einstein mdogo ambaye alipatwa na wazimu baada ya kutalikiana wazazi wake na akamaliza maisha yake kwa kulazwa katika hospitali ya wagonjwa wa akili, na mzazi wake hakumtembelea hata mara moja.[118]

Na mfano wa Einstein uliotokea kwa **Neil Armstrong** naye ndiye mtu wa kwanza nyayo zake kukanyaga juu ya mwezi. Ilikuwa tarehe 20 July 1969, isipokuwa alikuwa hana furaha na utulivu kwani alimtaliki mke wake na akahitalifiana na watoto wake na akamaliza maisha yake kwa mkanganyiko na huzuni.

**Kuhusu hali ya jamii ya Kimarekani:**

Jamii ya Kimarekani iko katika kilele cha maendeleo ya kimaada ya kileo, lakini pengo la kiroho katika jamii hiyo limezalisha ongezeko na mateso hatari katika maisha na tabia kwa Waamerika, ambapo kunaenea huzuni, na matukio ya kujinyonga yanaongezeka, na makosa ya ubabe yanaongezeka, hata katika kiwango cha wanafunzi wa shule za msingi kama vilivyozungumzia hayo vyombo vya habari, ukiachilia mbali kiwango cha ufisadi wa tabia ulioenea.

Mwaka uliopita ilitoka orodha ya vitabu vinavyouzwa zaidi Marekani. Kulingana na gazeti la *New York Times*, kitabu ***Final Exit*** kilichotungwa na Mwingereza Derek Humphry kinachozungumzia mbinu za kujinyonga na njia zake mbalimbali, kilichoandikwa kwa lugha ya mwongozo na kuelekeza, ndicho

[118] *Al-Hayatu*: Jarida la kila siku – London 14 Swafar 1414H.

kinachoongoza.[119]

Hali hii mbaya ilizindua macho ya wanafikra wa kimagharibi sehemu ya kasoro katika maendeleo ya kimaada, nayo ni pengo na mwanya wa kiroho, kama ambavyo ilisukuma makundi ya jamii ya Kiamerika na ya kimagharibi kutafuta juu ya chanzo cha ilhamu ya kiroho, inayoziba pengo hilo, na kujaza pengo hilo, jambo ambalo limetoa nafasi ya kustawi mielekeo ya uongo na ukhorafi.

Na kuhusu hali hii anazungumza mtafiti wa Kimarekani Rostow katika kitabu chake *Stages of Growth,* anaona: Hakika dola zinapita katika hatua nyingi: Hatua ya jamii ya mwanzo, hatua ya kujitayarisha kuanza, hatua ya kupevuka, hatua ya utumiaji wa jamhuri na baada yake. Na anatilia mkazo kwamba majimbo ya Amerika yaliyoungana ni jamii pekee ambayo imefikia kwenye hatua ya utumiaji wa jamhuri, na kwamba inahamia kwa yaliyo baada yake. Na katika muonekano wa hatua hii ni kwamba jamii inazalisha zaidi kuliko inavyotumia, na inapunguza tatizo lake la kiuchumi katika kutengeneza mahitaji, na sio kutimiza lengo. Na vinatawala humo vyombo vya habari na zana za propaganda, ambapo inageuka kuwa ushibishaji wa kimaada kwenda kwenye ambayo yanaweza kuitwa mwelekeo wa kiroho, na kisha unaenea ukhorafi na dhana, madhehebu, bidaa na udanganyifu, ni sawa sawa unaambatana na dini au nje na dini au dhidi yake.

Kama inavyoashiria katika jamii ya Kiamerika yenye umahususi na sifa maalumu nayo ni utajiri, bali hakika Marekani ni dola tajiri ambapo pato la taifa kwa jumla linazidi dola trillion 5.5, wakati ambapo wastani wa pato la mtu binafsi linazidi dola 22 elfu, pamoja na kuinuka kiwango, utengenezaji, maendeleo na teknolojia, na umri unatarajiwa wakati wa kuzaliwa. Na mwenye kudadisi katika maisha ya kiamerika anaweza kushituka kwa mandhari mbalimbali kutoka kwenye mdororo wa kijamii hadi

[119] *Safir*; Jarida la kila siku – Beirut 30 Muharram 1412 H.

kwenye fujo ya ndani ambayo haina mafungamano nayo.

Na katika mambo ambayo yanazungumzwa na runinga ya Marekani vilevile ni mas'ala ya kufichua yaliyojificha, na kujua bahati, au kisomo cha msomaji, na kutafuta yaliyopotea hata kama ni mpenzi au rafiki au huenda ni mali na cheo. Katika hali hii ni juu yako kuwasiliana na namba iliyoandikwa katika runinga na kueleza unayokabiliwa nayo, au unayoyatafuta au pengine unayotaka kujiepusha nayo, na utapewa jawabu kuhusu unayoyataka: Je umepoteza mali ? Je, umepoteza karatasi na nyaraka muhimu? Ataoneka kwako mtu kivuli au tabibu anaku-ongoza kwa maelekezo ili kupata ulichokipoteza, na hatimaye atapata kutoka kwako haja yake nayo ni mali bila shaka.[120]

**Somo na zingatio:**

Sio makusudio katika kueleza chanzo cha udhaifu na kasoro katika maendeleo ya kimaada, kueleza sura mbaya yenye giza au maendeleo haya, na wala sio kudhihirisha hali ya jamii hizo tu kwani ni maendeleo yanayolazimisha utawala wake katika hali ya maisha, kwa mafanikio yake ya kielimu na teknolojia. Na ni wajibu kuwa na matarajio ya jamii zetu ili kuungana na msafara wake wenye kuendelea, na ili tufahamu umuhimu wa upande wa kiroho. Hivyo tusiupuuze na kuuacha, katika sensa ya hali ya jamii zetu bali tuzingatie ratiba na mikakati ambayo inastawisha uelewa wa kiroho na inayashibisha.

Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anamhadharisha mwanadamu kwa kusahau upande wa kiroho kwamba kunasababisha huzuni ya mtu binafsi na mkanganyiko wa kijamii, na kisha kusababisha maisha ya dhiki, na maisha mabaya. Anasema (swt):

"وَمَن أَعرَضَ عَن ذِكرى فَإِنَّ لَهُ مَعيشَةً ضَنكًا ....."

[120] *Al-Hayatu*: Jarida la kila siku – London, 29 Shawwali 1415 Hijiria

**"Na atakayejiepusha na mawaidha Yangu, basi hakika atapata maisha yenye dhiki….." (Surat-Twaha 20:124),** wakati ambapo uwiano na ukamilifu katika kuitikia mahitaji ya mwanadamu katika maelekezo yake ya kimaada, kiakili na kiroho unadhamini kwa mwanadamu maisha mazuri na mafanikio:

> **"مَن عَمِلَ صٰلِحًا مِن ذَكَرٍ أَو أُنثىٰ وَهُوَ مُؤمِنٌ فَلَنُحيِيَنَّهُ حَيوٰةً طَيِّبَةً….."**
>
> **"Mwenye kutenda mema, mwanaume au mwanamke, naye akawa ni muumini, tutamhuisha maisha mema….." (Surat An-Nahl; 16:97).**

## MAENDELEO YA MTU BINAFSI NA MAENDELEO YA JAMII

Kila mwanadamu aliye sawa sawa ana matarajio ya kuiletea nafsi yake maendeleo na utukufu katika maisha yake, na kuilinda dhati yake kutokana na mabaya na matatizo, nayo ni matumaini sahihi ya kisharia. Lakini ni njia ipi ya kufikia maendeleo? Na namna gani mwanadamu anafikia malengo yake na maslahi yake katika maisha haya?

Hakika njia ya kawaida ni mwanadamu kuibua uwezo wake na vipaji vyake, na kuitaabisha nafsi yake kwa ajili ya nafsi yake. Anajifunza, anatafakari na anafanya kazi. Anajituma na kujitahidi, na kila anapojitahidi zaidi ndivyo fursa ya kuendelea inakuwa kubwa zaidi. Lakini swali linalojitokeza ni juu ya upeo wa uhusiano baina ya maendeleo ya mtu binafsi na maendeleo ya jamii ambayo anahusiana nayo, je, hali ya jamii inaathiri katika kiwango cha mtu binafsi na hali yake? Au mtu binafsi anaweza kutengeneza hali yake kwa kujitenga, na kuiletea nafsi yake maendeleo kwa kufumbia macho hali ya jamii yake, sawa iwe na maendeleo au isiwe na maendeleo?

Hakika watu wengi wamejikita katika shughuli zao binafsi na wanajitahidi kupata maslahi yao binafsi bila ya kuwepo mambo makuu ya kijamii katika fikra zao au kutiwa katika orodha ya mazingatio yao, na hali ya kila mmoja wao ni: Mimi nashughulishwa na nafsi yangu kwa kujenga mustakabali wangu na kupanga mambo ya maisha yangu. Na mtazamo wenye uelewa katika maisha, unafichua kwa mwanadamu kwamba kuna uhusiano imara baina ya hali yake na hali ya jamii. Vyovyote utakavyokuwa uwezo wake na vipaji vyake, na vyovyote atakavyopata maendeleo na mafanikio, atabakia ni mwenye kuathirika na hali ya jumla ya jamii. Kwa hiyo inapasa fikira yake na mazingatio yake yawe ndani ya duara mbili za kimsingi: Kujijenga kwa ajili ya nafsi yake, na kuchangia jengo la jumla la jamii.

Na kwa kuzidi kuweka wazi zaidi tunaashiria katika baadhi ya nukta na ukweli ambao unadhihirisha kina cha mafungamano baina ya maendeleo ya mtu binafsi na maendeleo ya jamii.

**Kuandaa fursa za maendeleo:**

Ni sahihi kwamba mwanadamu anaendelea kwa juhudi zake na jitihadi zake na kwa vipaji vyake na uwezo wake. Lakini kupatikana fursa na maandalizi ya mazingira, ndio ambayo yanamuwezesha kuibua nguvu zake, na kutumia uchangamfu wake. Na jamii iliyoandaliwa inaleta kwa watu wake fursa za maendeleo, wakati ambapo jamii isiyoendelea zinakosekana au zinapungua humo fursa hizo. Kwa mfano katika nyanja za kujifunza, wanafunzi wetu katika nchi za Kiarabu sio wachache wa uelewa na uerevu kuliko wenzao wa Marekani, Japani au Ulaya, na baadhi ya watoto wetu wako juu katika juhudi na jitihada, lakini upeo wa maendeleo ya kielimu, na kiwango cha mfumo wa mafunzo na mazingatio ya kiwango cha uelewa na uerevu, na kupatikana nyenzo za kujifunzia katika jamii, katika

nyanja zote na ubobezi, ndio ambavyo vinatia nguvu fursa ya mwanafunzi zaidi.

Na katika nyanja za kifikra na maarifa kunapatikana katika nchi za Kiislamu akili shujaa na akili zenye mwanga, lakini uchache wa vituo vya utafiti na majaribio, na udhaifu wa vyombo vya kutoa rai unafanya fursa za maendeleo ya kielimu kuwa chache. Kwa ushahidi katika hilo, hakika baadhi ya watoto wetu katika jamii zilizoendelea wamepata maendeleo makubwa katika nyanja za kielimu na teknolojia mbalimbali, na Mwarabu wa kwanza kupata tuzo ya Nobel katika nyanja ya elimu ni Dokta Ahmad Zuwail, Mmisri ambaye anaishi Marekani na alipata tuzo mwaka 1999 katika Kemia.

**Athari ya mazingira:**

Ni kawaida mwanadamu kuathirika kwa mazingira ambayo jamii yake inaishi, na ikiwa mazingira ni mazuri anajipamba kwa maadili mema na yanashajiisha kwenye harakati na maendeleo. Hakika yanatengeneza mazingira yanayosaidia kumsukuma mtu na maendeleo yake, na ikiwa mazingira ya jamii ni mabaya yanatawaliwa na kutokuendelea na yanatawaliwa na hali ya uvivu na visingizio, na yamechanganyika na ufisadi na fitina, hakika yataacha athari zake na alama zake katika nafsi ya mtu na nyendo zake katika hali ya jumla. Mtu binafsi haishi katika kisiwa kilichojitenga au jangwani, bali yeye ni sehemu ya mkusanyiko, anaamiliana na anashirikiana pamoja na hali iliyotawala kwa kawaida. Na hii iko wazi katika nyanja ya kiafya kwa mfano, ambapo kuchanganyika kwake na watu waliopatwa na baadhi ya maradhi anaweza kupatwa na magonjwa kwa wepesi. Na vivyo hivyo, hakika fikira nyingi na nyenendo mtu anazichukua na kujipamba nazo kutokana na kuingiliana kwake na jamii.

**Matokeo na mwongezeko:**

Jamii ikipatwa na tatizo au fitina hakika matokeo yake na muongezeko utawakumba wote, bila ya kubagua aliyeshiriki na asiyeshiriki. Kuwepo kwa hali ya ufakiri katika jamii, kunaweza kuleta athari za ujeuri kwa matajiri na kuenea kwa maasi na maovu, yanayohadharisha hatari hata kwa wachamungu wema.

Na kwa sababu hiyo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

"وَاتَّقوا فِتنَةً لا تُصيبَنَّ الَّذينَ ظَلَموا مِنكُم خاصَّةً....."

> **"Na jikingeni na fitina ambayo haitawasibu wale waliodhulumu miongoni mwenu peke yao." (Surat Al-Anfal; 8:25).**

Na hapa Mwenyezi Mungu amewajibisha kuamrisha mema na kukataza maovu, na akambebesha mwanadamu sio jukumu la kutengeneza nafsi yake tu bali na kufanya juhudi kuwaongoa wengine na kuwarekebisha wao vilevile, ili kulinda jamii kutokana na uharibifu na ufisadi.

Na Mtume wa Mwenyezi ﷺ anafananisha matokeo ya vitendo vya mafisadi katika jamii yote na mwenye kutoboa meli. Ataisababisha kuzama na wote waliomo humo, anasema ﷺ: "Mfano wa mwenye kusimama katika mipaka ya Mwenyezi Mungu na mwenye kuanguka humo ni kama mfano wa watu waliopanda meli baadhi yao wako juu na baadhi yao wako chini. Wale waliopo chini wanapohitaji maji wanapita kwa walio juu yao wakasema: Lau tungetoboa katika sehemu yetu tundu na tusiwaudhi walio juu yetu, kama watawaachwa na waliyoyataka wataangamia wote, na wakiwazuia watanusurika na watanusurika wote.[121]

[121] Al-Bukhariy: Muhammad bin Ismail katika *Sahihul-Bukhariy*, kitabu sharikati Juz. 3 uk. 278, al- Maktabatu Thaqafiyah – Beirut.

Na mfano unaonekana mbele yetu wanayokabiliwa nayo wananchi wa Iraki waliopata balaa ya utawala wa Sadamu na siasa yake mbaya, ambapo hakusalimika na mbinyo na matokeo ya ufisadi huu yeyote miongoni mwao hadi ambaye anaona yuko mbali, na hahusiani na jambo kati ya mambo, hakika hakuwa ni mwenye kunusurika kutokana na adha na mateso.

**Nafasi ya jamii:**

Ikiwa unanasibiana na umma wenye nguvu na unafungamana na jamii tukufu, hakika hilo linakupatia ulinzi na kinga, na linatoa kwako nafasi za fursa yenye manufaa. Ama ikiwa umma wako hauna nguvu, au jamii yako ni dhaifu, imekandamizwa, hutopata bahati ya kuangaliwa kwa heshima na wengine, kwa kuchunga haki zako na kuheshimu kipaji chako. Na kisha nafasi yako ya kijamii na nafasi yako miongoni mwa jamii ina uhusiano katika kupanga nafasi yako na hali yako utake usitake.

Hakika sisi sasa hivi tunaona wazi namna gani kila upande katika ulimwengu unapigia hesabu, mara elfu moja katika kuamiliana na myahudi yeyote au jambo kati ya mambo ya myahudi, kwa sababu wao wamekuwa katika nafasi inayowapa wao hayo. Kabla ya muda serikali ya Misri iliamua kupasua njia ya kuzunguka Cairo kwa urefu wa kilometa 95, ili kupunguza msongamano wa mwendo katika mji mkuu, msongamano wa barabarani kila siku wa watu milioni 15, lakini njia hii inapitia katika makaburi ya zamani ya Wayahudi katika eneo la Basatin. Makaburi hayo yana zaidi ya miaka 70, na eneo lina makaburi 350 takriban, na ardhi ya makaburi kwa asili sio miliki ya Wayahudi, bali ni zawadi kutoka katika serikali ya Misri. Na serikali ilitaka kuondoa kaburi kwa kiasi cha mita 30 tu, ila Wayahudi walizua zogo kubwa ulimwenguni na wakaunda tume kati ya viongozi wa makundi ya Kiyahudi katika ulimwengu ili kukutana na Raisi wa Misri na viongozi wake. Na wakafungua madai kwa anwani mbalimbali katika mahakama ya Misri ili

kuzuia kuguswa kwa namna yoyote makaburi ya wafu, na matokea yake makaburi yalibakia na kujengwa na daraja juu yake.

**Nafasi ya mtu binafsi katika maendeleo ya jamii:**

Katika yote yaliyotangulia inabainika kwetu mafungamano yenye nguvu baina ya hali ya mtu binafsi na hali ya jamii, na kwamba anayefikiria katika kujenga mustakabali wake na kupata maendeleo kwa ajili yake ni juu yake alete fikra na kuzingatia hali ya jamii yake na afanye hayo ni sehemu ya msingi katika ratiba yake ya harakati zake na juhudi zake.

**Namna gani mtu binafsi anachangia katika maendeleo ya jamii yake?**

1. Hakika mazingatio ya mtu binafsi katika kujenga dhati yake, na juhudi yake katika kupata maendeleo na mafanikio kwa ajili ya nafsi yake, kwa hakika ni mchango kutoka kwake katika maendeleo ya jamii. Hiyo ni kwa sababu maendeleo ya jamii yanapatikana kwa maendeleo ya watu binafsi, hivyo kila mtu anaongeza nguvu katika hazina ya jamii kwa sharti la kuhisi kwake kunasibiana na jamii, na kushirikiana kwake pamoja na harakati za jumla za jamii.

2. Mtu binafsi anaweza kuelekeza juhudi zake na harakati zake ndani ya juhudi zake binafsi ili zilenge katika njia ya kuhudumia jamii, na kufanikisha mkakakti wa maendeleo yake. Mwanafunzi anapochagua ubobezi wa kielimu katika masomo yake ya juu ni wajibu wake aangalie haja ya jamii yake. Na mfanyakazi anapo-fikiria katika kuzalisha ni wajibu wake aelekee kwenye miradi ambayo inainua harakati za uchumi wa jamii na kutatua baadhi ya matatizo yake. Na mwanafasihi na mwanafikra atumie kipaji chake cha fasihi na uvumbuzi wake wa kifikra katika kuamsha

jamii na kuendeleza hali yake.

3. Kama jukumu la mtendaji analifanya mtu binafsi katika maendeleo ya jamii atenge sehemu katika uwezo wake wa kifikra, kielimu na kimaada ili aitumie katika huduma inayonufaisha watu wote, na hiyo ni kupitia kushiriki katika taasisi za kijamii na shughuli za kujitolea. Na vyovyote atakavyoshughulika mwanadamu na mambo yake maalumu, hakika anaweza kutumia kiasi cha wakati wake kila siku au kila wiki kwa ajili ya kuhudumia umma. Na baadhi wanadhani kwamba kubeba baadhi ya majukumu ya kijamii na kutoa baadhi ya wakati wao au juhudi zao au mali zao itakuwa ni kwa hesabu ya mambo yao na shughuli zao maalumu. Lakini dhana hii sio makini, kwani matokeo ya wanayoyatoa katika maslahi ya jumla yataakisi kwao kwa yale yaliyotangulia ubainifu wake katika athari na matokeo ya maendeleo ya jamii katika hali ya mtu binafsi. Na kwa hiyo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

"إِن أَحسَنتُم أَحسَنتُم لِأَنفُسِكُم ....."

**"Mkifanya uzuri mnajifanyia wenyewe" (Surat Bani-Israil; 17:7).**

Kama ambavyo tunayoyaitakidi katika rehema ya Mwenyezi Mungu na ukarimu yanatupa imani na matumaini ya kurejeshewa ambayo mtu ametoa katika njia ya Mwenyezi Mungu, na katika kuwasaidia waja Wake, kwa nyongeza maradufu zaidi ya aliyotoa. Anasema (swt):

مَثَلُ الَّذينَ يُنفِقونَ أَموٰلَهُم فى سَبيلِ اللَّهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ أَنبَتَت سَبعَ سَنابِلَ فى كُلِّ سُنبُلَةٍ مِائَةُ حَبَّةٍ وَاللَّهُ يُضٰعِفُ لِمَن يَشاءُ وَاللَّهُ وٰسِعٌ عَليمٌ

**"Mfano wa wale wanatoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje**

**inayochipuza mashuke saba; katika kila shuke pana punje mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mjuzi." (Surat Al-Baqara; 2:261).**

Na imepokewa kutoka kwa al-Habib al-Mustafaa ﷺ kwamba amesema: "Mbora wa watu ni yule mwenye kunufaisha, basi kuwa ni mweye manufaa kwao."[122] Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anambariki mwanadamu katika wakati wake, anapotoa sehemu yake katika kutumikia jamii, na anaongeza katika riziki yake anapotoa kwayo katika mambo ya kheri na anampa nguvu na uchangamfu katika kwenda kwake mbio katika haja za watu na mambo yao. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

"..... وَما أَنفَقتُم مِن شَىءٍ فَهُوَ يُخلِفُهُ وَهُوَ خَيرُ الرّٰزِقِينَ"

**"Na chochote mtakachotoa Yeye atakilipa. Naye ni Mbora wa wanaoruzuku." (Surat Saba' 34:39)**

Ni ahadi ya kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kumrejeshea ambaye anatoa katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Anasema Imamu Ali عليه السلام: "Waamrishe watu wako waende kuchuma mema na waingie katika haja za aliyelala. Naapa kwa ambaye usikivu Wake unasikia sauti zote, hakuna yeyote atakayetia furaha katika moyo isipokuwa Mwenyezi Mungu anamuumbia kutokana na furaha hiyo huruma, atakaposhukiwa na la kumshukia (kifo) itamwendea mbio kama vile mafuriko katika mteremko hadi ikifukuze kama ngamia anavyofukuza mgeni."

4. Kusaidia mwenendo wa maendeleo katika jamii, ni juu ya

[122] Al-Hindiy: Ali al-Mutaqiy katika *Kanzul-Umaal*, Juz. 16, uk. 128, hadithi namba 44154 chapa ya tano 1985 Muasasatu Rusalati – Beirut.

watu binafsi washajiishe kila juhudi za shughuli nzuri, inayotokana na ardhi ya jamii yao. Kushajiisha na kushughulika ni jambo la dharura ili kuhifadhi uzalishaji, na maendeleo yake katika nyanja mbalimbali. Mwanachuoni anapozungukwa na watu wa jamii yake, na khatibu anapoamiliana pamoja nao wasikilizaji, na mwanafikra anapoona upokezi wa fikra zake, na mwanafasihi anapohisi kukubalika utoaji wake na mtengenezaji inauzika bidhaa yake. Na mtangazaji watu wanaponunua uzalishaji wake yote hayo yanatengeneza nguvu ya maendeleo na mabadiliko katika harakati ya jamii.

5. Ama kudharau uzalishaji wa ndani, na nguvu ya uananchi, kwa maslahi ya uagizaji kutoka nje, na kujifunga na yaliyo nyuma ya mipaka, hiyo ni hali ya kushindwa na ubinafsi, wanaweza kupatwa baadhi ya jamii hadi ikaenea kwa watu methali inayosema: njiwa wa shamba haimbi (Jogoo wa shamba hawiki mjini).

Na baadhi wamekuwa wanajifakharisha kwamba ananunua kutoka nje ya nchi yake au anatumia bidhaa za nje ya nchi yake, na anaweza kutoa hoja kwa uzuri wake na umakini wake, lakini mambo wakati mwingine hayaepukani na kuvutiwa na nje, na kuathirika kwa propaganda. Na ili kinyanyuke kiwango cha ubora na maendeleo ya uzalishaji katika nchi, ni lazima kushajiisha na kuunga mkono, pamoja na kutoa angalizo la mabadiliko na ukosoaji wenye kujenga. Na mara nyingi tunalazimika kuleta ushahidi kutoka katika hali pinzani, nayo ni hali ya Kiyahudi, kwa ajili ya kupata zingatio na somo. Wayahudi kila sehemu wanazingatia kushajiisha baadhi yao kwa baadhi, na kuunga mkono uzalishji wao wa ndani. Na ulipoanza utalii, Waisiraili wanakuja Jordani, baada ya maafikiano ya amani baina ya Jordani na Israil. Yalishitushwa mazingira ya utalii Jordani – kama yalivyoeleza magazeti na vyombo vya matangazo – kwa siasa ya ubakhili ambao anasifika nao mtalii wa Israil. Wao wanabeba pamoja nao chakula maalumu kwao, chini ya madai kwamba wao wanahifadhi ibada ya kula chakula

cha kiyahudi, ambayo inalazimisha kwao kula chakula cha kiyahudi kilicho halali au al-kosher, lakini si kingine isipokuwa ni kisingizio, ambapo wao hawaleti chakula chao kilicho halili tu, bali na chupa za maji je kuna maji halali na mengine ni haramu? Na alikwishazungumza Waziri Mkuu wa Jordani wa zamani Abdu Salaam al-Majaaliy pamoja na viongozi wa Israil kuhusu maudhui kwa kuashiria kwamba chupa za maji Jordan ni rahisi zaidi kuliko Israil, pamoja na hivyo watalii wa Kiisrail, na wao ni kati ya wenye uwezo na matajiri wanaleta chupa za maji.[123]

**Mazingatio ya kijamii:**

Na mwisho hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu hakubali tuishi kwa ubinafsi, tufikirie na twende mbio katika mpaka wa duara la ubinafsi. Hakika hayo hayaafikiani pamoja na uswalihina halisi wa kweli, ambapo Qur'ani tukufu inatia mkazo kwamba kupuuza mambo ya jamii, na sehemu dhaifu humo, ni dalili na alama juu ya uongo wa madai ya kuwa na dini, anasema (swt):

أَرَءَيتَ الَّذى يُكَذِّبُ بِالدّينِ ﴿١﴾ فَذٰلِكَ الَّذى يَدُعُّ اليَتيمَ ﴿٢﴾ وَلا يَحُضُّ عَلىٰ طَعامِ المِسكينِ ﴿٣﴾

**"Je umemuona ambaye anakadhibisha dini. Huyo ni ambaye humsukuma yatima. Wala hahimizi kumlisha masikini." (Surat-Mau'n 107:1-3)**

Hakika kupuuza tu mayatima na kuwaacha na kutohimiza juu ya kujali haja za mafakiri, inamaanisha kwamba uswalihina ni wa uongo na wa udanganyifu. Mtume Muhammad ﷺ anamzingatia asiyejali mambo ya umma yuko nje ya duara la Uislamu "Mwenye kuamka na asijali mambo ya Waislamu basi sio Mwislamu."[124]

[123] *Al-Hayatu* – Jarida la kila siku – London 18 March 1995 uk: 12
[124] Al-Kulainiy: Muhammad bin Yaaqub katika *al-Usulu Minal Kaafiy*, Juz.2 uk. 163, Darul-Adhuwai – Beirut.

# JAMII YENYE UELEWA

Ili mwanadamu awe ni shakhsiya huru yenye kuweza kuchukua maamuzi na kufanya mikataba na wengine ni lazima afikie kwenye kiwango cha uelewa, kulingana na hukumu za fikihi ya Kiislamu. Hiyo ni kwa kuwa hukumu za mikataba kuhusiana na mwanadamu zinatofautiana kwa kutofautiana hatua za maisha yake kiasi kwamba ukamilifu wa uwezo na upungufu wake, yeye katika hatua ya kwanza, kuanzia kuzaliwa hadi umri wa utambuzi anakuwa ni mpungufu, na kwa istilahi ya kifikihi (hana utambuzi) hivyo hausihi muamala wake kikanuni kwa sababu hana uwezo.

Na katika hatua ya pili: Katika umri wa utambuzi hadi umri wa uelewa, ambapo anapambanua mambo na anatofautisha lenye manufa na lenye madhara, lakini yeye bado hajafika kwenye hatua ya ukomavu na uelewa, hapa vilevile wengi wa mafakihi wanaona kutokuwa huru kwake katika kufanya muamala na kuchukua maamuzi katika miamala, hata kama ni baleghe na ni mwenye akili. Kubaleghe na akili ni masharti mawili ya taklifu ya kisharia kwa maana kwamba analazimika kwa taklifu na maamrisho ya kidini, lakini kama hajafikia kiwango cha uelewa uwezo wake hauwi ni wenye kukamilika kupitisha maamuzi yake na kusahihisha miamala yake.

Hatua ya tatu: Mwelewa au mwenye ufahamu, ambapo inasihi miamala yake na maamuzi yake yote. Na maana ya mwelewa ni utendaji mzuri, na kuweka mambo katika mahala pake, na balehe inaweza kuambatana nao, na inaweza kuchelewa kidogo au zaidi, na inaweza kutangulia, lakini hakuna mazingatio kwake kabla ya kubaleghe.

Na kwa mwelewa hakuna umri maalumu kwa watu wa fikihi, bali jambo linaachwa kwa utayari wa mtu na malezi yake, na nususi za kisharia hazipangi hilo. Na aghlabu sheria za kimji za hali za watu katika dola zinamzingatia mwanadamu kamilifu muweza na

mwenye utu huru katika umri wa miaka kumi na nane, na baadhi yake kama vile sheria ya Misri inaisogeza hadi umri wa miaka 21.

Kama ambavyo kujua uelewa wa mwanadamu unarejea kwenye kuangalia vitendo vyake na muamala wake, anasema (swt):

"وَابتَلُوا اليَتٰمىٰ حَتّىٰ إِذا بَلَغُوا النِّكاحَ فَإِن ءانَستُم مِنهُم رُشدًا فَادفَعوا إِلَيهِم أَموٰلَهُم ....."

**"Na wajaribuni mayatima mpaka wafikilie umri wa kuoa. Mkiwaona wana uwekevu, basi wapeni mali zao." (Surat An-Nisaa'; 4:6).**

Ambapo mali ya yatima mdogo inakuwa chini ya mamlaka ya walii wake, na anapobaleghe na ukaonekana kwake uelewa anapewa mali zake, ili yeye abebe jukumu la kuisimamia. Na baadhi ya mafakihi wanatofautisha baina ya uelewa katika nyanja za kimali, na uelewa katika nyanja ya kijamii. Mwanadamu anaweza kuwa ni mzuri katika usimamizi wa mambo ya kimali lakini hamiliki ukomavu wa kijamii katika kuendesha maisha ya familia. Hapa hawi huru katika maamuzi ya kufunga ndoa, bali ni lazima kupatikane idhini ya walii wake, hata kama vitendo vyake vya kimali vinapitishwa na ni sahihi. Kama alivyoashiria hilo Sayyid Muhammad Kaadhim al-Yazidi katika *al- Ur'watul-Wuthqah* katika mas'ala ya nane katika mas'ala ya mawalii wa ndoa.

**Uelewa katika mantiki ya Qur'ani:**

Mazungumzo kuhusu uelewa yamekuja katika Qur'ani mara kumi na tisa, na katika baadhi yake yamekuja kwa kutia dhuma Rau na kutia sakna Shin (رُشْد) kama vile kauli Yake (swt):

"لا إِكراهَ فِى الدّينِ قَد تَبَيَّنَ الرُّشدُ مِنَ الغَىِّ ....."

**"Hakuna kulazimisha katika dini uongofu umekwisha pambanuka na upotofu." (Surat Al-Baqara; 2:256).** Na kauli yake: **"Mkipata matumaini ya uongofu kutoka kwao."** Kama vile kauli yake (swt): **"Na tuandalie sisi katika jambo letu uongofu." (Surat An-Nisaa': 6).** Na imekuja katika sehemu nyingine kwa kutia fatiha Rau (رَشَدا) kama vile kauli yake (swt): **"Na utuandalie sisi uongofu katika jambo letu. " (Surat al-Kahf: 10),** nayo ni maneno yenye kufanana na inaonekana kwamba makusudio ya *Rushd* (uongofu) katika mantiki ya Qur'ani, ni ambayo ni mukabala wa *Ghayi* (upotovu) nayo ni kwa maana ya uongofu katika mkabala wa upotovu na kupotoka. Nao ni mukabala ulio wazi katika kauli Yake (swt):

> **"....وَإِن يَرَوا سَبيلَ الرُّشدِ لا يَتَّخِذوهُ سَبيلًا وَإِن يَرَوا سَبيلَ الغَيِّ يَتَّخِذوهُ سَبيلًا ....."**
>
> **"Na wakiona njia ya uongofu hawaishiki kuwa ndio njia; lakini wakiona njia ya upotovu wanaishika kuwa ndio njia….." (Surat Al-A'araf; 7:146).**

Kama ilivyokuja kutumia neno Rushd mukabala wa safihi, na inakuwa kwa maana ya muamala mzuri na uendeshaji, katika mukabala wepesi wa rai na udhaifu wa uendeshaji, na haya ndio makusudio ya mukabala katika mazungumzo kuhusu kuchunga mambo ya mayatima katika kauli Yake (swt):

> **"وَلا تُؤتُوا السُّفَهاءَ أَموٰلَكُمُ الَّتى جَعَلَ اللَّهُ لَكُم قِيٰمًا وَارزُقوهُم فيها وَاكسوهُم وَقولوا لَهُم قَولًا مَعروفًا ﴿٥﴾ وَابتَلُوا اليَتٰمىٰ حَتّىٰ إِذا بَلَغُوا النِّكاحَ فَإِن ءانَستُم مِنهُم رُشدًا فَادفَعوا إِلَيهِم أَموٰلَهُم ....."**
>
> **"Na wala msiwape wapumbavu mali zenu ambazo Mwenyezi Mungu amewajaalia kuwaendeshea maisha. Na muwakimu katika mali**

**hiyo na muwavishe, na muwaambie maneno mazuri. Na wajaribuni mayatima mpaka wafikilie umri wa kuoa. Na mkiwaona wana uwekevu basi wapeni mali zao…..” (Surat An-Nisaa’; 4:5-6).**

Kabla ya kumiliki uwekevu mwanadamu anakuwa ni dhaifu wa rai, hana uwekevu, nayo ndio inayoitwa *safhi* (wasio na akili), akivuka hatua hii anaitwa Rashidi mwenye akili (uelewa).

**Uelewa wa kijamii:**

Tunaweza kuzungumza juu ya uelewa katika kiwango cha watu binafsi, na tunaona mtu binafsi ni mwelewa anapambanua maslahi yake na anafanya muamala mzuri na usimamizi katika mukabala wa mtu dhaifu wa rai, hachukui msimamo unaofaa katika yanayomkabili katika nyakati na mazingira. Na tunaweza kuzungumzia juu ya uelewa katika kiwango cha jamii na makundi, kuna jamii yenye uelelewa na jamii isiyo na uelewa na upevu, namna gani tutanyoosha jamii na makundi katika nyanja hii? Na nini alama za uelewa wa kijamii? Katika Qur’ani tukufu yamekuja mazungumzo kuhusu jamii yenye uelewa ndani ya kauli Yake (swt):

”….. وَلٰكِنَّ اللَّهَ حَبَّبَ إِلَيكُمُ الإيمٰنَ وَزَيَّنَهُ فى قُلوبِكُم وَكَرَّهَ إِلَيكُمُ الكُفرَ وَالفُسوقَ وَالعِصيانَ أُولٰئِكَ هُمُ الرّٰشِدونَ “

**“…..Lakini Mwenyezi Mungu amewapendezea Imani na akaipamba katika nyoyo zenu, na akauchukiza kwenu ukafiri na upotovu, na uasi. Hao ndio walioongoka.” (Surat Al-Hujurat; 49:7).**

Na aya tukufu inaashiria katika sifa muhimu katika jamii ongofu, nayo ni mshikamano wa kinafsi na kifikira na kimwenendo

pamoja na misingi na kanuni za kisharia. Msingi ambao jamii inaamini wakati mwingine ni anwani tu na wakati mwingine msingi unachukuliwa kwa msingi wa kupokea kutoka kwa waliotangulia bila ya uelewa na kukinai. Na jamii inaweza kuamiliana pamoja na itikadi kwa kiwango cha roho na nafsi, lakini katika upande wa kiakili na kifikra kuna uangalizi na matatizo na inaweza kutokea kinyume kwa uwepo wa kukinai kifikra ya nadharia bila ya kupatikana kushadidia kiroho na kinafsi, na inaweza kuwa itikadi na kanuni zake ni jambo limelazimishwa katika jamii ile na uwepo wake, wakati inaamini itikadi ya kurithi bila ya kukinai au inaamini itikadi na haijilazimishi kutekeleza mfumo wake na kanuni zake katika uhalisia wa maisha yake, au inanyenyekea katika sharia yake kwa nguvu na kulazimishwa. Ama jamii yenye uelewa ambayo aya inaiashiria kwa kauli “hao ndio walioongoka” inasifika kwa sifa zifuatazo:

1. Kupenda itikadi na imani (amependezesha kwenu imani) kwa linalobeba neno la upendo katika maana za kuvutia nafsi na mshikamano wa kiroho.

2. Kuelewa itikadi (na amepambia katika nafsi zenu) yaani mmejua kwa akili zenu usahihi wa manhaji yenu ya kiimani, kwamba ni bora zaidi ambayo mnastawisha kwayo maisha yenu.

3. Kemeo la dhati juu ya kukhalifu na upotovu (na akawafanya mchukie ukafiri na ufusuka na maasi) nayo inatokana na sifa mbili zilizotangulia. Ikiwa mwanadamu anapenda itikadi yake kutoka ndani ya nafsi yake na mwelewa wa dini yake katika fikra yake na akili yake, hakika yeye kwa dhati yake anachukia maasi na anakimbia kwa kutoka katika mipaka ya nidhamu na kanuni, na vivyo hivyo hakika hali ya jumla katika jamii ongofu nayo ni kushikamana na kujidhibiti kwa msukumo wa dhati, na kujiepusha kukhalifu.

4. Hakika wakati Muumba Mtukufu anaponasibisha katika nafsi yake kupenda na kuchukia (amependezesha kwenu) na (amefanya mchukie) hakika haimaanishi kulazimisha kimaumbile katika hilo, bali makusudio ni kuandaa wasila na mazingira yanayofaa, na taufiki katika kukubali na kuitikia.

Na kupitia aya tukufu na katika mwanga wa waliopanga mafakihi maana ya uelewa ambao ni sharti kutimia ili kukiri kufaa kufanya mkataba na kufaa kitendo kwa mwanadamu, tunaweza kuashiria kwenye alama muhimu na sifa za jamii yenye uelewa.

**1. Uelewa na maarifa:**

Ikiwa mafakihi wanazingatia uwezo wa kupambanua maslahi na kutaofautisha kati ya kinachonufaisha na kinachodhuru, ndio mwanzo wa viwango vya uelewa ambao kwamba kunapatikana athari ya kisharia na kikanuni katika upande wa kukubali uwezo wa mwanadamu na uhuru wa utu wake, tunaweza kuiga kutokana na hilo kupanga mwanzo wa viwango vya uelewa wa kijamii, nao ni uelewa wa jamii na kujua kwake mambo na shughuli ambazo zinafungamana na hali yake ili aweze kubainisha maslahi yake na kutofutisha baina ya yale ambayo yanainufaisha na yale yanayoidhuru kama jamii.

Hakika wengi kati ya watu katika jamii wanazama katika huzuni zao binafsi, au wanashughulika na mas'ala ya pembezoni na wala hawaangalii katika mambo ya jamii yao, wala hawasaidii mazingira na hali ambazo zinazunguka umma wao. Na Qur'ani inatusimulia kuhusu jamaa yenye uelewa katika zama za Uislamu wa mwanzo, siku walipokuwa wachache Makkah wako katika mazingira ya ushirikina wakati huo, namna gani walikuwa wanazingatia matokeo ya vita baina ya Urumi na Uajemi. Yanayotokea katika nchi ya karibu Urumi na mpaka wake wa karibu na Uajemi, pamoja na umbali huu wa kijiografia ila hakika waumini Makkah walikuwa wanafuatilia vita. Na Waajemi

washirikina walipowashinda Ahlul-Kitabu wa Urumi, waumini waliathirika kwa kushindwa kwa Urumi, pamoja na kutokuwepo mawasiliano au muungano baina yao, jambo ambalo linaonyesha juu ya uelewa na ufahamu wa vita hivyo, na athari zake na uakisi wake. Na kwa hiyo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameteremsha sura kamili ya Qur'ani kwa jina la Surat Rum inayozungumzia kuhusu vita hivyo, na kuhusu harakati za waumini pamoja na matokeo yake na kuwabashiria wao kwa kubadilisha uwiano ndani ya muda mfupi, ambapo Urumi itanusurika katika miaka michache ijayo. Anasema Mwenyazi Mungu Mtukufu:

الم ﴿١﴾ غُلِبَتِ الرّومُ ﴿٢﴾ فى أَدنَى الأَرضِ وَهُم مِن بَعدِ غَلَبِهِم سَيَغلِبونَ ﴿٣﴾ فى بِضعِ سِنينَ لِلَّهِ الأَمرُ مِن قَبلُ وَمِن بَعدُ وَيَومَئِذٍ يَفرَحُ المُؤمِنونَ ﴿٤﴾

**"Alif Lam Mim. Warumi wameshindwa katika nchi iliyo karibu. Nao baada ya kushinnndwa kwao watashinda. Katika miaka michache. Amri ni ya Mwenyezi Mungu kabla yake na baada yake. Na siku hiyo waumini watafurahi." (Surat Ar-Rum; 30:1-4).**

Na tukichukua kwa jicho la mazingatio dauru ya ushahidi wa ulimwengu, ambao Mwenyezi Mungu amewapa waumini

"وَكَذٰلِكَ جَعَلنٰكُم أُمَّةً وَسَطًا لِتَكونوا شُهَداءَ عَلَى النّاسِ ....."

**"Na kama hivyo tumewafanya kuwa umma wa wastani, ili muwe ni mashahidi juu ya watu wote….." (Surat Al-Baqara; 2:143).**

Hakika hayo yanamaanisha dharura ya uelewa wa jamii ya kiimani kwa kiwango cha juu katika uelewa, wanaweza kwayo kufuatilia mabadiliko ya kiulimwengu, na uwiano wa kimadola ukiachilia mbali kuelewa kwake hali zake na mambo yake. Anasema Imamu Ali عليه السلام: "Ni lazima kwa mwenye akili mambo

matatu: Kuangalia jambo lake, kuhifadhi ulimi wake, na kujua wakati wake."[125]

## 2. Muamala mzuri:

Namna gani jamii inaamiliana katika mazingira, matatizo na shida? Je, inatawaliwa na hali ya kujisalimisha na kusubiria muujiza kutoka kwa asiyefahamika? Au inatawaliwa na hasira, hisia na kuendeshwa na hamasa zisizokuwa na mkakati sahihi? Au inakabiliwa na changamoto kwa kufikiria kimaudhui, na ratiba yenye hekima?

Uelewa wa jamii na upevu wake unapimwa kwa yale inayochagua na kufuata katika machaguo haya. Kushindwa mbele ya matatizo kunafichua ukosefu wa matakwa na udhaifu wa kujiamini, wakati ambapo kutumbukia katika hali ya hisia na hasira, na kutoweka hekima na kutafakari, kunaweza kuongeza na kuimarisha matatizo. Na kinachohitajia uelewa ni muamala mzuri, na kuchukua msimamo unaofaa katika nyakati zinazofaa. Mazingira yanaweza kuhitajia ukali na nguvu, na yanaweza kuhitajia hamasa na jaziba, na yanaweza kuhitajia upole na uelewa.

Na katika sira ya Mtume Muhammad ﷺ kuna mifano ya muamala mzuri katika nyakati mbalimbali. Waislamu wa mwanzo pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ walikuwa kama alivyowasifia Mwenyezi Mungu Mtukufu "Ni wana nguvu mbela ya makafiri." (Suratul-Fatih; 48:29). Na vita na mapigano ambayo walipigana yanafichua juu ya ushujaa wao na kujitolea kwao, lakini hawa wenye nguvu mbele ya makafiri, walikubali suluhu ya Hudaibiya katika mwaka wa sita hijiria, kwa yale ambayo yalidhamini itifaki ya suluhu kwa masharti yaliyoo-

[125] Ibun Shuubatu al-Haraaniy: al-Hasan bin Ali katika *Tuhful-Uqul*, uk. 144, chapa ya tano 1974 Muasasatu al-A'alamiy lilimatubuati – Beirut.

nekana kwa dhahiri yake, kuwa ni maslahi kwa washirikina na ni kushusha utukufu wa Waislamu, hadi baadhi ya masahaba walitawaliwa na hali ya jazba na hasira na kupinga yaliyotokea, kama anavyotaja Ibnu Hishamu na wanahistoria wengine: Kwamba Umar bin al-Khatab alimwendea Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu je, wewe si Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: Ndio (mimi ni Mtume). Akasema Je, sisi si Waislamu? Akasema: Ndio (sisi ni Waislamu). Akasema: Je, wao si washirikina? Akasema: Ndio (wao ni washirikina). Akasema: Kwa nini tunakuwa dhalili katika dini yetu? Akasema: “Hakika mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, sitokhalifu jambo lake, na hatonipoteza!” Mwandishi anasema: Umar alikuwa anasema: “Sikuacha kuwa ni mwenye kutoa sadaka na kufunga na kuswali na kuacha huru (watumwa) kwa kuhofia maneno yangu niliyozungumza siku hiyo, hadi nilipotarajia kuwa itakuwa kheri.”[126]

Suhail bin Amru, mzungumzaji wa makuraishi alikataa kuandikwa katika waraka wa suluhu: *Bismillahi Rahmani Rahiym*, na akang’ang’ania aandike badala yake: *Bismika Allahuma*. Mtume ﷺ akaafiki juu ya hilo. Kisha Suhail akapinga neno “Haya ndio aliyokubaliana Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu” kwa kusema: Kama ningeshuhudia kwamba wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu nisingekupiga vita, lakini andika jina lako na jina la baba yako tu: Mtume akaafiki katika hilo vilevile. Na Suhail akatoa sharti: Kwamba atakayemwendea Muhammad kati ya makuraishi bila ya idhini ya walii wake atamrudisha kwao, na atakayewaendea Makurasihi kati ya ambao wako pamoja na Muhammad basi hawatomrudisha kwake. Pamoja na kwamba ni sharti baya lakini Mtume ﷺ aliliafiki. Na ikatokea alikuja mmoja wa Waislamu mnyonge Makkah anakokota pingu zake na minyororo akakimbilia kwenye kambi ya Waislamu naye ni

[126] Ibnu Hishamu: *Siratun-Nabawiya*, Juz. 346 chapa ya kwanza 1415 Hijiria Daru Ihiyai Turathi al- Arabiy – Beirut.

Jandal bin Suhail bin Amru. Akasimama baba yake Suhail na akampiga uso wake na akataka kutoka kwa Mtume ﷺ amrejeshe kwa makurasihi, na akatae kukimbia kwake. Mtume akaafiki juu ya hilo, Abu Jundal akapiga kelele: "Enyi Waislamu Je, narudi kwa washirikina na wananifitinisha na dini yangu?" Jambo ambalo lilichochea jazba kwa Waislamu lakini Mtume ﷺ akamwambia: Ewe Jandal subiri na hesabia hilo kwa Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atajalia kwako na kwa walio pamoja nawe katika wanyonge kuwa ni faraja na ukombozi.[127]

Pamoja na yote hayo, Mwenyezi Mungu aliichukulia suluhu hii ni ushindi mkubwa "Hakika sisi tumekufungulia ushindi wa dhahiri" (Suratul-Fatih; 48:1). Kwa sababu matokeo yake yalikuwa ni kheri katika maslahi ya Uislamu, hivi ndivyo inavyohukumu akili katika msimamo na sio hisia tu. Na jamii yenye uelewa ndio ambayo inapambana na mazingira na kuchukua msimamo unaofaa mukabala wake kimaudhui na kutafakari.

3. **Kunufaika kutokana na uwezo**

Kila jamii ina uwezo wake wa kimazingira na wa kibinadamu ambao unatofautiana na unapitana kutoka jamii hadi nyingine. Na kinachotofautisha jamii yenye uelewa na nyingine ni mazingatio ya kuibua vipaji na kufanya kazi ya kuviendeleza na kunufaika navyo, na kuvitumia katika maslahi ya maendeleo ya jamii.

Hakika baadhi ya jamii zinapuuza sehemu zake za kimazingira na kusahau vipaji na uwezo wa watu wake, wakati ambapo jamii zenye uelewa zinakwenda mbio kukuza sehemu zake na kunufaika na uwezo wake wa kimazingira na kibinadamu kadri iwezekanavyo.

[127] Rejea iliyotangulia, uk. 347.

Na hii Cyprus kisiwa kidogo karibu yetu kinatoa mfano wa kunufaika na vipaji vya mazingira nacho kipo kona ya kusini mashariki ya bahari nyeupe ya kati, na kipo umbali wa kilometa 64 kusini mwa Uturuki na kilometa 100 Magharibi mwa Syria na wakazi wake ni chini ya watu 700,000. Na wao wako katika kiwango cha juu kama watu wa ulaya, na kiwango cha watu waliosoma humo ni asilimia 90. Pamoja na kwamba hawana utajiri wa mafuta na madini lakini wao wameendeleza mazingira mazuri na wamebadilisha nchi yao kuwa ni sehemu ya utalii muhimu, utalii unatengeneza humo sehemu ya kiuchumi na kisiasa, ukiongezea uzalishaji wa kilimo uliopo.

Na katika nyanja ya kuendeleza sehemu za kibinadamu, Japani inatoa mfano mzuri, ambapo nguvu yake ya kielimu na kiuchumi inatokana na kuendeleza kiwango cha utendaji wa kiteknolojia na kiviwanda kwa watu wake. Japani hivi sasa ni nguvu kuu ya kiuchumi katika ulimwengu pamoja na uchache wa sehemu zake za kimazingira, nayo inaagiza sana mali ghafi ambazo viwanda vyake vinazihitajia.

Ni kiasi gani zinamiliki jamii za umma wetu wa Kiislamu mion-goni mwa vipaji na uwezo mkubwa, lakini unachokihitaji ni maelekezo ya kuziendeleza na kuzistawisha na kuzitumia kwa ajili ya maendeleo na ustawi.

## MWANZO WA KUTENGENEZA UPYA

Inasifika historia ya mwanadamu kwamba imejaa mabadiliko na mageuzi wakati ambapo viumbe vingine hai, vinaendesha maisha yao kwa muundo mmoja tu, na njia moja muda wote wa historia. Hakika baadhi ya wanyama wanaweza kufanya kazi na kute-keleza jukumu linalomshangaza mwanadamu kwa uzuri wake na ufanisi wake, lakini wanafanya hayo ndani ya hali iliyopangwa na namna thabiti, hayatokei kwayo mabadiliko au mageuzi yoyote.

Nyuki, kwa mfano, huyu mdudu mzuri mwenye manufaa ambaye anatuzalishia asali, na anazalisha nta ambayo tunaitumia katika uzalishaji mbalimbali kama vile gundi, mshumaa na vifaa vya urembo kama ambavyo anahamisha mbegu za kiume kutoka ua hadi lingine, na kusaidia mimea kuzaliana.

Huyu nyuki anaishi ndani ya nyumba ya mfano katika mapori au masega ya nyuki, kwa muundo wa sanduku ambalo linamasega ya asali, nalo ni mrundikano wa vijimawe vyenye umbo la sudusi. Wanalitengeneza wafanya kazi wa nyuki kutokana na nta inayozalishwa na miili yao, na kila sentimita 10 ina chembe 50,000 – 60,000 za sudusi (1/6) na baadhi ya makundi yana nyuki 50,000 – 60,000. Miongoni mwao kuna malikia mmoja kazi yake pekee ni kutaga mayai kwa wastani wa mayai 2000 kwa siku wakati wa vuli, yaani yai moja kila baada ya sekunde 43, na kundi moja lina mamia ya madume katika kizazi cha malikia. Hayana kazi isipokuwa kumzalisha malikia tu. Lakini sio kwamba malikia ndiye aliyewazaa, kwa sababu kwa kawaida wanaoana na madume yaliyozalishwa katika kundi lingine. Na kuna maelfu ya nyuki watumishi, wanafanya kazi ya kusafisha njia za masega, kuwaletea nyuki asali kuzalisha nta, kutengeneza masega ya asali, kulinda nyumba ya nyuki, na kukusanya utomvu unaoletwa na nyuki (wengine). Wafanyakazi wa nyuki wanaweza kuruka kwa kasi ya kilometa 25 kwa saa na kukusanya katika maisha yao utomvu unaotosha kutengeneza jamu 45 za asali.

Huu ni mpangilio mzuri na utaratibu makini katika maisha ya nyuki, nayo ni hali madhubuti, hadi sasa imekwishapita miaka 80 milioni takriban tangu kuwepo kwa nyuki kulingana na makisio ya maulamaa, hajaguswa na mabadiliko au mageuzi.[128]

[128] Al-Mausuatu al-Arabiya al-Alamiyati juzuu 25 uk: 268 – 278 chapa ya ya pili 1999 Riyaadh

**Mabadiliko ni sifa ya mwanadamu:**

Mwanadamu peke yake anamiliki akili, na kwayo anaweza kubadilisha na kujadidisha katika maisha yake. Ama wanyama na viumbe vingine wanaendeshwa na utashi wao na mazingira yake ambayo Mwenyezi Mungu amewaumbia, wala hawana uwezo wa kufikiri na kubadilisha. Hivyo inabakia njia yao katika maisha ni thabiti na ya mazoea, wakati ambapo yanaendelea mabadiliko na mageuzi katika maisha ya mwanadamu.

Mwanadamu kila anapotumia akili yake na kutumia fikira yake, akanyanyuka kwa elimu yake na maarifa yake zinaongezeka njia za uboreshaji na mabadiliko katika maisha yake. Na kwa hiyo ananyanyuka kwenda katika kiwango kinachompambanua kama mwanadamu. Na anaposahau uwezo wake wa kiakili na akadumaza fikira yake na asiendeleze elimu yake na maarifa yake, anaishi maisha ya kulala na kudumaa, na kusogea kwenye uduni wa ulimwengu wa wanyama usio na mabadiliko.

Na waliosoma historia ya mabadiliko katika maisha ya mwanadamu, wanaona wigo wa uhusiano wake na kiwango cha fikra na kielimu kwa mwanadamu. Hivyo hakika kizazi chetu cha sasa kinaonekana kana kwamba kimeshazaliwa katikati ya historia, kwa sababu kilichotokea katika kizazi chetu tangu kuzaliwa kwake hadi sasa kinalingana takriban na yaliyotokea katika historia ya binadamu tangu kwa Adamu عليه السلام hadi wakati uliopo.

Na kwa mfano katika hilo: Katika mwaka 600 kabla ya kuzaliwa Isa, chombo cha usafiri wa haraka kilichokuwepo kwa mwanadamu ni ngamia, kwa kiwango cha maili 8 kwa saa, na kiwango hiki kimebakia kwa muda wa miaka 1600 takriban kabla ya kuzaliwa Isa. Walipogundua mkokoteni wenye matairi, ukaongezeka wastani wa kasi kwa kiasi cha maili 20 kwa saa, na kiwango hiki kimebakia maelfu ya miaka, karne 80 zilizopita na kwa fadhila ya meli za moshi zilizoendelea mwanadamu ameweza

kufikia kasi ya maili 100 kwa saa, lakini baada ya mika 58 ya kutumia meli za moshi, ameweza katika mwaka wa 1938 kuruka kwa haraka kwa kasi ya maili 400 kwa saa, mara nne zaidi ya kiwango kilichotangulia. Na baada ya miaka 20, katika miaka ya tisini katika karne hii kasi ya ndege ya roketi imefikia hadi maili 4000 kwa saa, na mwanadamu ameweza kuzunguka ardhi hii kwa vipando vya angani ambavyo vinakwenda kwa kasi ya maili 18,000 kwa saa.[129]

Hivyo mabadiliko na uboreshaji ni alama ya kunyanyuka kwa mwanadamu katika kiwango kinachompambanua na viumbe wengine, na ni kiashirio cha kuendeleza neema ya akili ambayo amepewa na Mweneyzi Mungu Mtukufu.

**4. Ulimwengu ni uboreshaji wenye kuendelea:**

Ulimwengu huu ambao tunaishi humo, uko katika hali ya kuendelea daima, ni uborekaji wenye kuendelea. Kuna nyota mpya zinazaliwa katika anga kwa mwendelezo, na wanaanga wanakiri kwamba wao hawafahamu upeo wa upana wa ulimwengu, pengine unapanuka bila ya kuwa na mwisho. Na wanaanga wamegundua kwamba mkusanyiko mwingi unaogelea baadhi yake uko mbali na baadhi kwa kasi sana. Na kwa kuongezea katika hayo inaonekana kwamba mkusanyiko ulio mbali zaidi na ardhi ndio ambao wenye mwendo kasi zaidi, kwa hiyo hakika Maulamaa wengi wanaitakidi kwamba ulimwengu unapanuka kwa mwendelezo. Anga la ulimwengu ulioundwa na mabilioni ya mikusanyiko uko katika hali ya upanuzi wa haraka, na utafiti wa anga umeashiria uwepo wa dalili zinazoonesha kwamba kuna hali ya kutengenezeka mkusanyiko mpya ndani ya anga.

Na ukweli huo Qur'ani tukufu inaukubali. Anasema (swt):

وَالسَّماءَ بَنَينٰها بِأَييْدٍ وَإِنّا لَموسِعونَ

[129] *Qafilatul Zait*, uk. 16 tolea la Muharram 1416 Hijiria.

**"Na mbingu tumezifanya kwa nguvu na uwezo na hakika Sisi bila ya shaka ndio wenye kutanua." (Surat Adh-Dhariyat; 51:47).**

Na katika aya nyingine anasema (swt):

يَسأَلُهُ مَن فِي السَّمٰوٰتِ وَالأَرضِ كُلَّ يَومٍ هُوَ فِى شَأنٍ

**"Vinamuomba Yeye viliyyo katika mbingu na ardhi. Kila siku Yeye yumo katika jambo." (Surat Ar-Rahman; 55:29).**

Hivyo hali ya kutanuka ulimwengu ni yenye kuendelea kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ni kila siku. Na makusudio ya siku hapa ni wakati, yaani kila wakati na kila sekunde, na sio wakati maalumu kuanzia alfajiri hadi usiku. Katika kila sekunde kuna jambo kubwa na tukio muhimu linatokea katika ulimwengu.

Al-Alusi amesema: Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu bado angalia anaumba watu na kuwauwa wengine na kuleta hali na kuondoa hali, kulingana na yanavyotaka matakwa ya Mwenyezi Mungu yaliyojengewa katika umakini wa hali ya juu. Na al-Bukhari amepokea katika *Tarikh* yake, Ibnu Maajah, Ibnu Hiban na jamaa kutoka kwa Abu Dardai kutoka kwa Nabii ﷺ kwamba amesema katika aya hii: Kwa uwezo wake anasamehe dhambi na kumnusuru mwenye matatizo, anawanyanyua watu na anawateremsha wengine."[130]

Na imekuja katika hotuba ya Imamu Ali عليه السلام: "Namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye hafi wala hayamaliziki maajabu Yake kwa sababu kila siku yuko katika jambo kati ya matukio mazuri

[130] Al-Alusiy al-Baghdadiy: Sayyid Mahamuud katika *Ruhul-Maaniy* katika *Tafsiril-Qur'ani*, Juz. 27, uk. 110 chapa ya nne 1985 Daru Ihiyai turathi al-Arabiyi – Beirut.

ambayo bado hayajawa."[131]

Na miili yetu kama sehemu ya ulimwengu huu inaishi katika hali ya mabadiliko na kujijadidi daima. Mada ya kimiminika ambayo inapatikana katika chembechembe za damu zetu inaharibika kisha inajitengeneza upya. Na mfano wake ni mfano wa chembechembe zote za mwili, zinakufa na kuja mahala pake chambechembe mpya. Na utafiti wa kielimu unasema kwamba damu ya mwanadamu inajitengeneza upya ndani ya muda wa miaka minne, na chembechembe zote za mwili zinabadilika ndani ya miaka michache, hivyo mwili ni kama mto unaotiririka. Kila dakika katika mwili wa mwanadamu zinakufa chembechembe bilioni tatu takriban, na katika muda uleule zinazaliwa chem.-bechembe kwa idadi mpya mfano wa hizo kwa kugawanyika chembechembe, badala ya chembechembe zilizokufa. Na chembechembe za ngozi iliyokufa zinadondoka, wakati ambapo zinapita chembechembe zilizokufa katika chembechembe za viungo vya ndani kwenda nje ya mwili pamoja na uchafu. Na unatofautiana muda wa chembechembe. Chembechembe za damu nyeupe kwa mfano zinaishi kwa muda wa siku 13 wakati ambapo chembechembe za damu nyekundu zinaishi kwa muda wa siku 120. Na chembechembe za ini zinaishi miezi 18 takriban. Ama chembechembe za mishipa zinaishi miaka 100 takriban.[132]

Hivyo kuna harakati ya kujadidi ndani ya asili ya vitu na wanafalsafa walikuwa wanaitakidi kwamba harakati haiwezekani katika kitu chenye kiwiliwili kabisa, kwa sababu kila harakati inapasa kuwa na kiwiliwili chenye kutembea kilichothabiti, ila viungo vyake vinaweza kubadilika, vinginevyo hakika harakati hazitakuwa na maana inayofahamika. Lakini wanafalsafa waliokuja baadae walipinga nadharia hii na wakaamini harakati ya asili, na wakasema: Hakika msingi wa harakati ni dhati (asili)

[131] Al-Huwaiziy: *Tafsir Nuru Thaqalain*, Juz. ,5 uk. 193 chapa ya nne 1412 hijiria Muasasatu Ismailiyaan Qum.

[132] *Al-Musuatu al-Arabiya*, Juz. 10, uk. 147 chapa ya pili 1999 Riyaadh

ambayo inadhihiri athari yake katika viungo. Na wa kwanza aliyebainisha nadharia hii kwa ufafanuzi wa dalili ni al-Maula Swadir Diyn Shiraziy ambapo alisema: Hakika kila chembe za viumbe na ulimwengu wa kimaada ni zenye harakati, au kwa maneno mengine, hakika mada ya viwiliwili vya uwepo ni kama maji yanayotiririka ambayo hali yake ni yenye kubadilika, kila sekunde yanakuwa na hali mpya inayotofautina na uwepo wa awali na kwa kuwa mabadiliko haya yanaungana na baadhi yake hakika yanahesabiwa kuwa ni kitu kimoja.[133]

**Malengo ya kutafakari na kudadisi katika ulimwengu:**

Wakati Mwenyezi Mungu anapotuamuru kutafakari na kudadisi katika ulimwengu, na kutukumbusha hali ya kujadidi na uvumbuzi wa daima katika viumbe, ni kwa malengo yafuatayo:

**Kwanza:** Kufahamu ukubwa wa Muumba Muweza (swt).
**Pili:** Kuelewa mazingira ya kanuni zinazotawala katika uwepo ili tusipatwe na kukata tamaa.
**Tatu:** Kufahamu dauru ya mabadiliko na kujadidisha katika harakati.

Tunapata kutokana na hayo somo na mazingatio katika muamala wetu pamoja na hali za kijamii na nyenendo zetu za kimaisha.

**5. Ushindani wa mabadiliko:**

Maisha ni medani ya ushindani, wanasongambele humo viongozi wa mabadiliko na kujadidisha. Jamii yenye kujadidisha kwa wingi na yenye kasi ya mabadiliko inapata maendeleo na inazatiti nguvu yake na utawala wake, wakati ambapo jamii iliyosimama, chache ya harakati inaharibika hali yake na inapatwa na uzee, na inarudi nyuma na inanyenyekea katika utawala wa wenye

[133] Shiraziy: Sheikh Naswir Makarim katika al-Amthali juzuu 17 uk: 347 chapa ya kwanza 1992 Muasasatu al-Biithah Beirut.

kuendelea.

Na hususan katika zama hizi, ambapo yametoweka masafa na imeondoka mipaka na vikwazo, na hakuna tena nafasi ya kusimama na kudumaa. Ama uwe ni mzalishaji wa harakati ya mabadiliko na kujadidisha au uwe tayari kuipokea na kuielewa kwa daraja la pili, ili usigongane na uthabiti wako na misingi yako, vinginevyo utakumbwa na harakati zake zenye kusomba, bila ya hiari yako, na kuwa ni mfuataji mwenye kutumia wanayoyazalisha wengine miongoni mwa bidhaa za fikra, ratiba na tabia.

**6. Kukabiliana na changamoto:**

Katika mwenendo wa maisha jamii inakabiliwa na matatizo na changamoto, na inaweza kuhitajia kukabiliana nayo kwa aina ya kujadidisha katika fikra, na kubadilisha katika ratiba, na kuboresha katika njia na mbinu. Jamii ikidumaa katika harakati ya mabadiliko na ikashikamana na iliyoyazoea na desturi, basi changamoto zitaishinda, na matatizo na shida zitakwamisha harakati zake.

Na tunaona namna gani changamoto za mazingira na matatizo ya maisha ndio ambayo yanamsukuma mwanadamu kugundua na kuvumbua. Kuvumbua mbinu na nyenzo katika nyanja mbalimbali, na kwa hiyo amevuka changamoto hizo na matatizo kwa kiasi kikubwa, na hali ni hiyo hiyo katika kiwango cha kijamii. Ni lazima kuvumbua na kubadilisha, ndipo jamii inaweza kupambana na hali mbaya iliyopo, na kushinda ushawishi wa hali na mazingira.

**7. Uislamu: Ni Daawa ya Kujadidisha:**

Ujumbe wa mbinguni umekabiliwa na hali ya kudumaa katika jamii zake, na zikashikamana humo na waliyoyarithi kutoka kwa

watangulizi wao na kuyazoea katika maisha yao. Hivyo ujumbe huo ukajikita katika kulingania jamii kwenye kujikomboa kutokana na utumwa uliopita na minyororo ya sasa na kushikamana na haki na usahihi. Lakini maneno ya wasioendelea mbele ya Manabii wao yalikuwa: "Hakika sisi tuliwakuta baba zetu juu ya desturi na tunaongoza nyayo zao." (Sura Zukhurufu: 22).

Waliyoyafuata baba (zetu) na iliyoyazoea jamii, ni wajibu yabakie na yaendelee, na fikra yoyote mpya wanaikabili kwa tahadhari na upinzani chini ya nembo ya: "Hatujasikia haya kwa baba zetu waliotangulia." (Suratul-Muuminina: 24). Na Uislamu kama hitimisho la ujumbe wa mbinguni unalingania binadamu kujinasua na pingu ambazo zinakwaza na kuzuia harakati zake kuelekea kwenye haki na maendeleo. Anasema (swt) kuhusu Nabii Wake Muhammad ﷺ:

"..... وَيَضَعُ عَنهُم إِصرَهُم وَالأَغلٰلَ الَّتى كانَت عَلَيهِم ....."

**"Na kuwaondolea mizigo yao na minyororo ambayo iliyokuwa juu yao." (Surat Al-A'araf; 7:157).**

Na inamhamasisha mwanadamu kufungua rai na fikra mbalimbali, ili avumbue zilizo bora kati ya fikra hizo,

"الَّذينَ يَستَمِعونَ القَولَ فَيَتَّبِعونَ أَحسَنَهُ ....."

**"Ambao husikiliza maneno, wakafuata mazuri zaidi…" (Surat Az-Zumar; 39:18).**

Na inalaumu akili yenye kudumaa na hali ya kudumaa, kwa sababu inampelekea mwanadamu kurudi nyuma katika msafara wa maisha na kumuweka katika orodha ya wafu. Imepokewa katika riwaya kutoka kwa Imamu Ja'far Swadiq عليه السلام: "Mwenye kulingana siku zake basi ana hasara, na ambaye siku yake ni shari

zaidi kuliko jana yake basi ana mtihani. Na ambaye haoni upungufu katika nafsi yake utadumu upungufu wake, na mwenye kudumu upungufu wake basi mauti ni bora kwake."[134] Na kwa madhumuni hayo hayo kuna riwaya kutoka kwa Imamu Musa al-Kadhim عليه السلام[135] na nyingine kutoka kwa Imamu Ali عليه السلام.[136]

Hivyo ndio vyanzo muhimu vya kuanzia harakati ya mabadiliko na kujadidisha katika maisha ya mwanadamu Mwislamu. Na kujadidisha kuna manhaji yake, na vidhibiti vyake, na nyanja zake, na zana zake ili kuwe katika maslahi ya mwanadamu na kwenda sambamba pamoja na misingi na maadili.

## ROHO YA KUJADIDISHA

Kwa nini ongezeko la hali ya kujadidisha na mabadiliko inakwenda haraka katika baadhi ya jamii, wakati ambapo inadorora na ni ya taratibu au inakosekana katika jamii nyingine? Baadhi wanaweza kusema: Hakika sababu katika hilo ni kupatikana uwezo hapa na kukosekana au kupungua kule. Jamii ambayo inamiliki uwezo na utajiri inaweza kupatikana humo hali ya maendeleo, ama jamii fakiri hali yake ni kuishi kwa kusimama na kudumaa.

Na wengine wanaona kwamba mas'ala yana uhusiano na mizizi ya jamii na historia yake/Ikiwa inatokana na historia yenye maendeleo na historia kongwe, hakika hilo litaisukuma katika mabadiliko na maendeleo, ama ikiwa ni jamii mpya au mwanzo wake ulikuwa ni uzembe hakika itakuwa na mwendelezo wa historia yake iliyotangulia. Na kundi la tatu linaweza kusema kuathirika hali ya jamii kwa uwezo wa harakati yake, ambapo uhuru wa jamii na uhuru wake au kuangukia chini ya utawala wa

[134] Al-Majilisiy: Muhammad Baqir katika *Biharul-Anuwar*, Juz. 75, uk. 277
[135] Rejea iliyotangulia uk. 327
[136] Rejea iliyotangulia, Juz. 74 uk. 377

adui au nguvu pinzani kunadumaza matakwa yake na kuzuia maendeleo yake.

Rai hizi na mfano wake ingawa zina kiasi fulani cha ukweli, na zina akisi sehemu ya picha, lakini hazifichui kwetu siri ya tofauti na asili ya tatizo. Historia ya maendeleo na umma za leo zinatusimulia kuhusu jamii zenye utajiri mchache, zilizopata miujiza ya maendeleo kama vile Japan. Na jamii changa zimekuwa kileleni kama vile Wamarekani, na jamii iliyozingirwa na kushindwa, imeweza kuvuka hali yake na kujenga nguvu yake upya kama vile Ujerumani na Japan baada ya vita kuu ya pili ya dunia. Wakati ambapo umma zingine zinamiliki utajiri na ukongwe wa kihistoria, na mazingira ya nje yanayofaa lakini hakika zinaishi katika uduni, kutokuendelea na kudumaa.

Anasema Pawel Kenedy katika kitabu chake *al-Tahadhir Liliqarni al-Wahid wal-ishirini*: Hakika Korea na Ghana zilikuwa zinaishi katika kiwango cha uchumi kinachokaribiana mwaka 1960, na pato la mtu katika nchi mbili hizi ni kwa kiwango cha dola 230 kwa mwaka, na baada ya miaka 30 (1990) liliongezeka pato la Mkorea mara kumi na mbili na kuwa dola 2760, wakati ambapo limebakia pato la Mghana katika hali yake dola 230!!

Kama ambavyo Japani na Misri walianza harakati zao mpya mwaka mmoja, na Japani ilikuwa inaishi katika wakati mgumu na mbaya baada ya kushindwa kwake katika vita kuu ya pili ya dunia na kupigwa kwake na kombora la nyuklia, lakini ni tofauti ilioje hivi leo baina ya maendeleo ya Japani na Misri?

Mwamko na kujadidisha ni roho na ni hali ya ndani, kabla ya kuwa hali na uwezo wa nje. Ikienea roho hii katika umma, inaleta humo harakati na uchangamfu, na inatoka kutafuta uwezo, na kutengeneza historia, na kukabiliana na changamoto. Na umma ukikosa roho hii, uhai wake unageuka na kuwa mauti, na unashambuliwa na maadui kutoka kila sehemu na kila upande.

Na kwa hiyo Qur'ani tukufu inatia mkazo juu ya umuhimu wa kubadilisha nafsi na inazingatia ni sharti pekee la kubadilisha hali ya nje. Mabadiliko yanaanza ndani ya nafsi ya mwanadamu na umma; anasema (swt);

"..... إِنَّ اللَّهَ لا يُغَيِّرُ ما بِقَومٍ حَتّىٰ يُغَيِّروا ما بِأَنفُسِهِم ....."

**"Hakika Mwenyezi Mungu habadilishi yaliyopo kwa watu mpaka wabadilishe yaliyo katika nafsi zao." (Surat Ar-Ra'd; 13:11).**

Na vyovyote jamii itakavyomiliki vipaji na uwezo, kupatikana uwezo na utajiri hakika bila ya roho ya mwamko na kujadididsha nafsi yake haitopata kitu, bali utapotea uwezo wake bure. Na utajiri wake utapotea bure, na kuishi katika hali ya kudumaa na inakuwa karibu na maisha ya wanyama, kama anavyosema (swt):

"..... لَهُم قُلوبٌ لا يَفقَهونَ بِها وَلَهُم أَعيُنٌ لا يُبصِرونَ بِها وَلَهُم ءاذانٌ لا يَسمَعونَ بِها أُولٰئِكَ كَالأَنعٰمِ بَل هُم أَضَلُّ أُولٰئِكَ هُمُ الغٰفِلونَ "

**".....Wana nyoyo lakini hawafamu kwazo, wana macho, lakini hawaoni kwayo, na wana masikio, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanayama bali wao ni wapotea zaidi; hao ndio walioghafilika." (Surat Al-A'araf; 7:179).**

Hakika wao ni wenye kughafilika kwa ambayo amewapa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika neema, na iliyo muhimu zaidi ni neema ya akili na kufikiri "wana nyoyo lakini hawafamu kwazo" na hata viungo vyao na hisia zao hawanufaiki nazo faida inayotakikana "na wana macho lakini hawaoni kwayo, na wana masikio lakini hawasikii kwayo," na hivyo hayatabadilika maisha yao, bali yanakuwa kama ya mnyama aliyesimama amedumaa kwa kuondolewa kwao katika uongofu wa Mwenyezi Mungu

"hao ni kama wanyama." Na ikiwa wanyama wanasamehewa kwa sababu wana matamanio bila kuwa na akili, nini udhuru wa mwanadamu? Hivyo "bali wao wamepotea zaidi" na wana hali mbaya zaidi kuliko wanyama.

Na katika aya nyingine anatia mkazo Mwenyezi Mungu (swt) juu ya umuhimu wa undani wa mwanadamu, na ambayo yanauzunguka undani wa nafsi yake kwa kauli Yake (swt):

وَلَو عَلِمَ اللَّهُ فيهِم خَيرًا لَأَسمَعَهُم وَلَو أَسمَعَهُم لَتَوَلَّوا وَهُم مُعرِضونَ

**"Na kama Mwenyezi Mungu angelijua wema wowote kwao, angeliwasikilizisha; na kama angeliwasikilizisha, wangeligeuka hali wakipuuza." (Surat Al-Anfal; 8:23).**

Ikiwa nafsi hazizungukwi na kheri wala hazibebi raghaba wala matakwa ya maendeleo na mabadiliko, basi hazitanufaika na jaribio lolote au fursa ya nje.

**Alama na sifa za uvumbuzi:**

Hakika roho ya kujadidisha na mabadiliko, inamaanisha kumiliki sifa na alama. Inajaza maisha ya mwanadamu uchangamfu na kuisukuma kwenye uvumbuzi na mafanikio, na kumfanya kuvuka vikwazo na vizuizi na kutafiti alama hizo muhimu.

1. **Uelewa na matarajio:**

Hali ambayo anaishi mwanadamu ikiwa ni mbaya isiyo na maendeleo, hakika haileti natija thabiti wala uwezo unaotakiwa, bali ni matokeo ya sababu na visababishi mukabala wa mabadiliko na mageuzi. Na katika mwanzo wake kuchuma nafsi yake, kwani anabeba kwa daraja la msingi jukumu la hali ambayo anaishi nayo. Anasema (swt):

**"وَما أَصٰبَكُم مِن مُصيبَةٍ فَبِما كَسَبَت أَيديكُم ....."**

**"Na misiba inayowasibu ni kwa sababu ya yaliyotendwa na mikono yenu." (Surat Ash-Shura; 42:30).**

Na kwa hiyo fursa inayotolewa kwa mwanadamu ili aondokane na hali hiyo mbaya, anapokataa kujisalimisha kwayo na kutaka kuivuka hatofanikiwa. Na historia imejaa mabadiliko ya kijamii. Ni jamii ngapi dhaifu zimekuwa na nguvu, na ni jamii ngapi zimetawala kisha zikaporomoka, na matakwa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yako pamoja na kila jamii inayokwenda mbio ili kuamka

**وَنُريدُ أَن نَمُنَّ عَلَى الَّذينَ استُضعِفوا فِي الأَرضِ وَنَجعَلَهُم أَئِمَّةً وَنَجعَلَهُمُ الوٰرِثينَ**

**"Na tunataka kuwafadhili waliodhoofishwa katika ardhi na kuwafanya wawe ni viongozi na kuwafanya ni warithi." (Surat Al-Qasas; 28:5).**

Na ikiwa hali ya maisha ni nzuri sana, hakika ni juu ya mwanadamu asizingatie hali yake kuwa ndio mwisho na kikomo, wala asipatwe na ghururi na majivuno, na kusimama kuacha maendeleo. Na ikiwa hataendelea hakika anarudi nyuma, anasema Imamu Ali (a.s): "Asiyejua anahadaika na nafsi yake, na siku yake inakuwa ni mbaya zaidi kuliko jana yake." [137] Mwenye kuhadaika na hali yake unapungua ujanja wake,[138] na majivuno yanazuia maendeleo."[139] Hakika kutarajia yaliyo bora zaidi, na kutarajia yaliyo mazuri zaidi, ndio kichocheo cha kwanza

[137] Al-Amadiy: Tamiymiy: Abdul-Wahdi katika *Ghurar al-Hikami wa durarил-Kalami*

[138] Rejea iliyotangulia

[139] Rejea iliyotangulia

ambacho inachomoza kwacho harakati za kujadidisha na kubadilisha, wakati ambapo uzembe na kuridhia hali ya kujisalimisha kwake, au ghururi na majivuno kwa aliyoyapata, yanamfanya mwanadamu anabakia katika sehemu yake, wala hahifadhi juu yake, kisha anarudi nyuma.

Hakika taasisi zenye kufaulu ni ambazo zinasimamia utekelezaji wake kwa mpangilio, na zinaweka mkakati kwa ajili ya kunyanyua kiwango na kuongeza juhudi na uzalishaji. Na mafunzo ya Kiislamu yanatuelekeza katika uelewa na matumaini ya daima, katika nyanja mbalimbali. Katika dua ya *Makarimul-Akhilaq* ya Imamu Zainul-Abidiin Ali bin Husein عليه السلام kuna ukumbusho kwa mwanadamu kutafakari katika maendeleo, katika upande wa imani na maarifa na kazi, na yanakuja haya maelekezo katika muundo wa dua na maombi, anayoomba mwanadamu kutoka kwa Mola Wake, ili ajizatiti ndani ya nafsi yake. Anabadilika kwenye ratiba katika maisha yake, dua inasema: "Na ifikishe imani yangu katika ukamilifu wa imani, na jaalia yakini yangu iwe ni yakini bora zaidi, na ifikishe nia yangu kwenye nia nzuri zaidi, na amali yangu kwenye amali nzuri zaidi." Na ibara za dua zinamaanisha kwamba kiwango chochote cha imani au yakini au nia nzuri na amali njema, hakimaanishi mwisho au kikomo. Unabakia upeo wa ukamilifu na maendeleo uko wazi mbele ya mwanadamu, ili kufikia yaliyo mazuri zaidi na yaliyo kamilifu zaidi na yaliyo bora zaidi.

**2. Kujiamini:**

Mwanadamu anapoona mafanikio ya wengine na uvumbuzi wao, ni wajibu hilo limsukume kujiamini na kuelekea katika kuibua vipaji vyake na uwezo wake, kwani yeye ni mwanadamu mfano wao, anamiliki wanayoyamiliki miongoni mwa akili na matakwa kama walivyotumia akili zao. Na wametumia matakwa yao wakavumbua na wakafanikisha. Ni juu yake mfano wa hayo ili avumbue na azalishe. Hii ndio ratiba sahihi. Lakini baadhi ya

watu ni kinyume cha hayo. Wanashangaa kwa mafanikio ya wengine hadi wanakosa kujiamini, na kudumaza akili zao na vipaji vyao kiasi kwamba hawaoni kuwa nafsi zao zinaweza kuwa jirani na kufanana, ukiachilia mbali kuhusu kuwa juu na kuendelea. Na kwa haya zinasimama harakati na inashindikana kubadilisha na kujadidisha. Na mara nyingine kuvutiwa na waliotangulia, kama vile kizazi kilichotangulia, au shakhsiyati za kihistoria, kunaongeza kwake na hali ya kujitukuza na kujikuza, inakuwa ni uzio wa fikra baada yake na mpaka katika mafanikio haiwezekani kuipita na kuivuka. Na kutumia kusimama katika kiwango cha ufahamu wa waliotangulia, na njia ya maisha yao, au kutukuza shakhsiya iliyokuwa na utukufu, na dauru ya kihistoria yenye kusifika, hajasiri yeyote kuikosoa, au kukhalifu rai zake na nadharia zake.

Hakika asiyekuwa maasumu, vyovyote utakavyokuwa uwezo wake na kipaji chake, yeye ni binadamu ana kikomo cha muda na wakati wake na mazingira yake, na juhudi zake hazizuii ijitihadi baada yake, na rai yake inatarajiwa humo kukosea na kupatia. Hakika watangulizi wa umma wema inapasa kuwaheshimu na kunufaika kutokana na rai zao na uzoefu wao, lakini haipasi kusimama kwenye mpaka wa fahamu zao. Mwenyezi Mungu amekwishatupa akili kama alivyowapa wao, na ametusemesha kwa wahyi Wake kama alivyowasema wao. Huenda baadhi ya rai zao au mbinu za muamala wao zilikuwa ni kutokana na mazingira yao, kama ambavyo mabadiliko ya maisha na mrundikano wa uzoefu, unaweza kutufungulia upeo au unafichulia mambo ambayo hayakuwa yanapatikana kwao.

Na shakhsiya za uongozi katika nyanja za elimu na kazi, vyovyote kitakavyokuwa kiwango cha elimu yao au ukubwa wa elimu yao, hakika mmoja kati yao hamaanishi ni mwisho wa elimu, wala kikomo cha kazi, na “ni mangapi ameyaacha wa kwanza kwa mwengine” kama anavyosema mshairi wa Kiarabu.

Na anasema mshairi mwingine:

“Hakika mimi hata kama ni wa mwisho katika zama zake, nitaleta ambayo hawakuyaweza waliotangulia.” Na yenye ukweli zaidi ni kauli Yake (swt):

“.....وَفَوقَ كُلِّ ذى عِلمٍ عَليمٌ”

**“Na juu ya kila mwenye elimu yupo ajuaye zaidi.” (Surat Yusuf; 12:76).**

Na kwa mfano katika dauru ya kutukuza shakhsiya na kushangazwa nayo kwa kiasi cha kusimama na kudumaa, tunaashiria katika waliyoyataja maulamaa katika maelezo ya Sheikhe Tusiy Muhammad bin Hasan, Mwenyezi Mungu amrehemu (aliyezaliwa mwaka 384H na kufariki mwaka 460 H), hakika kwa utukufu wa nafasi yake ya kielimu katika nafsi za wanafunzi wake na walio baada yake, ilishapita kwa mashia miaka mingi vizazi vingi na haikuwa rahisi kwa yeyote miongoni mwao kukosoa nadharia za Sheikh Tusiy katika fatwa, na walikuwa wanahesabu maneno yake ni msingi uliosalimika, na wanatosheka nao, na wanahesabu kukosoa utunzi wake na fatwa yake ni kujasiri mbele ya Sheikh na kumdharau. Na hali iliendelea hivyo hadi zama ya Sheikh Idrisa-Muhammad bin Ahmad bin Idrisa al-Hiliy aliyefariki mwaka 598 Hijiria – walikuwa wanamwita al-Muqalidah, naye ni wa mwanzo kukhalifu baadhi ya fatwa zake na kufungua mlango wa kupinga nadharia zake.”[140] Na kama si ushujaa wa Sheikh Ibnu Idrisi na kujiamini na kupinga hali ya kushangaza na kunyenyekea mbele ya Sheikh Tusiy, ilikaribia kufungwa mlango wa ijitihadi katika mazingira ya kidini na kielimu.

[140] Al-Amin: Sayid Muhsin katika *A’ayan Shaiati*, Juz. 9, uk. 160 Daru Taaruf lilimatubuatai – Beirut 1986.

### 3. Mwanzo wa akili:

Kuna uhusiano madhubuti baina ya harakati za mabadiliko na harakati za kufikiri. Ikiwa watu watakandamiza akili zao kwa hofu au raghaba, kutawaliwa na hali ya ukandamizaji na ugaidi wa kifikra, kiasi kwamba inamzuia mwanadamu katika akili yake kutoka nje ya yaliyozoeleka, au jamii kukataa rai mpya za mabadiliko, wala hauzipi fursa ya kuzitoa, kuzijadili na uzoefu, wakati huo utasimama mwenendo wa kujadidisha, wala hayatapatikana mabadiliko au mageuzi.

Hakika uhuru wa kufikiri na rai ni haki ya msingi, ni kati ya haki muhimu sana za mwanadamu, kwayo anahisi mwanadamu utu wake na anaistawisha neema kubwa aliyopewa na Mwenyezi Mungu, na kupitia hiyo anaweza kuudhalilisha ulimwengu, na kujenga maisha ambapo Mwenyezi Mungu ametaka hayo kwake.

Na Uislamu umezingatia kulinda uhuru huu na kuudhamini, na kuelekeza utekelezaji wake ili asitumbukie chini ya athari za hawaa na matamanio. Aya nyingi katika Qur'ani tukufu zinamlingania mwanadamu kuhimiza kutumia akili yake na kutumia fikra yake katika nyanja na sekta mbalimbali, na katika mtiririko wa mazungumzo kuhusu ulimwengu na maisha katika mambo ya jamii na dini, na inajirudia kauli Yake (swt): "Je, hamtafakari" (Suratul-An'am: 50). Na ikiwa dini inaamrisha kutafakari na kutumia akili, haiwezekani kamwe kuridhia kupokonywa uhuru wa kutoa rai au ugaidi wa kifikra. Ndio, kuna vidhibiti vya kuhami uhuru huu, kutokana na upuuzi wa wapuuzi na ufisadi wa waharibifu.

### 4. Ushujaa na ujasiri:

Mwanadamu anaweza kufichua kosa la fikra kati ya fikra zake au nukta ya udhaifu katika baadhi ya nyenendo zake na vitendo vyake. Na anaweza kujua mfumo ulio bora zaidi, njia nzuri zaidi,

katika jambo kati ya mambo ya maisha yake, lakini ushujaa na ujasiri unamfanyia hiyana na yanamteka mazoea aliyoyazoea, au inamchukua huzuni kwa dhambi - kulingana na maneno ya Qur'ani tukufu – na hapa anapoteza kwa nafsi yake fursa ya mabadiliko na kujadidisha, na kuchagua kilicho sahihi zaidi na kilicho bora zaidi.

Ni sahihi kwamba mazoea yana mbinyo wake na nguvu zake katika maisha ya mwanadamu, kama anavyosema Imamu Ali عليه السلام: "Mazoea ni mtawala kwa kila mwanadamu."[141] "Na siasa ngumu zaidi ni kuhamisha mazoea."[142]

Lakini nguvu ya matakwa inaweza kukabiliana na mazoea, na mwanadamu mwelewa ni ambaye anatoa maamuzi yake kutoka katika mbinyo wa mazoea na nguvu zake. Anasema Imamu Ali عليه السلام: Zishindeni nafsi zenu kwa kuacha mazoea na pigeni vita matamanio yenu mtayamiliki"[143] "Zidhalilisheni nafsi zenu kwa kuacha mazoea na ziongozeni kwenye utii ulio bora zaidi."[144]

Na katika upande wa kijamii hakika baadhi ya jamii zinajipamba kwa upole unaotosha na zinamiliki ushujaa na ujasiri wa kubadilisha baadhi ya mazoea yao na ada zao, inapobainika kwao yaliyo bora kuliko hayo. Lakini jamii zingine zinajikanganya kwa ambayo zimeyazoea, hata kama hayo ni kwa hesabu ya misingi yake na maslahi yake. Na kwa mfano juu ya hilo baadhi ya mazoea yaliyoenea katika minasaba ya ndoa na maombolezo, ambayo yanatugharimu matumizi mengi na kusababisha taabu na uchovu, pamoja na kwamba watu wengi wanaona ni jukumu zito wanatamani kuondokana nalo, na kuna kukinahi nadharia kwa hiyo, lakini ushujaa na ujasiri haupatikani kwa kiasi kinachotakiwa kwa kubadilisha mazoea haya, na kuyabadilisha kwa

---

[141] Al-AmadiyTamiymiy: Abdul-Wahid katika *Ghurarul-Hikami wa Duaraul-Kalimi*
[142] Rejea iliyotangulia
[143] Rejea iliyotangulia
[144] Rejea iliyotangulia

kilicho bora na rahisi zaidi.

Na vilevile baadhi ya jamii za ghuba zimekwishazoea muundo maalumu wa maisha ya utumiaji siku za neema ya kiuchumi – kama wanavyosema – pamoja na kwamba hali ya kiuchumi imeshabadilika na imekuwa inabana maisha ya wengi kati ya watu, isipokuwa mazoea ya muda uliopita bado yangali yanatawala mahala pake kwa ugumu wa kuyabadilisha na kuyavuka kwa namna ya jumla.

Hizi ni alama nne: Uelewa, matarajio, kujiamini na kutumia akili, ushujaa na ujasiri ndio muonekano wa roho ya kujadidisha, ambapo zikienea katika maisha ya jamii zinaiongoza kwenye mabadiliko na mageuzi, na zikikosekana hakutofaa nembo na matamanio, wala mapendekezo na nadharia hazinufaishi.

**KANISA: HISTORIA YA DHULUMA KWA JINA LA DINI**

Hakika sheria za mbinguni na dini za Mwenyezi Mungu zimekuja ili kuleta uadilifu katika maisha ya mwanadamu na kupambana na dhulma na ujueri:

"لَقَد أَرسَلنا رُسُلَنا بِالبَيِّنٰتِ وَأَنزَلنا مَعَهُمُ الكِتٰبَ وَالميزانَ لِيَقومَ النّاسُ بِالقِسطِ ....."

**"Kwa hakika tuliwatuma Mitume Wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na mizani, ili watu wasimamie uadilifu…" (Surat Al-Hadid; 57:25)**

Na hakuna kitu kibaya baada ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu kuliko dhulma na kuzifanyia uadui haki za watu. Huo ndio msingi wa daawa za Manabii na Mitume. Lakini masikitiko ni kwamba baadhi ya wanaojidai kuwa ni wanadini, wanatumia fursa ya nafasi zao za uongozi na utashi wa

matamanio yao ya utawala na shahawati zao za kimaslahi kwa hesabu ya heshima ya watu, uhuru wao na haki zao. Wanafanya dhulma na uadui kwa jina la dini, chini ya bendera yake na nembo yake. Na hiyo ni kwa kisingizio cha ujeuri wao na kuwapotosha watu na kuwadhalilisha kwao.

Na ikiwa dhulma ni mbaya kwa kila aina zake na sura zake, hakika iliyo mbaya zaidi na uovu zaidi ni inayokuwa kwa jina la dini, kwani changamoto inayokanganya katika jambo la Mwenyezi Mungu, mosi ni kumzulia uwongo Mwenyezi Mungu:

**"قُل إِنَّ اللَّهَ لا يَأمُرُ بِالفَحشاءِ أَتَقولونَ عَلَى اللَّهِ ما لا تَعلَمونَ قُل أَمَرَ رَبّى بِالقِسطِ ....."**

> **".....Sema: Hakika Mwenyezi Mungu haamrishi machafu; je, mnasema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua? Sema Mola Wangu ameamrisha uadilifu….." (Surat Al-A'araf; 7:28–29).**

Na pili ni kufanya uovu kwa waja Wake. Na wanadamu wameteseka sana kwa aina hii ya dhulma, ambayo inafanywa kwa kivuli cha dini, jambo ambalo limezua kulipiza kisasi kwa baadhi ya jamii dhidi ya asili ya dini, na kutengeneza kundi la ulahidi linalotuhumu dini kwamba ni ulevi wa wananchi. Na hivi ndivyo inavyokuwa, kutumia dini ni kutayarisha mazingira ya ulahidi na ukafiri.

Na kanisa katika historia yake ndefu linawakilisha mfano wazi katika kutumia dini na kufanya dhulma kwa jina lake na chini ya nembo zake, kwani linanasibishwa kwa Nabii mtukufu wa Mwenyezi Mungu Isa bin Mariyam عليه السلام na kutawala sehemu kubwa na uwanja mpana wa kidini kwa binadamu. Kanisa hili kwa kuzingatia kwamba ni rejea ya dini ya Masihi, na taasisi ambayo inachunga mambo ya wafuasi wa dini, limetumia vibaya nafasi yake. Badala ya kueneza upendo na uadilifu na kutetea

waliodhulumiwa na wanyonge, na kupiga vita ujeuri na dhulma, kama ulivyo msingi wa ujumbe na dini za mbinguni, ikawa ni kinyume cha hivyo kabisa.

**Msamaha wa Papa:**

Kimeongezeka kiwango cha uelewa na maarifa kwa watu, na ukweli umeendelea kafahamika. Watu wa kanisa hawanyenyekei tena na kupotoshwa kama mwanzo, bali zimefululiza humo harakati za malalamiko na sauti zikapaa za ukosoaji na upinzani. Na katika upande mwingine hakika wananchi wengine na jamii zilijaa ukandamizaji, dhulma na ujeuri, na zilirejesha kujiamini, na kuanza kudai haki zake na kurejesha mazingatio ya historia yake. Yote hayo yalikuwa ni sababu iliyomsukuma Papa Paulo kukiri baadhi ya makosa na kuomba msamaha, na kuomba radhi na maghfira, kuhusu historia mbaya ya kanisa.

Kujitolea huku kwa kanisa kumekuja kwa ajili ya kujibu mbinyo wa ndani na wa nje, ambapo kuliundwa kamati ya makasisi wanane waliofanya kazi kwa muda wa mwaka kamili, kuandaa utafiti wa kurejea makosa yaliyopita katika kanisa na kutoa ripoti kwa Papa yenye kurasa 46, na kuamua baada yake kufanya sherehe maalumu Jumapili iliyopita 12/3/2000 ambayo iliitwa siku ya kusameheana, kutangaza ripoti na kutangaza kuomba msamaha na udhuru kutoka kwa Papa.

Ilifanyika hafla kubwa ya kidini (ibada) katika kanisa takatifu la Petro Vatikan, kwa kuhudhuria idadi kubwa ya viongozi wa Italia na wanadiplomasia na watu wengi zaidi ya elfu ishirini takriban ndani ya kanisa na katika uwanja rasmi wa Vatikani. Ripoti inakiri kwamba pamoja na uovu na ubaya uliotokea katika historia ya kanisa: “Haikuja katika historia ya kanisa wito wowote wa kutubia na kupinga makosa na kuomba msamaha, na kwamba jaribio bora katika nyanja hii, lilikuwa linaishia kuwasifu makasisi ambao kulifanywa katika zama zao baadhi ya

makosa, kwamba wao walikuwa nje ya ibada na mafunzo ya kanisa, na wakafungamanisha makosa haya kwa watu wake bila ya kanisa lenyewe."[145]

**Ubabe wa ugomvi wa kimadhehebu:**

Ripoti ilizungumzia juu ya ubabe wa ugomvi wa kimadhehebu, na ukali wa mfarakano ambao ulitokea baina ya wafuasi wa kanisa Katholiki: "Kulitokea ikhitilafu kubwa baina ya wakristo na hususan katika karne inayomalizika. Katika mwanzo wa karne iliyopita (1054) ilijitokeza ikhitilafu kali baina ya kanisa la Mashariki na kanisa la Magharibi, na ikaendelea kwa muda mrefu na likaparaganyika kwa uadui. Na wakatuhumiana, na kukakosekana kuaminiana. Na angalizo ni kwamba kati ya vikwazo ambavyo vinasimama dhidi ya umoja wa wakristo ni sababu za kiutamaduni na mambo ya kihistoria na kasumba ambazo zinasheheni ikhitilafu miongoni mwa wakristo.[146]

Hakika ni ishara ndogo tu katika ambayo walikabiliwa nayo wakristo kutoka kwa uongozi wa kanisa lao, ambapo kanisa liligawanyika lenyewe na madhehebu ya kikristo yakawa mengi: Wakatholiki, Othodox na Waprotestanti.

Na viongozi wa kanisa na madhehebu wanachochea wafuasi wao dhidi ya makanisa mengine, na wafuasi wa madhehebu mengine. Mfalme wa Kiitaliano alipoingia katika ukristo katika mwanzo wa karne ya nne na akajiunga na rai za Paulo, ambaye alikuwa myahudi mwenye kasumba dhidi ya unaswara, na mshirika katika kuwapiga vita, lakini yeye aligeuka ghafla kwenda kwenye ukristo kwa kudai kwamba yeye amekutana na Masihi. Na amekuwa mlinganiaji wa ukristo anayejulikana kwa jina la Mtume Paulo, mwasisi wa ukristo mpya, unaosimama katika kumfanya Masihi kuwa mungu na utatu, na akakandamiza rai

---

[145] *Bayaanati al-Fatikani*: tovoti ya Vatican katika intaneti
[146] Rejea iliyotangulia

pinzani ndani ya Wakristo.

Alipopinga Arius mwaka 336 kauli ya uungu wa Masihi, lilifanyika kongamano la kanisa la kwanza ambalo lilijulikana kwa jina la kongamano la Nikai mwaka 325, na kuamua kumtuhumu Arius na kuchoma kitabu chake, na kuharamisha kukinunua, na kuwavua wafuasi wake nyadhifa zao na kuwafukuza, na kuhukumiwa kunyongwa kila mwenye kuficha kitabu chake.

Na yalidhihiri madhehebu ya Protestant katika Ukristo, kwa kupinga rai iliyoenea katika kanisa la Kikatoliki. Na maana ya Protestant kwa kilatini ni: Mpinzani. Kanisa liliwakabili kwa ubabe na ukandamizaji, na mauji yakawa mengi, na yaliyo muhimu zaidi ni mauaji ya Paris 24/8/1572, ambapo wakatoliki waliwachapa fimbo wageni wao wa Kiprotestant ambao waliitwa Paris kuleta ukuruba baina ya mitazamo, kisha wakauliwa kwa hiana na wao wakiwa wamelala, na damu zao zikatiririka katika barabara za Paris. Na pongezi zikamiminika kwa Charles IX wa Ufaransa kutoka kwa Papa, wafalme wa katoliki na wakuu wao kwa kitendo hiki kiovu!! Na cha ajabu ni kwamba waprotestant walipopata nguvu walifanya uovu ule ule uliofanywa na wakatoliki, na hawakuwa ni wachache wa uovu katika muamala na maadui zao.

Na kanisa la katoliki lina wakristo wengi zaidi, nalo linabeba jukumu la msingi la kukandamiza madhehebu mengine yenye watu wachache, na kukandamzia rai pinzani katika kufasiri kwake dini.

**Ugaidi wa kifikra:**

Kanisa lilifuata katika zama za kati rai za Aristotle na Ptolemy myunani katika mazingira na anga. Na wakayaita Jiografia ya Kikristo, na wakafanya kazi ya kuilazimisha kwa watu kwa kuizingatia ni itikadi ya kidini, na kwamba kinachoikhalifu ni

ukafiri na uasi katika dini. Na zikaanzishwa mahakama za upekuzi mwaka 1183, kwa kuwauliza watu kuhusu rai zao katika mambo ya mazingira na ulimwengu, na kumwadhibu mwenye kukhalifu miongoni mwao. Na inakadiriwa idadi ya watu ambao waliaadhibiwa na mahakama hizi ni watu 300,000, kati yao 32,000 walichomwa moto wakiwa hai, miongoni mwao ni mtaalamu wa mazingira maarufu kwa jina la Giordano Bruno, ambaye alihukumiwa kuuliwa, na kwamba lisimwagike tone la damu yake juu ya ardhi, hivyo akachomwa akiwa hai mwaka 1600. Na vilevile alihukumiwa kuuliwa mtaalamu wa anga wa Kitaliano, Galileo Galilei mwaka 1642 kwa sababu alisema rai yake kuhusu kuzunguka kwa ardhi na kulizunguka kwake jua.

**Ukandamizaji na ukoloni:**

Ripoti ya kuomba msamaha iliashiria baadhi ya mateso ambayo yaliwapata wengi katika wananchi na jamii nyonge, miongoni mwa nguvu ya Ulaya na wamagharibi, ambayo ilikuwa inafanya uovu wake na utawala wake wa kikoloni chini ya mtazamo wa kanisa na uangalizi wake na kubariki kwake. Wahindi wekundu, nao ni wakazi wa asili wa Amerika, ambao walihamia kutoka Asia kabla ya zaidi ya miaka 20,000, kulingana na makadiro ya wataalamu, lakini wazungu weupe walipoigundua Amerika na utajiri wake walikuja kuikalia na wakaingia katika vita ya muda mrefu na kali na Wahindi wekundu, iliyomalizika mwaka 1900 kwa kuwaangamiza na kupora ardhi zao. Na kuwafukuza na kuwakandamiza waliobakia miongoni mwao. Idadi ya Wahindi wekundi Amerika ilikuwa ni zaidi ya watu milioni moja, na katika mwisho wa vita vya maangamizi idadi yao ilipungua hadi 237,000!!

Na Waafrika walikuwa wanashambuliwa na meli za kijeshi na za kibiashara za wazungu na kuwakandamiza kama wanyama bila ya huruma au utu. Mtoto anaporwa katika mapaja ya mama yake

na ndugu anaporwa mbele ya ndugu zake, na kuchukuliwa kama mateka hadi Ulaya. Wanauzwa na wananunuliwa, na wanawatumikisha katika kuwahudumia wazungu weupe kwa unyonge na udhalili. Na kwa kuingia karne ya 19 wazungu walikuwa wameshapeleka Amerika watumwa milioni kumi wa Kiafrika!!

Kama ambavyo kanisa lilifurahia ukandamizaji wa Wayahudi na kuteketezwa kwao na Wanazi, na kwa kuitikia mbinyo wa Kiyahudi kimataifa, mazungumzo kuhusu kadhia yao yamekuja wazi kuliko kadhia nyingine yoyote katika ripoti ya kuomba msamaha. Ama mateso ya wananchi wa Kiislamu kutokana na uovu wa wazungu katika vita vya msalaba, mateso yaliyobarikiwa na kanisa, hayakuja mazungumzo yake, pamoja na kwamba yalikuwa ni mateso mabaya na ya muda mrefu, ambapo wazungu walipanga mashambulizi manane makuu ya kijeshi. Na yakaendelea kwa zaidi ya miaka 200 kuanzia mwaka 1096 hadi 1270, kwa kuiteka Palestina na viunga vyake kati ya nchi za Kiislamu. Mfalme wa Italia Alexios I Komnenos, mwaka 1095 aliomba msaada kutoka kwa Papa Urban wa pili, Papa wa kanisa la katoliki, katika vita vyake dhidi ya Waturuki, na Papa akaafiki katika hilo. Papa alifanya mkutano wakati wa kipupwe wa viongozi wa kanisa huko Ufaransa. Alihimiza humo wazungu kusimamisha vita baina yao, na kuteka ardhi takatifu ya Palestina na akawaahidi malipo ya kiroho na kimaada mkabala wa vitendo vyao, na akachochea raghba katika kuipiga vita Ulaya Magharibi. Maelefu yakajiunga na jeshi la wavamizi.

Na yalitokea kutokana na ukoloni wa nchi za kimagharibi katika nchi nyingi za Kiislamu baada ya kuanguka ukhalifa wa Uthmaniya. Na kilichotokea katika hayo miongoni mwa ujeuri, hayakuwa ni yenye kufichikana kwa kanisa wala hayakuwa mbali na baraka zake. Na kuishi Wazayuni waporaji ndani ya nchi za Kiarabu na za Kiislamu, kuhami kwake na kuunga kwake mkono katika uwepo wake na uadui wake, sio kingine ila ni muonekano kati ya muonekano wa njama na chuki ya kima-

gharibi dhidi ya Uislamu na Waislamu.

**Somo na Mazingatio:**

Qur'ani tukufu imetufundisha kwamba mazungumzo kuhusu dhulma na ufisadi wa umma zingine, ni wajibu yawe ni chimbuko la kutafakari na mazingatio. Na kufaidika na mafunzo na uzoefu kutokana na mabadiliko ambayo yalikumba umma zingine, ili tujiepushe na yale ambayo walitumbukia humo miongoni mwa makosa. Na kwa hiyo Qur'ani imezungumzia juu ya Ahlul-Kitabu kwa kushiriki kwao pamoja na Waislamu katika kujiunga na ujumbe wa mbinguni, na kumwamini Nabii aliye-tumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Imekuja katika mazungumzo kuhusu Ahlul-kitabi kwa jina hili, katika zaidi ya aya 32 katika Qur'ani, kama ambavyo yamekuja mazungumzo kuhusu Wayahudi mara 18 takriban, na kuhusu Manaswara mara 15 takriban. Ili Qur'ani kuhadharisha Waislamu waliyoyafanya Wayahudi na Manaswara katika dini yao, ambapo waliipotosha na kuichezea na wakatumia anwani ya dini na nembo zake vibaya.

Na kiongozi wa kanisa anapokiri makosa yaliyopita kwa kifupi na kwa muhtasari, na kuomba msamaha na maghufira juu ya historia yenye giza, hakika hilo ni wajibu taasisi zetu zote na pande zake za kidini kuwa makini na kujihadhari kwa uelewa na kuwa macho, ili Uislamu usipakwe matope kutokana na vitendo vyake na harakati zake. Dhulma inapelekea kumghadhibisha Mola na kuwakasirisha watu, kwa namna yoyote itakavyotokea, na kwa upande itakaotokea. Na Uislamu ni dini ya uadilifu na haki, ni wajibu kurasa zake ziwe safi zenye kuangaza na kumeremeta.

## ASHURA: UELEWA NA UPEO

Aya nyingi za Qur'ani tukufu zinamkumbusha mwanadamu neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu juu yake, na zinazungumza

kuhusu aina za neema hizo mbalimbali, ambazo Mwenyezi Mungu amemneemesha mwanadamu.

"أَلَم تَرَوا أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُم ما فِى السَّمٰوٰتِ وَما فِى الأَرضِ وَأَسبَغَ عَلَيكُم نِعَمَهُ ظٰهِرَةً وَباطِنَةً ....."

**"Je, hamjaona kwamba Mwenyezi Mungu amevifanya viwatumikie vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini na akawakamilishia neema Zake zilizo dhahiri na siri?....." (Surat Luqman; 31:20)**

"وَءاتىٰكُم مِن كُلِّ ما سَأَلتُموهُ وَإِن تَعُدّوا نِعمَتَ اللَّهِ لا تُحصوها ..."

**"Na akawapa kila mlichomuomba. Na mkihesabu neema za Mwenyezi Mungu hamtuwezi kuzidhibiti….." (Surat Ibrahim; 14:34)**

Kama ambavyo aya nyingi zinatia mkazo kuzihudhurisha neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuziweka mbele ya macho na fikra, na katika sehemu nane imekuja kauli Yake (swt) **"Na kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu juu yenu."** Na katika sehemu tatu zingine imekuja kauli Yake (swt) **"Kumbukeni neema yangu ambayo nimewaneemesha juu yenu."** Kwa kuongezea na makumi bali mamia ya aya tukufu, ambazo zinaeleza neema za Muumba Mtukufu na utoaji Wake usio na mpaka. Hakika ukumbusho huu kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa neema Zake na upaji Wake unalenga mambo mawili:

**Kwanza**: Ili mwanadamu azingatie kutekeleza wajibu wa kumshukuru mneemeshaji, kwa kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kushikamana na amri Zake, na kujiepusha na makatazo Yake.

**Pili**: mwanadamu aangalie katika neema zinazomzunguka, na afikirie katika kuziendeleza na kunufaika nazo, kwani zimeumbwa kwa ajili yake, na zimedhalilishwa kwa ajili ya kutumikia maslahi yake na kutimiza mafanikio yake.

Na kwa kadri mwanadamu atakavyoelekea kwenye kheri za ulimwengu na utajiri wa maisha, na juhudi zake za kuzivumbua na kuziendeleza, anatengeneza kiwango cha maendeleo yake na kubadilisha maisha yake.

Neema za Mwenyezi Mungu ni nyingi na pana, zinawazunguka wanadamu wote, na zinamwenea kila mtu, lakini kuna anayeangalia baadhi ya neema na kunufaika nazo, na kuna anayeghafilika nazo na wala hazizingatii, kwa uzembe au kutojua. Anasema (swt):

وَكَأَيِّن مِن ءايَةٍ فِى السَّمٰوٰتِ وَالأَرضِ يَمُرّونَ عَلَيها وَهُم عَنها مُعرِضونَ

**"Na ni ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazipita na hali ya kuwa wanazipuuza." (Surat Al-Yusuf; 12:105).**

Na jamii zilizoendelea, siri ya maendeleo yake na mabadaliko yake ni utambuzi wake na uendelezaji wake katika uwezo na utajiri uliopo, wakati ambapo unapatikana uwezo uleule katika jamii zingine na unabaki bila ya kufanyiwa kazi na umedumaa.

**Utajiri wa kimaanawi**:

Harakati za mwanadamu na juhudi zake katika maisha haya, zinategemea kwa daraja la kwanza juu ya nguvu zake na uwezo wake wa kiroho na kimaanawi, utashi mkubwa na matakwa yenye nguvu, na msimamo wa kinafsi, na upeo mpana, na uhuru wa kifikra, na mwamko wa uwepo na dhamira, subira na uma-

dhubuti na vipaji. Na sifa zingine njema zote zinatengeneza chimbuko na nguvu ambayo inamuongezea mwanadamu nguvu ya kuendesha mambo ya maisha, na kukabiliana na changamoto zake.

Na pande na sababu ambazo zinakuza sifa hizi katika nafsi ya mwanadamu zinazingatiwa kuwa ni chanzo cha utajiri wa kimaanawi na nguvu ya kiroho. Kila inapokuwa hazina ya jamii katika vyanzo hivi, na sababu hizi ni kubwa zaidi, uwezo wake unakuwa ni bora zaidi, na kisha atakuwa na harakati zaidi na mafanikio na ufaulu.

Kwa hiyo, hakika maadili matukufu, na misingi ya haki, na manhaji salama ni kati ya neema kubwa ambazo zinatajirisha maisha ya mwanadamu na kumfurahisha. Na kama ambavyo Mwenyezi Mungu ananeemesha waja Wake kwa neema Zake za kimaada na anawakumbusha kwazo, vile vile anawaneemesha kwa neema za kimaanawi ambazo ndio bora zaidi kwao kupitia uongofu wake wa kiungu, na ujumbe wake wa mbinguni, na anawazindua kwazo na anawakumbusha kwazo. Anasema (swt):

لَقَد مَنَّ اللَّهُ عَلَى المُؤمِنينَ إِذ بَعَثَ فيهِم رَسولًا مِن أَنفُسِهِم يَتلوا عَلَيهِم ءايٰتِهِ وَيُزَكّيهِم وَيُعَلِّمُهُمُ الكِتٰبَ وَالحِكمَةَ وَإِن كانوا مِن قَبلُ لَفى ضَلٰلٍ مُبينٍ

**"Hakika Mwenyezi Mungu amewaneemesha waumini kwa kuwaletea Mtume miongoni mwao anayewasomea aya Zake na anayewatakasa na kuwafundisha Kitabu na hekima. Na hakika kabla ya hapo walikuwa katika upotofu wa dhahiri." (Surat Aali-Imran; 3:164).**

".....وَاذكُروا نِعمَتَ اللَّهِ عَلَيكُم وَما أَنزَلَ عَلَيكُم مِنَ الكِتٰبِ وَالحِكمَةِ ....."

**"…..Na kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu juu yenu, na Kitabu alichowateremshia na hekima,…" (Surat Al-Baqara; 2:231).**

"…..وَاذكُروا نِعمَتَ اللَّهِ عَلَيكُم إِذ كُنتُم أَعداءً فَأَلَّفَ بَينَ قُلوبِكُم فَأَصبَحتُم بِنِعمَتِهِ إِخوٰنًا ….."

**"Na kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu juu yenu mlipokuwa maadui, naye akaziunganisha nyoyo zenu; hivyo kwa neema Zake mkawa ndugu….." (Surat Aali-Imran; 3:103).**

Hakika uwepo wa uongofu wa kiungu, na manhaji sahihi katika maisha, na mafunzo na maelekezo ambayo yanatatua matatizo ya kinafsi na kijamii, na kulea mwanadamu na kustawisha uwezo wake na nguvu zake, na kuelekeza katika njia sahihi, hakika hilo linazingatiwa kuwa ni neema kubwa, hakika ni neema ya uongofu:

"….. الحَمدُ لِلَّهِ الَّذى هَدىٰنا لِهٰذا وَما كُنّا لِنَهتَدِىَ لَولا أَن هَدىٰنَا اللَّهُ ….."

**"Sifa njema zote zinamstahiki Mwenyezi Mungu ambaye ametuongoza kwenye haya; na hatukuwa ni wenye kuongoka kama asingetuongoza Mwenyezi Mungu." (Surat Al-A'araf; 7:43).**

Lakini kupatikana neema za kimaanawi ni kitu kimoja na kuzitambua na kuziendeleza na kunufaika nazo ni kitu kingine, sawa kabisa kama ilivyo hali katika neema za kimaada.

Ni jamii ngapi zinaishi katika hali mbaya na kutoendelea, na wanateseka na upotovu na maradhi yenye kuangamiza – ya kinafsi na kijamii – na zinatawaliwa na hali ya ujahili na mpasuko, na nyuma yao kuna ujumbe wa Mwenyezi Mungu, na

Vitabu Vyake vitukufu, na mafunzo yake ya kidini matukufu. Lakini vimehamwa, vimepuuzwa, havitumiki kama manhaji ya maisha au kama chanzo cha nuru na mwangaza?

Na katika mfano mkubwa Mwenyezi Mungu Mtukufu anafananisha jamii ya kiyahudi, ambayo Mwenyezi Mungu aliteremsha kwao Tawrati, na wakashikamana nayo kwa anwani na muundo tu, na wakaacha madhumuni yake na manhaji yake katika maisha yao, kwamba hakika wao ni kama punda ambaye anabeba vitabu muhimu vya elimu katika mgongo wake, lakini hakika hanufaiki navyo kwa chochote:

مَثَلُ الَّذينَ حُمِّلُوا التَّورىٰةَ ثُمَّ لَم يَحمِلوها كَمَثَلِ الحِمارِ يَحمِلُ أَسفارًا بِئسَ مَثَلُ القَومِ الَّذينَ كَذَّبوا بِـٔايٰتِ اللَّهِ وَاللَّهُ لا يَهدِى القَومَ الظّٰلِمينَ

**"Mfano wa waliobebeshwa Tawrati kisha wasiibebe, ni mfano wa punda anayebeba vitavu vikubwa. Mfano muovu mno wa watu waliokadhibisha Ishara za Mawenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu." (Surat Al-Jumu'a; 62:5)**

Na umma wa Kiislamu unamiliki ujumbe wa mwisho na ulio bora zaidi wa mbinguni na sharia kamilifu zaidi. Hakika ni Uislamu, kwa mfumo wake wenye kuenea nyanja zote za maisha na mafunzo yake na manhaji yake ya kiakhilaqi, ndio ambao unamuongoza mwanadamu katika yaliyosawa zaidi, na kumfungulia njia ya mafanikio na wema. Na Waislamu walipokuwa wanajua uwezo wa neema hii, na wanashikamamna nayo na wanatengeneza maisha yao katika mwangaza wake, walikuwa ni umma bora ulioletwa kwa watu.

Kinachosikitisha sana ni hali unayoishi nayo umma wa Kiislamu sasa hivi katika kutoendelea, kunakotokana na unyonge na

udhaifu katika uwezo wa kimaanawi, na uwezo wa kiroho, pamoja na kwamba unamiliki pato kubwa na hazina ya kimaanawi na kiroho. Hakika kila manhaji katika manhaji ya Kiislamu inamuwezesha kutengeneza chemchem ya kiroho tajiri inayoleta azma na nguvu, na kuleta harakati na uchangamfu, kwa sharti la kuitambua, na kushikamana nayo na kuitumia katika uhalisia wa maisha. Ama vitendo vya kijuu juu na utendaji wa kijuu juu kwa pamoja katika manhaji ya dini, hakika unadhoofisha utendaji wa manhaji hiyo na unadumaza kazi yake inayotakiwa.

**Msimu wa Muharam:**

Katika mwanzo wa kila mwaka wa Hijiria, Waislamu wanapokea kumbukumbu ya shahada ya Imamu al-Husein bin Ali, mjukuu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na manukato yake. Na jamii za Kishi’ah za Kiislamu zimekwishazoea kuadhimisha kumbukumbu hii, kwa kuitikia maelekezo ya maimamu wa Ahlul-Bayt عليهم السلام ambapo waliwaamuru Mashi’ah wao na wafuasi wao kuhuisha kumbukumbu hii na kuizingatia. Na limekuwa kumi la mwanzo katika mwezi wa Muharam katika kila mwaka ni msimu wa Husein, unajaa ratiba nyingi na harakati za kijamii, ambazo wanashiriki humo wanajamii wanaume na wanawake, wadogo kwa wakubwa, na kuupa msimu huu hali ya kipekee na hali ya upambanuzi katika hali jamii ya Kishi’ah katika sehemu mbalimbali ulimwenguni.

Hakika kuadhimisha kumbukumbu ya Ashura kunatokana na msukumo wa kidini wa dhati kwa jamhuri ya Mashia, kwa kuwapenda Ahlul-Bayt عليهم السلام na kuimarisha mapenzi maalumu katika kushikamana nao, na zinatolewa juhudi kubwa katika ratiba hii ya kuadhimisha, na uwezo mkubwa, ndani ya shughuli za kijamii za kiwananchi, humo yanashiriki makundi yote na tabaka zote.

Mazingira ya Ashura na maadhimisho yake kuleta fursa kubwa inawezekana kuzistawisha na kuzinufaisha jamii hizi, na kuima-

risha hali ya kidini, na kutatua mengi ya matatizo ya kijamii. Hiyo ni kwa sababu hakika nafsi zinakuwa zimeandaliwa, na harakati za watu ni kubwa, na ambayo wanayasikia katika sira ya Imamu al-Husein عليه السلام yanawafanya wewe na utayari zaidi katika kuitikia, kujitolea na kutoa. Lakini baadhi ya watu wanafanya ratiba hizi kama ibada ya kuiga na nembo za kurithi zilizozoeleka bila ya kuzingatia kuziendeleza na kuzitumia kwa ajili ya kuhudumia maslahi ya jumla katika jamii na nchi.

Kwani ni utajiri mkubwa na mwingi, na kuna uwezekano wa kutoa mengi katika kheri na utoaji katika jamii, wapi utapata mfano wa mkusanyiko huu ambao unakuja wenyewe otomatiki bila ya kutangaza wala vivutio vya kimaada, na kwa muda wa siku kumi asubuhi na jioni? Wapi utakutana na harakati na uitikiaji wa kihisia mkubwa? Na lini utaona mfano wa utoaji wa ukarimu katika mali kutoka kwa mafakiri kabla ya matajiri? Yote hayo yanapatikana katika msimu wa muharam katika jamii za Kiislamu za Kishi'ah katika kuadhimisha kumbukumbu ya al-Imamu al-Husein عليه السلام. Namna gani tunanufaika na utajiri huu? Na namna gani tunatumia ambayo yanapatikana katika fursa hii nzuri na kubwa?

**1. Kuimarisha Uchamungu:**

Watu hawa ambao wanakusanyika kwa jina la al-Imamu al-Husein, na wanatumia wakati na juhudi katika kuhuisha kumbukumbu yake, na wanawasikiliza makhatibu na waelekezaji katika majilisi za maombolezo, hakika wanatangaza ufuasi wake wa kidini, na mshikamano wake wa kimoyo na kihisia kwa Maimamu wa dini na uongozi wake, na uitikiaji wake pamoja na maadhimisho na mambo ya kidini. Na hii inatubebesha majukumu na kutuandalia fursa ya thamani kwa ajili ya kuelimisha hawa watu mambo ya dini yao, na kuimarisha hali ya uchamungu katika nafsi, na kutengeneza nyenendo, tabia na misimamo katika uongofu wa dini.

Hakika ratiba ya Ashura inatoa fursa bora ya kuelimisha na kuelekeza, na watu wana haja sana na maarifa na mafuhumu ya dini ya kweli, na kuwaondolea vumbi la uongo, na mrundikano wa ufahamu wa kijuu juu na mwepesi. Pamoja na mwanadamu kuzama katika zama hizi katika mazingatio ya kimaada yenye kusomba, na kukabiliwa kwake daima na vyombo vya matangazo ambavyo vinahamasisha humo matamanio na hawaa, ili kumfanya awe ni mwanadamu wa kimaada wa kimatamanio, anatafuta ladha na ana abudu maslahi, ni kiasi gani huyu mwanadamu anahitajia mazingira ya kiroho ya uhamasishaji, yanayomkumbusha maadili na kumfungamanisha na misingi, na mwelekeo wake katika vigezo vyema miongoni mwa Manabii, Maimamu na Mawalii.

**2. Ustawishaji wa kijamii:**

Kupitia ratiba ya Ashura watu wanakutana baadhi na baadhi yao, jambo ambalo linaimarisha umoja wao wa kijamii, na kuzatiti kwao hisia ya wingi. Na katika jamii kuna mahitaji, nukta za udhaifu, na mianya ya kasoro, ni lazima kuzalisha tariba hizi ili kuwaelekeza watu katika kubabiliana nazo na kuzitatua.

Katika kiwango cha mafunzo inapasa kuhamasisha wanafunzi wa kiume na wa kike katika juhudi na jitihada ili kupata alama za juu na kupata kiwango bora na wastani, na haisihi kufumbia macho kuteremka kiwango cha mafunzo kwa ambayo yanapatikana katika hayo miongoni mwa kuchelewa na kurudi nyuma.

Na katika kiwango cha kivitendo na kikazi ni juu ya wanajamii kuimarisha nguvu zao na kuchangia katika kujenga nchi yao, na kupitia ikhlasi zao katika kazi, na kutafuta fursa mpaya na miradi ya uvumbuzi na kutayarisha vipaji na ujuzi katika nyanja za teknolojia za kisasa na kwamba wasiweke rehani mustakabala wao kwa kupata kazi zilizotayari na kuzizingatia kuwa ndio

chaguo pekee katika kujenga maisha yao.

Na kijamii kuna nukta za udhaifu katika jamii miongoni mwa mafakiri, mayatima na wagonjwa, na kuna haja, mahitaji na huduma za kijamii. Inapasa kukumbusha jukumu la kijamii, na kushajiisha taasisi za jumla kama vile jumuiya rasmi za kheri, na yale ambayo kamati zinashughulika nayo kati ya vitengo vya kuangalia mayatima na mifuko ya kuozesha ya kheri na hafla za ndoa za pamoja na nyinginezo. Ili kuamsha nafasi yake na majukumu yake katika nyanja hii.

Hakika kuna uwezekano wa mazingira ya Muharam kuleta msukumo mkubwa wa kimaanawi kwa ajili ya maslahi ya kustawisha jamii na kutumikia malengo yake matukufu.

### 3. Mafunzo ya Ashura:

Tunaweza kusoma Ashura kama kisa cha kihistoria, matukio yake yaliyotokea katika zama na sehemu maalum, na kutoka kwa watu maalumu. Na tunaweza kuisoma kama mzozo baina ya makundi mawili juu ya malengo na mambo mbalimbali. Na tunaweza kuisoma kama mateso na kuamsha huruma zetu na hisia zetu. Lakini kinachotakiwa ni kuisoma kama msiba wa kidini na wa kibinadamu wenye kigezo, tuwe tunachukua kutoka humo mafunzo na mazingatio na tunachukua kwayo maadili na vigezo.

Katika matukio ya Ashura inabainika kulazimiana kiukweli na dini, na kujitolea kwa ajili ya misingi yake na kuchora picha nzuri ya utekelezaji na misimamo ya kishujaa. Katika Karbalaa kulikuwa na kijana ambaye alizatiti ujana wake kwa ajili ya kuhudumia ujumbe na umma, na mwanamke ambaye alipambana kwa hijabu yake na heshima yake na maneno yake na uvumilivu wake sanjari na kunusuru haki, na mzee kikongwe katika umri ambaye haukumkalisha nje udhoofu wake na uzee wake katika kushiriki katika vita vya kujitoa muhanga, na ndugu mtekelezaji

mwenye kumliwaza ndugu yake katika nyakati ngumu kabisa, na kundi la waumini ambalo halikuzembea kutekeleza swala katika wakati wake chini ya mpishano wa mishale na mikuki, na majeruhi waliojeruhiwa ambao huzuni na mateso hayakuathiri uimara wao na misimamo yao.

Hakika ni picha nzuri na mafunzo makubwa, inatupasa tuyasome ili tupate kwayo maadili na mazingatio, kwa ambayo yanatufaa kwa ajili ya kutengeneza wakati wetu wa sasa na kujenga mustakabali wetu katika mwangaza wa misingi na maadili.

### 4. Kujenga umoja wa kitaifa na Kiislamu:

Changamoto ambazo zinatukabili katika kiwango cha nchi na Kiislamu ni wajibu zitusukume sote katika kushikamana na kushirikiana. Pamoja na madhehebu yetu Sunni na Shi'ah, hiyo isiwe ni kisingizio cha kuwa mbali na kuhitalifiana, maadamu sisi tunaafikiana katika misingi, ambayo inatukusanya nchi moja na maslahi ya ushirikiano.

Na ratiba ya Ashura inawezekana kunufaika nayo katika kuimarisha umoja wa nchi na wa Kiislamu na lugha ya mazungumzo ya Kiislamu iepuke uchochezi na dharau ya kiubaguzi. Na ratiba ya Ashura itengeneze fursa nzuri ili kuwafahamisha Waislamu waliobaki rai na vitendo vya ndugu zao Shi'ah, ambapo imeenea katika baadhi ya jamii propaganda na maelezo ya kupaka matope na ya kimakosa kuhusu ukweli wa itikadi ya Kishi'ah na namna ya kuhuisha msimu wa Muharam.

Alhamdulillhi! Huseiniya zimefunguliwa katika kila sehemu katika ulimwengu, na ratiba ziko wazi na hakuna kisingizio cha kukanganyikiwa na propaganda za ushawishi, maadamu kuna fursa ya kufahamiana moja kwa moja. Na kumbukumbu za Imamu Husein ni wajibu iwe ni mnasaba wa kuimarisha umoja wa umma. Husein ni kadhia ya Kiislamu kwa ujumla, na sio mradi wa madhehebu maalum. Naye hakika amefanya mapinduzi

na amekufa shahidi kwa ajili ya kutengeneza umma na maslahi yake kama anavyosema عليه السلام: "Hakika mimi sikutoka kwa shari wala kwa kiburi wala kwa uharibifu wala kwa dhulma, bali nimetoka kwa ajili ya kutaka kutengeneza katika umma wa babu yangu. Nataka kuamrisha mema na kukataza maovu, na kwenda kwa mwendo wa babu yangu na baba yangu Ali bin Abi Twalib. Atakayenikubali kwa kuikubali haki basi Mwenyezi Mungu ni aula zaidi kwa haki, na atakaye nikataa nitasubiri hadi Mwenyezi Mungu ahukumu baina yangu na kaumu kwa haki. Naye ni Mbora wa kuhukumu."

Amani iwe kwa Husein siku aliyozaliwa, siku aliyokufa shahidi na siku ya kufufuliwa.

## SHI'AH NA ULIMWENGU[147]

Ushi'ah sio kundi la kiitikadi wala madrasa ya kifikihi ya kimadhehebu tu, bali ni mtazamo na msimamo mukabala na hali ambayo unaishi nayo umma wa Kiislamu.

Sisi tuna haja ya mazingira huru na kufunguka kifikra na akili kufanya kazi na kuvumbua fikra. Umewadia wakati wa kufanya mijadala yenye kujenga na mikutano yenye malengo ili kusahihisha na kutafiti uhalisia wa hawza na maraji'i. Tunahitaji vyuo maalumu kwa ajili ya khutuba za Huseiniya ndani ya hawza zetu za elimu.

**Swali:** Mnaonaje hali ya uhusiano na muamala baina ya mitazamo na mikusanyiko mbalimbali ndani ya makundi ya Kishi'ah?

Ni lazima tuamue mwanzoni kwamba wingi na ikhitilafu katika

[147] Majadiliano yaliyofanywa na Muadham Sheikh Hasan Saffar na *Majalatu al-Muusimu fuswiliya muswawara* linalojihusisha na athari na hazina linalotolewa kuhusu Darul-Muusimu liliilaam - Beirut toleo namba 11 mujaladi wa tatu 1990 / 1412 Hijiria.

jamii za kibinadmu ni hali ya kawaida na haki ya kisharia. Kama tukipembua hali za jamii za binadamu katika zama za historia, vyovyote zitakavyokuwa dini zao na madhehebu zao, tungeona hali ya ikhitilafu na makundi ipo na imesimama. Na baadhi wanaweza kuona kwamba jamii ya kidini haina nafasi humo ya kukhitilafiana na kuwa na makundi. Maadamu sote tunaamini dini moja, nini sababu ya ikhitilafu na kuwa na rai na mitazamo mingi? Lakini kwa kutafakari mwanadamu anavumbua kwa urahisi dhana hii. Kuna sababu na mambo mengi yanayolazimu kupatikana kutofautina na kutengana baina ya jamii ya kidini, na tunayo mafuhumu na mafunzo yanayoweka wazi sababu hizi na kutuelekeza namna ya kuamiliana pamoja nayo.

**Kwanza:** Kutofautiana katika kiwango cha imani na daraja zake, ambapo imepokewa katika nususi nyingi, amezitaja al-Allammah al-Majilisiy ﵀ katika rejea ya *Biharul-Anwaar* katika mlango maalum chini ya anwani: (Darajaatul-Imani wa Haqaiqihi) katika kitabu *Imanu wal-kufur*, Juz. 6, uk. 154 hadi 175.

Na kwa hakika kutofautiana kiwango cha imani kunaweza kusababisha kutaofautiana katika rai, mwenendo na vitendo. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

هُم دَرَجٰتٌ عِندَ اللَّهِ وَاللَّهُ بَصيرٌ بِما يَعمَلونَ

> **"Wao wana daraja mbele ya Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona yale wanayoyafanya." (Surat Aali-Imran; 3:163).**

Na kutoka kwa Abdul-Aziz al-Qatwisiy amesema: Aliniambia Abi Abdillahi Swadiq ؑ: Ewe Abdul-Aziz; hakika imani ina daraja kumi kama ngazi, anapanda kwayo daraja baada ya daraja. Asiseme mtu wa daraja la pili kwa wa daraja ya kwanza: 'Huna lolote,' bali hadi afikie daraja ya kumi. Usimdharau aliye chini yako asije akakuangukia aliye juu yako. Ukimuona aliye chini yako kwa daraja mnyanyue humo kwa upole na wala usimbe-

beshe asiyoyaweza na kumvunja. Hakika mwenye kumvunja muumini ni juu yake amfunge bandeji."[148]

Na katika hadithi hii kuna ishara muhimu kwamba unapomtenga anayehitalifiana pamoja na wewe, hakika wengine watakutenga kwa kuhitalifaiana kwako pamoja nao, kama inavyoelekeza hadithi onyo kali kwa wanaoporomosha mazingatio ya ndugu zao waumini na wanasahau haki zao na shakhsiya zao, si kwa jingine ila kwa kuwa wao hawawaafiki katika kila wanayoyaitakidi au wanayoyafanya.

Na katika riwaya nyingine kutoka kwa Imamu Swadiq عليه السلام vile-vile anaipokea Swabaah Abu Siyaabah kutoka kwake عليه السلام kwamba amesema: "Mna nini nyinyi na chuki, baadhi yenu wanachukia baadhi? Hakika waumini baadhi yao ni bora kuliko baadhi, na baadhi yao ni wengi wa swala kuliko baadhi, na baadhi yao ni wenye uoni kuliko baadhi, nayo yana madaraja."[149]

**Pili:** kutofautiana kiwango cha maarifa na uelewa: Sio kila ukweli anauvumbua kila mtu, na kwa daraja moja la uwazi. Na uelewa wa watu katika elimu sio mmoja. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

"..... نَرفَعُ دَرَجٰتٍ مَن نَشاءُ وَفَوقَ كُلِّ ذى عِلمٍ عَليمٌ"

**".....Tunawatukuza kwenye vyeo tuwatakao, na juu ya kila mwenye elimu yuko ajuaye zaidi." (Surat Al-Yusuf; 12:76).**

Na kutofautina kiwango na maarifa kunasababisha kuhitalifiana katika rai na mtazamo. Ukweli unaweza kuwa wazi, baadhi yetu unawapelekea kukinai na kazi fulani, wakati ambapo wengine wanakataa kukinahi huko na kazi hiyo, kwa kutokujua kwao na

[148] Al- Majilisiy: Muhammad Baaqir katika Biharul-Anuwar juzuu 66 uk: 165.
[149] Rejea iliyotangulia 168

kuweza kukinahi na ukweli huo kimsingi, na kwa hiyo anasema Imamu Ali عليه السلام: "Watu ni maadui wa wasiyoyajua."

Na anaweza kupata mmoja wetu maalumati yanayomsukuma kuchukua msimamo fulani, pamoja na kwamba asiye na maalumati hayo au asiyeyategemea hawezi kuchukua msimamo huo. Na haya yanawezekana sio tu miongoni mwa waumini bali hata kwa manabii na mawalii maasumina na muqarabina. Inapotaka hekima ya Mwenyezi Mungu kumfahamisha Nabii juu ya uhakika maalum, anauficha kwa Nabii mwingine. Matokeo yatakuwa ni aina ya tofauti na ikhitilafu katika rai baina ya manabii hao wawili. Kama kinavyoonekana kisa cha Nabii Musa na al-Khidhir عليهما السلام ambacho Qur'ani tukufu inakitaja katika Suratu Kahfi. Na vilevile hukumu ya Manabii wawili, Daud na Suleiman عليهما السلام walipohukumu katika shamba kama ilivyopokewa katika Suratul-Anbiyai.

Na katika mazingira haya inatokea ikhitilafu baina ya mafaqihi na mujitahidina katika fat'wa, ambapo kila mmoja anataoa juhudi yake ya elimu na anatumia uwezo wake wa ijitihadi ili kuvumbua hukumu ya Mwenyezi Mungu katika kila mas'ala, lakini wao wanaweza kutofautiana katika fat'wa zao hata katika madhehebu moja kama ilivyo mashuhuri kwetu. Na ikhitilafu yao ni muonekano katika uhalisia wa ikhitilafu katika maisha ya binadamu na Uislamu kukubali hali hii.

**Tatu:** Ikhitilafu ya maslahi: Maasumu tu ndio anakuwa hana msukumo katika fikra zake na vitendo vyake, na misimamo yake inatokana na haki na inakusudia haki. Na umaasumu ni daraja tukufu, ni mahususi kwa malaika ambao:

".....بَل عِبادٌ مُكرَمونَ ﴿٢٦﴾ لا يَسبِقونَهُ بِالقَولِ وَهُم بِأَمرِهِ
يَعمَلونَ ﴿٢٧﴾"

> **"…..Bali hao ni waja waliotukuzwa. Hawamtangulii kwa neno nao wanafanya kwa amri Yake." (Surat Al-Anbiya; 21:26–27).**

Na Manabii, Nabii ni maasumu (hatamki kwa matamanio. Ila ni wahyi unaofunuliwa, na Maimamu ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na akawatakasa kabisa.

Ama watu wengine, na miongoni mwao ni waumini, vyovyote zitakavyokuwa juu daraja za imani zao, wao ni binadamu wana maslahi, na matamanio yanaingilia na kuathiri juu ya rai zao na misimamo yao. Kila upande au kundi au jamaa inakwenda mbio kutetea maslahi yake na manufaa yake. Na katika msingi huo inachukuliwa misimamo na kujenga kukinahi kwake.

Katika yote yaliyotangulia tunaamua kwamba hali ya kuhitalifiana na kutofautina ni hali ya kawaida kwa Shi'ah kama ilivyo kwa wasiokuwa wao. Lakini maneno kuhusu muamala pamoja na hali hii, ambapo ikhitilafu hii inakuwa na tofauti katika nyakati nyingi, ni sababu ya kuwa mbali na uadui na mizozo. Na haya ndio ambayo zinakabiliwa nayo baadhi ya jamii zetu, ambapo imekuwa ikhitilafu katika kumfuata Marjaa huyu au kumfuata Marjaa yule au ikhitilafu katika msimamo wa kisiasa na ufuasi wa chama au ikhitilafu hata katika baadhi ya rai na fikra. Katika baadhi ya wakati hata baina ya wenye Huseiniya na misafara ya maombolezo, ikhitilafu hizo zimekuwa ni sababu ya mzozo na ni kikwazo cha umoja na ushirikiano!!!

Na kinachotakiwa kwetu sasa hivi ni kuingia katika hatua mpya, tuvuke humo kasoro za ikhitilafu, kwani ulimwengu pembezoni mwetu sasa hivi unaingia zama za wigo mpya, baada ya muda mrefu wa vita baridi baina ya kambi ya Magharibi na Mashariki. Na nchi zetu za mashariki ya kati zinaweza zikakaribia kuingia katika hali mpya, kama yanavyoashiria maneno ya wakuu wa siasa ulimwenguni. Na muongo uliopita ulijaa uzoefu na

matukio, ni wajibu utupe uzoefu na upevu katika muamala wetu pamoja na baadhi yetu kwa baadhi ndani ya mpaka ufuatao:

**Kwanza:** Kutambua hali ya vyama vingi na uhalali wake:

Ama kila mmoja wetu akipinga uwepo wa mwingine, na akazingatia uwepo wake ndio sharia ya asili, na akataka kulazimisha amri zake juu ya wengine na waingie humo na wajiunge naye, hakika hilo litatufanya ni walengwa wa ugomvi na fitina. Na maslahi yetu yanakuwa kama madhehebu na kama kundi ni muhanga wa lengo hili lisilo na uhalisia.

**Pili:** Kuweka kikomo cha mizozo na ugomvi, ili itawale tabia ya kuheshimiana. Tumekwishaona namna gani imerejea kwetu hali ya mzozo na propaganda na kutuhumiana. Imerejea kwetu sote kwa madhara, na pande za nje zimeitumia, na sehemu za uchochezi ndani mwetu. Hapa inakuja dauru ya watu, wakati wa kheri, walinganiaji na urekebishaji na miongoni mwa waelewa wenye ikhilasi, na ulamaa wa umma na mashujaa wake, kwamba wajitolee kwa ajili ya kutatua ikhitilafu inayotokea au sintofahamu inayotokea. Na kwa masikitiko makubwa, ni nadra aina hii katika misimamo, ambapo hakika wengi, ama wanakanganyikiwa katika mzozo na wanaingia katika moja ya pande zake au wanaacha kamba kwa watu wa Magharibi na wala hawaoni jukumu la nafsi zao katika jambo hili.

**Tatu:** Utamaduni wa usamehevu na ushirikiano na kupiga vita fikra na uchochezi ambao unashajiisha kasumba na madhambi. Kutoka kwa Imamu Swadiq عليه السلام: “Mwenye kumtuhumu ndugu yake katika dini yake hakuna utukufu baina yao.” Na katika hadithi nyingine kutoka kwake عليه السلام: “Jihadharisheni na ugomvi katika dini, hakika unashughulisha nyoyo na utajo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na unaleta unafiki, na kuchuma chuki, na kuchochea uongo.”

Na kitu kibaya zaidi ni kuongozea sifa ya kisharia katika ugomvi

na mzozo ambapo baadhi wanaitakidi kwamba taklifu yao ya kisharia inakuwa katika kuangusha wengine wenye kuwakhalifu, na kwamba wana thawabu katika kusambaza maovu juu yao!!

**Nne:** Kuweka tamko la ushirikiano baina ya pande mbalimbali katika kiwango cha jumla au katika pande za ndani, na hapa kuna bishara na matumaini makubwa katika kuanza hatua mpya inayotawaliwa na usafi na ushirikiano baina ya pande mbalimbali za makundi na katika kila kiwango chake inshaallah. Na nataraji jarida la msimu kufanya jukumu lake la uelekezi katika nyanja ya utangazaji na utamaduni kwa ajili ya kutumikia umoja na ushirikiano ndani ya umma na kwa Waislamu wengine na kuwa ni mimbari iliyowazi kwa kila rai na pande zenye harakati.

**Swali:** Je, kuna anayeona kwamba shughuli za kisiasa na kazi za ijitihadi ambazo wamezifanya baadhi ya harakati na pande za Kishi’ah katika muongo uliopita zimeacha athari mbaya katika hali ya Kishi’ah, kijamii na kisiasa, kama ambavyo umeondoa kisingizio cha kupaka matope sura yao katika kiwango cha kimadola, nini rai yenu?

Inafahamika kwamba kuna mielekeo miwili katika kufahamu Uislamu, Ushi’ah na uhusiano wake wa kijamii. Mwelekeo wa kwanza unatazama dini katika mpaka wa mas’ala ya kiitikadi na kiibada na wa kimawaidha, bila ya kuzingatia na kuingilia katika mambo ya kisiasa na kijamii. Na kwa kujengea juu ya fahamu hii, harakati na shughuli za Kishi’ah zinazingirwa katika kushikamana na fiqihi ya Ahlul-Bayt عليهم السلام na kuhuisha nembo zao, na kueneza fikra zao na fadhila zao. Na haipasi kuvuka hayo kwenda kwenye kazi ya jihadi na kisiasa, kwa sababu hayo yanapingana na mafuhumu ya taqiya (kulingana na mtazamo wao) na kwa namna ya kuwahi na kuharakisha dauru ya mabadiliko ya jumla ambayo atayafanya Swahibu Zaman عليه السلام. Na kwa wenye mtazamo huu wana rundo la fikra na harakati, wanatoa hoja kwazo kwa nususi mbalimbali za kidini na

misimamo ya kihistoria, na sasa hivi hatuko katika sehemu ya kujadili maudhui haya lakini tunataka kuashiria kwamba swala linaloulizia undani huu, na kuanzia kwalo linapata matatizo haya.

Ama mwelekeo mwingine unaona kwamba dini inahusika na pande zote za maisha ya mwandamu na jamii, na mambo ya kisiasa yana dauru yake ya kimsingi na athari kubwa katika nyanja zote za maisha. Haiwezekani kusahau umuhimu wake kwa mwanadamu muumini. Na Ushi'ah sio kundi la kiitikadi wala sio madrasa ya kifikihi ya kimadhehebu tu, bali ni mtazamo wa msimamo mbele ya hali ambayo unaishi nayo umma, na maelekezo ya Ahlul-Bayt عليهم السلام, yanawasukuma wafuasi wake katika kubeba jukumu katika kutetea maslahi na mambo ya wanyonge. Amirul-Muuminina Ali عليه السلام, anasema: Mwenyezi Mungu hakuwafanya maulamaa "wakubali shibe ya dhalimu wala njaa ya mwenye kudhulumiwa." Na Imamu al-Husein عليه السلام anapokea kutoka kwa babu yake Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم kauli yake: "Mwenye kuona mtawala dhalimu anayehalalisha haramu ya Mwenyezi Mungu, mwenye kutengua ahadi ya Mwenyezi Mungu, mwenye kukhalifu Sunnah ya Mtume wa Mwenyezi Mungu anawafanyia waja wa Mwenyezi Mungu madhambi na uadui na wala hakubadilisha juu yake kwa kitendo wala kwa kauli, ni haki ya Mwenyezi Mungu kumwingiza motoni."

Na nyinginezo kati ya riwaya zilizopo katika madhumuni yake, na sambamba na mafunzo haya na maelekezo haya kuna maisha ya Maimamu wao wenyewe ambayo yalikuwa yamejaa misimamo na jihadi na mapinduzi na upinzani dhidi ya ufisadi na dhulma. Na matokeo ya hayo Ahlul-Bayt wamevumilia mateso ya misimamo ya kiujumbe, wametoa maisha yao thamani ya misimamo hiyo, na wameishi machungu, balaa na kufukuzwa na mateso. Na wafuasi wa Ahlul-Bayt na Mashi'ah wao wame-julikana katika historia ya umma kwamba wao ni dhamira ya umma na walinzi wa ujumbe, na wanamapinduzi wa Alawiyina na Hashimiyina daima ni mfano katika hayo.

Na harakati za kisiasa na harakati za jihadi katika harakati za Kishi'ah leo hakika ni mwendelezo wa historia hiyo. Na ni chimbuko linalotokana na ufahamu huo katika dauru ya dini katika maisha na jukumu la muumini mbele ya uhalisia wa maisha, na kujengea juu ya fahamu hiyo na mwelekeo usio na lawama katika kuvumilia taabu na kusubiria juu ya msimamo wa kiimani wa kiujumbe na wenye mshikamano, kwa kuwaiga Ahlul-Bayt عليهم السلام ni kigezo kwao. Shakhsiya yao ilipakwa matope na baadhi wakashuku katika dini yao, kama hali ilivyo katika makhawariji kumtuhumu Imamu Ali kwa shiriki, na propaganda ya Muawiya dhidi yake kwamba haswali wala haogi janaba. Kama ambavyo walimtuhumu Imamu al-Husein kwamba ametoka katika dini, wakatekwa wake zake na familia yake. Na inawezekana kusema kwamba maisha ya Ahlul-Bayt عليهم السلام ni mlolongo unaoendelea katika jihadi na kujitolea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na wanyoge.

Na katika upande mwingine, hakika zilichokifanya harakati za Kishi'ah miongoni mwa jihadi na harakati, hakika yanakuja ndani ya medani ya mwamko wa Kiislamu. Ulivuma upepo wake kwa Waislamu wote, ambapo uliamsha jamhuri ya umma katika nafsi yake ili uone kwamba hali yake iko mbali na manhaji ya Mwenyezi Mungu na kwamba unaishi maisha ya kufuata na kutoendelea na unazungukwa na ukosefu na ujahili, na hatamu za mambo yake zipo katika mikono isiyo na uwezo na isiyo na ikhilasi. Ikatikisika ghera na hisia ya majukumu kwa wenye kuelewa na wenye ikhilasi, na wakatengeneza harakati na vyama, na yakatokea maandamano na mapinduzi katika nchi mbalimbali za Kiislamu. Na Shi'ah wao ni sehemu isiyojitenga na Umma wa Kiislamu. Haikuwa inasihi kwao kurudi nyuma na msafara wa medani ya mwamko wa Kiislamu ambao unalenga kuitawalisha dini katika maisha na kunyanyua neno la Mwenyezi Mungu, na kurejesha utukufu wa Waislamu. Na yaliyotokea yalikuwa ndani ya mtiririko huu na ni katika jumla ya sababu ya kujifakharisha na utukufu, kama ambavyo ukali wa dhulma na ukandamizaji na

mateso ambayo umma ulipata katika baadhi ya nchi unatengeneza sababu yenye kubinya na yenye kusukuma katika mwelekeo wa mapambano na kulipiza kisasi.

Na ikiwa kuna machungu, mateso na kibano basi imetokea kwa umma wa Shi'ah kwa sababu ya vitendo hivyo vya kisiasa na vya jihadi. Hakika haisihi kuzuia kwetu kuona mafanikio na faida ambayo imepatikana katika Uislamu na Waislamu kutokana na harakati hizo, ambapo lilipanuka duara la uelewa wa kidini na ikaongezeka kujongea watu katika mambo ya Kiislamu, na wengi wakalazimika. Katika serikali nyingi zikajali Uislamu na kujidhihirisha kwa kushikamana nao, na Uislamu ukawa ni ukweli unaoafikiwa, unaotambulisha nafsi yake katika kiwango cha juu kiulimwengu, kisehemu na kijamii.

Kwa hakika kuzungumzia uhalali wa harakati na sababu zake, shughuli zake za kisiasa na za jihadi haimaanishi kukubali vipengele na ufafanuzi wa vitendo vyote ambavyo vinapatikana kutokana na hayo. Na uwanja uko wazi na medani ni pana, kwa njia mbalimbali za kazi na namna zake mbalimbali, na inawezekana kujadili kuhusu baadhi ya vitendo, au kuelekeza ukosoaji kwa baadhi ya misimamo. Jitihada zimekwishakuwa nyingi, kumetokea mwingiliano na kupatikana makosa.

Na haitupiti kuashiria kwamba pande za dola na utawala wa sehemu, na baadhi ya wapinzani wa kimakundi, wamefanya kazi sana ya kukuza baadhi ya dosari, uchochezi na tuhuma dhidi ya harakati za Kiislamu za jihadi kwa namna ya ujumla na hususani harakati za Kishi'ah miongoni mwazo. Na ni juu yetu tusiingie katika vita vya kinafsi, na kushindwa mbele ya upotoshaji wa matangazo. Matangazo yalikuwa na bado yangali ni silaha inayotumiwa na mabeberu na madhalimu dhidi ya harakati za wanyonge na wenye kudhulumiwa.

**Swali:** Mukabala wa uchochezi wa fitina ya makundi na mfara-

kano wa kimadhehebu baina ya Sunni na Shi'ah kuna mapendekezo na harakati za kuleta ukuruba baina ya madhehebu ya Kiislamu na kuimarisha hali ya umoja baina ya Waislamu. Na kwa kuzingatia nyinyi ni kati ya wenye kuzingatia kupendekeza mambo haya katika maandiko yenu na khutuba zenu je, mnaona katika medani mapendekezo makini katika njia hii?

Mizozo ya kimakundi katika umma na uchochezi wa mfarakano wa kimadhehebu kawaida nyuma yake kuna sababu mbili:
Sababu ya kisiasa. Wakati pande za kigeni au serikali potofu zinapopanga kuwashughulisha Waislamu na mambo ya maendeleo au kusambaratisha umoja wao, na mara nyingi ilikuwa inatokea katika miongo iliyopita, kwa sababu ya jambo hili, uliogopa ubeberu wa kiulimwengu, na mifumo potovu ikahisi hatari kubwa ya kustawi harakati za Kiislamu, na harakati za Waislamu na kulingania kwao kwenye dini yao na kutaka kuitawalisha katika maisha. Na katika makabiliano haya ya mwamko wa Kiislamu maadui wametumia hatua nyingi na miongoni mwa hizo ilikuwa ni kufufukua nyaraka za ikhitilafu za kimakundi na kimadhehebu.

Na sababu ya pili ni hali ya kutoendelea ambayo zinaishi nayo sehemu kubwa za umma katika nyanja za utamaduni na akhlaqi. Na kutoendelea huku ambako kunadhihirika katika kutojuana Waislamu baadhi yao kwa baadhi, na katika kutokuwepo na kufunguka na majadiliano mazuri, na katika tabia za kasumba na ukali mbele ya rai nyingine, na muda wote wa historia kulikuwa na harakati mbili na aina mbili katika kuamiliana na ikhitilafu na wingi wa madhehebu, harakati za usamehevu na kuvuka sehemu za ikhitilafu kwenda kwenye wigo wa umoja wa Kiislamu na maslahi ya pamoja, na kundi la kasumba na ugaidi wa kifikra ambalo daima linachochea vipengele vya ikhitilafu na kuvikuza ili kusiwepo na fursa ya kukutana au kujadili na ushirikiano, na maelekezo ya jumla ya Maimamu wa Ahlul-Bayt عليهم السلام na wafuasi wao wenye uelewa, ni katika mapito ya harakati ya kwanza. Na sio katika upande wa maelekezo na muongozo tu, bali hata katika

kiwango cha vitendo na utawala katika muda ambao utawala unakuwa katika mikono yao, kama anavyopokea Sheikh Tuusiy kwa mfano katika *Tahadhib* kuhusu msimamo wa Imamu Ali عليه السلام alipochukua ukhalifa katika mas'ala ya kifiqihi yanayo-khalifu rai yake na wala haruhusu kutokea tatizo linaloharibu umoja au linalotumikia malengo ya wapinzani kwa ajili ya mas'ala ya pembezoni.

Imekuja katika *Tahadhib* kwamba: Alipowasili Amirul-Muumi-nina عليه السلام mjini Kufah alimwamuru Hasan bin Ali awatangazie watu: Hakuna swala katika mwezi wa Ramadhani katika misikiti kwa jamaa – yaani swala ya tarawehe ambayo alitoa fat'wa kwayo Umar bin al-Khatab katika zama zake – Hasan bin Ali akawatangazia watu yale aliyoamrishwa na Amirul-Muuminina, watu waliposikia maneno ya Hasan bin Ali wakapiga kelele: '*Waa Umaraa* …..' Hasan aliporejea kwa Ali akamuuliza sauti hii ni ya nini? Akasema: Ewe Amirul-Muuminina watu wanapiga kelele: **Waa Umaraa waa Umaraa!!** Amirul-Muuminina عليه السلام akasema: Waambie waswali…[150]

Na hakika mimi nina matumaini sana katika hatua ya sasa kwamba kuna uelewa wa umoja umeanza kuenea katika safu za Waislamu, na kwamba tabia ya usamehevu, ukunjufu wa moyo na kuheshimu rai ya mwingine ndio kati ya alama ya zama hizi ambapo zinanyanyuka humo sauti za kulingania demokrasia na kuheshimu haki za binadamu.

Huenda kati ya yanayotumikia umoja wa Kiislamu, ni kufunguka Waislamu baadhi yao kwa baadhi na kuenea maarifa ya kimadhehebu, kwa kutoa fursa mbele ya kila Mwislamu ili kujua kwa namna ya moja kwa moja rai za madhehebu mengine ya Kiislamu, ama ujahili na kujifungia ni maandalizi ya kukubali propaganda za upotovu wa wapinzani.

[150] Tuusiy katika *Tahadhib* Juz. 3, uk. 70

**Swali:** Mazungumzo aliyoyaeleza Muadhamu al-Allammah Sayydi Muhammad Husein Fadhilullahi katika *Majalatul-Muusim* katika toleo la nane yamechochea mijadala na maswali mengi na hususan katika yanayohusiana na maudhui ya umariji'i wa kidini, nini rai yenu na maelezo yenu katika upande huu?

Kwanza napenda kuheshimu na kujali dauru ambayo anaifanya Muadhamu al-Allammah Fadhwilullahi katika kutajirisha utamaduni wa Kiislamu kwa mwelekeo wake wa kifikra ambao unabainika katika ufuatiliaji wake wa mahitaji ya medani na utatuzi wake wa matatizo na shida za kileo. Na vilevile ushujaa na ujasiri katika kupendekeza mambo na mas'ala ambayo wengi wanaogopa kuyaeleza.

Na katika yanayohusiana na mazungumzo ya Muadhamu kuhusu umarji'i na hali wanayoishi nayo Mashi'ah, napenda kuashiria katika nukta zifuatazo:

**Kwanza:** Hakika sisi ni wajibu tuvuke hali ya hofu ya kukosolewa, na kuchukua misimamo mibaya na kupinga dhidi yake, maadamu sisi hatudai umaasumu kwa nafsi zetu, na tunatarajia kilichobora zaidi, na tunaamini dauru ya nasaha na kuusiana. Ni juu yetu kukubali kukosolewa na kusahihishwa katika hali zetu zote na mambo yetu yote, na ambao wanakataa kukosolewa kana kwamba wao wanadai umaasumu au hawatarajii kilichobora zaidi, na wanaona kwamba hakuna uwezekano wa kilichobora zaidi katika kazi zao, au wanajikweza na wanajinyanyua katika kukubali nasaha na wasia.

Na Qur'ani tukufu inapotaja maelekezo na Mwenyezi Mungu Mtukufu kumfunza adabu Nabii wake Muhammad ﷺ katika masikio ya vizazi, na anazungmza juu ya makosa na kasoro za jamii ya Kiislamu ya awali kwa kuwaelekeza katika kuyarekebisha na kuyasahihisha, hakika ni ili kuulea umma wa Kiislamu na binadamu kwa ujumla katika dharura ya kusahihisha, kurejea na kukosoa.

Na kusawazisha sio msimamo wa kiuadui, wala haisihi kutazama ukosoaji wowote kwamba ni kujeruhi au kudhihirisha au kudharau. Na pengine baadhi wanadhani ndani ya dini kwamba ukosoaji unasababisha kufichua upungufu wetu na nukta za udhaifu wetu mbele ya wengine, na mbele ya jamhuri na kupungua na kudhoofika uaminifu wake katika upande wa kidini. Lakini dhana hii inatokana na kutoelewa kuliko wazi, ambapo hali ya Mashi'ah na hali ya umarji'i sio tena ni jambo la kificho bali liko chini ya darubini na kuangaziwa. Na inajiri pembezoni mwake hali za utafiti upembuzi, na inaweza kuwa wanayoyajua wengine katika ufafanuzi wa hali zetu ni mengi zaidi kuliko wanayoyajua wengi wetu, na sababu ya kuenea uelewa na maarifa na kufunguka jamii yetu katika ulimwengu hakika maswali mengi na mzungumzo mapana yanazunguka ndani ya jamhuri ya Shi'ah kuhusu taasisi zake za kidini na za kiongozi. Na ni juu yetu kuelekeza na kufafanua kadhia na mambo ili wasiyatumie maadui kwa kupotosha jamii zetu, na hayo ni kwa kuyajadili na kuyaeleza na kujadiliana kuhusiana nayo na sio kwa kificho na kuzuia.

**Pili:** Hakika sisi tuna haja ya mazingira huru na kufunguka kifikra, ili akili zifanye kazi na kuvumbua fikra. Ama ukitawala ugaidi wa kifikra, na tukamtuhumu kila anayetoa fikra mpya, na tukashuku katika nia ya kila anayekosoa au anayepinga, hakika sisi kwa hayo tunaziharamishia nafsi zetu uvumbuzi wa kifikra, na tutadharau rai zenye kupatia na kudumaza akili na fikra.

**Tatu:** Ikiwa maadili yetu na misingi yetu ni thabiti daima hakika ratiba, njia na mbinu zinakubali mabadiliko na kuboresha kila unapopita muda, kwenda kwenye uzuri zaidi na ubora zaidi. Na haya ni ambayo inayasisitiza dini yetu tukufu kama yalivyo madhumuni ya hadithi tukufu kutoka kwa Imamu Musa al-Kaadhim عليه السلام: "Ambaye siku zake zitafanana basi ni mwenye hasara, na ambaye mwisho wa siku zake mbili ni mbaya zaidi basi yuko katika upungufu, na ambaye yuko katika upungufu basi

mauti ni bora kwake kuliko uhai."

Na iliyokaribu nayo ni hadithi ya Imamu Ali عليه السلام na nyingine kutoka kwa Imamu Swadiq عليه السلام kama ilivyo katika Bihrul-Anuwar, Juz. 78, uk. 277, uk. 327 na Juz. 77, uk. 377, na katika dua ya siku ya Jumapili ya Imamu Zainul-Abidin عليه السلام : "Na ijaalie kesho yangu na baada yake iwe ni bora kuliko saa yangu na siku yangu hii."

Na mwenendo wa maendeleo na mabadiliko katika maisha yetu ya leo yanakwenda mbio katika pande mbalimbali na teknolojia na njia za maarifa na matangazo na uendeshaji, na tukishikamana na mbinu zilezile na vifaa na manhaji za kurithi katika mazingira yetu ya kielimu na kidini, masafa ya kutenganisha baina yetu na msafara wa maendeleo ya kisasa yatakuwa ni makubwa na mapana.

Na zimetoka ndani ya hawza za kidini na mazingira ya marji'i sauti zenye ikhilasi na uelewa ambao zinalingania juu ya dharura ya mabadiliko na kuboresha katika manhaji za utafiti wa hawza na mbinu za kimalezi ya kielimu, na njia za kuelimisha na kuelekeza, na njia za jukumu la uongozi wa umarji'i. Na maandiko ya Khomeni قدس سره na misimamo yake inazingatiwa kuwa ni madrasa kamili katika nyanja hii, kama ambavyo Marji'i Shahidi Sayyid Swadir رحمه الله katika rai na fikra za ukosoaji na mabadiliko katika hali ya hawza na nafasi ya maraji'i, ameashiria kwenye baadhi yake katika utangulizi wa harakati zake katika elimu ya Usuul na katika mapendekezo yake kuhusu umarji'i yenye manufaa na katika mhadhara wake wa mwisho ambao umechapishwa chini ya anwani *"al- Mihnatu."*

Na nchini Iran maudhui ya kuboresha hali ya umariji'i ni mahali pa utafiti na mjadala kutoka kwa wengi katika maulamaa na wanafikra baada ya kufariki Sayid al-Burjurudiy رحمه الله. Na vili-fanyika vikao ambamo alishiriki humo mfano wa Marhum Sayid

al-Twalaqaaniy, Shahidi al-Mutwahariy, na mwanafikra Muhammad Taqiy Shariatiy na wengineo. Na kumechapishwa kutokana na hayo utafiti mwingi katika kitabu kwa anwani "Marjiiyatu waruhaniyati" kwa lugha ya kifursi. Na ume-kwishatarijumiwa utafiti wa Sheikh Mutwahariy kwa lugha ya Kiarabu na umechapishwa kwa jina la "*al-Ijitihadu fil-Islaam*". Na hatuwezi kusahau katika nyanja hii rai za ujasiri ambazo amezitoa al-Allammah al-Maruhum Sheikh Muhammad Jawadi Mughuniya ndani ya maandiko yake mbalimbali na mengi.

Na umekwishawadia wakati maudhui ya maendeleo na utafiti wa hali ya hawza na umarjii yawe ni mahala pa utafiti na mjadala makani, ndani ya kamati zenye kujali au mikutano yenye malen-go au majadiliano yenye kujenga kupitia mimbari za kiutamaduni na kimatangazo.

**Nne:** Umarjaa wa kidini una nafasi yake muhimu katika umma na uhalisia wake unaathiri athari kubwa juu ya hali ya kundi la Kishi'ah, na hivyo hauko mbali na kubeba jukumu la ambayo kundi linaishi nayo miongoni mwa hali na mazingira. Na ikiwa kuna vikwazo na vizingiti vinavyodhoofisha uwezo wa umarji'i katika kukabiliana na uongozi, ni wajibu kundi lote kubeba jukumu la kuondoa vikwazo hivyo na kuondoa vizingiti. Na ikiwa changamoto kubwa za kileo zinalazimisha umma kuwa katika kiwango cha kukubali changamoto hizi, hakika umarji'i ndio unahusika na hilo kwa daraja la kwanza.

Kwa hiyo, ni haki ya wenye ikhilasi na wenye uelewa kupiga kengele ya hatari na kuonyesha hofu yao na huzuni yao juu ya mustakabali wa umaraji'i wa kidini. Na matumaini yetu yapo kwa Maraaji'i watukufu, na viongozi watukufu katika hawza za elimu, wasishughulishwe na mbinyo wa washabiki na wenye kuunga mkono katika kusikiliza sauti za wenye ikhilasi na wenye uelewa.

**Swali:** Mimbari ya Husein na majilisi za Huseini zina nafasi kubwa na wazi katika hali ya jamii ya Kishi'ah, na kwa kuzingatia kuwa nyinyi ni kati ya makhatibu wa mimbari hizo, vipi mnatathimini jukumu la nafasi ya mimbari na hotuba za Huseiniya hivi sasa je, zinaendana na mazingira na mabadiliko ya kisiasa na kijamii?

Kama ilivyo maarufu, mimbari ya Huseini imekuwa ni njia inayotoa nafasi ya kuelimisha umma kwa Mashi'ah, na imefanya kazi kubwa katika kustawisha ufuasi wa Ahlul-Bayt عليهم السلام, uimara wa kinafsi katika historia yao na kumbukumbu yao ndani ya jamii ya Kishi'ah.

Na kuna vitu na mambo ambayo ni nguvu kubwa inayopatikana katika mimbari na majilisi za Huseini miongoni mwazo ni: Hali ya uananchi ya watu katika muonekano huu, ambapo zinafanyika majilisi kwa kujitolea wananchi, hakuna shughuli wala nafasi ya utawala humo, na watu wanachagua makhatibu wao kulingana na raghba zao bila ya kuingiliwa na yeyote. Vile vile uitikiaji wa watu kuhusu majilisi za Huseiniya hususan katika siku za Muharramu na minasaba mingine ya kidini ni jambo linaloleta mvuto na mshangao. Kama ambavyo mazingira na huruma iliyojaa ambayo inatawala katika majilisi yanafanya nyoyo na nafsi kuwa tayari kuathirika na kuamiliana pamoja na anayoyaeleza khatibu.

Na kwa hiyo majilisi za Huseiniya zimeweza kufanya mengi, na kuacha athari katika jamhuri ya Mashi'ah, isipokuwa kuna baadhi ya vikwazo ambavyo vinadhoofisha dauru ya mimbari na uwezo wake katika kuleta athari kubwa kadiri inavyowezekana nazo ni:

- Hali za kisiasa ambazo zinabana uhuru wa khatibu katika kutoa maudhui yanayoendana na mazingira na kujali mambo ya wakati. Maadamu uhuru wa kifikra na kisiasa haupatikani katika nchi nyingi, hakika mimbari inakuwa imebanwa na yanayoizunguka miongoni mwa mazingira.

Na tunajua namna gani baadhi ya makhatibu ambao walitaka kufikisha ujumbe wao bila ya kujali mazingira yanayozunguka na wametoa uhai wao kama thamani ya ushujaa wao. Na baadhi wamevumilia jela na mateso na kufukuzwa, kama ilivyotokea kwa makhatibu wa Kiirani wapigana jihadi katika zama ya Shah, na kama ilivyotokea Iraki.

**- Mbinyo wa kuiga**: Ambapo baadhi ya jamii zinang'ang'ania khatibu kujilazimisha na muundo na njia ya kuiga na ya kurithi katika khutuba yake, na kukariri kwao waliyoyazoa miongoni mwa visa na mambo ya sira, bila ya kuzungumzia matatizo ya jamii na shida zake, kama ambavyo kipimo cha uzuri wa khatibu ndani ya uigaji huu unatokana na upeo wa uwezo wake wa kuamsha hisia na kiwango cha uzuri wa sauti katika kueleza masaibu ya Ahlul-Bayt عليهم السلام. Kwa hakika ni lazima tuseme hakika mfano wa vibano hivi vimeanza kumalizika na kwisha kwa kuenea uelewa na ufahamu.

**- Kiwango cha khatibu na lengo lake**: Pamoja na uzamani wa hotuba ya mimbari kwetu, na haja kubwa ya makhatibu, na kuenea majilisi za Huseiniya, isipokuwa maandalizi ya makhatibu inatimu kwa bahati mbaya na msukumo wa ratiba binafsi. Hatuna vyuo katika hawza zetu za elimu kwa ajili ya kuandaa makhatibu au kuboresha viwango vyao, na hakuna ratiba ya kusaidia kulea makhatibu na kuwaendeleza. Na kwa masikitiko hata kozi fupi ya kutengeneza hotuba katika kitabu cha mantiki cha Marhum Sheikh Mudhwafar, mara nyingi waalimu wanashughulika na wanafunzi na kulisomesha katika hawza za elimu, na yote hayo yamepelekea kuwa wengi wa makhatibu katika jamii yetu hawako katika kiwango kinachotakiwa katika kupevuka kwao kielimu na kiutamaduni.

**- Na jambo la mwisho**: Kiwango cha lengo la ujumbe. Baadhi ya makhatibu, mimbari kwao imekuwa ni kazi na chanzo cha maisha, na baadhi ya wengine hotuba kwao imekuwa ni shughuli

na kazi, na wala haipingiki kwamba tunalo – walhamdulillahi – kundi la makhatibu wenye lengo wanaharakati ambao wanaizingatia mimbari kuwa ni njia ya kuhudumia lengo tukufu, na wanaitumia mimbari katika kuelimisha watu na kuwaelekeza ili kubeba majukumu yao ya kidini na kijamii.

Na kinachotakiwa katika hatua hii muhimu ni kuzingatia hali ya mimbari na majilisi za Huseiniya katika jumla ya makhatibu na pande zenye uelewa katika umma na inawezekana kutimia hilo kupitia mapendekezo yafuatayo: **Kwanza:** Maraji'i wa kidini waonyeshe mazingatio katika upande huu, kwa kuchunga mambo ya makhatibu na kuwajulia hali zao na kutoa maelekezo kwao. Kwa mfano anapotaka mariji'i wa dini kwa makhatibu kutia mkazo katika majilisi zao katika msimu huu (Muharamu au Ramadhani) katika maudhui maalumu anayoona umuhimu wake, hakika hilo litapokewa na kukubalika na makhatibu wengi. Na alikwishafanya hayo Marhum Imam al-Khumainiy قدس سره ambapo alikuwa anapokea makhatibu wa Kiirani au makhatibu wa Tehran karibu na siku kumi za Ashura na kuwapa nasaha zake na rai yake na hiyo ilikuwa ni ishara nzuri pamoja na kuchukua tofauti kwa jicho la mazingatio.

**Pili:** Kuweka ratiba ndani ya hawza ya elimu ili kulea makhatibu na kuwaendeleza.

**Tatu:** Kufanya makongamano ya kiulimwengu baina ya makhatibu ili kubadilishana rai na uzoefu, na majadiliano katika kuchagua kwao maudhui na kuboresha malengo na mbinu za khitwaba. Hakika sisi tunashangazwa na habari za makongamano ambayo yanafanywa ulaya kuhusu mambo madogo na ya kipuuzi kama nilivyosoma mwishoni kuhusu kongamano la haki za wavutaji ambalo lilifanyika Helsink Finland mwishoni mwa mwezi wa kumi na moja mwaka 1990, na ambalo limesambazwa na jarida la wakala wa habari na kwamba liliendelea kwa siku mbili na lilihudhuriwa na wawakilishi 120 kutoka dola za ulaya,

Marekani, Latini Amerika, Australia na Japani!!

Wakati ambapo wito wa kongamano la makhatibu linakuwa ni jambo linaloleta mshangao na majadiliano katika mazingira yetu! Na baadhi wanaweza kutoa udhuru kwamba mazingira ya kisiasa hayatoi ushirikiano katika mfano wa haya, lakini hili halipo kila sehemu. Kuna nchi inawezekana kwa makhatibu wake kukutana au kubadilishana rai na uzoefu.

Na katika kumbukumba ya huzuni katika nafsi yangu katika nyanja hii mwaka 1399H/1979 nilihamia katika sehemu ya Abadan, Khurasan na niliwaita makhatibu huko kutoka Abadan, na lengo ni ushirikiano wa kijamii na kuunda kundi la makhatibu, na walikuwa wanashiriki humo takriban makhatibu 40 kwa viwango vyao tofauti. Na tulikuwa tunakutana kila wiki, na kubadilishana faida, lakini kulitokea matatizo ya kisiasa huko kisha ikatokea vita ikabomoa umoja na mkusanyiko huo.

**Nne:** Kutoa jarida maalumu ambalo linajishughulisha na khitwaba na mambo ya makhatibu. Na ulimwengu umejaa majarida maalumu katika nyanja mbalimbali za kifikra na za kijamii, na vilevile kuhusu umakenika na fani, na kuhusu mavazi, na kuhusu nyanja nyingi. Inafaa sana kutoa jarida linalojali habari za makhatibu na maelezo yao, waliopita na waliopo na habari za majilisi za Huseiniya na mambo ambayo yanajali makhatibu katika kiwango cha khutuba au mbinu zake.

**Tano:** Wajitolee makhatibu wenye uwezo wenye kufaulu kwa kutoa uzoefu wao na fikra zao ili wanufaike makhatibu wengine, kama vile al-Allammah khatibu Muhammad Taqiy Falsafiy, Ustadh khatibu Dokta Sheikh Ahmad al-Wailiy na khatibu mahiri Sheikh Abdul-Hamid al-Muhajir. Hakika rai na uzoefu wa mfano wa hawa maustadhi viongozi utakuwa ni wenye manufaa na faida kwa makhatibu wapya na wanaoinukia.